

**MIKAKATI NA MITINDO KATIKA UJIFUNZAJI WA KISWAHILI KAMA  
LUGHA YA BIASHARA MIONGONI MWA WAFANYABIASHARA JIJINI  
KAMPALA-UGANDA**

**NA**

**MUTENYO AIDAH**

**TASNIFU INAYOWASILISHWA KWA MINAJILI YA KUTOSHELEZA BAADHI  
YA MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMIFU KATIKA KISWAHILI**

**SHULE YA SANAA NA SAYANSI JAMII**

**CHUO KIKUU CHA MASENO**

**©2023**

## **IKIRARI**

Tasnifu hii ni kazi yangu binafsi na haijawahi kuwasilishwa katika chuo kingine kwa mahitaji ya shahada yoyote ile.

**Mutenyo Aidah**

PhD/FA/00088/2016

Sahihi ..... Tarehe.....

Tasnifu hii imetolewa kwa idhini yetu kama wasimamizi wa kazi hii katika Chuo Kikuu cha Maseno.

**Dkt. Deborah Nanyama Amukowa**

Idara ya Kiswahili na Lughu nyingine za Kiafrika

Chuo Kikuu cha Maseno

Sahihi ..... Tarehe.....

**Dkt. Benard Odoyo Okal**

Idara ya Kiswahili na Lughu nyingine za Kiafrika

Chuo Kikuu cha Maseno

Sahihi ..... Tarehe.....

## SHUKRANI

Namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uhai, ari na nguvu zilizoniwezesha kukamilisha kazi hii na kufanya ioneckane jinsi ilivyo. Shukrani zangu za dhati ziwaendee wasimamizi wangu Dkt. Deborah Nanyama Amukowa na Dkt. Benard Odoyo Okal kwa maelekezo yao na busara kama wazazi na wataalamu nilipokuwa nikifanya utafiti huu. Nawashukuru wahadhiri wote wa Idara ya Kiswahili na Lughu nyingine za Kiafrika wa chuo Kikuu cha Maseno kwa usaidizi wao. Shukrani zangu za dhati ziwaendee waajiri wangu wa Chuo Kikuu cha Kabale kwa kuniruhusu kuendelea na masomo yangu. Ninatambua pia wafanyabiashara wa Ekedi ya Mukwano, Simlaw Uganda Limited na soko la Kikuubo ambao walinifaa kwa maoni katika ukusanyaji wa data za msingi. Napenda pia kuwashukuru wahadhiri wa kitengo cha Kiswahili katika idara ya lugha na mawasiliano Chuo Kikuu Kyambogo kwa kunijengea msingi dhabiti wa shahada ya awali pamoja na idara ya lugha na fasisi katika Chuo Kikuu cha Kiislamu cha Mbale ambayo iliniandaa kuzamia katika Kiswahili. Sitosahau wahadhiri wa Kiswahili wa Idara ya Mawasiliano na Isimu kutoka chuo Kikuu cha Maasai Mara ambao walinijengea msingi bora wa kufanikisha mada yangu ya utafiti.

Napenda kumshukuru hayati Profesa Beja Karisa ambaye aliniandaa katika taaluma ya Ufundishaji wa Lughya ya pili kwani matunda haya ni kwa ajili ya msingi alionijengea. Aidha, shukran za dhati ziwaendee Prof. Ernest Sangai Mohochi na Prof. Kenneth Inyani Simala kwa kuniongoza kujiunga na Chuo Kikuu cha Maseno wakati nilikuwa natatizika kuteua chuo cha kujiendeleza kimasomo. Mwongozo wao umenifanya nimekuwa sehemu ya historia ya Chuo Kikuu cha Maseno ambacho kilinipa fursa ya kusoma kozi yangu ya uzamifu.

Shukrani ziwaendee marafiki zangu ambao tulianza nao ndoto ya uzamifu na kuikamilisha kwa pamoja; Mulei Martin na Atukunda Edwine. Nashukuru familia yangu ambayo ilinivumilia niliposhughulika na masomo. Muda wa starehe na kujumuika na familia ulikuwa finyu sana. Hata hivyo, naziba pengo hilo na furaha tele. Natupa kijiti kwa vijana wangu Ogema Moses, Omuse Calvin, Omunyini Junior na binti zangu Maria Magarita, Ensieta Mgulo, Makhame Diana na Khalayi Shakira kwamba usukani sasa ni wenu. Mungu awajalie na kuwapitisha mahali nitaishia. Kwa mamangu mpendwa Bi. Sabina Nakami Sophia unahitaji taji kwa kunilea na kunifanikisha katika masomo. Nani kama mama. Hakuna njia nyingine ambayo naweza kuwashukuru ila Mungu ndiye mwema na fadhlila zake ni za milele na kwa neno moja ninasema, **ASANTENI.**

## **TABARUKU**

Kazi hii naitabarukia mamangu mpendwa Bi. Sabina Nakami Sophia, watoto wangu niloachiwa na marehemu dadangu na ndugu yangu Namakoye Beatrice na Natsambwa Shiundu Samuel, mabinti zangu Makhame Diana Juliet, Khalayi Shakirah na wadau wa Kiswahili hasa wale ambao wanashughulikia taaluma ya ufundishaji wa Kiswahili kama lugha ya pili na Isimujamii.

## IKISIRI

Dhima mojawapo ya lugha ya Kiswahili ni ukuzaji wa sekta ya uchumi. Kiswahili kama lugha ya pili nchini Uganda, kilianzishwa kwa ajili ya kuendeleza biashara na dini. Ujifunzaji na matumizi yake hayajaendelezwa kwa kina. Hata hivyo unapokwenda katika maeneo ya biashara, utakuta Kiswahili kikitumika mionganoni mwa wafanyabiashara. Hali ya jinsi wanavyojifunza na kutumia Kiswahili kuendeleza biashara na changamoto wanazokumbana nazo katika matumizi ndilo pengo lililosughulikiwa katika utafiti huu. Azma ya utafiti huu ilikuwa kuchunguza mikakati na mitindo katika ujifunzaji wa Kiswahili kama lugha ya biashara mionganoni mwa wafanyabiashara jijini Kampala, Uganda. Madhumuni mahsusiyalikuwa: Kufafanua mikakati na mitindo ya kujifunza Kiswahili kama lugha ya kibiashara jijini Kampala Uganda, kutathmini jinsi mikakati na mitindo mbalimbali huwezesha kujifunza Kiswahili kama lugha ya kibiashara jijini Kampala na kupambanua changamoto zinazokumba wafanyabiashara wakati wa kujifunza Kiswahili kibiashara na kuchanganua mikakati ya namna ya kutatua changamoto zinazowakabidhi wafanyabiashara kujifunza Kiswahili kibiashara. Utafiti huu uliongozwa na kiunzi cha nadharia mbili: Kwanza, Nadharia ya Stephen Krashen (1987) ambayo ina mihimili mitano; nadharia tete ya upataji/ujifunzaji, nadharia tete ya mfumo asili, nadharia tete ya dhana mpya na nadharia tete ya kichujio athari. Pili, Nadharia ya modeli ya elimu ya Richard Gardener (2000). Mihimili iliyohusika ni; mhimili wa jitihada, nia/ari, motisha changamani, uwezo wa kufanikiwa na mwelekeo chanya. Utafiti ulifanyika mjini Kampala nchini, Uganda katika Ekediy Mukwano, Simlaw International Limited na soko la Kikuubo. Utafiti ulijikita katika ujifunzaji na ufunzaji wa lugha ya pili na Isimujamii. Utafiti huu ulichanganua mikakati na mitindo ya kujifunza na kutumia lugha ya Kiswahili kibiashara pamoja na changamoto za ujifunzaji wa Kiswahili kama lugha ya biashara mionganoni mwa wafanyabiashara jijini, Kampala. Usampulishaji dhamirifu ultumiwa kwa kurejelea aina yake ya usampulishaji mpokezano kifu ambapo uteuzi dabwa dabwa ultumiwa kuteuwa sampuli ya wasailiwa 260 ya wafanyabiashara kutoka Ekediy Mukwano, Simlaw International Limited na soko la Kikuubo. Sampuli kusudio ilitumika kuteua Ekediy 2 na soko Moja la biashara anuwai kuhusika katika utafiti huu. Mbinu za hojaji, usaili na uchuzaji zilitumiwa kukusanya data mionganoni mwa wafanyabiashara nyanjani. Vifaa vya utafiti ni pamoja na hojaji, dodoso, mwongozo wa uchunzaji vilitumika kukusanya data nyanjani. Data ilichanganuliwa kutumia mkabala mseto na kuwasilishwa kimaelezo ukishirikisha majedwali. Matokeo ya utafiti yalionyesha kwamba wafanyabiashara walitumia mikakati ya nyimbo/ukariri, mwanafunzi kwa mwanafunzi, matumizi ya lugha chanzi, kuongea, mawasiliano, mitagusano ya ukuruba kati ya wanunuza na wauzaji, teknolojia, mapango binafsi, utambuzi na urejeleaji. Mitindo ya mwingiliano iliyodhahirika ni dukuduku, kusikiza, ujifunzaji asilia, mwelekeo, hamasa, kuashiria na tabia za mjifunzaji. Hii ilifanyika kuititia kusikiza nyimbo, wafanyabiashara kufundishana wenyewe kwa wenyewe, uhamishaji sheria kutoka lugha chanzi, mawasiliano baina yao na wanunuza, kutagusana na wajuo Kiswahili, matumizi ya teknolojia, kujipangia namna ya kujifunza, utambuzi, dukuduku, hamasa, mwelekeo, kuashiria na tabia ambazo baadhi ya wafanyabiashara walikuwa nazo. Utafiti huu ulibaini changamoto za kisarufi, muda wa kujifunza, kutumia lugha kimshitukizo, mwelekeo hasi, athari za kisiasa, umri, uoga, tofauti za kijinsia na kanuni za kiisimu. Utafiti huu utachangia katika taaluma ya Isimujamii na ujifunzaji wa lugha ya pili. Utafiti huu ulipendekeza tafiti zaidi kufanyika katika kutambua mikakati na mitindo zaidi katika sekta nyinginezo.

## **ABSTRACT**

One of the roles of Kiswahili language is the development of the economic sector. Kiswahili as a second language in Uganda was established to promote business and religion. Its learning and use have not been developed in depth. However, in business places, the use of Kiswahili is evident amongst the business people. How they learn and use Kiswahili to develop business and the challenges they face in using is the gap of our study. The aim of this study was to investigate the strategies and styles of learning a second language that facilitate the learning of Kiswahili as a business language, to determine the challenges faced by traders when learning Kiswahili for business and how to solve those challenges. The specific objectives were: To explain the strategies and styles of learning Kiswahili as a business language in Kampala Uganda, to evaluate how different strategies and styles enable learning Kiswahili as a business language in Kampala and to identify the challenges faced by traders when learning Kiswahili for business and to analyze the strategies of how to solve the challenges assigned to traders to learn commercial Kiswahili. This study was guided by the framework of two theories: First, the theory of Stephen Krashen (1987) which has five tenents; the acquisition/learning hypothesis, the natural system hypothesis, the monitoring hypothesis, the new concept hypothesis and the effect filter hypothesis. Second, the theory of Richard Gardener (2000). The tenents involved are; effort, intention, complex motivation, ability to succeed and attitude. The research was conducted in Kampala, Uganda in Mukwano Ekedi, Simlaw International Limited and Kikuubo market. Research focused on second language learning, applied linguistics and sociolinguistics of Kiswahili language. The study investigated strategies, styles and challenges in the learning and usage of Kiswahili as a business language among traders and how to solve those challenges in Kampala, Uganda. Purposive sampling was used with reference to its type of random sampling to saturation to select a sample of 260 interviewees of traders from Mukwano Arcade, Simlaw International Limited and Kikuubo market. Purposive sampling was used to select 2 achades and One market of various businesses to be involved in this study. Questionnaire, interview and observation methods were used to collect data among traders in the field. The research tools used to collect data from the field includes Questionnaires, interview guide and observation checklist. Data was analyzed using a mixed approach and presented descriptively using tables. The results of the study showed that without knowing the traders used strategies of songs/recitation, student to student, use of source language, speaking, communication, close contacts between buyers and sellers, technology, personal programming, recognition and recycling. Interaction styles, creativity, listening, and natural learning, orientation, motivation, and signalling and learner behaviours. This was done through listening to songs, traders teaching each other, transfer of language rules from the first language, communication between traders and buyers, contact with those who know Kiswahili, use of technology, planning a way of learning, awareness, motivation, direction, signalling and behaviour which some of the traders had. This study identified grammatical challenges, learning time, language use by instinct, negative attitudes, political influences, age, fear, gender differences and linguistic norms. This research will contribute to the field of sociolinguistics and second language learning. This study suggested that more research be done to identify more strategies and styles in other sectors.

## YALIYOMO

IKIRARI .....	ii
SHUKRANI.....	iii
TABARUKU .....	iv
IKISIRI .....	v
ABSTRACT.....	vi
YALIYOMO.....	vii
VIFUPISHO VILIVYOTUMIKA .....	xii
UFAFANUZI WA ISTILAHİ .....	xiii
ORODHAYA MAJEDWALI.....	xiv
ORODHA YA MICHORO.....	xv
<b>SURA YA KWANZA: UTANGULIZI .....</b>	<b>1</b>
1.1 Usuli wa Utafiti.....	1
1.1.1 Historia ya Kiswahili nchini Uganda .....	3
1.1.2 Matumizi ya Kiswahili katika Biashara .....	5
1.1.3 Uhusiano uliopo kati ya mikakati na mitindo ya ujifunzaji wa L.2 .....	6
1.2 Umuhimu wa kujifunza Kiswahili kama lugha ya biashara.....	9
1.3 Swala la Utafiti .....	13
1.4 Maswali ya Utafiti.....	14
1.5 Madhumuni ya utafiti.....	14
1.6 Umuhimu wa Utafiti .....	15
1.7 Upeo wa Utafiti.....	15
1.8 Kiunzi cha nadharia .....	16
1.8.1 Nadharia ya Ufuatilizi.....	16
1.8.2 Nadharia ya Motisha ya Ujifunzaji Lugha ya Pili.....	19
1.8.3 Mihimili ya nadharia.....	22
1.8.3.1 Nadharia ya Stephen Krashen (1987) .....	22
1.8.3.2 Nadharia ya motisha ya ujifunzaji lugha ya Richard Gardener (2000) .....	23
1.9 Namna nadharia zilivyotumika katika utafiti .....	23
1.10 Hitimisho.....	23
<b>SURA YA PILI: TAHAKIKI YA MAANDISHI .....</b>	<b>25</b>
2.1 Utangulizi.....	25
2.2 Mikakati na mitindo ya ujifunzaji lugha ya pili .....	25
2.2.1 Mikakati ya jumla ya ujifunzaji lugha ya pili .....	25

2.2.2 Mitindo ya jumla ya ujifunzaji lugha ya pili .....	33
2.3 Jinsi mikakati na mitindo hutumiwa katika kujifunza lugha .....	43
2.3.1 Jinsi mikakati inatumiwa katika ujifunzaji lugha.....	43
2.3.2 Jinsi mitindo hutumiwa katika kujifunza lugha .....	50
2.4 Changamoto zinazotokana na ujifunzaji wa lugha ya pili .....	56
2.5 Mikakati ya namna ya kutatua changamoto zitokanazo na ujifunzaji wa lugha ya pili ....	68
2.6 Hitimisho.....	70
<b>SURA YA TATU: MBINU ZA UTAFITI.....</b>	<b>72</b>
3.1 Utangulizi.....	72
3.2 Muundo wa Utafiti .....	72
3.3 Eneo la Utafiti .....	74
3.4 Idadi lengwa.....	74
3.5 Usampulishaji na Sampuli .....	75
3.6 Mbinu za ukusanyaji data .....	77
3.6.1 Hojaji.....	78
3.6.2 Usaili .....	79
3.6.3 Uchunzaji .....	79
3.7 Vifaa vya kukusanya data .....	80
3.7.1 Hojaji lililo na maswali ya kujaza.....	80
3.7.2 Dodoso .....	81
3.7.3 Simu mahiri.....	82
3.7.4 Mwongozo wa uchuzaji .....	82
3.7.5 Ufaafu na utegemezi wa vifaa vya kukusanya data .....	83
3.8 Uchanganuzi na uwasilishaji wa data .....	84
3.9 Maadili ya utafiti.....	85
3.10 Hitimisho.....	86
<b>SURA YA NNE: UCHANGANUZI, MJADALA NA UWASILISHAJI WA MATOKEO .....</b>	<b>87</b>
4.1 Utangulizi.....	87
4.2 Mikakati na mitindo mbalimbali ambayo ilitumiwa na wafanyabiashara kujifunza Kiswahili kama lugha ya biashara .....	87
4.2.1 Mikakati iliyotumiwa na wafanyabiashara kujifunza Kiswahili kama lugha ya biashara jijini Kampala, Uganda .....	89
4.2.1.1 Nyimbo/ Ukariri.....	92

4.2.1.2 Mkakati wa ujifunzaji kati ya Mwanafunzi na mwanafunzi .....	94
4.2.1.3 Mkakati wa Matumizi ya lugha chanzi .....	95
4.2.1.4 Mkakati wa Kuongea .....	97
4.2.1.5 Mkakati wa Mawasiliano .....	99
4.2.1.6 Mtagusano na ukuruba kati ya wanunuvi na wafanyabiashara .....	100
4.2.1.7 Mkakati wa Teknolojia .....	102
4.2.1.8 Mkakati wa Mpango binafsi .....	103
4.2.1.9 Mkakati Kufidia .....	104
4.2.1.10 Mkakati wa Utambuzi .....	105
4.2.1.11 Urejeshaji .....	107
4.2.2 Mitindo iliyotumiwa na wafanyabiashara kujifunza Kiswahili .....	108
4.2.2.1 Mwingiliano .....	109
4.2.2.2 Dukuduku .....	111
4.2.2.3 Kusikiliza .....	112
4.2.2.4 Mtindo wa Ujifunzaji asilia .....	114
4.2.2.5 Mtindo wa Mwelekeo .....	116
4.2.2.6 Mtindo wa Hamasa .....	118
4.2.2.7 Kuashiria .....	120
4.2.2.8 Mtindo wa Tabia za mjifunzaji .....	121
4.3 Jinsi mikakati na mitindo mbalimbali iliwezesha kujifunza Kiswahili .....	123
4.3.1 Mikakati iliyowezesha ujifunzaji wa Kiswahili kama lugha ya biashara .....	123
4.3.1.1 Nyimbo/Ukariri .....	123
4.3.1.2 Mwanafunzi kwa mwanafunzi kufanikisha mawasiliano .....	129
4.3.1.3 Matumzi ya Luga chanzi .....	133
4.3.1.4 Kuongea .....	142
4.3.1.5 Mawasiliano .....	143
4.3.1.6 Mitagusano ya ukuruba kati ya wanunuvi na wauzaji .....	147
4.3.1.7 Matumizi ya Teknolojia .....	150
4.3.1.8 Mkakati wa Mpango binafsi .....	153
4.3.1.9 Utambuzi .....	156
4.3.1.10 Mkakati wa urejeleaji .....	159
4.3.2 Jinsi mitindo ilivytumiwa na wafanyabiashara kujifunza Kiswahili kama kibiashara jijini Kampala Uganda .....	161
4.3.2.1 Mwingiliano .....	162

4.3.2.2 Dukuduku.....	166
4.3.2.3 Kusikiliza .....	169
4.3.2.4 Ujifunzaji halisia .....	173
4.3.2.5 Mwelekeo.....	175
4.3.2.6 Hamasa.....	179
4.3.2.7 Kuashiria .....	182
4.3.2.8 Hulkta za mjifunzaji.....	185
4.3.2.9 Mpango binafsi .....	187
4.4 Changamoto zinazowakumba wafanyabiashara wakati wa kujifunza Kiswahili kibiashara .....	190
4.4.1 Changamoto za kisarufi .....	191
4.4.2 Muda wa kujifunza.....	194
4.4.3 Kutumia lugha ya Kiswahili kimshutikizo.....	195
4.4.4 Lugha mseto.....	196
4.4.5 Mwelekeo hasi dhidi ya lugha ya Kiswahili .....	198
4.4.6 Ukosefu wa mafunzo rasmi ya Kiswahili .....	199
4.4.7 Athari za kisiasa .....	200
4.4.8 Mazingira ya kufanya biashara .....	201
4.4.9 Uoga.....	202
4.4.10 Tofauti za kijinsia.....	202
4.4.11 Kanuni na vipengele vya kiisimu.....	203
4.5 Kuchanganua mikakati ya namna ya kutatua changamoto zinazowakabidhi wafanyabiashara kufanikisha ujifunzaji Kiswahili kibiashara .....	204
4.6 Hitimisho.....	207
<b>SURA YA TANO: MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO .....</b>	<b>209</b>
5.1 Utangulizi.....	209
5.2 Muhtasari wa Utafiti .....	209
5.3 Hitimisho.....	211
5.3.1 Mikakati na mitindo ya kujifunza Kiswahili kama lugha ya biashara jijini Kampala, Uganda.....	211
5.3.2 Namna mikakati na mitindo mbalimbali iliwezesha ujifunzaji wa Kiswahili kama lugha ya biashara jijini Kampala, Uganda .....	212
5.3.3 Changamoto ambazo wafanyabiashara walikumbana nazo wakati wa kujifunza Kiswahili kama lugha ya biashara jijini Kampala, Uganda .....	213

5.3.4 Mikakati ya namna ya kutatua changamoto zinazowakabili wafanyabiashara ili kufanikisha ujifunzaji Kiswahili kibishara jijini Kampala, Uganda.....	214
5.4 Mapendekezo kwa mujibu wa madhumuni ya utafiti .....	214
5.4.1 Mapendekezo kuhusu mikakati na mitindo ya ujifunzaji wa Kiswahili kama lugha ya biashara jijini Kampala.....	214
5.4.2 Mapendekezo kuhusu Jinsi mikakati na mitindo inavyowezesha ujifunzaji Kiswahili kama lugha ya biashara jijini Kampala, Uganda .....	215
5.4.3 Mapendekezo kuhusu changamoto zinazowakabili wafanyabiashara wakati wa ujifunzaji wa Kiswahili kama lugha ya biashara jijini Kampala, Uganda.....	216
5.4.4 Mapendekezo kuhusu mikakati ya kutatua changamoto zinazowakabili wafanyabiashara ili kufanikisha ujifunzaji Kiswahili kibishara jijini Kampala, Uganda.....	217
5.5 Mapendekezo ya tafiti za baadaye .....	218
5.6 Hitimisho ya sura hii .....	218
<b>MAREJELEO .....</b>	<b>219</b>
<b>VIAMBATISHO .....</b>	<b>238</b>

## **VIFUPISHO VILIVYOTUMIKA**

<b>BAKITA</b>	:	Baraza la Kiswahili Tanzania
<b>CPH</b>	:	Critical Period Hypothesis
<b>KACITA</b>	:	Kampala City Traders Association
<b>KAKAMA</b>	:	Kamisheni ya Kiswahili Afrika Mashariki
<b>L1</b>	:	Lugha ya kwanza
<b>L2</b>	:	Lugha ya pili
<b>LAD</b>	:	Language Acquisition Device
<b>NELI</b>	:	Nuffield Early Language Intervention
<b>NIED</b>	:	National Institute of Education Development
<b>SSBI</b>	:	Style and Strategies Based Instruction
<b>TY</b>	:	Tafsiri yetu
<b>TUKI</b>	:	Taasisi ya uchunguzi wa Kiswahili
<b>KAKAMA</b>	:	Kamisheni ya Kiswahili Afrika Mashariki

## **UFAFANUZI WA ISTILAHİ**

**Mikakati ya ujifunzaji lugha:** Mikakati ni stadi za ujifunzaji L.2 zinazoonekana Mjifunzaji anapodhihirisha tabia ambazo zinamsaidia kujifunza L.2. kwa jumla. Inarejelea mikabala mahsus ambayo hutumiwa na mjifunzaji wa lugha kuhifadhi, kuhakiki na kutumia ujumbe ambao amepata.

**Mitindo ya kujifunza lugha:** Mitindo ni hulka zisizoonekana ila tu kwa kutumia hisi wakati wa kujifunza L.2. Hulka huwa ni za kisaikolojia ambazo zinashughulikia jinsi mjifunzaji anachukulia lugha, kuingiliana na watumiaji lugha na mazingira ambayo anajifunza lugha.

**Mfanyabiashara:** Inarejela mtu ambaye anaanzisha biashara kutokana na mawazo ambayo amepata kutoka kwa mtu mwingine ama namna hali ilivyo. Yule ambaye hununua na kuza bidhaa kwa wingi kwa wanunuizi mbalimbali. Aidha, ni mtu anayejipatia riziki kununua vitu na kuviuza kwa ajili ya kupata faida

**M/wanunuizi:** Hawa ni watu ambao hununua bidhaa wanazozitaka. Wao hutambua bidhaa zinazohitajika katika soko na kununua kwa wingi kisha kuwauzia wateja wao. Katika biashara, kuna aina tofauti za wanunuizi, kila mmoja ana majukumu lake kama muuzaji wa bidhaa kwa jumla ama rejareja.

**Mwanafunzi:** Binadamu ambaye ana sifa za kujifunza lugha ya pili.

## **ORODHAYA MAJEDWALI**

Jedwali 2.1: Mifano ya sauti zinavyotamkika.....	64
Jedwali 3.1: Idadi ya wasailiwa.....	77
Jedwali 4.1: Kupata mafunzo ya Kiswahili kibashara.....	88
Jedwali 4.2: Mikakati ya ujifunzaji lugha ya pili ambayo ilitumiwa kujifunza Kiswahili kibashara.....	90
Jedwali 4.3: Mikakati iliyokuwa ikitumiwa na wafanya biashara kujifunza Kiswahili.....	92
Jedwali 4.4: Mitindo iliyokuwa ikitumiwa na wafanyabiashara kujifunza Kiswahili kama lugha ya biashara kutoka kwa hojaji.....	109
Jedwali 4.5: Namna mikakati ilivyotumiwa na wafanyabiashara kujifunza Kiswahili kibashara.....	123
Jedwali 4.6: Matumizi ya fomula katika sentensi.....	134
Jedwali 4.7: Matumizi ya maneno katika sentensi.....	135
Jedwali 4.8: Kuhamisha sauti kutoka lugha chanzi hadi Kiswahili.....	136
Jedwali 4.9: Baadhi ya maneno ya biashara ya kiasili na Kiswahili.....	137
Jedwali 4.10: Matumizi ya msamiati wa biashara katika sentensi.....	138
Jedwali 4.11: Msamiati wa mavazi katika Lugha asili na Kiswahili.....	139
Jedwali 4.12: Msamiati katika matumizi ya sentensi.....	140
Jedwali 4.13: Matumizi ya mpango binafsi katika sentensi.....	156
Jedwali 4.14: Jinsi Mitindo iliwezesha Kujifunza Kiswahili kama lugha ya biashara.....	162
Jedwali 4.15: Changamoto wasailiwa walikumbana nazo kujifunza Kiswahili kama lugha ya biashara jijini Kampala.....	191
Jedwali 4.16: changamoto za kisarufi.....	192

## **ORODHA YA MICHORO**

Mchoro 1.1: Modeli ya saikolojia ya jamii (Gardner, 2000).....	20
Mchoro 4.1: Kupanga maneno kutoka Kiganda hadi Kiswahili.....	154

## SURA YA KWANZA

### UTANGULIZI

#### 1.1 Usuli wa Utafiti

Sura hii imetanguliza vipengele mbalimbali vya awali vya tasnifu. Vipengele hivyo ni pamoja na : ni: usuli wa utafiti; swala la utafiti, maswali ya utafiti; madhumuni ya utafiti; umuhimu wa utafiti; upeo wa utafiti; kiunzi cha nadharia za utafiti na namna nadharia zilivyotumika katika utafiti.

Maendeleo ya nchi hurahisishwa na matumizi ya angalau lugha moja ya mawasiliano. Dhima mojawapo ya lugha ya Kiswahili ni ukuzaji wa sekta ya Uchumi. Kiswahili kama lugha ya pili nchini Uganda, kilianzishwa kwa ajili ya kuendeleza biashara na dini (Chiraghdin na Mnyampala, 1977) katika falme za Kiganda ambazo hurejelewa kama *obwakabaka* (Chimerah, 2010). Miaka mingi nyuma watu wengi mashinani na taasisi mbalimbali nchini Uganda hawakuthamini matumizi ya Kiswahili. Baadhi yao walihusisha Kiswahili na ujambazi, ulagha'i na ukora kulingana na athari awali za matumizi mabaya ya Kiswahili ya wakati wa mkoloni na jeshi tawala la wakati huo. Sapir (1985) anasema kuwa, binadamu haishi kwa minajili ya madhumuni ya shughuli za mtagusano na ukuruba kati ya wanunuvi na wauzaji kama namna wengi wajuavyo, lakini lugha inachangia pakubwa katika kuendeleza mawasiliano na kuelezea hisia za jamii. Anaendelea kusema kwamba watu wanadhani lugha ipo kwa kutatua shida mahsus za mawasiliano, lakini muhimu ni kwamba katika dunia ya leo kwa kiwango kikubwa lugha huleta pamoja makundi mengi ya watu. Makundi haya huwa na madhumuni na malengo tofauti ya kushirikiana ambapo mumo humo wafanyabiashara wanaunda moja wapo wa makundi hayo.

Wazungumzao lugha za Kibantu nchini Uganda na hata nje mwa Uganda wana namna wanavyoweza kuelewana ila lugha moja inapokuwa mwafaka kukuza mawasiliano, ushirikiano na maendeleo hivyo basi hufanya ujifunzaji Kiswahili kuwa rahisi kwao kimatumizi. Kwa wale amba si Wabantu kwa mfano Wanailotiki mara nyingi hukumbana na changamoto katika matamshi kwa sababu ya tofauti za kilekiskoni. Kwa mfano, Kiganda kina Konsonanti 20 na irabu tano kwa mujibu wa Nakibuuka (1995), ambapo za Kiswahili ni konsonanti 31 zikiwemo irabu tano (BAKITA 2019). Mionganoni mwa hizo utapata kwamba kuna sauti zinazofanana katika lugha zote mbili ukizingatia mahali pa kutamkia na namna ya utamkaji. Kwa wale amba si Wabantu mara nyingi hupata changamoto wakati wa kutamka maneno ya Kiswahili. Kwa mfano, kwa Wanailoti wa Uganda neno sasa latamkwa “chacha”

na shule – “sule”. Hii inamaana kuwa /š/haipo katika sauti za Wanailoti. Hivyo basi wakiona sauti hii wanaihawilisha kuwa /s/ pia /z/ -/s/. Hata hivyo hili halijawafungia katika ujifunzaji wa Kiswahili. Ukuaji wa lugha ya Kiswahili kutoka kuwa lugha mama katika karne ya kumi na nane na kuwa lugha ya kimataifa unaweza kikitwa kwa nyanja nyingi. Miongoni mwa nyanja hizo ni biashara, maandishi, dini, vyombo vyta habari, vita, elimu mawasiliano na sera za serikali.

Kulingana na Shelly (2017), lugha huonyesha kiwango cha maendeleo na kumuinua binadamu kutoka kiwango cha ukale hadi pale anapoweza kusafiri kutumia ndege. Anaendelea kusema kwamba hii imemfanya mwanadamu atofautiane na kiumbe kingine kama mnyama kwa sababu binadamu pekee ndiye profesa wa lugha. Japo wanyama wana kiwango fulani cha mawasiliano, mawasiliano ya binadamu ni ya kipekee ya kutumia maneno. Hivyo basi sifa moja ya binadamu ni kuwa na lugha. Kwa hiyo, umuhimu wa lugha miongoni mwa binadamu hauwezi kufumbiwa macho. Sio chombo cha kuwasiliana tu bali pia kushauriana katika maswala mbalimbali ya maendeleo.

Dhana ya kushauriana ni pana sana kutegemea muktadha kwani ni mojawapo ya sifa muhimu ambazo huchangia maendeleo katika nchi yoyote ile. Katika biashara, lazima watu washauriane namna wanavyoweza kufanikisha biashara zao. Aghalabu kushauriana huleta maafikiano. Lengo hili hufikiwa kupitia kwa ubadilishanaji wa huduma au bidhaa na pesa. Lugha hufaa kuleta maelewano kati ya muuzaji na mnunuzi kupitia mawasiliano kwa kutumia lugha (Toboso na Mosol, 2018). Wengi hujilaumu na kunungu'unika mambo yanapokosa kuwaende vyema na kukuza dhana ya kwamba sisi Waafrika tumo miongoni mwa nchi zilizo nyuma kimaendeleo. Suluhu linapokosa kupatikana, lawama huwekwa kwa maswala ya jamii na utamaduni kwamba lugha inaelezea tu utamaduni na wala siyo maendeleo, ndio sababu miradi imeshindikana (Williams, 1999). William (keshatajwa) anaendelea kusema kwamba imekuwa nadra wafadhili kuelewa kwamba kutokuwa na uwezo wa kuzungumza lughanyingine mbali na LI ndiyo inayofanya watu kutokuwa na uwezo wa kuleta mawazo mapya. Hivi kwamba, lugha ridhiwa za kikoloni kwa mfano Kiingereza na Kifaransa sio rahisi kwa kila mtu kujieleza ili aeleweke. Katika mazingira ya ufanyaji biashara huenda wasitarajie ufadhili namna Williams ametaja ila Kiswahili ni nguzo muhimu katika kuendeleza biashara nchini Uganda.

Matumizi ya Kiswahili kama chombo katika biashara, yamepanua huduma hasa kwa watu

wa mjini na vijijini na hivyo kuhusisha jamii na kukuza biashara (Bosire, 2002). Biashara hudhaniwa kuwa njia ya kipato cha wakaazi wengi mjini Kampala ambao hawako kwa mfumo wa ajira rasmi. Hata hivyo, kwa sababu ya muingiliano na makabila mengi ya Uganda na nchi nyingine, Kiswahili kinatumika kwa mapana. Biashara hizi hufanyika ndani na nje mwa Uganda. Kutokana na hali hii wafanyabiashara wanalazimika kutumia lugha ya Kiswahili wakati wa kuendeleza biashara. Kutegemea na hali hiyo wanalazimika kutumia Kiswahili ambapo kwao ni lugha ya pili ama hata ya tatu ambapo inawabidi watumie mikakati na mitindo ya ujifunzaji L.2 ili kutumia Kiswahili katika shughuli za biashara.

### **1.1.1 Historia ya Kiswahili nchini Uganda**

Lugha na maandishi ya Kiswahili yalikuwa yameshaanza kutumika katika baraza la kifalme za Buganda, Bunyoro kabla hata Mzungu wa kwanza kufika pande hizo katika mwaka wa 1862. Awali ya hapo Waswahili walikuwa wameshaueneza uswahili huko katika shughuli za biashara, dini, lugha na mila za Kiswahili (Chiragdhin na Munyapala, 1977). Uenezaji huo uliambatana na masharti tofauti kulingana na falme husika. Kwa mfano inasemakana mwaka wa 1919 baada ya J.E Phillips kufanywa kiongozi wa dini wa sehemu ya Kigezi, aliwafuta viongozi ambao walikuwa Waganda ambao walitumia Kiganda kubagua wengine na kuweka viongozi walitumia Kiswahili ambao walikuwa Baziba kutoka Bukoba enzi hizo ikiwa Tanganyika. (Mfitumukiza, 2018). Mfumo rasmi ulivyoanzishwa, Ssekamwa (2000) anaeleza kwamba Tume ya Phelp Stoke (1924-1925) ilipendekeza swala la ufundishaji wa lugha za Kibantu, kama vile Kiswahili, hivyo kurasimisha matumizi yake nchini Uganda. Hata hivyo, hakukuwa na mafanikio yoyote katika mradi na mapendekezo ya tume hiyo. Ufundishaji wa Kiswahili ulianza mwaka wa 1927 katika Shule ya Makerere kabla hajakuwa Chuo Kikuu wakati wa ukoloni. Gavana Gowers alipendekeza Kiswahili kitumike katika shughuli za biashara na shulen. Jambo hili halikuwapendeza watu wengi nchini Uganda miongoni mwao akiwemo Katibu katika ufalme wa Kabaka Bw. Kulubya alipohudhuria mkutano wa kuamua lugha mwafaka ambayo itatumika bungeni, ofisini na katika asasi zingine katika kikao kimoja huko Ulaya. Yeye na wenzake kina Zirabamuzale (Chiragdin na Mnyampala 1977) walipendekeza Kiingereza badala ya Kiswahili. Kulubya alipinga vikali maandalizi yoyote ambayo yangelifanya Kiswahili kutumika kama lugha rasmi ya Buganda badala ya lugha yao asili. Waliona kwamba hali kama hii ingepelekea kupoteza hadhi ya lugha yao (Kiganda) na utamaduni wa lugha asili za Afrika. Alipendekeza Kiingereza kwa madai kwamba ndiyo mlango wa maarifa.

Mwaka wa 1990 Chuo cha Walimu wa Shule za Sekondari kilianzishwa Kakoba chini ya uongozi wa Bw. Kakooro Emmanuel Ahimbisiwe. Wanafunzi wa kwanza kujiunga na chuo hicho hawakuwa wamesoma somo la kiswahili (Aidah, 2020) katika kiwango chochote cha elimu ya chini. Aidha wengine walikuwa wamesoma fasihi ya Kiingereza katika kidato cha sita. Baadhi yao walijiunga na somo hilo kwa ari ya kupenda Kiswahili. Ari hii ilitokana na msukumo wa baadhi ya viongozi wa shule ambao waliwahi kupendekeza matumizi ya Kiswahili katika shule za sekondari zilizoanzishwa na wamishonari (Muranga, 2018). Kakoba ilitoa idadi kubwa ya walimu wa shule za sekondari na hivyo Kiswahili kikaanza kufundishwa katika shule za sekondari kama somo la hiari. Jambo la kutofanya Kiswahili somo la lazima lilifanya watu kutotilia maanani kujifunza lugha ya Kiswahili (Aidah & Mulei, 2023). Ni kwa sababu za harakati za muungano wa Afrika Mashariki ndio ulifanya hamasa za kufundisha Kiswahili kwa kila kiwango cha elimu kutiliwa maanani. Mitaala ya shule za upili iliandaliwa na Kiswahili kuanza kutumika. Hata hivyo, mchakato wa kutahini somo hili ulichukua muda mrefu hadi sasa Kiswahili hakitahiniwi katika shule za Msingi ila katika shule za sekondari. Pia kuibuka kwa viwanda kwa mfano jua kali nchini Kenya uliwapa wakaaji wa Uganda nao kuwa na wazo kama hilo ila walibadilisha jina na kuita '*magezi maganda*.' Hili ni soko ambalo bidhaa nyingi zinauzwa na watu wa elimu ya chini. Wanunuzi wao ni watu wa kawaida kutoka sehemu mbalimbali mwa nchi. Hata hivyo iliibuka kwamba uendelezaji wa biashara ungekuwa mgumu bila matumizi ya lugha inayoeleweka na wengi hivyo ikawa kujifunza Kiswahili hakungeepukika (Chimerah, 2010). Hata hivyo, hadi sasa somo la Kiswahili halijapewa kipaumbele kwa watu kama hao. Isitoshe, katika viwango vyatuu ni somo la lazima kwa mafunzo ya walimu wa shule za msingi peke yao na kwenye kidato cha kwanza na cha pili katika shule za sekondari.

Chuo Kikuu cha Kyambogo na Taasisi ya Uundaji wa Mitaala Nchini Uganda walitoa silabasi mpya ya Vyuo vya elimu ya Shule za Msingi Mwaka wa 2013. Mionganoni mwa masomo yaliyoteuliwa, Kiswahili kilipewa nafasi kama somo la lazima kwa mwaka wa kwanza na wa pili. Kuanzia 2009, somo hili lilikuwa likifundishwa bila kutahiniwa lakini mwaka wa 2013 lilianza kutahiniwa ili kutimiza malengo ya Government White Paper (1992- 17,R;18). Kamati hiyo ilipendekeza kwamba Kiswahili kina hadhi ya juu kwa kukuza umoja kuliko lugha yoyote ile nchini Uganda. Aidha, masomo haya mawili Kiswahili na Kiingereza yangefundishwa kama masomo ya lazima kwa wanafunzi wote wa shule za msingi kijijini na mjini. Muda mwafaka uliwekwa katika ratiba, nyenzo za kufundishia na

ufadhili wa walimu ungeshughulikiwa baadaye. Vile vile mwaka wa 2015, silabasi ya kidato cha tano na sita iliandaliwa lakini vivyo hivyo Kiswahili kilikuwa somo la hiari. Kwa wale wanaoamua kulichukua kama somo la hiari huishia kujifunza kozi ya ualimu au masomo ya sanaa katika vyuo vikuu. Katika shule za upili, mtaala mpya wa 2020 umeweka Kiswahili kuwa somo la lazima kidato cha kwanza na cha pili. Kwa wale wanaojifunza kwa kiwango cha juu, hufanya hivyo kwa kutaka kujua lugha ili wanapopata bahati ya kutoka nje ya Uganda wasije wakatatizika na mawasiliano kama wengine au wanasoma ili wapate alama nzuri za kuwavukisha kutoka daraja moja hadi lingine kwa mfano kidato cha sita hadi chuo kikuu huku wakiepuka masomo ambayo yanaonekana kuwa magumu kwao.

Licha ya Kiswahili kufundishwa kama somo la lazima katika kidato cha kwanza na cha pili, Vyuo vya Walimu wa Shule za Msingi, sio kwamba ni sharti somo hilo litafundishwa kwa wanafunzi wa shule za msingi. Wengi hukichukulia tu kama somo la kawaida kupita mitihani na sio kama nguzo ambayo itawasaidia katika harakati mbalimbali maishani kimaendeleo hususan kibashara na katika asasi nyingine. Kwani hata baadaye mwanafunzi huyu akipata ufasaha wa Kiswahili anaweza kufanya kazi ya ukalimani na kazi nyingine ili kujikimu maishani. Hata katika kiwango cha shule za upili ni shule chache tu ambazo zimeona umuhimu wa kufundisha Kiswahili hasa shule za kibinasi ambazo husajili wanafunzi wengi wazawa wanaotumia lahaja za lugha tofauti tofauti zinazopatikana ndani na nje mwa Uganda. Ingawa Kiswahili kimekuwa kikitajwa kila wakati tangu jadi, mwelekeo umekuwa wa kukifundisha katika mafunzo rasmi. Mafunzo ya wakati wa ukoloni yalilenga kukuza dini wala siyo mafunzo msingi ya elimu. Kiswahili hakikupata fursa kutumika au kufundishwa kwa shughuli rasmi hivyo kikabaki kwa mtu binasi kufikiria kama atakitumia ama la. Namna ya kujifunza iliendelezwa na mjifunzaji mwenyewe kwa mazingira yasiyo rasmi kwa madhumuni yaliyojulikana kwa mjifunzaji mwenyewe.

### **1.1.2 Matumizi ya Kiswahili katika Biashara**

Pamekuwepo mjadala mpana sana kuhusu ujifunzaji wa Kiswahili katika mazingira ya darasa tangu enzi za ukoloni. Kiswahili kiliyumbishwa na viongozi wa jadi wakidhani Kiswahili kitafanya lugha za asili kupotea. Hata hivyo hoja hiyo ilikuwa tu Buganda (Ssekamwa, 2000) ila sehemu za magharibi hawakuona tatizo la Kiswahili kutumika kwani lugha za kibantu hujengana na kukuza msamiati wa kiisumu katika lugha tofauti za Kibantu (Muranga, 2018). Hata hivyo kwa wale ambao walipenda kujiunga na jeshi ama askariwalipenda sana kujifunza Kiswahili kwa sababu kiliwasaidia kupita mahojiano. Wakati

huo kulikuwa na Wahindi wengi ambao walikuwa wakitumia Kiswahili na waliwaajiri watu kutoka pembe tofauti za Uganda kuwasaidia kuendeleza biashara zao. Wahindi hawa waliendeleza biashara zao sehemu tofauti za Uganda ikiwemo Kampala, Jinja, Iganga, Soroti na kwingineko. Waajiriwa wa Wahindi walisafiri ama na waajiri wao au wao wenyewe kutafuta ajira Kenya ama Tanzania kwa sababu tayari walikuwa wamejifunza Kiswahili kwa kuingiliana na Wahindi.

Emma (2022) anasema kwamba nchini Uganda Wajasiriamali waliwasiliana na mashirika ya kibiashara ambayo yalianzisha mizizi ya biashara nchini Uganda. Emma (Keshatajwa) anaendelea kusema kwamba kufikia mwaka 1840 wafanyabiashara wa Zanzibar walikuwa wamefikia Ufalme huo wa Buganda kama sehemu ya upanuzi wa njia zao za biashara ya pembe za ndovu, dhahabu, viungo vya nafaka na watumwa. Zaidi ilianzisha bidhaa mpya, mavazi kama Kanzu na lugha ambazo zilikuwa Kiswahili na Kiarabu. Utafiti huu hauko mbali sana na namna shughuli za biashara ziliendelezwa nchini Uganda. Kinachochochaea fikra zetu ni je hawa wajasirimali na wafanyabiashara nchini Uganda hasa kwa ufalme wa Buganda ulioko mjini Kampala waliendeleza vipi mipango hii bila lugha. Kuna uwezekano mkubwa kwamba walitumia lugha ya Kiswahili katika mapatano yao.

Kwingineko (Ssekamwa 2000) anaendelea kusema kwamba mwaka wa 1972 uongozi wa Idi Amini Dada uliwatimu wahindi kutoka Uganda ili wanauganda wapate uhuru wao na kujiendeleza kiuchumi ambao ulimilikiwa na wahindi tangu 1962. Kuondoka kwa Wahindi kulifanya wanauganda wengi kuridhi biashara zao. Wakati huo Kenya ilikuwa na viwanda vingi kuliko nchi nyinginezo Afrika Mashariki na wafanyabiashara walikimbilia huko kununua bidhaa. Ilikuwa vigumu wafanyabiashara kushirikiana na wenzao kule Kenya bila kujifunza Kiswahili. Kwa mantiki hiyo mwelekeo ~~ha~~ dhidi ya Kiswahili ulianza kudidimia.

Kwa wale ambao wanajikuta wanakitumia, hufanya hivyo kulingana na mahitaji ya maisha. Mara nyingi walimu wamejikita katika kusisitiza ubora wa ufundishaji na mbinu za ufundishaji katika mazingira ya darasa badala ya kuhusisha pia namna mtu anaweza kujifunza Kiswahili nje ya darasa. Utofauti huu ndiyo ulichochea azma ya kuelezea jinsi wafanyabiashara huweza kutumia mikakati na mitindo ya kujifunza Kiswahili kama lugha ya biashara ambayo ni sehemu pana ambayo imefumbiwa macho na tafiti nyingi.

### **1.1.3 Uhusiano uliopo kati ya mikakati na mitindo ya ujifunzaji wa L.2**

Wanasaikolojia na wataalamu wa lugha ya pili kama kina Maclyntyre (1995); Lam (2010);

na Li (2021) wanasema kwamba kila mtu ana uhuru wa kutumia mikakati anuai wakati wa kujifunza lugha ya pili. Kuna wale ambao hutawaliwa na mikakati fulani halafu mingine wakaiacha. Hakuna mkondo mmoja wa jinsi ya kutumia mikakati hiyo. Matumizi ya mikakati mingi imekuwa ikitawaliwa na mwelekeo dhidi ya ujifunzaji hivi karibuni. Mitindo na mikakati ndivyo vielelezo mwafaka vinavyoamua ni jinsi au namna gani wanafunzi wa L2 ama lugha ya kigeni wanaweza kufanikisha ujifunzaji wa L2 (Oxford, 2003).

Ifahamike kwamba kuna tofauti kati ya mikakati na mitindo ya kujifunza lugha ya pili kutegemea kiwango cha madhumuni na malengo. Ehrman na Oxford (1989, 1990), wanasema kwamba kwa miaka mingi kumekuwepo makubaliano kwamba vipengele viwili yaani mitindo na mikakati ya ujifunzaji lugha ya pili kwa pamoja husaidia katika ujifunzaji wa lugha ya pili. Ehrman na Oxford (1989, 1990) walisisitiza kwamba vile vile husaidia katika ujifunzaji wa lugha ya kwanza. Mitindo huwa ni hulka mtu huwa nazo zisizoonekana ila kutumia hisi ambazo humsaidia katika ujifunzaji wa lugha ya pili. Mikakati kwa upande wake ni stadi zinazazoonekana na zinazoweza kumsaidia mwanafunzi kujifunza lugha ya pili. Mitindo ni ile hulka ya uvumilivu wakati wa kujifunza ambao unatofautisha mtu mmoja na mwingine wakati wa kujifunza lugha ya pili (Brown, 2007). Bialystok (2001) anaeleza kwamba baadhi ya mikakati inayotumiwa kujifunza lugha ni ya kijumla na inajitokeza kitabia. Walitoa mfano wa mtu anayeuliza maswali kila mara kwa nia ya kujifunza lugha kama mojawapo ya mtindo wa kujifunza lugha ambayo ni mpya kwake. Galloway na Labarca (1991) wanashadidia kuwa ujifunzaji wa lugha ya pili kwa kiwango kikubwa hutegemea tajriba aliyonayo anayejifunza kuhusu ujifunzaji wa lugha ya pili. Waliendelea kueleza kwamba motisha anayopewa na imani aliyonayo mjifunzaji wa lugha ya pili huchangia ufanisi wa ujifunzaji wake.

Kulingana na (TUKI 2007), dhana ya mikakati ni mbinu mahsus za kufanikisha kitu ama jambo ama kufanikisha ujumbe fulani. Mtaalamu wa L2 (Cohen 1996,1998) amefasili mikakati kama jinsi ya kuonyesha tabia ama stadi ambazo kwa makini zimeteuliwa na mjifunzaji wa lugha ya pili ili kumsaidia kujifunza lugha yoyote ile. Ni rahisi kufahamu mbinu zinazotumika tofauti na mikakati pale ambapo mitindo inadhihirika kihulka na kulingana na motisha ambayo anayejifunza lugha huwa nayo katika ujifunzaji wa lugha hiyo. Huenda Cohen alichanganya dhana hizi mbili kimuhtasari kuonyesha namna anaweza kuelekeza ujifunzaji wa lugha ya pili. Maelezo ya Bachman (1990), Oxford na Shearin (1994), Cohen, (1996) na Chamot (2005) kuhusu Mtindo ni kwamba, ni mchakato mahsus

ambao mjifunza L2 hutumia wakati wa kujifunza lugha lengwa. Tabia nayo huelekeza mjifunzaji wa lugha ya pili namna atakavyojipanga na kutumia mbinu mwafaka za ujifunzaji wa lugha ya pili. Mbinu zilizoshughulikiwa hapa huenda zinakaribiana na wala sio lazima ziwe sawa na mbinu za kawaida ambazo walimu hutumia wakati wa kufundisha bali ni mikakati ambayo inatumiwa na mjifunza lugha wakati wa kujifunza lugha ya pili.

Licha ya hiyo tofauti ndogo, Cohen (1998), alitumia *Style and Strategies Based Instruction* akronimu (SSBL) ambayo inahusisha uhusiano uliopo baina ya hizi dhana mbili wakati wa ujifunzaji wa lugha yoyote ile. Vipengele hivi viwili vinakamilishana kimotisha na kimaarifa katika ujifunzaji wa lugha ya pili (Reid, 1998). Ili ujifunzaji wa lugha ya pili ukamilike lazima kuwe na msukumo na mikakati ya kufanya mwanafunzi ajifunze lugha ya pili. Wale wanaojifunza lugha kutohana na mazingira mara nyingi huhamisha muundo wa L1. hadi L.2 ili kurahisisha mawasiliano. Uhamishaji huu unawapatia ari ya kujifunza lugha ya pili. Kulingana na maelezo ya Tarone na Yule (1989), utafiti huu unashadidia kwamba hakuna jinsi mjifunza lugha anaweza kujifunza lugha ya pili bila kuhusisha mikakati, mitindo na msingi wa L.2. Endapo mikakati inaegemea sana vipengele vya isimu na mawasiliano basi mtindo unaangazia msukumo alio nao mwanafunzi ili kujifunza lugha ya pili. Kuna uwezekano kwamba ari ndiyo ilikuwa msukumo mkubwa kwa wafanyabiashara kutumia mikakati ya kujifunza lugha ya pili ambayo iliwasaidia katika kujifunza Kiswahili kama lugha ya biashara.

Krashen (1976) alishughulikia mikakati ya kujifunza lugha ya pili ambayo alisema kwamba ujifunzaji wa lugha ya pili hutendeka kupitia miondoko. Griffths (2004) anadai kwamba Krashen (keshatajwa) alipotoka katika kauli yake na kudai kwamba mtu anaweza pia kujifunza lugha ya pili kupitia tabia alizo nazo. Kwamba lugha inaweza kufunzwa kama tabia na mwanafunzi akaamua namna ataendeleza ujifunzaji wake. Baadaye Krashen na Terrell (1983) waliibuka na njia tano za ujifunzaji lugha ya pili zikiwemo: upataji na ujifunzaji kupitia mawasiliano ya kawaida, mfumo halisi, ufuutilizi, kujifunza kupitia ufahamu na kupenda. Katika kupenda alisema kwamba hisia na mwelekeo wa mwanafunzi ndiyo humuwezesha kujifunza lugha ya pili. Ni bayana kwamba wazo la motisha na mwelekeo wa Habermas (1981) Dianne na Michael (1991) na Gardener (2000), linashadidia kwamba hakuna namna mikakati peke yake inaweza kujisimamia kufanikisha ujifunzaji wa lugha ya pili. Yote kwa pamoja hushirikiana ili mjifunzaji lugha awezeshwe katika mchakato mzima wa ujifunzaji wa lugha lengwa.

Oxford (1990) katika utafiti wake wa kuainisha mikakati ya ujifunzaji lugha ya pili alisema kwamba madhumuni ya mikakati ya ujifunzaji lugha ya pili ni kwa ajili ya kufanikisha uendelezaji wa umilisi wa mawasiliano. Aliainisha mikakati yake katika makundi makuu mawili yaani mikakati ilio wazi na ile ambayo si wazi. Katika ugawaji wake alisema kwamba mikakati ya ujuzi inasaidia ujifunzaji na mwanafunzi kupenda kile anachojifunza. Inajihuisha na hisia za mwanafunzi kama vile ukakamavu na mikakati ya mtagusano na ukuruba kati ya wanunuzi na wauzaji inatumiwa kujifunza lugha lengwa. Kundi la pili ni lile la mikakati ya ukuzaji wa ujifunzaji lugha lengwa. Mumo humo kuna mikakati ya utambuzi ambayo inamsaidia mwanafunzi kuhifadhi ujumbe. Uainishaji huu ulielekeza utafiti huu kubaini namna mikakati na mitindo hushirikiana katika ujifunzaji wa lugha ya pili. Gardener (2000) hachukulii dhana ya kupenda kama mkakati ila ni mtindo ambaa hujengeka katika misingi ya nia, motisha na jitihada. Mwanafunzi akiwa na jitihada za juu zitampa ari ya kutaka kujifunza lugha lengwa na kupenda kuitumia. Hapa ndipo Hajimia, Sigh, na Chethiyar (2020) wanasema kwamba ujifunzaji wa L2 hauwezi kufanikishwa na nadharia moja kama ya Krashen peke yake ila ujuzi wa nadharia hiyo pamoja na nadharia ambazo zimeshughulikia tabia za mjifunzaji kwa pamoja zinafanikisha ujifunzaji wa L.2. Utafiti huu ulibaini kwamba dhana ya mikakati na mitindo ni chanda na pete ambazo kwa pamoja zinawezesha ujifunzaji wa Kiswahili kwa wafanyabiashara mathalan wafanyabiashara wa jiji la Kampala.

## **1.2 Umuhimu wa kujifunza Kiswahili kama lugha ya biashara**

Ujifunzaji zaidi ya lugha moja husaidia kujenga uhusiano na mtagusano wa watu kutoka eneomoja na jingine. Kuna pia uwezo wa kujiimarisha na kujiendeleza kimaisha ili kukidhi mahitaji ya utandawazi. Ujifunzaji wa lugha zaidi ya moja huwezesha mawasiliano na utambulisho kwa watu wengi ambapo wanakuwa na uwezo wa kuomba kitu, kusihi, kuomba msamaha kuarifu, kutoa amri, kutoa ahadi na kukataa jambo fulani. Kwingineko kujifunza (Bosire 2002, Herman 2015) L.2 kunasaidia ukuzaji wa kuliwaza kati ya msemaji na msikilizaji kwa kutumia tamathali za usemi kama vile tanakali sauti, takrir, methali, mashairi, nyimbo, na tanzu nyingine zinazotekeleza matumizi ya lugha. Mchakato unaokuzwa kati ya msemaji na msikilizaji ni mawasiliano. Uendelezaji wa biashara umefanikishwa na vipengele vingi ambavyo vimetajwa hapo juu.

Larsen na Long (1991) wametoa sababu nyingi za kujifunza lugha ya pili. Wanasema kuna sehemu nyingi ambapo matumizi ya lugha ya pili huhitajika. Kwanza kabisa ujifunzaji wa

lugha ya pili unavutia na pia ni wa kipekee. Kuelewa kwake lazima uhusishe ufahamu wa kisaikolojia, isimu, sosholojia, anthropolojia, isimunafsia, isimu jamii na mengine mengi. Ni mambo mengi tunayoweza kujifunza ya kiakademia na mengi tunahitaji kuyafahamu kama si wakati huo lakini wakati mwingine baadaye maishani ilhali wale wamebobea kiakademia wamefanya hivyo kwa kujifunza lugha mbali mbali (David, 1997; 2010). Lugha ya kibiashara imejengeka katika misingi ya kisosholojia, kisaikolojia, isimujamii na inahusisha jamii ya kundi fulani kwa ajili ya shughuli fulani. Lugha ambayo walijifunza ni Kiswahili ambacho kiliwasaidia katika mchakato wa kufanikisha biashara.

Ujifunzaji wa lugha ya pili vile vile umesaidia kuchanganua maswala anuwai pale ambapo lugha awali haiwezi kuyachanganua kinaga ubaga na palipo na mahitaji mahsus. Tukiegemea mahitaji mahsus kwa wafanyabiashara ilikuwa ni matumizi ya Kiswahili kibiashara. Hakuna namna wauzaji wangewafafanunulia wanunuzi baadhi ya bidhaa katika lugha asili wakati wanunuzi hao hawaelewi lugha asili. Rosenberg (2008) anasema kuwa ni vigumu kushughulikia watoto wenyewe ulemavu ama upungufu wa kuzungumza ambao wako kwenye mazingira ambamo lugha mama siyo inayotumika inakuwa vigumu hivyo ni bora mwelekezi awe na umilisi wa lugha zaidi ya moja. Tukihusisha maoni ya (Lucy, 2014, Rosenberg, 2008) na shughuli ya biashara, kutokuwa na uwezo wa kutumia lugha ya Kiswahili katika biashara ni kama kuwa na ulemavu. Lugha ambayo inasaidia kufanikisha biashara ni matumizi ya lugha moja ambayo ni Kiswahili.

Fauka ya hayo Rosenberg (keshatajwa) anaendelea kusema kwamba elimu kutoka lugha nyingine na asasi zingine husaidia katika kutambua mila na desturi ya utamaduni wa lugha lengwa. Kuna biashara nyingi ambazo zinaendelezwu jijini Kampala. Kwa mfano kuna sehemu za mikahawa ambazo zinapika vyakula vya aina tofauti tofauti. Kwa wafanyabiashara wa mikahawa ya vyakula vya Kiswahili lazima wawe wamejifunza msamiati wa vyakula hivyo kutoka kwa wazungumzao Kiswahili ama wazawa wa lugha hiyo. Hivyo inakuwa ni mahitaji ili kuendeleza biashara zao.

Kwa mujibu wa Herman (2009), lugha ina mashiko katika maisha ya binadamu kwa awamu zote yaani, kuzaliwa, kukua, dini hata siasa katika ulimwengu mzima. Lugha husaidia kuwasilisha hisia zetu, matarajio na maswali anuwai katika dunia iliyotuzunguka. Maneno, ishara na toni hutumiwa kuwasilisha hisia za mtu. Upekee na ustadi ambao mwanadamu anaweza kutumia kuwasiliana ni kupitia maandishi au mazungumzo. Jambo hili linafanya

binadamu kuishi pamoja na kutegemeana ambapo inamtenganisha na kundi zima la wanyama. Maneno, ishara na toni vina mchango mkubwa katika kuendeleza mawasiliano kibiashara. Kiswahili kina toni shawishi inapofuatia maswala ya biashara. Mchakato wa kuendeleza biashara hutumia lugha shawishi ili kufanikisha biashara.

Herman (2009) anaendelea kusema kwamba, umuhimu wa kipengele cha stadi za mawasiliano umefumbiwa macho licha ya kuwa na uwezo wa kutekeleza mawasiliano. Kutoelewa na kufasiri vibaya maneno huwa ni jambo la kawaida. Mtu huwa na kiburi kuwa anaweza kusafiri ulimwengu mzima na kutarajia kila binadamu kuelewa lugha yake ya mama. Ili kuzuru ulimwengu, ama kwa biashara au starehe, ni muhimu kujifunza tamaduni mpya. Kukabiliana na hali hii, ni pamoja na uwezo wa kuwasiliana na watu katika lahaja tofauti tofauti. Anasema kutokuwa na uwezo wa kuwasiliana katika nchi ni kama kuishi na ulemavu ambao huwezi kutibika. Ni vigumu kuiga na kuzoeana na watu wapya kama hakuna mawasiliano baina yao. Maelezo ya Herman (Keshatajwa) yalilenga kuelekeza mtu na manufaa anayoweza kupata wakati wa kujifunza lugha na matumizi yake katika mawasiliano.

Shelly (2017) anasema mtu hawezi kupata maarifa mapya kutumia teknolojia na kujikita tu kwenye mawasiliano. Pia kujifunza L2 sio tu kujifunza sarufi na msamiati, ila ni kujifunza sauti mpya, kujieleza na jinsi ya kutatua mambo. Anaendelea kusema kwamba biashara nyingi hufanya kazi pamoja na makampuni mengi kutoka nchi nyingi. Kwa hivyo, huajiri watu tofauti ambao wanaweza kuwasiliana kwa lugha tofauti na kuelewa tamaduni nyingi. Unaposomea kozi yoyote ile na ujifunze L2 utakuwa na umuhimu zaidi kuliko yule aliye na umilisi wa L1 peke yake. Ameendelea kutoa mfano kwamba ukiwa na makanika anayejua Kirusi na Kijerumani na mkuu wa kampuni ajuaye Kijapani ama Kihispania, mhasibu ajuae Kifaransa na Kichina, atafanya kazi vizuri na watu wengi kuliko yule ambaye anajua lugha moja tu. Hii michango yote inajenga dhana ya umuhimu wa wafanyabiashara jijini Kampala kujifunza Kiswahili.

Whyte (2006) alitoa sababu nne kwa nini stadi za lugha zinakuwa na umuhimu katika kuendeleza biashara hasa biashara za kimataifa. Anasema kwamba kuzungumza zaidi ya lugha moja kunamsaidia mtu kupanua matarajio yake ya kazi, kupanua fursa na kushughulika kikamilifu katika biashara za kiulimwengu. Kuna wazo pia kwamba kuna fursa zingine mtu anaweza kupata ambazo zinajishughulisha na ujifunzaji wa lugha ya pili. Anasema kuna tafiti

ambazo ziliangalia maarifa na athari ya ujifunzaji uwili lugha ama lugha nyingi na matokeo mengine yanapendekeza kwamba uzungumzaji wa lugha nyingine unaweza kusaidia uendelezaji wa stadi za kibiashara. Kulingana na mwelekeo wake, ili mfanyakibashara aendeleze biashara kimataifa, kuna sababu nne muhimu kwake kujifunza zaidi ya lugha moja.

Kwanza, ni kufanya uamuzi thabiti; Anasema kwamba utafiti kutoka kwa wanasaikolojia kutoka Chuo Kikuu cha Chicago ulipendekeza kwamba watu wafanye uamuzi wa kimantiki wakati wa kutumia lugha ya pili. Kama ilivyoripotiwa na jamii ya wanasaikolojia wa Uingereza; walijiuliza kwa nini watu huwa wanakuza fikira, mawazo na busara katika lugha ya kigeni, walikubaliana kwamba ni dhana inayotokana na upana wa kisaikolojia. Utumiaji wa lugha ya kigeni hufanya mzungumzaji atumie mantiki kutiririka na wala si mihemuko wakati anafanya uamuzi.

Pili, kuendeleza mambo tofauti; Alisema kwamba utafiti wa hivi karibuni ulionyesha kwamba watoto wanaozungumza zaidi ya lugha moja wako na nafasi kubwa kutambua mwelekeo wa mtu mwingine kuliko wale walikuwa wakizungumza lugha moja. Hii inasaidia kuendeleza fikra na mwelekeo ambayo ni stadi muhimu katika kuendeleza biashara. Anasema hali kama hiyo inasaidia wafanyakibashara kushirikiana na kupatana vizuri na wanunuzi wao wakati wa kuendeleza biashara.

Tatu, ushirikiano thabiti; Stadi za lugha humkutanisha mzungumzaji na watu kutoka tamaduni tofauti na tabia zao. Kwa biashara za kimataifa ambazo hujishughulisha na wanunuzi, wahudumu na wafanyakazi kimataifa, wingilugha huziba pengo kati ya tamaduni tofauti na kuendeleza ushirikiano amba ni msingi bora unaojenga kuendeleza biashara. Kabla ya kuzingatia mataifa yaliyo nje ya Afrika, Kiswahili kinasaidia kufanikisha huduma za biashara Afrika Mashariki hasa jijini Kampala Uganda.

Nne, kujishughulisha; Hii ni hali ya mtu kufanya shughuli nyingi kwa wakati mmoja. Anasema kwamba utafiti uliofanyika chuo kikuu cha Pennsylvania ulionyesha kwamba watu walio na zaidi ya lugha moja huwa wana mambo mengi ya kufanya kwa wakati mmoja. Hivi kwamba mtu akiwa na zaidi ya lugha moja humfanya kuwa na maarifa mengi na kila wakati ubongo wake unafikiria cha kufanya. Uwezo wa kufanya mambo mengi unapewa thamana katika uendelezaji wa biashara pale ambapo usasa unafanya watu kubadilisha miradi na biashara kutegemea nini kinachopewa kipaumbele kwa wakati huo. Anaendelea kusema, maarifa ya biashara hufaidi wafanyakazi na waajiriwa lakini umuhimu wa lugha unakita

mizizi zaidi katika ulimwengu wa biashara. Kampuni ambazo asili ya wafanyakazi ni mataifa mbalimbali, muingiliano wa tamaduni na tabia kutoka lugha zao huathiri utendakazi na uzalishaji mali wa makampuni hayo. Hali hii hutokea pale ambapo maelewano katika mawasiliano baina ya wafanyakazi hayapo.

Whyte (keshatajwa) anaendelea kusema kwamba matumizi ya lugha moja hufanya watu kushirikiana na kubadilishana mawazo hivyo kupunguza machovu na watu kupata msukumo wa kuwawezesha kufanya kazi vizuri. Kwa kampuni ambazo wanunuzi wao ni wa kimataifa basi lazima kuwepo na matumizi ya lugha ya kuwaunganisha. Kampuni ambazo zina wafanyakazi amba wana zaidi ya lugha moja hupunguza gharama za kulipa watafsiri. Whyte (2006) anazidi kufafanua kwamba utafiti wa hivi karibuni juu ya ufundishaji wa Wajerumani na Waingereza ulibaini kwamba asilimia sabini na mbili walikubali kwamba kujifunza lugha ya pili kunakuza fursa na kupata faida ya mauzo yao. Wafanyakazi amba waliingiliana na kuzungumza na wanunuzi wao kwa lugha wanayoilewa ulijenga ushirikiano mkubwa wa kuendeleza biashara. Whyte (2006) aliendelea kusema kwamba kile ambacho kimefanya Uingereza isichangamkie sana maswala ya biashara za kimataifa ni kwa sababu ya kutowekeza katika elimu ya ujifunzaji wa lugha za kigeni. Utandawazi wa leo unahitaji matumizi zaidi ya lugha moja ili kusaidia kushirikiana katika biashara za kimataifa. Japo Kiswahili ni lugha inayofunzwa katika shule mbalimbali na taasisi za elimu ya juu nchini Uganda, kuna wale wajifunzao lugha hii kwa njia nyinginezo zisizo rasmi kama vile kupitia biashara. Licha ya hali kama hii kutokea nchini utafiti huu ulikuwa bayana kuchunguza mikakati, mitindo na changamoto zinazowakumba wanaojifunza lugha ya Kiswahili katika muktadha wa kibiashara.

### **1.3 Swala la Utafiti**

Kiswahili kama lugha ya pili nchini Uganda, kilianzishwa kwa ajili ya kuendeleza biashara na dini. Hata hivyo, ujifunzaji na matumizi yake hayajaendelezwa kwa kina. Aidha, unapokwenda katika maeneo ya biashara, utakuta Kiswahili kikitumika miongoni mwa wafanya biashara. Hali ya jinsi wanavyojifunza na kutumia Kiswahili kuendeleza biashara na changamoto wanazokumbana nazo katika matumizi ndilo pengo lililosughulikiwa katika utafiti huu. Matumizi haya yanatokana na kuwa mji mkuu wa Kampala ni mji wa biashara ambapo wafanya biashara kutoka maeneo mbalimbali ya kanda ya Afrika hujumuika kufanya biashara za kuuza na kununua bidhaa na huduma. Uanuwai huu wa wateja na wafanyakabiashara kutoka maeneo mengi kumewalazimu wafanyakabiashara mjini Kampala

kujifunza na kutumia Kiswahili kufanikisha biashara zao. Utafiti huu kwa hivyo ulichunguza mikakati na mitindo inayotumika na wafanyabiashara katika kujifunza na kutumia Kiswahili kibiashara. Mathalani, utafiti huu ulipambanua changamoto ambazo wafanya biashara hukumbana nazo katika harakati za ujifunzaji na matumizi ya Kiswahili kuendeleza biashara zao, jijini Kampala.

#### **1.4 Maswali ya Utafiti**

- i. Je, ni mikakati na mitindo ipi ambayo hutumiwa na wafanya biashara kujifunza Kiswahili kama lugha ya biashara jijini Kampala, Uganda?
- ii. Ni kwa jinsi gani mikakati na mitindo ya ujifunzaji lugha huwawezesha wafanya biashara kujifunza Kiswahili kama lugha ya biashara Jijini Kampala, Uganda?
- iii. Je, wafanya biashara hukumbwa na changamoto zipi wakati wa kujifunza Kiswahili kama lugha ya biashara jijini Kampala, Uganda?
- iv. Ni mikakati ipi inayoweza kutumika kutatua changamoto zinazowakabili wafanyabiashara ili kufanikisha ujifunzaji na matumizi ya Kiswahili kama lugha ya biashara?

#### **1.5 Madhumuni ya utafiti**

Lengo kuu lilikuwa kuchunguza mikakati na mitindo katika ujifunzaji wa Kiswahili kama lugha ya biashara mionganini mwa wafanyabiashara jijini Kampala, Uganda.

Madhumuni mahsusini ya utafiti huu ni;

- i. Kufafanua mikakati na mitindo inayotumiwa na wafanyabiashara kujifunza Kiswahili kama lugha ya biashara jijini Kampala, Uganda
- ii. Kutathmini jinsi mikakati na mitindo mbalimbali huwezesha wafanyabiashara kujifunza Kiswahili kama lugha ya biashara jijini Kampala, Uganda.
- iii. Kupambanua changamoto zinazowakumba wafanyabiashara kujifunza Kiswahili kama lugha ya biashara jijini Kampala, Uganda.
- iv. Kuchanganua mikakati ya namna ya kutatua changamoto zinazowakabidihi wafanyabiashara kufanikisha ujifunzaji na matumizi ya Kiswahili kibiashara.

## **1.6 Umuhimu wa Utafiti**

Uganda ni mionganini mwa nchi ambazo ufundishaji rasmi wa Kiswahili haujaanza chekechea hadi sekondari kama somo rasmi. Hivi karibuni ni katika kiwango cha shule za upili ambapo kuanzia sekondari ya chini Kiswahili kimefanywa somo la lazima halafu katika kiwango cha juu ni somo la hiari kwa wale wanaotaka kusoma somo hili. Ina maana kwamba vyuo na taasisi nyingine zinahitaji wataalamu ambao watafanya utafiti kuhusu maswala ya Kiswahili hasa katika ujifunzaji wake kwa utafiti wa sasa kama lugha ya mawasiliano kibiashara ama na vipengele vingine vya ujifunzaji wa lugha ya pili.

Utafiti utawasaidia wanaojifunza Kiswahili kama lugha ya pili na kuenzi Kiswahili kama lugha ya biashara. Vile vile mikakati na mitindo ya ujifunzaji Kiswahili itawezesha wanaojifunza Kiswahili kupata umilisi katika Kiswahili ili kurahisisha mawasiliano kama lugha ya biashara na vilevile lugha ya kuendesha shughuli nyinginezo. Matokeo ya utafiti yalibainisha changamoto zinazotokana na kujifunza Kiswahili kama lugha ya biashara na namna ya kuzitatua. Aidha, matokeo ya kutatua hizo changamoto yatawasaidia wajifunzaji lugha kibiashara kuona namna ya kukabiliana ama kuepukana na changamoto hizo wakati wa kujifunza Kiswahili kibiashara. Matokeo ya utafiti yatatumiwa kama makala ya kuhakiki na kurejelewa na watafiti wengine ambao watafanya utafiti katika eneo la kiakademia ambalo litafanana au ambalo litakaribiana na hili. Pia utafiti unawaongezea maarifa kuhusu nafasi ya Kiswahili katika nyanja mbalimbali kama vile biashara. Aidha, utafiti huu utachangia uimarisaji wa Kiswahili katika Jumuiya ya Afrika Mashariki.

## **1.7 Upeo wa Utafiti**

Utafiti ulishughulikia mikakati na mtindo inayowezesha ujifunzaji wa Kiswahili kama lugha ya biashara. Aidha, changamoto za ujifunzaji wa Kiswahili kama lugha ya biashara na namna ya kukabiliana nazo zilishughulikiwa. Utafiti huu upo katika taaluma ya isimu ya ujifunzaji na ufundishaji wa lugha ya pili na isimujamii. Utafiti huu ulifanyika jijini Kampala, Uganda. Kampala ilichaguliwa kwa sababu ni eneo ambalo lina biashara nyingi na maduka makubwa mengi pamoja na wafanyabiashara wengi wanaotoka nje ya Kampala na mataifa jirani yanayotumia Kiswahili kama lugha ya kibiashara. Utafiti huu ulichagua Ekedi mbili za Ekedi ya Mukwano na Simlaw Uganda Limited na Soko moja la Kikuubo. Masoko haya yalichaguliwa kutopteka na umaarufu wake, ukubwa, bidhaa na huduma zinazopatikana katika maeneo haya na uanuwai wa wafanyabiashara wanaofika na wanaofanya biashara katika eneo hili. Mihimili ya nadharia mbili yaani nadharia ya ufuatilizi ya Stephen

Krashen (1987) na nadharia ya Richard Gardner (2000) ilitumiwa katika kuongoza utafiti huu kwa kueleza mikakati na mitindo ya kujifunza Kiswahili kama lugha ya biashara na changamoto zinazokumba ujifunzaji wa Kiswahili kama lugha ya biashara. Watafitiwa walengwa katika utafiti huu ni wafanyabiashara wanaofanyia shughuli zao katika Ekedo ya Mukwano na Simlaw Uganda Limited na Soko moja la Kikuubo. Wafanyibiashara hawa walichaguliwa kwa sababu wao ndio wanaohusika na shughuli za ununuzi na uuzaji wa bidhaa na huduma. Aidha, ni wafanya biashara hawa wanaotangamana miongoni mwao pamoja na wateja wanaotoka maeneo mbalimbali ya nchi na ujirani wa nchi. Ni wao wanaochagua lugha ya kutumia katika biashara na athari zinazotokana na matumizi hayo huwakumba wao. Mikakati na mitindo ya kujifunza na kutumia lugha ya Kiswahili kibbiashara pamoja na changamoto za ujifunzaji wa Kiswahili kama lugha ya biashara hutokana na utangamano wao na wateja wanaotumia Kiswahili.

## **1.8 Kiunzi cha nadharia**

Utafiti uliongozwa na nadharia mbili. Yaani, nadharia ya ufuutilizi ya Stephen Krashen, (1987) na nadharia ya motisha ya kujifunza lugha ya pili ya (Robert C. Gardner, (2000). Nadharia zote mbili zilijengana katika kukamilisha utafiti. Nadharia ya Gardner imehusishwa kwa vile mihimili ya nadharia ya Krashen haikushughulikia baadhi ya vipengele vya kisaikolojia kama ari, motisha na jitihada za kujifunza lugha ya pili, mielekeo chanya ya lugha anayojifunza mtu. Licha ya kuwa na mifumo na michakato mwafaka ya ujifunzaji lugha ya pili, mwelekeo na motisha huchangia pakubwa katika uthibitishaji wa kijifunza lugha ya pili. Matumizi ya Kiswahili nchini Uganda yana historia pana sana hivyo ni bayana kuelekeza mwelekeo kuntu wa kumfanya mtu kujifunza Kiswahili hasa kama lugha ya biashara.

### **1.8.1 Nadharia ya Ufuutilizi**

Hii ni nadharia ambayo iliasisiwa na Stephen Krashen (1981) na kuiendeleza (1987) ambapo alieleza kwa kina dhana ya ujifunzaji wa lugha ya pili (L2). Wataalamu wengi wamebainisha majina mengi kuhusu nadharia hii kama vile nadharia fuutilizi ya Krashen, Nadharia ya Krashen, kielelezo cha Krashen, nadharia elekezi, Kiunzi cha Krashen ama Nadharia ya Dhana mpya. Majina haya yalitokana na ukosefu wa tafsiri sanifu (Katrina, 2004).

Krashen ya ufuutilizi inasema kuwa ujifunzaji lugha ni mfumo wa ufahima ambapo mjifunzaji lugha hujua anajifunza lugha ya pili na kupitia mfumo huo huo uelewa wa lugha

hujengeka katika akili ya mjifunzaji kwa kuisoma ama kufundishwa lugha hiyo na watu wengine. Nadharia ya Krashen ya ufuatilizi ina viwango vitano vyta mihimili vifuatavyo: nadharia tete ya upataji – ujifunzaji lugha, nadharia tete ya mfumo asili, nadharia tete ya ufuatiliaji, nadharia tete ya dhana mpya, na nadharia tete ya kichungi athari.

Nadharia tete ya upataji - ujifunzaji ni ya msingi kwa nadharia tete zote katika nadharia ya Krashen. Mfumo wa upataji ni mchakato ulio akilini ambao unaendeleza umilisi wa kiisumu kutokana na utumiaji wa lugha katika mawasiliano na ni sawa na mchakato wa watoto wakati wanapojojanza lugha ya kwanza. Katika hali hii ujifunzaji unakamilika pale ambapo mjifunzaji lugha ya pili anaewala kile ambacho kinawasilishwa katika lugha ya pili. Kinachohitajika ni mawasiliano yenye maana ya lugha lengwa bali si mfumo wa matamshi yao, lakini kitendo cha mawasiliano. Mfumo wa kujifunza au “ujifunzaji” ni mchakato usiofichama akilini na elimu iliyofikiwa kuitia upataji na usomaji huhifadhiwa tofauti. Elimu iliyofikiwa kwa kusoma haiwezi kubadilishwa kuwa sawa na iliyofikiwa kwa upataji. Mfumo wa kujifunza unajumuisha mchakato ambao matokeo yake ni katika maarifa fahamu “kuhusu” lugha, kwa mfano elimu ya sheria ya sarufi.

Kulingana na Krashen “kujifunza” ni kiwango cha chini kuliko “upataji.” Nadharia tete ya mpangilio wa kimaumbile, inaelezea uhusiano kati ya upataji na ujifunzaji na amefafanua athari ya ujifunzaji kwa upataji. Kazi ya ufuatiliaji ni matokeo ya sarufi iliyofunzwa. Kulingana na Krashen, mfumo wa ujifunzaji, hufuatilia vitendo katika mipango, na kusahihisha kazi ya ujifunzaji. Miundo ya sarufi inaweza kutabiriwa. Anasema ni sawa kwa watu wazima na watoto wadogo na wajifunzaji mbalimbali wa lugha ya pili. Inaonekana kwamba jukumu la kujifunza ni kusahihisha. Ni hali ambapo mjifunzaji wa lugha ya pili anajifunza sheria zote za lugha ya pili na kuwa na uwezo wa kusahihisha makosa yanayoibuka wakati wa kujifunza. Mhimili huu uliongoza kuchanganua data ilioeleza mikakati na mitindo ambayo hutumiwa na wafanyabiashara bila kufahamu wakati wa kujifunza Kiswahili kama lugha ya kibiashara.

Nadharia tete ya mfumo asili hueleza kuwa mtoto hupata sheria za lugha kwa mfumo maalum wa kiasili ambao unatabirika sarufi sahihi hadi sarufi tata. Mfumo huu asili wa upataji lughani sawa sawa kwa watoto wote wanaojifunza L1 na L2. Mfumo huu hurejelewa kama mfumo wa umilisi mkuzi. Mfumo huu huelezwa kama ifuatavyo; Ujifunzaji huanza na muundo wa maswali ya neno moja moja: nini? Wapi? Matumizi ya viunganishi kwa

mfano: we bado sabua pesa? Matumizi ya njeo-wakati uliopo, ujao na uliopita, matumizi ya vimilikishi kama vile changu, chako, chake; Matumizi ya vivumishi kama vile nyeupe, nzuri, na chafu.

Krashen anasema mpataji L1 na mjifunzaji L2 hupata sheria za lugha kuitia hatua ama daraja tano zilizoorodheshwa hapo juu kwa mfuatano huo huo. Hii inamaanisha mtoto akiwa katika daraja la tatu anaweza kutabiri sheria anazojifunza na pia kutabiri sheria atakazozipata atakapofika daraja au hatua ya tano. Wafanyabiashara huenda wamepita kiwango cha utoto lakini wana uwezo wa kubainisha sheria za umilisi mkuzi kwa kubahatisha. Katika mawasiliano ya kibiashara lazima kuwepo kuuliza maswali na kujibiwa vivyo hivyo viunganishi kutumiwa na vipengele vingine vya lugha bila kufuatilia mfumo rasmi wa darasa. Huu mfumo wa umilisi mkuzi ulisaidia kuchanganua jinsi mikakati na mitindo ya ujifunzaji lugha ya pili unavyowezesha upataji/ujifunzaji wa Kiswahili kama lugha ya kibiashara.

Nadharia tete ya ufuutiliaji imejikita katika matokeo ya utafiti wa Dulay na Burt (1973), Fathman (1975), katika Krashen (1987) ambayo yalipendekeza kuwa upataji wa muundo wa sarufi ni wa kutabirika. Anasema elimu iliyopatikana kuitia kusoma inaweza kutumika kuyafanya matamshi tahariri ambayo ilizalishwa kutokana na njia ya ujifunzaji. Pale ambapo sheria au msisitizo juu ya muundo unapokuwepo ndipo ufuutiliaji wa lugha unaweza kutokea na hufanya kazi pale ambapo hakuna sheria ngumu. Ikumbukwe kwamba mjifunza lugha anapopata lugha ya pili, hukumbana na matatizo mengi ya sheria za muundo wa L2. Mara nyingi matatizo haya huibuka kama makosa kwa sababu huenda yametokana na athari ya lugha mama kwa kutojua. Vinginevyo hata kama makosa haya hujitokeza, athari yake huwa ni msingi bora wa kujifunza lugha ya pili. Mhilimi huu haukushughulishwa sana na utafiti huu kwa sababu utafiti ulikuwa hauangalii makosa yanayojitokeza wakati wa kujifunza L2 na kuyarekebisha kama njia moja ya ufuutilizi ila tuliangalia mjifunzaji anafanikiwa vipi kufahamiana na lugha anayojifunza ambayo ni Kiswahili.

Nadharia tete ya dhana mpya, huelezea namna ya upataji lugha unavyotokea. Wanafunzi wanapopewa pembejeo zenye sifa za kisarufi zilizo zaidi ya kiwango kidogo huwa na uwezo wa kupata sifa hizo. Krashen anasisitiza kuwa upataji ni matokeo ya pembejeo zinazoleweka na sio zile zinazozalishwa. Pembejeo hufanya kueleweka kwa msaada uliotegemea muktadha. Krashen anasisitiza pembejeo ziwe ni zenye kueleweka. Kwa muktadha wa utafiti huu, haukulenga wanafunzi ambao walijifunza lugha ya Kiswahili


darasani ili kupewa pembejeo zenyе sifa za kisarufi. Ulilenga wajifunzaji lugha ambao ni wafanyabiashara ambao katika ujifunzaji wao, walihitaji mfumo ambao utawasaidia kutumia Kiswahili kwa mawasiliano ya biashara tu. Kwa hivyo mhimili huu ulisaidia kuelekeza madhumuni ya pili. Mhimili huu ulisaidia kukusanya data ambayo ilihuksiana na jinsi wafanya bishara hutumia mitindo na mikakati ya kujifunza lugha ya pili katika ujifunzaji wa Kiswahili kibiashara. Kwao ilikuwa ni namna wanaweza kuboresha mawasiliano yao kutumia Kiswahili wakati wanawasiliana kwenye mazingira ambayo Kiswahili kilihitaji kutumika.

Nadharia tete kichujio athari/ingizi, huhusiana na vibadiliki vya kimwelekeo ambavyo huathiri upataji. Wanafunzi wenyе mielekeo mizuri huathirika kidogo na kichujio athari. Hii ina maana kwamba huwa wanajaribu kupata pembejeo nyingi zaidi na kuzipokea kwa wepesi. Uingizi huthibiti kiwango na kiasi cha mafanikio ya upataji lugha. Anaendelea kwa kusema, ujifunzaji lugha hasa hutekelezeka pale ambapo, mjifunzaji anapata fursa ya kupata dhana mpya ambazo ziko juu kidogo ya zile ambazo anazijua tayari (L1+1), mjifunzaji anazielewa na kuwa na welewa mkubwa na dhana hizo mpya anazofundishwa. Katika mchakato mzima wa mawasiliano lazima mjifunzaji lugha atakutana na changamoto za uhamishaji sheria za lugha mama na kuziweka kwenye lugha ya pili. Uhamishaji huo huenda utamsaidia kujifunza L2 ama utakuwa ni changamoto wakati wa kujifunza Kiswahili kama lugha ya kibiashara. Kutokana na utafiti, ilibainika kwamba wajifunzaji wa Kiswahili kibiashara hukumbana na changamoto nyingi sana pale ambapo wanataka kwa haraka kuhamisha sheria za lugha zao za kwanza na kuziweka katika lugha ya pili ambayo ni Kiswahili hasa kwenye mawasiliano ya kibiashara.

### **1.8.2 Nadharia ya Motisha ya Ujifunzaji Lugha ya Pili**

Nadharia ya motisha iliibuka mwaka wa 1950 mwasisi wake akiwa mwanasaikolojia Fredrick Herzberg. Baadaye wanasaikolojia mbalimbali waliibuka na modeli mbalimbali ikiwemo Modeli ya Elimu ya Gardner (1985) ambayo iliendelezwa (2000) kama modeli ya saikolojia ya jamii. Kwa jumla ni sehemu pana ya Nadharia ya Motisha ya Ujifunzaji iliyoshirikiana na nadharia ya Krashen ili kukamilisha malengo ya utafiti huu. Modeli hii inachukulia kuwa ujifunzaji wa L2 ni mchakato unaohusisha mambo mengi yaliyo ndani ya mjifunzaji na mengine yakiwa nje ya mjifunzaji. Kiini cha mafanikio katika kujifunza L2 ni motisha alionao mjifunzaji wa lugha husika. Gardner (keshatajwa) anabainisha kuwa, motisha katika ujifunzaji wa L2 ni mchanganyiko wa jitihada, nia/ari, motisha changamani

na uwezo wa kutaka kufanikiwa katika malengo pamoja na mwelekeo chanya dhidi ya lugha unayojifunza (Gardner, 1985). Modeli ya Elimu ya 1985 inaegemea sana motisha mwanafunzi huwa nao katika mazingira rasmi ya ujifunzaji. Modeli hii iliboreshw na Gardner (2000) ili kukidhi mahitaji ya mjifunzaji ambaye hayuko katika mfumo rasmi. Wazo hili lilichukuliwa kwa uzito mkubwa katika utafiti huu kwa sababu wengi waliohusishwa hawakupitia mfumo rasmi wa kujifunza Kiswahili darasani. Wajifunzaji wa Kiswahili nchini Uganda amba ni wafanyabiashara jijini Kampala kama lugha ya kibiashara wana motisha na mwelekeo upi dhidi ya matumizi ya Kiswahili kimawasiliano na kufanikisha matumizi yake katika kuendeleza biashara. Mchoro 1.1 unaonyesha utendakazi wa modeli ya saikolojia ya jamii katika kufanikisha ujifunzaji wa L.2.



**Mchoro 1.1: Modeli ya saikolojia ya jamii (Gardner, 2000)**

Gardener na Trembly (1994) wanasema kwamba motisha wa L2 hutofautiana na michakato mingine ya ujifunzaji lugha. Wanaendelea kusema kwamba motisha wa kujifunza lugha umefungamanishwa katika modeli ya elimu. Hata hivyo kulingana na uchangamano wake ndiyo sababu ya kuibua modeli ya saikolojia ya jamii (2000). Gardner (2010) anasema kwamba kuna vipengele vitatu ambavyo awali havikufafanuliwa katika modeli ya elimu ndiyo sababu ya kuboresha na kuongeza modeli ya saikolojia ya jamii katika modeli kuu ya elimu ambayo ni sehemu pana ya nadharia ya motisha. Vipengele hivyo ni jitihada, uvumilivu na kumakinika. Kwa hivyo katika kufasili motisha. Hivi vipengele ndivyo vinaelekeza mwelekeo juu ya lugha, motisha na mafanikio katika lugha.

Gardener (2010) ameeleza kwamba katika muktadha wa ujifunzaji lugha, motisha ya mtu binafsi huhusishwa na vigeugeu vitatu ambavyo ni ujumuishaji, mwelekeo kuhusu muktadha wa kujifunza na mwelekeo kuhusu lugha. Ujumuishaji unasaidia mjifunzaji lugha ya pili kukubali kuwa mwanajamii wa jumuiya fulani na kukubali utamaduni wao. Mwelekeo vile vile husaidia mjifunzaji lugha ya pili kujifunza lugha ya pili kwa ajili ya matumizi ya lugha hiyo. Anaendelea kusema kwamba mwelekeo kuhusu muktadha wa kujifunza na ujumuishaji hufanya wanafunzi wakawa na motisha chanya juu ya ujifuzaji wa lugha ya pili. Haya yote yanakamilika pale ambapo mjifunzaji lugha ya pili anaonyesha uwezo wa kujifunza na kuonyesha jitihada za ujifunzaji. Kwa hiyo anaweka msimamo katika mhimili ifuatayo; yaanijitihada za kujifunza lugha, nia/ari ya kujifunza, motisha changamani, uwezo wa kutaka kufanikiwa, na mwelekeo chanya.

Motisha hufanya mtu kutenda kitu ambacho anakipenda. Mhimili mitano ambayo Gardener anaangazia ilikuwa muhimu sana katika kufanikisha malengo ya utafiti huu. Kujifunza lugha yoyote ile kunahitaji jitihada. Mhimili wa kwanza ni jitihada. Pili, ni nia/ari pamoja na mhimili wa nadharia tete ya upataji-ujifunzaji wa lugha ulisaidia katika kushughulikia madhumuni ya kwanza ambayo ilichanganua mikakati na mitindo ya kujifunza Kiswahili kama lugha ya kibashara. Krashen anasema kwamba nadharia ya upataji/ujifunzaji lugha ni mchakato ulio akilini ambao unaendeleza umilisi wa kiisimu. Hoja hii iliwekewa mkazo na mhimili wa Gardener wa jitihada. Hata kama binadamu ana uwezo wa kuendeleza umilisi wa kiisimu, ni bayana kwamba jitihada na ari/nia ni muhimu katika ujenzi wa umilisi huo. Kwa mtu ye yote kujifunza L2 anahitaji kuwa na jitihada ili afanikiwe kujifunza lugha hiyo.

Aidha Gardener (2000) anadai kwamba ili mtu kujifunza lugha ya pili lazima awe na motisha changamani itakayomfanya kufanikiwa katika malengo yake. Utafiti huu unakisia kwamba kufanikiwa katika biashara ndiyo moja wapo wa malengo ya wafanyabiashara wa jiji la Kampala Uganda. Hivyo walipata msukumo wa motisha changamani kuona kwamba wanajifunza Kiswahili ili kuendeleza biashara zao vyema. Mtu hufanya na kutenda kutegemea ari aliyonayo kwa wakati huo. Mtu kama hana nia ya kujifunza lugha nyingine basi inakuwa vigumu kujifunza lugha hiyo. Licha ya kuwa na mfumo halisi na njia za upataji wa dhana mpya, ni bora kuwa na nia ya kupokea dhana mpya. Ilikuwa bayana kuhusisha dhana ya nia na upataji dhana mpya. Vile vile Mhimili wa pili yaani nia/ari, motisha changamani pamoja na mhimili wa nne wa uwezo wa kutaka kufanikiwa pamoja na mhimili wa pili na wa nne wa Krashen ulifanikisha madhumuni ya pili ya utafiti ambayo

yalishughulikia jinsi mikakati na mitindo mbalimbali huwezesha kujifunza Kiswahili kama lugha ya biashara.

Ujifunzaji wa lugha ya pili una changamoto zake. Gardener, (2010) katika module yake anaelezea ya kwamba mjifunzaji lugha hujaribu kujifunza lugha ya pili pamoja na kujizoesha na utamaduni wake. Kwa kuzingatia mwelekeo huu huenda kujifunza lugha kuwe chanya au hasi. Kwa mjifunzaji lugha ambaye ana mwelekeo hasi hukumbana na changamoto nyingi kulingana na mazingira ambamo anajifunzia hiyo lugha. Mwelekeo hasi juu ya ujifunzaji wa Kiswahili ulichangia sana katika ujifunzaji wa Kiswahili nchini Uganda katika mfumo ulio rasmi na usiorasmi. Ili mtu kujifunza dhana mpya anastahili kuwa na mwelekeo chanya juu ya lugha ambayo anajifunza. Mhimili wa tatu, nne na tano wa Gardener pamoja na mhimili wa nne na tano wa Krashen kuhusu mielekeo ya ujifunzaji Kiswahili kibiashara ulisaidia katika kufanikisha madhumuni ya tatu. Yaani kubainisha changamoto zinazotokana na ujifunzaji wa Kiswahili kama lugha ya kibiashara na jinsi ya kukabiliana na changamoto hizo.

### **1.8.3 Mihimili ya nadharia**

Utafiti huu uliongozwa na mihimili minne ya nadharia ya Stephen Krashen (1987) na mihimili mitano ya Richard Gardener (2000). Mihimili hii imefafanuliwa kama ifuatavyo:

#### **1.8.3.1 Nadharia ya Stephen Krashen (1987)**

Nadharia hii ina majina mengi kama vile; nadharia fuatilizi ya Krashen, Nadharia ya Krashen, kielelezo cha Krashen, nadharia elekezi, Kiunzi cha Krashen ama Nadharia ya Dhana mpya. Majina haya yalitokana na ukosefu wa tafsiri sanifu kama ilivyofafanuliwa na Katrina, (2004). Nadharia hii ina mihimili ifuatayo:

- i. Nadharia tete ya upataji-ujifunzaji huhusisha hatua 5
- ii. Nadharia tete ya mfumo asili –Mjifunzaji hupata sheria za lugha kwa mfumo
- iii. Nadharia tete ya ufuatiliaji. Mhimili huu haukutumika katika utafiti huu
- iv. Nadharia tete ya dhana mpya-Wanafunzi wanapata pembejeo zenyenye sifa za kisarufi zilizo zaidi
- v. Nadharia tete kichujio athari - hudhibiti kiwango na kiasi cha mafanikio ya upataji lugha. Mjifunzaji anapata fursa ya kupata dhana mpya.

### **1.8.3.2 Nadharia ya motisha ya ujifunzaji lugha ya Richard Gardener (2000)**

Nadharia ya motisha iliibuka mwaka wa 1950 mwasihi wake akiwa mwanasaikolojia Fredrick Herzberg. Kuanzia hapo wanasaikolojia mbalimbali waliibuka na modeli mbalimbali mukiwemo Modeli ya Elimu ya Richard.C. Gardner (1985) ambayo iliendelezwa (2000) kama modeli ya saikolojia ya jamii. Utafiti huu ulitumia nadharia ya Richard Gardener (2000) ikiongozwa na mihimili ifuatayo:

- (i) Mchanganyiko wa jitihada - jitihada, uvumilivu na kumakinika
- (ii) Nia/ari - ni muhimu katika ujenzi wa kujifunza lugha
- (iii) Motisha changamani – chaya ama hasi huathiri ujifunzaji wa lugha ya pili.
- (iv) Uwezo wa kufanikiwa – hutokana na motisha aliyo nayo mjifunzaji lugha.
- (v) Mwelekeo chanya dhidi ya lugha unayojifunza - motisha ya mtu binafsi huhusishwa na vigeugeu vitatu ambavyo ni ujumuishaji, mwelekeo kuhusu muktadha wa kujifunza na mwelekeo kuhusu lugha.

### **1.9 Namna nadharia zilivyotumika katika utafiti**

Mhimili wa kwanza wa Krashen wa upataji na ujifunzaji lugha na ule wa kwanza jitihada na wa pili nia wa Gardener iliongoza madhumuni ya kwanza ya kuchanganua mikakati na mitindo ya kujifunza Kiswahili kama lugha ya kibiashara. Mhimili wa pili na wa nne wa Krashen pamoja na mhimili wa 2, 3, 4 yaani nia, motisha changamani na uwezo wa kufanikiwa ilichanganua madhumuni ya pili ya kutathmini jinsi mikakati na mitindo mbalimbali huwezesha kujifunza Kiswahili kama lugha ya biashara jijini Kampala. Mhimili wa nne na tano wa Krashen yaani nadharia tete ya dhana mpya na nadharia tete ingizi na, Mhimili wa 3, 4, 5 yaani; motisha changamani, uwezo wa kufanikiwa na mwelekeo ya Gardener ilisaidia kuchanganua madhumuni ya tatu ambayo ni kubainisha changamoto za ujifunzaji Kiswahili kama lugha ya biashara na jinsi ya kukabiliana nazo. Hivyo kwa jumla nadharia ya Krashen na Gardener zilifanikisha ukusanyaji na uchanganuzi wa data kwa kujibu maswali ya utafiti, kuelekeza uhusiano uliopo kati ya yaliyoandikwa kuhusu mada na matokeo ya utafiti

### **1.10 Hitimisho**

Sura hii ilishughulikia usuli wa utafiti, historia ya Kiswahili nchini Uganda, matumizi ya Kiswahili katika biashara, na uhusiano uliopo kati ya mikakati na mitindo ya ujifunzaji wa lugha ya pili kuthibiti namna kwa pamoja yaliwezesha ujifunzaji wa Kiswahili kwa wafanyabiashara jijini Kampala na umuhimu wa kujifunza Kiswahili kama lugha ya biashara.

Katika sura hii sababu za kujifunza Kiswahili ziliangaziwa kwa kuhusisha maandishi mbalimbali na haja ya kuendeleza biashara kutumia lugha ya Kiswahili. Swala la utafiti lilihughulikiwa kikamilifu pamoja na maswali ya utafiti na madhumuni ya utafiti. Upeo wa utafiti uliangaziwa yaani Ekedi ya Mukwano, Simlaw Uganda Limited na soko la Kikuubo na kutoa sababu kwa nini maeneo hayo yalichaguliwa kwa ajili ya utafiti huu. Nadharia mbili kwa ajili ya utafiti zilihusishwa mukiwemo nadharia ya ufuatilizi ya (Stephen Krashen, 1978) na modeli ya saikolojia ya jamii ambayo iliingiza vipengele vingine katika modeli ya elimu (Gardener, 2000) ambayo ni sehemu pana ya nadharia ya motisha ya (Gardener, 2000). Sababu ya kutumia nadharia mbili ilikuwa kwamba hakuna nadharia moja ambayo ingetosha kushughulikia mikakati na mitindo ya ujifunzaji wa Kiswahili kama lugha ya kibiashara kwa wafanyabiashara. Hivyo katika kusaidiana mhimili wa kwanza wa Krashen na mhimili wa kwanza wa Gardener ulisaidia kuelekeza madhumuni ya kwanza, Mhimili ya pili na nne ya Krashen na mhimili wa pili, tatu na nne wa Gardener ilielekeza madhumuni ya pili halafu mhimili wa nne na tano wa krashen pamoja na mhimili wa tatu, nne, tano wa Gardener (keshatajwa) ilielekeza madhumuni ya tatu. Mhimili wa tatu wa Krasheni haukushirikishwa sana katika utafiti huu kwani ulilenga zaidi kudhibiti sheria za ujifunzaji wa lugha ya pili katika mfumo rasmi wa darasani. Kwa jumla utafiti ulionyesha namna nadharia hizo mbili zilivyosaidia kuelekeza mada ya utafiti, mapitio ya maandishi, mbinu na vifaa vya kukusanya data na uchanganuzi wa data.

## **SURA YA PILI**

### **TAHAKIKI YA MAANDISHI**

#### **2.1 Utangulizi**

Sura hii kimsingi ilishughulikia yaliyoandikwa yenyewe uhusiano kuhusu mikakati, mitindo na changamoto za kujifunza Kiswahili kama lugha ya biashara mionganini mwa wafanyabiashara jijini Kampala-Uganda. Tahakiki ya maandishi yalielekezwa na madhumuni ya utafiti, yanayoshadidia ama kuwacha pengo kulingana na mada na nadharia zilizotumiwa kuendelezautafiti.

#### **2.2 Mikakati na mitindo ya ujifunzaji lugha ya pili**

Sehemu hii ya tahakiki ya maandishi ilishughulikia ufanuzi wa mikakati na mitindo ya ujifunzaji lugha ya pili ambayo ilikuwa pana mno kwa sababu inahusisha vipengele viwili ambavyo kila kimojawapo ni kipana. Hali hii inafanya lugha ya Kiswahili kuwa kama lugha ya pili kwa wafanyabiashara. Hivyo tuliona ni bora kuigawa sehemu hii katika makundi mawili kama ifuatavyo;

#### **2.2.1 Mikakati ya jumla ya ujifunzaji lugha ya pili**

Faerch na Kasper (1980) na Brett (2000) wanasema kwamba, mikakati ni mbinu zinazotumiwa na wanaojifunza lugha ya pili na hata wazaliwa wa lugha hiyo ili kuviepuka vikwazo vya mawasiliano. Vikwazo hivyo vyaweza kuwa vya kimatamshi, kisarufi na kimsamiati. Faerch na Kasper (keshatajwa) wameainisha mikakati ya kufanikisha mawasiliano na mikakati ya kukuza mawasiliano. Mikakati ya kufanikisha mawasiliano inaweza kuwa ya kushirikiana au ya kutoshirikiana na wasikilizaji. Mikakati ya kushirikiana hutumiwa pale ambapo anayejifunza lugha ya pili hujaribu kukabiliana na vikwazo vinavyomkumba kwa kuomba msaada kutoka kwa wasikilizaji wake. Mionganini mwa mikakati tajwa ni kama kuomba msaada waziwazi, kuomba msaada kisiri siri, kuchanganya na kubadilisha msimbo.

Katika kuomba msaada waziwazi, wanasema mzungumzaji wa lugha ya pili anaweza kukwama kisha akawaomba wasikilizaji wake wamsaidie kutamka au kukumbuka neno linalomaanisha kitu fulani anachozungumza, kwa mfano anaweza kuwa uliza ‘Mtu anayewazalisha wanawake huitwaje’- Mkunga. Mkakati huu hupendwa sana na watu wasio wanyamavu, wasioona aibu wala soni kuuliza jambo wasilolijua. Ni mkakati unaoweza kuwasaidia wanaojifunza lugha ya pili kujifunza mengi kutoka kwa wenzao. Maelezo haya

yalisaidia sana utafiti huu kwani ni nadra sana kupata mfanyabiashara ambaye ni mnyamavu. Ili kufanikisha mawasiliano mfanyabiashara hutumia maneno mengi ili kumshawishi mnunuzi kununua bidhaa zake. Endapo atasahau neno mwafaka basi atafanya bidii ya kuomba msaada kwa mtu mwingine ili kufanikisha mawasiliano.

Wakati wa kuomba msaada mjifunzaji lugha ya pili hasemi kwamba anahitaji msaada lakini anatoa ishara fulani zinazowadokezea wasikilizaji wake kwamba anahitaji msaada kutoka kwao, kwa mfano, kuwakodolea macho pasipo kusema lolote, kupumua au kupumzika katika muda mfupi kabla ya kuendelea na mazungumzo au kujikunakuna kichwa, pua, na sehemu yoyote ya mwili. Hizi ni hulka ibuka kwa wajifunza lugha ya pili wote kwani badala ya kusema wazi wazi kwamba ameshindwa kutoa neno alilokusudia kutoa anajikuta kwa hali taabani. Wafanyabiashara wanapojikuta katika hali hii huwa hawatambui kwamba ni moja wapo wa mikakati ya ujifunzaji wa lugha ya pili.

Kwa upande mwingine, Rubin (1987) alipendekeza mikakati mitatu ambayo alifikiria inaweza kumsaidia mjifunzaji wa lugha ya pili. Awali ya hilo alipendekeza hatua ambazo mwanafunzi hupitia wakati wa kujifunza lugha ya pili; yaani, kufanya jaribio, kufafanua na kupanga kwa kila hoja kulingana na nafasi na ukakamavu wake. Hizi hatua zinamfaa sana mjifunzaji lugha darasani. Aliendela kukubaliana na wengine kwamba mawasiliano ni mkakati mwafaka katika ujifunzaji wa lugha ya pili; yaani, msikilizaji hujaribu kupata maana ya maneno ya mse maji, alisema nini ama kufafanua nini mse maji alimaanisha. Hapa sasa ndiyo tunapata ufaafu wa mkakati wa mawasiliano kwa wafanyabiashara ambao wanajifunza Kiswahili katika mfumo usio rasmi.

Rubin (1987) anaendelea kusema kwamba kuna mikakati ya mtagusano na ukuruba kati ya wanunuzi na wauzaji ambapo kuna shughuli ambazo huwasaidia wajifunzaji lugha ya pili kuimrisha tajriba ya msamati wa lugha ya pili. Kwa wafanyabiashara, swala la kujifanya majaribio namna atatumia Kiswahili kwa wanunuzi ni dhahiri sana katika kuimrisha mawasiliano na wanunuzi wao. Krashen (1987), naye anasema kuna mfumo wa umilisi mkuzi ambao ujifunzaji huanza na muundo wa maswali ya neno moja kama vile; nini? vipi? ngapi? nk, matumizi ya viunganishi, matumizi ya njeo, matumizi ya vimilikishi na vivumishi. Utafiti wetu ulishabihiana na wataalamu hawa kuwekea msisitizo kwamba mawasiliano ndiyo msingi imara ambao unawezesha uendelezaji wa hali ya maisha katika sehemu mbali mbali hasa sekta ya kibiashara.

Hymes (1975) alisema kwamba umilisi wa kuwasiliana ni uwezo wa kutumia lugha kutoa na kufasiri maana, hivyo kutokana na maelezo yake, Swain (1985) aligawa maelezo hayo katika makundi manne yaani; umilisi wa isimu (maarifa ya wanafunzi juu ya msamiati fonolojia na sheria za lugha), umilisi wa kidiskosi (uwezo wa mwanafunzi kuhusisha tamko na maana); umilisi wa kiisimu jamii (uwezo wa mwanafunzi kutumia lugha kiufasaha). Umuhimu wa maelezo haya unajikita kwa uwezo wa mwanafunzi kuweza kutumia lugha hiyo na wala siyo lazima kuzingatia mitindo na miundo ya lugha. Maandishi ya Hymes (1975) yana upenyu kidogo katika mwelekeo wa (Krashen, 1987) maana naye anasema mtu anaweza kupata lugha na kuitumia kimawasiliano kulingana na mazingira aliyomo. Kiswahili ambacho wafanyabiashara wanahitaji ni cha kuwawezesha mawasiliano wakati wanafanya biashara zao. Utafiti huu uliingiliana na kuupa muelekeo utafiti wetu kupambanua namna wafanya biashara huweza kujifunza Kiswahili kama lugha ya biashara.

Griffiths (2004) akirejelea (Rubin, 1975) alifasili mikakati kama stadi ama chombo ambacho mwanafunzi anatumia kupata ujumbe. Wanafunzi waliofanikiwa ni wale ambao walikuwa na motisha wakati wa kuwasiliana, uwezo wa kubahatisha bila uwoga wa kutaka kujua kwamba hawakuja waliyokuwa wakisoma ama kuwa mbumbumbu. Anaendelea kusema kwamba hii haimaanishi kwamba hawakujali makosa yaliyojitokeza ila wanafunzi wazuri wa ujifunzaji lugha ya pili hufanya miundo na maana kutokana na lugha wanayojifunza. Kwa kuongezea wanafunzi wazuri hufanya mazoezi na kufuatilia lugha wanayojifunza na lugha ya wale walio karibu nao. Rubin (keshatajwa) alisema kwamba kufanikisha kwa mikakati kama hii iliegemea na vigeugeu tofauti kama umilisi wa lugha lengwa, umri, hali na tofauti za kitamaduni. Utafiti wa Rubin ulishadidiwa na watafiti kama Wong-fillmore (1979) ambaye aliripoti juu ya utafiti wa tofauti za kimaumbile katika Chuo Kikuu cha California kuhusu mikakati ya mtagusano na ukuruba. Aliripoti kwamba wanafunzi wazuri wa lugha ya pili hujumuika na wengine nje ya darasa na kujaribu kujilingiza katika kila shughuli za wengine; huwa wanapenda kuwasiliana na wa lugha lengwa badala ya kukaa darasani kujifunza lugha lengwa: Tafakuri hizi hazikueleza ni wanafunzi gani walikuwa wakiwarejelea. Utafiti huu ulihuisha mtagusano na ukuruba kati ya wafanyabiashara na wanunuvi ambao ni wazungumzaji wa lugha ya Kiswahili katika kufanikisha ujifunzaji wa Kiswahili ili kufanikisha biashara zao.

Tafakuri zinaonyesha kwamba wakati wa kubadili na kuchanganya msimbo, mzungumzaji hutumia maneno, virai, vishazi au sentensi za lugha nyingine wakati anapowasiliana

kwa lugha ya pili. Jambo hili hutokea kwa sababu ya kupungukiwa na msamiati katika lugha ya pili au kwa sababu ya kisaikolojia na isimu jamii. Corder (1967) anaeleza kwamba kila lugha ina muundo wake na kuhamisha sauti ama mpangilio wa L1 katika L2 hudhihirika kama makosa. Hali hii ilipatia utafiti huu nafasi ya kuchunguza endapo uhamishaji wa muundo ama kuchanganya msimbo kama mkakati wa kujifunza L2 ulichangia katika kujifunza Kiswahili kama lugha ya biashara ama ulisababisha changamoto za ujifunzaji wa Kiswahili kama lugha ya biashara.

Mohochi (2018) alisema kwamba lugha ina nafasi muhimu katika ujenzi wa jumuiya kwa sababu ni kupitia kwa lugha ambapo wananchi wa mataifa mbalimbali wanachama wa Afrika Mashariki wanaweza kuwasiliana na kushirikiana katika shughuli zao mbalimbali. Moja wapo wa shughuli ambazo zinaweza kuleta ushirikiano ni shughuli za biashara. Shughuli hizi haziwezi kufanikishwa bila kutumia lugha moja. Katika utafiti huu utafiti ulieleza namna mikakati ya ujifunzaji wa L2 ilisaidia wafanya biashara wa Kampala kujifunza lugha ya Kiswahili kibiashara. Hii ni kwa ajili ya kufanikisha biashara zao nchini Uganda hasa jiji la Kampala ambalo ni kitovu cha biashara nyingi zinazounganisha wafanyabiashara na wanunuvi kutoka pembe tofauti za Afrika Mashariki na kwingineko.

Mohochi (keshatajwa) alishadidia kwamba ushirikiano wa mataifa ya Afrika Mashariki si suala geni. Mwaka wa 1900 Uganda na Kenya zilikubaliana kuufanya mji wa Mombasa kituo cha ukusanyaji wa mapato ya forodha. Mwaka 1917 mamlaka za forodha zikaunganishwa na kuunda umoja wa forodha. Mwaka wa 1940 kukaanzishwa Bodi ya Ushuru wa mapato ya Afrika Mashirika pamoja na Baraza la Kiuchumi. Hii ni ithibati kwamba ushirikiano wa kimataifa wa kibiashara ulianza kitambo hata kabla ya karne ya kumi na tisa. Kiswahili kilianzishwa Uganda kama lugha ya kuendeleza biashara na dini katika Ufalme wa Buganda Chiraghdin na Mnyampala (1977). Ina maana kwamba ufanyaji biashara siyo jambo geni katika ukanda wa Afrika ya Mashariki. Swali ni kwamba waliokuwa wakishirikishwa katika biashara hizi walitumia lugha gani? Ina maana kwamba Kiswahili kilitumika kibiashara tangu enzi hizo ila tafiti kuonyesha namna wafanyabiashara hao walijikuta wanatumia Kiswahili ndio suala lililohitaji uchunguzi.

Kwa upande mwininge O’Malley na Oxford (1990) wametambua mikakati ifuatayo ambayo mwanafunzi anaweza kutumia wakati wa kujifunza lugha ya pili. Mikakati hiyo ni kama: mkakati wa utambuzi, mkakati wa mpango binafsi, mkakati unaohusiana na kumbukizi na

mkakati wa Kufidia. Katika mkakati wa utambuzi, unawezesha mwanafunzi kuchanganua nyenzo za lugha mfano kuitia kuwaza, uchanganuzi, kuandika makala mafupi, kufanya muhtasari sahihi, kuorodhesha, kupanga ujumbe na kupata uelewa mahsus. Hii ni mikakati ambayo humuwezesha mwanafunzi kupanga vizuri sheria za lugha lengwa ili kumrahisishia uelewaji wake katika kujifunza lugha ya Kiswahili. Utafiti wetu umenufaika kwa mikakati ya O’Malley na Oxford (1990) kwamba mjifunzaji wa L2 hashirikishi tu sheria za L2 kujifunza lugha lengwa ila pia sheia za L1 zinamjengea msingi mjifunzaji kujifunza lugha lengwa.

Mkakati wa mpango binafsi ni pale ambapo mjifunzaji wa lugha ya pili hujipangia namna ya kusoma, huwa na nia na upangaji wa shughuli za ujifunzaji wa lugha ya pili, kukusanya nyenzo za kusomea, kupanga muda wa kusoma na pahali pa kusomea. Kwingineko mkakati wa kufidia hutokana na yale yanaskizwa na kusemwa, kutumia sinonimu na kutumia maneno yanayosaidia kuzungumza, kuandika na kutumia ishara. Hali hii husaidia wanafunzi kupata yale ambayo hayakuwepo. Utafiti wao katika kiwango hiki ulimuangalia mwanafunzi ambaye anakuwa katika mazingira rasmi ya ujifunzaji wa lugha ya pili. Tukumbuke kwamba wafanyabiashara hawahitaji mazingira rasmi ili kujifunza Kiswahili. Kwa wale ambao walipata mafunzo ya Kiswahili inakuwa ni fursa kwao kutumia mkakati huu. Aidha, mkakati wa Kufidia unaelezea kubahatisha kutokana na yale yanaskizwa na kusemwa, kutumia visawe, maneno yanayosaidia kuzungumza na kuandika na kutumia ishara husaidia wanafunzi kupata yale ambayo hayakuwepo. Oxford (1990) na Cohen (1998) wanakubaliana kwamba mikakati ya Kufidia inayotumiwa kwa kuzungumza na kuandika ni ya matumizi ya lugha na sio lazima iwe mikakati ya kujifunza lugha. Tafiti nyingi zimeonyesha kwamba, matumizi ya lugha huanzia pale ambapo mtu amewezeshwa katika kuwasiliana. Sifa moja wapo ya ujifunzaji lugha yoyote ile ni kwa ajili ya mawasiliano bora.

Kwingineko, mkakati wa mpango binafsi hufanikisha kutambua mtindo wa kusoma, nia, upangaji wa shughuli za ujifunzaji lugha ya pili, kukusanya nyenzo za kusomea, kupanga muda wa kusoma na pahali, kuchunguza makosa na kutathmini shughuli zilizofanywa na kutathmini aina ya mkakati wa kusoma. Hutumiwa ili kunufaisha ujifunzaji bora. Purpura (1999) aligundua kwamba mkakati wa mpango binafsi ni mkakati bayana ulio mwafaka kwani unasaidia wanafunzi kumaliza shughuli zao za kimasomo wakati mwafaka. Wakati mwingine mwanafunzi huenda akaandika maneno katika vijikaratasi ambavyo atarejelea wakati anapotaka kuvitumia au sivyo kuandika maneno machache mkononi mwake ili iwe rahisi kwake kuyatumia. Labda mkakati huu ulilenga wanafunzi wale ambao tayari wanajua

mikakati hii lakini utafiti huu ulilenga wale wanafunzi ambao wakati mwingine hawatambui ikiwa kwa kweli kuna mkakati fulani ambao wanatumia katika ujifunzaji wa lugha ya pili. Kwa wakati huu inatambulika kwamba wanafanya makosa mengi. Hata hivyo, katika utafiti huu makosa kwa mfano ya kisarufi yanatambulika kama kigezo cha kumsaidia mwanafunzi huyu kujifunza L2. Anapopata kukosolewa kwa makosa haya inakuwa msingi bora kwake yeeye kujifunza neno jipya.

Kwa kuongezea, Minti (2012) alichunguza maingiliano ya biashara ya miraa baina ya Wasomali na Waigembe katika eneo la Muhingerena Maua. Katika utafiti wake alilenga kubainisha mikakati ya kimazungumzo ambayo wanajamii walitumia katika ununuza na uuzaaji wa bidhaa hiyo. Alibainisha kuwa walizingatia mikakati kama vile utengaji, ushirikishaji; ukosefu wa urasmi na ukavu wa kimsamiati. Biashara ya miraa mara nyingi huhusishwa na msamiati wa kimatusi. Ikumbukwe kwamba lugha hutumiwa tofauti tofauti kulingana na mazingira na muktadha wa mazingira hayo. Miraa ni sehemu ya madawa ya kulevyta na soko ni sehemu rasmi la kufanya biashara. Lugha ambayo inatumika lazima iwe ya kushawishi na kutumia nidhamu. Ushirikishaji ni kipengele kizuri katika uhusishaji wa biashara. Utafiti wetu ulishadidia kwamba hakuna biashara ambayo huendelea bila ushirikiano na ushirikishaji wa wauzaji na wanunuza na kutumia misamiati mwafaka kulingana na mazingira ya kufanikisha biashara lengwa.

Ellis (1994) na Rubin (1975) wanaeleza kwamba walimu wanafaa kutumia mawasilisho ya maigizo ya mbinu zinazotumiwa kujifunza lugha. Vile vile walieleza kwamba mikakati ya kutafsiri na kutathmini ilikuwa mwafaka katika ujifunzaji wa lugha ya pili. Kitu ambacho Ellis (keshatajwa) hakuweka bayana ni upeo wa utafiti wake yaani mkakati hutofautiana kulingana na mazingira ya yule ambaye anajifunza lugha. Namna na wakati mfanyabiashara anajifundisha Kiswahili kama lugha ya biashara ni tofauti na namna mwanafunzi wa kawaida alijifunza Kiswahili katika mazingira ya shule. Alipendekeza pia mbinu ya maigizo na tafsiri. Utafiti huu ulichukulia tafsiri kama mojawapo ya mikakati ya ujifunzaji wa lugha kwa namna ambavyo wanya biashara waliitumia ili kupata maneno ya Kiswahili ambayo yaliendeleza na kufanikisha mawasiliano yao.

Cohen na Weaver (2011) walipendekeza mikakati kadhaa katika ujifunzaji wa lugha ya pili ambayo ni pamoja na mkakati wa upatikanaji tena. Yaani, mwanafunzi anafanya mazoea kulingana na dhamira tegemezi kwa unyambuaji wa vitenzi tofauti tofauti. Ni mkakati amba

kwa kufahamu au kutofahamu hufanya wanafunzi wasionekane kana kwamba hawaelewi lugha wanayoitumia. Kwa mantiki hii mjifunzaji lugha ya pili huandika orodha ya vitenzi kulingana na maudhui ya matukio ya siku. Kila mara atakuwa anaona kitenzi alivyokiorodhesha na baadaye kuangalia na kuhakikisha katika orodha kwamba kitenzi anachokitumia ni mwafaka. Kitensi ni moja wapo wa kipashio kinachojenga tungo katika sentensi. Sentensi ni tungo ambayo inabeba maana ya neno. Matumizi ya vitenzi hutegemea muktadha na maudhui vinamotumika. Kutaja vitenzi kwa jumla namna ilivyofanywa na Cohen na Weaver (2011) ni vigumu kukadiria ni sentensi gani zinastahili kutungwa kutokana na vitenzi hivyo. Wafanyabiashara wanastahili kuhusisha vitenzi ambavyo vitaandamana na msamiati wa biashara.

Anaendelea kusema, kwamba kwa vile shughuli zote za lugha huhitaji kutatuliwa darasani na wakati mwingine mambo huonekana magumu, wanafunzi hujaribu kutafuta mbinu rahisi ya haraka na hivyo kutumia mikakati hakuepukiki. Makala ya Ellis (1994) yana mchango mkubwa kuonyesha kwamba kuna uwezekano wa wanafunzi wa lugha ya pili kujuu kwamba wanatumia mikakati ya ujifunzaji lugha ya pili. Hali hii inakuwa tofauti na wafanyabiashara ambao hawako katika mfumo rasmi wa kujifunza Kiswahili kama L.2 darasani. Ikumbukwe kwamba shughuli za lugha kibiashara hazitatuliwi darasani ila katika mazingira halisi ya kufanyia biashara.

Kwingineko Minti (2012) alichunguza maingiliano ya biashara ya miraa baina ya Wasomali na Waigembe katika eneo la Muhingerena Maua. Katika utafiti wake alilenga kubainisha mikakati ya kimazungumzo ambayo wanajamii walitumia katika ununuzi na uuzaji wa bidhaa hiyo. Alibainisha kuwa walizingatia mikakati kama vile utengaji, ushirikishaji; ukosefu wa urasmi na ukavu wa kimsamiati. Biashara ya miraa mara nyingi huhusishwa na msamiati wa kimatusi. Ikumbukwe kwamba lugha hutumiwa k w a n a m n a tofauti kulingana na mazingira na muktadha wa mazingira hayo. Miraa ni sehemu ya madawa ya kulevyia na soko ni sehemu rasmi la kufanyia biashara. Lugha ambayo inatumika lazima iwe ya kushawishi na kutumia nidhamu. Utafiti wetu ulishadidia kwa kutilia mkazo kwamba hakuna biashara ambayo huendelea bila ushirikiano na ushirikishaji kati ya wauzaji na wanunuzi na kutumia msamiati mwafaka kulingana na mazingira ili kufanikisha biashara lengwa.

Wenden na Rubin (1987) wanasema kwamba, wakati mwingine inakuwa vigumu kubaini kama mkakati fulani ndiyo unafaa kutumiwa katika kujifunza lugha. Wanaeleza kwamba

kuna hata kwa mfano mikakati shirikishi na mikakati ya ku{j}onea ambapo inakuwa vigumu kubaini ni mikakati ipi imetumiwa na yule anayejifunza lugha lengwa; Hivyo walibaini kwamba siyo dhahiri kwamba anayejifunza anatumia lugha moja; kuna wale ambao wanatumia zaidi ya njia moja hivyo inakuwa vigumu kubaini anapobadilisha kutoka mkakati mmoja hadi mwingine. Utafiti huu ulijikita moja kwa moja kwa kutumia usaili na uchunzaji kubaini mikakati yote iliyotumiwa na wafanyabiashara jijini Kampala kujifunza Kiswahili kama lugha ya biashara.

Chien (2010), katika utafiti wake alishughulikia mikakati ya kujifunza lugha ya pili kwa kuchunguza uhusiano kati ya tofauti ya tamaduni mbalimbali na mikakati ya ujifunzaji wa lugha ya pili, mikakati mipya ya ujifunzaji wa lugha ya pili, na vifaa vyta kutumia wakati wa kujifunza lugha ya pili. Alikubaliana na Rubin (1987) kwamba mikakati ya ujifunzaji lugha ilikuwa mazoezi, utathmini, ubainishaji na uamuzi mkali. Mbali na kutaja mikakati hiyo, ni dhahiri kwamba utafiti wetu ni tofauti na wa Chien (keshatajwa) unaoonyesha mikakati iliyotumiwa katika ujifunzaji wa lugha ya pili kwa wafanyabiashara ambao walijifunza Kiswahili katika mazingira yasiyo rasmi. Hata hivyo utafiti huu ulirejelewa na utafiti wetu kubainisha kwamba dhana ya uamuzi mkali ni dhana ya kisaikolojia ambayo inalenga mwelekeo ambapo kulingana na Gardner (1985) ameellezea hali kama hiyo kuwa ni mtindo na wala si mkakati. Kwa mujibu wa utafiti huu, tunakubaliana na dhana kwamba hakuna namna mikakati na mitindo inaweza kutenganishwa wakati wa kujifunza lugha ya pili bali hufanya kazi kwa pamoja ili kufanikisha ujifunzaji wa lugha ya pili hasa Kiswahili kwa wafanyabiashara jijini Kampala.

Wataalamu mbalimbali wamejadili kwa mapana juu ya mikakati ya ujifunzaji wa lugha ya pili ambapo tafiti mbali mbali ambazo aidha zimeonyesha pengo ambalo utafiti huu ulishughulikia ama michango ambayo ilielekeza utafiti huu. Miongoni mwa mikakati ambayo ilijadiliwa kwa kina ni; mawasiliano, kuomba msaada ama waziwazi au kisirisiri, kuchanganya msimbo, utambuzi, mpango binafsi, kumbukizi, Kufidia, upatikanaji tena, mtagusano na ukuruba kati ya wanunuzi na wauzaji, utengaji, ushirikishaji, ubainishaji, uamuzi kali na mkakati wa mazoezi.

## **2.2.2 Mitindo ya jumla ya ujifunzaji lugha ya pili**

Mitindo ni mielekeo ya jumla mjifunzaji lugha hutumia wakati wa kujifunza L2 haswa kwaajili ya mawasiliano. Ellis (2003) anasema mitindo ni seti za kibiolojia zinazokuza tabia ambazo hurahisisha ufundishaji ama uwe rahisi au mgumu kwa wengine endapo hawazielewii.

Kuna aina nne ya mitindo ya kujifunza lugha kwa mujibu wa Advanog (2017) kwa kumrejelea Fleming (2001) ambaye alifanya utafiti wake miaka ya themanini. Alieleza ya kwamba kundi la kwanza ni la kutazama, yaani mjifunzaji lugha hujifunza kwa kuelekezwa na picha, sanamu na muundo wa vitu angani. Kwa mfano, mtu anahuishisha picha au sanamu halafu anapata neno ambalo anafikiria ni mwafaka kwa kile ambacho anaenda kukitamka. Kuna pia mtindo wa kusikiliza ambapo kwamba mjifunzaji L2 mara nyingi husaidiwa na nyimbo, sauti, mdundo, ukariri na kuongea. Huu mwelekeo ulifaa sana utafiti huu kwani wengi katika maduka ya uuzaaji bidhaa katika jiji la Kampala siyo eti wameenda darasani na kujifunza Kiswahili kirasmi lakini kuna njia ambazo pia wao wenyewe hawatambui kwamba ni mitindo ya kujifunza lugha walikuwa wakitumia kujifundisha Kiswahili. Wao hujikuta wanasikiliza, wanaongea na kusikiliza mziki wa Kiswahili. Wao huibuka na misamiati ambayo huwawezesha kuzungumza Kiswahili.

Kundi lingine ni la kusoma na kuandika, yaani mtu anajifunza vizuri kupitia kusoma na kuandika. Kundi hili la kusoma huweka jitihada nyingi katika kusoma kila kitu katika lugha ya pili na kujaribu kuandika. Kusoma na kuandika ni stadi ambayo hufanikishwa baada ya mjifunzaji L2 kuweza kusikia na kuongea kile ambacho amekisikia na kukielewa. Ingekuwa bora utafiti huu wa awali wa kuonyesha mjifunzaji huanza wakati gani kusoma na kuandika? Je katika mazingira ya wafanyabiashara ni stadi gani ambayo ingewafaa zaidi. Kusikiliza na kuongea ama kutilia mkazo kusoma na kuandika? Huenda mtindo huu unafaa wale wanafunzi ambao wanajifunza Kiswahili katika mazingira ya darasa. Hili ni dhihirisho kuwa si mitindo yote hufaa katika miktadha yote. Hali ambayo utafiti huu utachanganua tu mitindo ambayo inatumika katika muktadha wa bishara jijini, Kampala.

Mwelekeo mwingine ni wa matumizi ya viziada lugha. mjifunzaji lugha anaweza kutumia mikono yake kugusa kitu, kuandika ama kuchora majedwali yaani chochote ambacho viungo vya mwili vinaweza kufanya. Kuna uhusiano mkubwa kati ya mtagusano wa wafanyabiashara na wanunuzi. Utafiti wao haukuonesha katika mazingira yapi mjifunzaji

lugha ya pili anastahili kutumia viungu vya mwili. Hoja hii ilichochea utafiti huu kubainisha endapo mfanyabiashara anashindwa kutaja jina la kitu na ni kwa namna gani anajikuta amefanikiwa kuwasiliana katika mazingira ya uendelezaji biashara jijini Kampala.

Mitindo ya ujifunzaji lugha ya pili huhusisha vipengele vinne; yaani, mtindo wa kiujuzi - namna akili ya mtu inavyojishughulisha na ujifunzaji, mwelekeo na motisha ya mjifunzaji lugha kulingana na hali, miundo ya mtu binafsi ya kumuwezesha kujifunza, na namna ya kushughulisha mitindo ya ujifunzaji ambayo atahitaji na kuwacha mingine (Lawrence, 1984). Kwa hiyo kuna angalau mitindo kadhaa ambayo (Parry, 1984; Shipman na Shipman, 1985) wameorodhesha kuonyesha namna inavyoweza kusaidia katika ujifunzaji wa lugha ya pili kama ifuatavyo; kujishughulisha na taaluma ya kujifunza na kujishughulisha katika ujifunzaji, hapa mwanafunzi hufanya maandalizi ya yale atakayojifunza kulingana na ugumu na uchangamano katika ujifunzaji; Wanafunzi kama hawa huonyesha mafanikio mazuri sana wakati wa ujifunzaji. Kuna mtindo wa uhakiki na uchanganuzi mpana: Hali hii inaonyesha kwamba sehemu ya kushoto ya ubongo hujishughulisha sana na kuhakiki lugha na vizuio vyake wakati upande wa kulia wa ubongo hujishughulisha na kutathmini miundo ya lugha lengwa (Shipman na Shipman, 1985). Leaver (1986) anasema kwamba wanafunzi ambao ujifunzaji wao hutegemea sehemu ya kulia ya ubongo huwa ni wepesi wa kujifunza sauti na miundo ya lugha lengwa kuliko wanafunzi ambao hutumia sehemu ya kushoto ya ujifuzaji wa lugha ya pili. Huu utafiti ulielekea kuhusisha sana sayansi ambayo ni tofauti na utafiti huu ambao uliangalia tu kwa jumla mitindo ambayo wafanyabiashara wanaweza kutumia kujifunza Kiswahili kwa ajili ya mawasiliano yao ya biashara.

Kuna pia mitindo ya ushirikiano na mashindano kulingana na Lawrence (1984) ambapo anasema Reid (1987) alifanya utafiti na kutambua kwamba katika darasa la ujifunzaji wa lugha ya pili wanafunzi huwa hawatoi ripoti juu ya matumizi ya tabia za ushirikiano ila badala yake huonyesha mashindano katika ujifunzaji wa lugha ya pili. Anaendelea kusema kwamba hali hii hukuza stadi za lugha, kujiamini motisha na mwelekeo chanya juu ya wenzao na mfumo mzima wa ujifunzaji wa lugha lengwa. Wakati wa kumshawishi mnunuzi kila mfanyabiashara hujitahidi kuonyesha kwamba ana uwezo wa kutumia lugha hiyo. Katika hali hii anashirikiana kwa ukaribu na mnunuzi ambaye amevutiwa na bidhaa zake.

Kwa kuongezea Kiango (2002) anasema kwamba maingiliano ya jamii zenye tamaduni na lugha mbalimbali hutokana na ushirikiano katika shughuli za biashara na nyinginezo za

Mtagusano na ukuruba kati ya wanunuzi na wauzaji. Shughuli hizo huzua haja za kuwepo kwa lugha moja itakayoweza kuwaunganisha watu wenye tamaduni na lugha mbalimbali. Kiwango cha kwanza ni kile cha mtu binafsi ambapo mtu hutoka kwenye jamii yake na kwenda kuishi kwenye jamii inayozungumza lugha tofauti na ile ya kwao. Katika hali kama itabidi mtu huyo ajifunze lugha ya jamii ile ya pili ili aweze kuwasiliana nao. Kiwango cha pili ni kile kinachohusisha mkusanyiko wa watu waliotoka kwenye tamaduni mbalimbali na hawana hata lugha moja ya kuwaunganisha. Watu kama hawa wakikaa pamoja huweza kuzua lugha ya kati ambayo katika hatua za mwanzo itajulikana kama pijini na ikiendelea kutumiwa na vizazi vya baadaye hujulikana kama Krioli. Kiwango cha tatu ni kile cha maingiliano ya watu wenye tamaduni na lugha mbalimbali ambapo hulazimika kuteua lugha moja miongoni mwa lugha zao na kutumia kama chombo cha mawasiliano na cha kuziunganisha jamii zote husika. Maandishi ya Kiwango yanaakisi vipindi ambavyo wafanyabiashara wa Kampala wamekuwa wakipitia kujifunza Kiswahili. Japo tunahuishisha vipindi hivi na utafiti wetu, Kiango (keshatajwa) alihuisha vipindi hivi kwa jumla, tofauti na hali ambamo utafiti huu ulifanyika ukilenga wafanya bishara katika mazingira ya jijini Kampala, Uganda.

Ehrman na Oxford (1990) walidokeza kwamba kuna mitindo tisa ambayo inahusiana na ujifunzaji wa L2. Ehrman (1996) aliongezea kuwa mitindo hii inategemea hali ya mtu, mtu anaweza kuwa mnyamavu au anayezungumza sana. Alisema watu kama hao hutumia mitindotofauti. Wazungumzao sana hujifunza L2 kwa maingiliano na wengine ambao nao pi wanajifunza lugha. Walieleza kwamba mitindo hiyo tisa ni, ufahamu unaojumuisha mikondo minne iliyopendekezwa na shirika la NIED (2009), tabia za kipekee ambazo zinajumuisha wanyamavu na wazungumzao sana, kuhisi ovyoovyo na kujiundia nadharia zao kwao wenyewe, kufikiria na kuhisi, tafsiiri, ukumbukaji, kujadili na wengine matumizi ya misamati popote mradi tu msamiti husika umetajwa pamoja na kutumia vifupisho ambavyo huwasaidia kukumbuka huo msamiati.

Waliendelea kuzungumzia aina mbili ya wanafunzi; wale huijundi nadharia zao ambazo huwawezesha kujifunza lugha na wale ambao huhitaji maelezo. Ehrman (1996) anaeleza kwamba watu kama hawa wanahitaji kusaidiwa na walimu. Kwa wafanyabiashara jijini Kampala walihitaji wanunuzi wao ambao wanakielewa Kiswahili kuwasaidia kuwafafanulia baadhi ya msamiati unaohusika na ufanya biashara. Kuna uwezekano kwamba walijiundi maneno ambayo yaliwasaidia kukielewa zaidi Kiswahili kibiashara hasa pale ambapo

walikuwa na misamiati finyu ya kujieleza namna utafiti huu ulikusudia kubaini.

Kia, Alipour na Ghaderi (2009) katika makala yao ya mchango wa mitindo katika ujifunzaji wa lugha ya pili kwa wanafunzi wanaopata mafunzo yao mtandaoni, waliainisha mitindo mingine saba ya kusaidia ujifunzaji wa lugha ya pili kama ifuatavyo:

*Kuona:* Kuna wale wanafunzi ambao hutumia mitindo ya kuona wakati wa kujifunza lugha ya pili. Wao hutumia picha na ujenzi wa taswira wakati wa kujifunza lugha ya pili. Kile ambacho huwa wamekiona huhifadhiwa akilini mwao na kuwawezesha kukumbuka wakati wanataka kuashiria kilichokuwa kinastahili kusemwa.

*Kusikia:* Kwamba watu hawa hupenda kujifunza lugha kwa kusikia sauti za lugha hiyo ama muziki kutokana na lugha ambayo wanana kujifunza. Huwa wanasikia sauti na kuziunganisha ili kupata neno ambalo litawafaa. Ikiwa vigumu kutumia sauti basi wao hutatafuta maana ya neno ambalo waliskia kutoka kwa muziki.

*Matamshi:* Hawa hupenda kujifunza lugha kwa kupitia mazungumzo na maandishi. Mazungumzo yanaweza kuwa yaliyorekodiwa ama ya ana kwa ana. Wao hufuutilia namna mzungumzaji lugha ya kwanza huhusisha ala za matamshi katika kuzungumza.

*Kuashiria:* Hawa hupenda kutumia viashiria wakati wa kujifunza lugha. Wanaweza kutumia mikono kuashiria ama hisia kulingana na kile wanachogusa. Kuashiria kunawafanya wanapata usaidizi kutoka kwa wazungumzaji wa lugha lengwa.

*Mantiki:* Hawa hupenda kutumia mantiki yao kujifunza lugha ya pili. Hii inategemea namna wanafafanua jambo. Wanaweza pia kuunda mfumo wa kiuhesabu au muundo wao wa kujifunza lugha.

*Ushirikiano:* Hawa hupenda kujifunza kwa kupitia makundi na watu wengine. Mara nyingi huwa kwa makundi ambayo yanatumia lugha lengwa wakati wa kuwasiliana. Katika hali hii huwa hawajali makosa ambayo wanakuwa wakifanya kwa sababu wanajua katika kufanya hayo makosa kuna wale ambao watawasahihisha na kuwaelekeza katika matumizi mwafaka ya lugha lengwa.

*Kujitenga:* Hawa ni watu ambao hujitenga na wanapenda kujifunza ama kujisomea wenyewe ili kujifunza lugha. Wao huona kwamba wanauwezo wa kujifanyia mambo yao. Hawa huwa ni wanafunzi wanyamavu ambao hawapendi kujihuisha na wengine wakati wa kujifunza

lugha ya pili. Wanasema katika mitazamo hii mtu anaweza kuamua kutumia mtindo mmojaau miwili wakati wanajifunza Lugha. Hata hivyo wanaweza kuchanganya mitindo ili kufanikisha ujifunzaji wao wa lugha ya pili. Mitindo hii ilituwekea misingi muhimu katika utafiti huu kwa namna ambavyo tulitambua kuwa ujifunzaji wa L2 unaweza kuhusisha Zaidi ya mtindo mmoja hata katika muktadha wetu wa kibiashara jijini Kampala, Uganda.

Uainishaji wa Moenikia na Zahed (2010) ulisaidia sana kupata data juu ya jinsi wafanyabiashara hutumia mitindo wakati wa kujifunza Kiswahili kwa ajili ya biashara. Katika mfumo mzima wa kuendeleza biashara, ushirikiano ni muhimu sana. Muziki umehusishwa na mambo mengi ya maisha mkiwemo kuburudisha, kuliwaza, kuonya, kukosoa na kufunza. Kufunza kunaweza kutokana na maudhui ya nyimbo ama msamiati ambaeo umetumiwa katika nyimbo husika. Aidha, mtagusano wao na wazungumzaji wa lugha ya Kiswahili kutoka lugha nchi zilizo na uzoefu wa Kiswahili kama Kenya na Tanzania, kuliwasaidia watafitiwa kubainisha kama mtagusano huo uliwasaidia wafanyabiashara kujifunza baadhi ya misamiati ya kutumia Kiswahili kibiashara.

Naye Keefe (1979) anasema kwamba mitindo hutegemea athari za tabia, ujuzi na saikolojia ambazo zinasaidia utambuzi, uwiano na mwitiko kulingana na mazingira yanayomuzunguka mwanadamu. Alishikilia kwamba, kwa kiwango kikubwa ni kwamba tabia, ujuzi na uwezo wa kisaikolojia husaidia kumuandaa mwanafunzi kujifunza lugha ya pili. Hoja za Keefe (keshatajwa) ni kuntu yaani, kwa mfanyabiashara yeoyote yule ni sharti awe amejiandaa kisaikolojia ndipo ujifunzaji wa lugha ya pili utimie. Pasi kufanya hivyo huenda mwelekeo dhidi ya ujifunzaji wa lugha ya pili ukaathirika. Kwa mantiki hii maandalizi mazuri kisaikolojia yanamjengea mjifunzaji lugha mazingira mazuri ya kupata motisha na msukumo wa kujifunza lugha ya pili. Utafiti huu ulichangia katika kuwekea madhumuni ya pili msingi kwa kuonyesha namna wafanyabiashara hujifunza Kiswahili kwa ajili ya biashara.

Wanajamii hutambuana na kukubali sheria za maingiliano kila mara wanapoingiliana kilugha. Katika biashara huwa kuna pande mbili za washiriki; wauzaji na wanunuzi. Naye Eckert (2007) anasema lugha husaidia wanajamii kuendeleza mahusiano na kudhihirisha mipaka ya utangamano wao. Ni kupitia lugha ndiyo mtu anaweza kujitambulisha na aila fulani. Katika mazingira ya biashara ushirikiano ni mtindo wa kibinagsi ambaeo unajengwa kati ya muuzaji na mnunuzi; sheria za maingiliano zinajengeka kati ya wauzaji na wanunuzi wenyewe ili kufanikisha mchakato mzima wa kuendeleza biashara. Gumperz (1982) na

Eckert (2003) walielezea muingiliano bila kubainisha muingiliano huo ulikuwa ni wa kundi gani la watu. Utafiti wetu ulijikita katika muingiliano wa wanunuzi kutoka sehemu tofauti za Afrika Mashariki na kwingineko ambao waliingiliana na wafanyabiashara wa mjini Kampala Uganda. Lugha ambayo ilihushishwa ni lugha ya Kiswahili.

Ehrman na Oxford (1990) walianisha mitindo ya jumla inayosaidia katika ujifunzaji wa lugha ya pili. Hiyo hubainika kihulka pale ambapo mjifunzaji wa lugha ya pili anaweza kuwa mnyamavu, mwenye kusema sana, mwenye kumakinika na yule asiye makinika kama ifuatavyo:

*Kufahamu:* Hii aina inaweza kugawanywa katika makundi madogo madogo ama vile kuona, kusikia na kuhisi na kugusa. Wanasema kufahamu ni mkondo mjifunzaji lugha huchukuwa ambao ni rahisi kwake kumuwezesha kujifunza lugha ya pili. Kuna wale ambao hupenda kujifunza kuitia mafunzo ya maelekezi ya kimasimulizi, kuna wale ambao hutaka tu kusikiza yanayofundishwa halafu waelewe. Hawa mara nyingi hupata utata wa kuandika hivyo huishia tu kujifunza kile walielewa kuitia kusikiliza.

*Tabia za mtu binafsi:* Kwamba tabia za mtu binafsi hutegemea wale wanyamavu na wale wenye kupenda kuzungumza. Kwa wale ambao ni wanyamavu hujifunza kimya kimya na ni vigumu kueleweka kwamba wanajifunza lugha ya pili, ilhali wenye kuzungumza sana hupenda kuonyesha kwamba wana uwezo wa kufikiria na kutatua mambo. Hili watalifanya ili kila mtu atambue kwamba wana uwezo fulani. Kina Ehrman na Oxford (1990) waligundua kwamba uhusiano uliopo kati ya tabia na umilisi wa lugha katika wanafunzi waliokuwa Waingereza waliokuwa wakijifunza lugha za kigeni ulichangia ama ukuzaji wa umilisi mzuri au kutopata umilisi mzuri katika lugha lengwa. Wazungumzaji hujumuika mara moja na jamii ya nje na huwa wanapenda kuingiliana na watu wote hivyo kuwa na marafiki wengi. Wanyamavu wao hutumia nafsi zao kufikiria nini cha kufanya, hupenda kujitenga na huwa na marafiki wachache. Hata hivyo inasemekana makundi haya mawili yakiwekwa kwa pamoja wanafanya wanyamavu kupata motisha ya kuzungumza ikiwa watapewa muda mwingi.

*Kuhisi kwa haraka haraka na kupanga fikra:* Wenye kuhisi kitu kwa haraka haraka hufanya hivyo kidhahania bila kufikiria. Huweza kujitungia nadharia na uwezekano na hupenda kujifundisha wenyewe wakati wanapotumia fikira na ufahamu. Wao hupenda kudhibiti wanayojifunza na kudhibitiwa.

*Kutumia mguso na kufikiria:* Hawa ni wanafunzi ambao hupenda ukweli hata kama unauma watu wengine. Hupenda kujionyesha kwamba wanaweza na sio kwa kujigamba hata kama wanataka wasifiwe. Wanafunzi wa kutumia mguso huthamini watu na kuonyesha kujali wenzao kupidia maneno matamu na wala sio tabia na husema kile kinaweza kutatua shida Fulani. Licha ya hayo hupenda kupewa heshima kwa ajili ya jitihada zao

*Hukumu na kubahatisha:* Kwa wenge kutoa hukumu hupenda kufikia uamuzi haraka haraka au hutaka ufanuzi haraka haraka. Hawa wanafunzi huwa wanabidii ambapo hupenda kupewa ujumbe kimaandishi na hupenda kazi mahsusiliyo na makataa. Hii haraka yao hufanya wakazungumza haraka ila hawa wa kubahatisha hupenda kuendelea kuonekana na huwa wanachukulia ujifunzaji lugha ya pili kama swala la muhimu.

*Kiwango cha juu cha kujumuika:* Hawa wanafunzi hufuata kile wanataka na hupenda kujumuika na wengine katika shughuli za mazungumzo yaani mahali wanaweza kuzungumza wakasikika bila kujali makosa ya kisarufi. Huwa wako sawa hata kama hawana ujumbe wa kutosha na hupenda kukisia yale yanazungumzwa na wengine. Hujali sana msamiati wanaotaka kutumia na kujeipusha na maneno ya kawaida. Huwa hawakisii kiholela bali huwa makini kwa makisio yao na kuwa na uhakika kwamba wanachokikisia ni cha ukweli.

*Tofauti za kibiolojia:* Tofauti za ujifunzaji lugha ya pili kunaweza kuhusishwa na hali kama vile ukariri, kuhimili na mazingira. Kwa wale wenge kupenda kukariri huonyesha muda wakati katika siku lini mwanafunzi anafikiri anaweza kujifunza. Kuna wale hupenda kusoma asubuhi, mchana, jioni na wengine usiku wakati kuna utulivu. Kwa wenge kuhimili ujifunzaji hupenda kusoma huku wakila ama wakinywa. Wanafunzi wengi wanaojifunza lugha ya pili

hawajisikii vyema kusoma kana kwamba hakuna kitu cha kunywa. Aina hii ya mitindo husahaulika na walimu wengi ila inakuwa bora mwalimu kukubali na kuutumia wakati wa kumfundisha mwanafunzi anayejifunza lugha ya pili.

Mitindo iliyojadiliwa hapo juu ni mapendekezo yalifanywa na Ehrman na Oxford (Keshatajwa) ili kuelewa na kusaidia wanafunzi wanaojifunza lugha ya pili. Ujifunzaji hutokea kwa aina mbili, kwa njia iliyo rasmi na isiyo rasmi. Wataalamu hawa walifanya uchunguzi wao juu ya wanafunzi Waingereza ambao walikuwa wanajifunza lugha za kigeni kama lugha zao za pili. Vile vile walieleza tofauti za ujifunzaji kulingana na muda mkiwemo majira ya asubuhi, mchana, jioni nk. Wafanyabiashara hufanya shughuli zao wakati wa

mchana tena kwa mazingira maalum ya kufanya biashara. Pili wafanyabiashara huenda wawe na msamiati ama maneno mahsus ya Kiswahili ambayo wanataka kukariri ili yawawezeshe kutumia katika kuendeleza biashara zao. Hali hii inazua utofauti katika utafiti wetu na utafiti huo uliofanywa na hawa wataalamu wa awali.

Oxford (1992), katika maandishi yake kuhusu mitindo inayotumiwa kujifunza lugha ya pili aliorodhesha vipengele vinavyomwezesha mwanafunzi kujifunza lugha ya pili yaani, kuona kile kinachofundishwa, kutembea na kuona kinachofundishwa na kugusa kile kinachofundishwa. Mtafiti alikubaliana na utafiti wa Oxford (Keshatajwa) kwani kuwepo kwa kirejelewa kunampa mjifunzaji lugha ya pili kujua kile ambacho anajifunza. Kwa mfano kuna maneno yanayofanana kati ya Kiganda na Kiswahili ambapo usipomtofautishia mjifunzaji Mganda utagundua kwamba maana anaielewa vibaya. Kwa mfano neno ‘meza’ katika Kiswahili ni tofauti na ‘meeza’ ya Kiganda. ‘Meeza’ ya kiganda haina maana zaidi ya kifaa cha nyumbani na ofisini tofauti na ‘meza’ ya Kiswahili ambapo inaweza kuwa meza nomino kifaa na meza tendo/kitenzi. Dhana ya kugusa na kuona ni msukumo utokanao na motisha ya mnunuzi kutaka kuona kile ambacho anataka kununua. Utafiti huu ulikuwa msingi wa kuegemewa kuchanganua namna motisha kupitia kuona na kugusa kuliwawezesha wafanyabiashara kujifunza Kiswahili kibiashara.

Krashen (2011) naye alisema kwamba kando na motisha, mwelekeo una mchango mkubwa wakati wa kujifunza lugha ya pili. Hii ina maana kwamba mwelekeo una uhusiano mkubwa na motisha. Aliendelea kusema kwamba mwelekeo unaweza kuwa kikwazo ama athari chanya katika ujifunzaji lugha ya pili. Alisisitiza kwamba ujifunzaji wa lugha ya pili unawezekana endapo kuna mwelekeo chanya, ukakamavu, na ari ambayo inajengea dhana ya kupenda ujifunzaji lugha lengwa. Hoja za Krashen ni kana kwamba zilishadidia mawazo ya Gardener (2000) kwamba motisha huwa na mchango mkubwa katika ujifunzi wa lugha ya pili. Ili mwanafunzi afanikiwe katika ujifunzaji wa lugha ya pili lazima awe na mwelekeo chanya, ari na jitihada ya ujifunzaji lugha lengwa. Athari hizi zilisaidia utafiti huu kutathmini ufaafu wa hivi vipengele ambavyo vilipelekea wafanyabiashara kujifunza Kiswahili kwa ajili ya kukuza matumizi ya Kiswahili na kuendeleza biashara zao.

Kiswahili kimehusishwa na maswala mengi; lugha inayojenga amani na kusaidia utatuzi wa migogoro nchini Kenya; Kama chombo cha kuboresha uchumi, lugha ya kufundishia: Kiswahili na utangamano wa kanda mbalimbali, Kiswahili nje ya Afrika Mashariki na

ughaibuni (Kembo-Sure na Ogechi, 2006 na Ryanga, 2018). Kila kinachozungumziwa katika hizi makala ni lugha na hasa kusisitiza Kiswahili kama chombo cha kuboresha uchumi na utangamano. Mtagusano baina ya watu mbalimbali kutoka nchi na wilaya tofauti ndiyo msingi bora wa kuimarisha biashara. Biashara haziwezi kuimarika pasi kuwepo kwa lugha moja ya mawasiliano. Hii inakuwa sababu kuntu ya wafanyabiashara jijini Kampala kujifunza Kiswahili kibiashara.

Kwingineko, biashara baina ya Uganda na nchi zingine hazijaanza hivi leo ila zilianza kitambo sana wakati waaarabu kupitia misafara mirefu na pia walifika nchini Uganda (Ssekamwa 2000). Biashara zilizostawi wakati huo zilikuwa ni uuzaaji wa pembe za ndovu, karafuu na watumwa hata (Chiraghdin na Mnyampala (1977) misafara hiyo iliyofanyika barani Afrika Mashariki, wafanyabiashara walitumia Kiswahili. Kwamba wazungu walioshukia Unguja walikijua kwa sababu zao mbalimbali. Watu hawa walifahamu kuwa lugha ya maingiliano ilikuwa ni Kiswahili. Tunaweza kuleta visingizio vingi vya kufikiri kwamba Kiswahili kinaanza leo nchini Uganda. Tukubali kwamba kimekuwepo ila kupuuzwa tu katika matumizi anuwai. Maandishi ya Chiragdin na Munyapala (1977) hayakuonyesha bayana visingizio hivyo ni vipi. Na kama kutojua Kiswahili sanifu ilikuwa mojawapo wa visingizio, utafiti huu haukuwa na haja ya kutatua visingizio vilivyokuwa ni vya kinadharia tu ila kuonyesha namna mikakati na mitindo imewasaidia wafanyabiashara kujifunza Kiswahili Kama lugha ya biashara.

Maandishi ya wataalamu mbali mbali yamepigiwa upatu ya matumizi ya Kiswahili kwa ajili ya maendeleo. Senkoro (2018) anasema hata kwa maisha ya wananchi wa Afrika Mashariki kuwa na lugha moja inayowaunganisha ni jambo ambalo haliendelezi tu muungano na umoja wa wananchi hao bali pia lugha moja kuu huwa ni mwanzo wa maelewano na ushirikiano katika nyanja mbalimbali zikiwemo za utamaduni, biashara, mawasiliano, ulinzi na hata utatuzi wa migogoro.

Senkoro (keshatajwa) ameshadidiwa na Mazrui na Njogu (2018) kwa kusema kwamba Kiswahili katika muktadha wa mazungumzo yetu ni muhimu si kwa kuleta mapatanisho ya kitamaduni tu baina ya mataifa ya Afrika Mashariki lakini pia ni muhimu katika kusaidia Jumuiya kutekeleza baadhi ya malengo yake mengine. Moja kati ya malengo hayo ni kujenga uchumi kwa njia itakayonufaisha kila nchi na vile vile nchi zote za jumuiya kwa jumla. Uhusiano kati ya maandishi ya wataalamu hawa na utafiti huu ni kuwepo na lugha moja ya

Kiswahili ambayo italeta maendeleo. Hata hivyo inatakikana kuweka wazi ushirikiano wa biashara unaendelezwa vipi mionganoni mwa wafanyabiashara wa Kampala ambao lugha yao asili si Kiswahili.

Watu kutoka jamii, tamaduni, taifa na lugha mbalimbali huingiliana kila mara ili kufanikisha shughuli zao za kila siku. Jamii kama vile za kisiasa huwa na Imani ya ujamaa-kujali maslahi ya watu wengine wanaotoka katika jamii zao. Jamii za kimagharibi kwa upande wake hushikilia misingi ya kibepari ambapo kila mtu hujali maslahi yake mwenyewe. Mawasiliano yanahuisha watu kutoka makabila tofauti kusheheni chembechembe za utamaduni wa kila mmoja. Haya huwa ni matokeo ya lugha kwani ni mali ya jamii. (Scollon na Scollon, 2001). (TY). Mwelekeo huu katika mazingiria ya kiafrika huzusha hisia hasi na kufikiria kwamba heri kuwa na lugha moja ya kuunganisha jamii kubwa iliyo na makabila mengi.

Phillips (2007) anasema migawanyiko kutoka lugha mbalimbali katika jamii huletwala na mirengo ya kisiasa kwani binadamu wote ni sawa. Uganda ni nchi ambayo imejengeka katika misingi ya ubepari na hivyo kila mtu ana hiari ya kutenda kile anafikiri kinamfurahisha alimradi asivunje sheria. Biashara katika mazingira ya kibepari humpa mfanya kazi kuwa na uhuru wa kutumia lugha anayotaka mradi ajue ndiyo itamfanya awe na wanunuvi wengi. Licha ya hayo yote lazima pawepo na mawasiliano kupitia lugha moja ili kunufaisha biashara. Ni kutokana na mantiki hii utafiti huu ulijenga dhana kwamba matumizi ya lugha moja ni bayana mionganoni mwa wafanyabiashara. Chambilecho Kiswahili kilikuwa mwafaka kutumika kibiashara jiji Kampala.

Kwa muhtasari watafiti mbalimbali walifanya utafiti na kubainisha mitindo mingi ambayo mwanafunzi anaweza kutumia kujifunza lugha ya pili (Oxford na Cohen 1992; Scollon na Scollon, 2001). Mitindo hii haitofautiani na mitindo ya kujifunza Kiswahili kama lugha ya biashara. Mingi yayo imegusia dhana ya uhisivu ambapo mwanafunzi anatumia viungo vyake vya mwili mkiwemo kuona, kusikiliza, kusoma kuandika na kugusa. Kuna mitindo mingine pia ambayo inahusisha tabia za mtu, mwelekeo, ufahamu, viwango tofauti tofauti vya usomaji, uhakiki na uchanganuzi, uvumilivu na hali ya kukumbana na ugumu wa ujifunzaji, kuashiria, kupanga fikra, uvumilivu, motisha kujitenga, kujumuika, uvumilivu, uhakiki, ushirikiano, ufahamu, na kushirikiana. Bila kusahau kuhisi kwa haraka haraka, hukumu na kubahatisha, kiwango cha kujumuika, tofauti za kibayolojia, motisha na mwelekeo. Kwingineko, wataalamu hao wa awali walifanya utafiti wao katika mazingira

tofauti ya watusika hasa wanafunzi walioko katika msingi rasmi wa ujifunzaji wa lugha ya Kiingereza ambao walikuwa wakijifunza lugha za Kigeni ambazo wengi wa wataalimu hawakuzitaja. Hata hivyo tafiti zao zilizua uchochezi wa kujadiliwa kubaini ikiwa mitindo hiyo pia ilitumiwa na wafanyabiashara jijini Kampala walijifunza Kiswahili kwa ajili ya biashara.

### **2.3 Jinsi mikakati na mitindo hutumiwa katika kujifunza lugha**

Sehemu hii kama ilivyokuwa katika kupambanua mikakati na mitindo ya ujifunzaji wa lugha, imeshughulikia mapitio ya maandishi yanayohusu jinsi mikakati na mitindo hutumiwa katika ujifunzaji Kiswahili kibiashara jijini Kampala. Lugha ya Kiswahili ni lugha ya pili kwa wafanyabiashara jijini Kampala.

#### **2.3.1 Jinsi mikakati inatumiwa katika ujifunzaji lugha**

Ellis (2003) akirejelea Jenkins (2000) anaeleza kwamba walimu wanafaa kutumia mikakatiya mawasiliano na maigizo katika kujifunza L2. Vile vile alieleza kwamba mikakati ya kutafsiri na kutathmini ni mwafaka wakati wa kujifunza lugha yoyote ile. Mjifunzaji wa lugha ya pili anaweza kutafsiri dhana kutoka lugha yake ya kwanza hadi lugha ya pili. Kutafsiri kunategemea ari ya mjifunzaji lugha ya pili na motisha alionao. Maelezo ya Ellis (2003) yanayohusu tafsiri na maigizo ni dhahiri kwamba yanaweza kufanikisha ujifunzaji wa lugha ya pili lakini pia mikakati inatofautiana kutegemea ujuzi na hasa kiwango cha uelewa wake kuhusu lugha lengwa. Ingawa anapendekeza kutafsiri na maigizo, huenda maigizo yasiwe mwafaka kwa wafanyabiashara jijini Kampala. Maigizo yanahitaji mtu aliye na uwezo wa kubaini mifumo ya uandishi wa lugha chanzi na lugha lengwa. Jambo hili si rahisi kwa wafanyabiashara wa maduka ya Ekedo ya mukwano ambao kiwango chao cha elimu katika masomo ya Kiswahili ni kidogo tena si wataalamu katika taaluma ya uigizaji. Kando na maigizo amependekeza kutumia mawasiliano katika ujifunzaji wa L2. Kuwasiliana hasa kupitia matamshi huhusiha wazungumzaji wawili au zaidi ambao wanatumia lugha moja. Tafiti mbali mbali zinaonyesha kwamba wakati wa kuzungumza hasa kwa mazingira kama ya biashara mtu halazimishwi kutumia lugha fasaha almradi wanaelewana wao kwa wao. Utafiti huu ulibaini namna mawasiliano yaliwasaidia wafanya biashara jijini Kampala kujifunza Kiswahili kwa ajili ya biashara.

Unapochunguza toni ya silabi za Kiingereza na Kijapani wazungumzaji ambao si wazawa wa Uingereza hifuata toni ya lugha mama wakati wazawa wa Kiingereza wakifuata muundo wa Kiingereza (Bachman, 1990). Utafiti huu ulionyesha kwamba matamshi ya toni za sauti za

Kijapani yalikuwa mapana kuliko ya wazaliwa wa Kiingereza. Kuwepo kwa mfanyiko huu uliletwa na sifa za wazungumzaji wa Kijapani kama L1. Kwamba matamshi yao ya kuvuta maneno kulileta tofauti ya kifonolojia wakati wa kutamka maneno ya Kiingereza. Bachman (1990) alifanya utafiti kati ya wazungumzaji wa Kijapani waliokuwa wakijifundisha Kiingereza kama L2. Hizo lugha zote mbili hazina asili ya Kiafrika. Hata hivyo kuna mfano ambao umetolewa na Massamba (2012) kwa kumrejelea McCawley (1974) kwamba kuna makundi manne ya lugha za Kibantu ambapo toni zimegawanywa kwa kuzingatia, toni ndani ya leksika, kuna kundi la lugha ambalo lina vijitoni ambavyo vinachombeza toni, kundi lingine halina kabisa, badala yake lina mkazo tu, kuna pia kundi la lugha ambalo lina vijitoni na mkazo na kila toni ina sifa pambanuzi.

Kwenye utafiti huu lugha inayolengwa ni Lugha ya Kiswahili ambayo ina muingiliano mkubwa sana na baadhi ya lugha za kibantu nchini Uganda. Hivyo utakuta kuna baadhi ya sauti ambazo zinatamkika sawa kutoka lugha chanzi hadi lugha lengwa. Hii inakuwa fursa bora kwa mjifunzaji wa Kiswahili kwa ajili ya mawasiliano. Kwingineko, utafiti wa Bachman (1990) ulifanywa kwa wanafunzi ambao mazingira yao yalikuwa ni ya darasani ambapo wanafunzi wa Kijapani walikuwa wanajifunza Kiingereza kama lugha ya pili. Utafiti huu ulikuwa tofauti na wa Bachman (keshatajwa) kwa sababu ulilenga wafanyabiashara waliojifunza Kiswahili kama lugha ya pili kwa ajili ya kuendeleza biashara zao jijini Kampala-Uganda.

Utafiti wa Rubin na Thompson (1994), uliohusu wanafunzi wa Kiingereza uligundua kwamba mkakati wa mazungumzo ulikuwa mwafaka kwa ye yote anayejifunza lugha ya pili. Kwao walikuwa wanashughulikia changamoto zinazowakumba katika ujifunzaji wa lugha ya pili. Walikubaliana na Ellis (1997) kwamba ili mkakati wa kuzungumza uwe wa kufaa, unastahili kuzingatia mambo yafuatayo; Kuuliza maelezo vizuri, kuuliza mtu na kukariri yale ambayo amesema, Kusita na kutumia maneno ya mseto ili aweze kuendelea vizuri, kutumia vidokezo vya maneno kama, ndiyo! aha! sawa nk. Kumuomba mtu azingatie mnayoyazungumzia, Kuomba kuelewa neno linaloongoza mazungumzo, na Kutumia vitabia ili kuendeleza na kuwasilisha maana. Hakuna biashara yoyote ile ambayo inaweza kuendeleza bila kuwa na mazungumzo. Mazungumzo husaidia mnunuzi na mfanyabiashara ama kuridhiana au kutoridhiana kulingana na ubingwa wa namna mfanyabiashara atafinyanga lugha kibiashara ili kuchota hisia za mnunuzi. Hali hii hujitokeza pale ambapo watu wawili au zaidi wanashirikiana kupokezana maneno. Hali ambayo inamsaidia

mjifunzaji wa lugha ya pili kuchota msamiati ambao unamuwezesha kukuza umilisi wake katika lugha lengwa.

Massamba (2012) kwa kumurejelea Sapir (1949) anasema kwamba msemaji wa kawaida huhisi kwamba lugha yake imejengeka kwenye idadi ndogo ya sauti pambanuzi, na kwamba tukiacha sauti chache, sauti zinazotumika katika lugha za kigeni ni zilezile ambazo yeye naye anazijua, ingawa anazitumia kwa namna tofauti. Kwa kushadidia maelezo ya Sapir (1949) na Massamba (2012) kuna uwezekano kwamba wanaojifunza Kiswahili katika Ekedo na soko lililoteuliwa wanakisia kwamba kuna baadhi ya sauti ambazo ziko katika lugha yao chasili ambazo zinaweza kutumiwa kujifunza Kiswahili. Hivyo kujaribu kupata mikakati ambayo inawawezesha kujifunza Kiswahili kama lugha ya biashara.

Wazungumzaji wa lugha ya pili pia huhusisha muundo wa silabi za L1 na ule wa L2 wakati wa kujifunza Lugha ya pili. Archibald (1998) wamehusisha matamshi ya Kikorea yaani wanaongeza vokali katika baadhi ya maneno ya Kiingereza lakini sio kwa yote. Kuongeza silabi ambapo tunaweza kusema ni uchopekaji katika neno husaidia kufanana kwa maneno ya Kiswahili ambayo si ya mkopo kwa sababu hali ya kuongeza silabi katika neno huwezesha utamkaji mzuri wa silabi za Kiswahili. Japo utafiti wa Archibald (Keshatajwa) ni juu ya Wakorea katika kujifunza Kiingereza, ulisaidia utafiti huu kuangalia jinsi muundo wa silabi za lugha ya kwanza ulivyosaidia katika kujifunza Kiswahili. Uundaji wa silabi ni kipengele mwafaka wakati mtu anajaribu kupata tamko la neno fulani. Kwa vile baadhi ya hawa wafanyabiashara hawajakuwa kwa madarasa ya kuwafundisha sarufi kuna uwezekano kwamba walijitafutia mikakati ya kuhusisha silabi awali za L1 na kuzihamisha kwa L2 ili ziwarahisishie mawasiliano kwa ajili ya kuendeleza biashara kati yao na wanunuizi ambao wanatumia Kiswahili.

Mawasiliano mazuri huleta maendeleo. Mkwinda-Nyasul (2013) na Wanyanya (2020) wanasisitiza kuwa mawasiliano mazuri huleta maendeleo na hutekelezwa kuititia lugha. Mawasiliano ni jambo la kimsingi na hutekelezwa kuititia mapokezano ya maneno ama maandishi kuititia lugha. Kwa hiyo lugha inastahili kuonekana inawasilisha maana lengwa ili kutimiza malengo wala si kuwa lugha tu. Utafiti huu haukuweka bayana ni malengo gani ambayo yanastahiki kufanikishwa. Hata hivyo maandishi ya kina Wanyanya na Mwinda yameshadidiwa na Shelly, (2017) ambaye anasema kuna uaminifu kisaikolojia kati ya mnunuizi na mfanyabiashara wakati wa kuendeleza biashara ambayo yanahuisha utafiti

huu. Kwamba wanunuzi wataamini kile mfanyabiashara anazungumzia yeye mwenyewe kuliko vile ambavyo angetumia mkalimani wakati wa kuendeleza mchakato wa biashara. Maandishi ya hawa wataalamu yalisaidia sana huu utafiti katika ujenzi wa dhana kwamba jinsi mawasiliano yanastaamilishwa ndivyo wafanya biashsara wanapata ule umilisi wa kutumia Kiswahili kibiashara.

Mkwinda-Nyasulu (2013) akirejelea Arcand (1996) anasema lugha huwa inapunguza gharama katika biashara endapo washiriki wanazungumza lugha moja. Jambo hili hupelekea biashara kuongezeka na hivyo ukuaji wa uchumi. Anaendelea kusema kwamba lugha humwezesha mwajiri kuafikiana na mfanyakazi wake vizuri. Wao hufikia maafikiano bila tashwishi na kuelewana kwa urahisi. Lugha hupanua soko, huchangia ukuaji wa uchumi ajira na hali ya kung'anga'nia biashara. Kauli ya kung'ang'ania wanunuzi jijini Kampala imepelekea wafanyabiashara jijini Kampala walazimike kujifunza Kiswahili kwa sababu wanunuzi wengi wanatoka nje mwa Uganda. Namna wanajikuta wamezungumza Kiswahili ni jinsi ambavyo wamejibidiisha kuongea kimapokezano wakati wa kung'anga'nia wanunuzi. Huu mkakati kwa wajifunzaji wa lugha ya pili huwawezesha kujifunza lugha hiyo kwa wepesi sana.

Hardach (2018) anasisitiza kwamba lugha huunganisha jamii na kukuza uchumi wa nchi; Wingilugha huleta ushirikiano baina ya nchi au watu na kuwawezesha kuwa na soko moja kama vila soko moja la nchi za Ulaya. Mtu anapofika jijini Kampala ni kana kwamba mji mzima ni soko la Afrika Mashariki. Utakutana na watu wa aila tofauti tofauti katika maeneo ya Ekedi na masoko wakinunua na kuuziwa bidhaa mbali mbali. Utotfauti wa lugha unafanya Kiswahili kiwe lugha unganishi ambayo ilifanikisha asilimia themanini ya biashara zilizokuwa zinaendelezwa jijini Kampala. Kulingana na mazingira, kwa mara ya kwanza kweli utaona wauzaji wakitumia Kiganda ila wakati wanang'amua kwamba wanaowasiliana nao hawaelewi Kiganda mara moja wanabadilisha kwa lugha ya Kiswahili hasa kulingana na namna walivyomtathmini mnunuzi huyo. Kwa hali ya kuendana na wakati wafanyabiashara wanalazimika kubadili msimbo. Mazoezi ya kubadilisha msimbo kila wakati muuzaji anatangamana na mnunuzi ni muhimu kuwezesha muuzaji kuwa na uzoefu wa kutumiabaadhi ya maneno ya Kiswahili kibiashara.

Chiraghdin na Munyapala, (1977) anaeleza kuwa wito wa matumizi ya lugha moja yaani Kiswahili nchini Uganda na Raisi Idi Amini mwaka wa 1971, ulishadidiwa na maraisi wa

baadaye akiwemo Rais Museveni. Taasisi mbalimbali zikiwemo umoja wa Afika Mashariki na maono ya 2050 na ajenda ya 2063 yanatambua umuhimu wa kutumia Kiswahili kwa mawanda mapana. Hakuna namna nchi wanachama za Afrika Mashariki zitaendelea bila makubaliano ya lugha moja. Aidha, asasi moja wapo ya kuleta maendeleo ni biashara; Maandishi haya yalipatia nguvu utafiti huu kuchunguza namna wafanyabiashara wanajizatit katika kujiimashiria matumizi ya Kiswahili kibiashara bila kupitia mafunzo rasmi ya kujifunza Kiswahili kibiashara na namna wanaweza kutumia fursa za utangamano kujiendeleza kibiashara.

Matumizi ya Kiswahili yamepigiwa upatu katika utafiti uliofanywa na Kamisheni ya Kiswahili (2019). Katika mapendekezo ya utafiti wao walitaja kuwa stadi za Kiswahili siyo za kujifunga katika muktadha wa isimu ama lugha sanifu ila katika muktadha wa ukuwaji wa uchumi hasa katika biashara, lugha inastahili kupewa kipaumbele. Ni muhimu kushadidia ukuzaji na uendelezaji wa Kiswahili sanifu, hata hivyo kwa upande wa biashara kinachohitajika ni msamati mchache tu ambao huenda usifuate kanuni rasmi lakini uwezeshaji mawasiliano kibiashara. Ripoti hii ni msingi yakinifu katika utafiti huu pale ambapo utafiti huu ulilenga kuchunguza namna wafanyabiashara wamejifunza Kiswahili kwa ajili ya kuendeleza kibiashara. Kuchunguza jinsi walitumia mikakati mbali mbali ambayo iliwawezesha kutumia Kiswahili kibiashara.

Kiango (2002) ameonyesha hatua muhimu za maingiliano. Amesema kwamba kuna wafanyabiashara ambao wakati wa vita vya Raisi Idi Amin walitorekea nchi jirani. Mfano mmoja ni wakaazi wa Masaka ambao pia ni idadi kubwa ya wafanyabiashara jijini Kampala. Wakaaji hawa wakati huo wa uhasama walilazimika kutoroka nchi kupitia Mutukula kuelekea Bukoba na Mwanza. Hali hii iliwafanya waingiliane na watanzania na baadaye kujifunza Kiswahili. Baada ya nchi kutulia wengi walirudi na kuendelea kukitumia Kiswahili katika shughuli zao. Kwa mazingira kama hayo utafiti huu ultambua kwamba kuna wafanyabiashara wa aina hiyo ambao walijifunza Kiswahili kupitia hatua hiyo.

Hatua ya pili ya muingiliano ni wale ambao hujikuta wamechanganyika kuegemea makaazi walioishi na kulelewa mkiwemo mitaa ovyo ovyo, kambi za jeshi na polisi, kambi za wakimbizi walizuka na Kiswaluganda na hata mara nyingi wanakitumia wakati wa kufanya biashara. Mara nyingi utakuta uchanganyaji ndimi kwa mfano, *mwana olifikabaya nnyo* (kumaanisha yakhe wewe ni mbaya sana), *Nsaba Mungu leero ampe kuriziki* (Naomba

Mungu leo anipe riziki), *wewe unachukuwa bintu yangu mimi bado nafanyizia* (wewe wachukua vitu vyangu bado ninatumia), *bizineesi leero yaba ngumu* (biashara leo imekuwa ngumu) *ingia apa nauza muzuuri* (ingia hapa nauza vizuri), Ukiwa mgeni katika mazingira ya aina hii ya Kiswahili unaweza kufikiria kwamba baada ya muda watabadilisha na waweke Kiswahili chao katika hali sanifu. Hata hivyo huu huenda ikawa mionganoni mwa juhudhi walizozitumia katika kufanikisha mazungumzo ya biashara.

Cohen (1996) anasema, kuna takriban njia tatu ambazo mwanafunzi anaweza kutumia kuhusisha mkakati katika ujifunzaji wa lugha ya pili ambazo ziliibuka wakati ambapo alikuwa anafundisha wanafunzi wa Kiingereza lugha ya Kihispania. Kwanza, anasema kwamba ili mwanafunzi ajifunze vizuri ilibidi agawe wanafunzi wake katika makundi tofauti na kuwapa orodha ya vitenzi. Walikariri vitenzi hivyo na kuwashimiza kutunga sentensi kutokana na vitenzi alivyokuwa amewapa. Kulikuwa na kijisanduku kilichowekwa vijikaratasi vilivyoandikwa vitenzi tofauti tofauti. Ilifanyika hivyo ili mwanafunzi anavyokuwa na uzoefu navyo huweza kutambua tofauti yavyo kisemantiki wakati anaunda sentensi. Jinsi ya pili ya kujifunza lugha ya pili ni mwanafunzi mwenyewe kutumia akili yake, kupenda kujifunza ama kutumia jamii kujifunza. Wenye kutumia akili, hushughulisha utambuzi, uhifadhi wa misamiati na kutumia misamiati, vipashio na elementi nyingine za lugha ya pili. Namna ya tatu ni kutumia mawasiliano. Hapa anasema kwamba mjifunzaji wa lugha ya pili anaweza kujiundia ama kuingiza msamiati ambao kwake anafikiria ni sawa. Hali hii ilifanyika katika mazingira ya ujifunzaji darasani. Hata hivyo katika namna ya pili inaonyesha namna mfanyabiashara anaweza kujiundia na kuingiza msamiati ambao unaweza kumfaa wakati wa kutumia Kiswahili kwa ajili ya kuendeleza biashara.

Kuna mikabala mitatu ambayo inafanikisha namna ya kutumia mikakati wakati wa kujifunza lugha ya pili (Montano, 2017). Mkabala wa kwanza ni ule wa kutumia sarufi. Anasema mkabala huu unahitaji mwanafunzi kutumia vipengele vya lugha lengwa ambayo wanastahili kujifunza. Mkabala huu unahuishwa kutafsiri sarufi kutoka lugha chanzi hadi lugha lengwa, kuwa makini wakati wa kusikiliza na kutamka sauti za lugha lengwa. Mwanafunzi anastahili kutumia kukariri, dialojia, urudiaji rudiaji wa maneno kama njia za kutumia mikakati mwafaka wakati wa kujifunza lugha ya pili. Mkabala wa pili ni wa kimawasiliano. Kanuni za mkabala huu ziliibuka tangu miaka ya 1960 na husaidia ukuzaji wa umilisi wa mawasiliano na mawasiliano katika jamii husika. Wakati wa kuwasiliana, wanafunzi wanastahili kujiundia umilisi wa kuwasiliana, sarufi, isimujamii na diskosi kupitia vifaa na

shughuli mbalimbali za mikakati ya ujifunzaji.

Charmot na O'Malley (1987), walifanya utafiti kuhusu mikakati ambayo walimu walitumia sambamba na ile wanafunzi walitumia kujifunza lugha ya pili. Waliuliza wanafunzi kuwaeleza mikakati walikuwa wakitumia kujifunza lugha ya pili. Wanafunzi hao waliwaambia walitumia vijitabu kuandika msamiati ambao walifikiri uliwasaidia katika mawasiliano na namna walimu wao walivyowashurutisha kuliwasaidia kujifunza. Hali ya kutumia vijitabu na kuijundia misamiati ilitokana na ari waliyokuwa nayo katika kujifunza lugha ya pili. Williams na Burden (1979) waliwaunga mkono kwamba njia ya kuijundia misamiati ilikuwa bora wakati wa kujifunza lugha ya pili. Wanafunzi walioshughulikiwa na Charmot (1987) walijua kwamba walikuwa wanatumia mikakati ya ujifunzaji lugha ya pili .Walitambua pia namna walitumia mikakati hiyo wakati wa kujifunza lugha ya pili. Tofauti na utafiti wetu ambao ulishughulikia wafanyabiashara jijini Kampala na huenda hata hawakuja kwamba walikuwa wakitumia mikakati ya ujifunzaji lugha ya pili kujifunza Kiswahili. Mbinu alizotumia Charmot (1978) katika utafiti wake ikiwemo hojaji ilitoa mwangaza kwa jinsi gani mbinu tulizotumia zilifanikisha utafiti wetu. Kwa hali hiyo, utafiti huu ultumia mbinu tofauti za hojaji, usaili na uchunzaji ambazo zilikuwa mwafaka kupata data kutoka kwa wafanyabiashara jijini Kampala, Uganda.

Oxford (1990) na Cohen (1998) wanaendelea kusema kwamba ili mfanyakibashara ajikute anazungumza lugha nyingine, lazima awe na utaratibu wa kujipanga na kuwa na kiwango cha juu cha kukumbuka yale ambayo alijifunza. Dhana ya kumbukuzi pia inamsaidia kupanga maneno haya wakati anawasiliana na wengine. Pia humwezesha mwanafunzi kupata muda kuweza kuhamisha sheria za uzungumzaji wa lugha ya Kiganda ama lugha yoyote ile ya asili yake na kuzijengea katika kujifunza lugha ya pili ambayo ni ya Kiswahili. Alipopata umilisi wa kupanga sauti, ulimsaidia mfanyakibashara kuijundia maneno ambayo yalimsaidia kuendeleza biashara zake. Vile vile mkakati inayohusiana na kumbukizi husaidia wanafunzi kuhusisha dhana moja na dhana nyingine hata kama haihusishi uelewaji wa kina. Mikakati mingi inayohusiana na kumbukizi unasaidia wanafunzi kupata tena mfuatilio kama akronimu halafu ujuzi mwengine husaidia kukumbuka kutumia sauti (kwa mfuatano wa mdundo), taswira (picha inayojengeka akilini asikiapo neno), msisimko wa mwili, nyenzo kwa mfano kadi za kusoma, pahali. Mkakati huu hausaidii sana wanafunzi kupita mtihani kwani hutumika katika kukumbuka msamiati na sentensi kwa kiwango cha mwanzo cha ujifunzaji lugha ya pili lakini kiwango cha ujifunzaji unapopanuka kimsamiati na sentensi basi

mwanafunzi hahitaji tena mkakati huu. Huenda mtetezi wa mkakati huu aliangalia ukariri kama njia moja ya kupita mtihani. Lakini kwa msingi wa utafiti huu, ilifikirika kwamba mjifunza lugha huweza kukariri sauti kutoka L1 ambazo zinaweza kumuwezesha kuzihusisha na sauti za L2 na kumsaidia kujifunza Kiswahili kwa ajili ya biashara. Utafiti wao ulisaidia utafiti huu kutathmini namna mfanyakibashara hupanga shughuli zake za ujifunzaji, kwa mfano itakuwa rahisi mjifunzaji L2 kupanga sauti za Kiswahili kuunda silabi halafu baadaye aibuke na neno?

Mkabala wa tatu amba Montano (2017) anasema unawezesha ujifunzaji wa lugha ya pili ni wa utambuzi. Mkabala huu ulizuka kati ya 1998-1990 wakati wa utafiti juu ya utendaji wa utambuzi katika ujifunzaji wa lugha ya pili. Mkabala huu ulihuishwa sana na wanafunzi walikokuwa wakijifunza Kiswahili katika mazingira ya darasa. Mkabala unaegemea sana utambuzi katika ukuzaji wa lugha. Mwanafunzi anatumia ujuzi wa lugha ya kwanza katika kujifunza lugha ya pili. Katika kiwango hiki mwanafunzi anastahili kutumia akili yake huku akihusisha zana za kujifunza. Kupitia vifaa mwafaka na marejeleo, mwanafunzi anaweza kuijundia maneno, kufanya muhtasari, kujenga taswira juu ya yale anayosoma na kufanya muhtasari. Hata hivyo inahitaji utayari wa wanafunzi ili kuhusisha mikabala ya namna hiyo.

Mikabala yote mitatu ambayo imewasilishwa na Montano (keshatajwa) inaonesha namna mikakati inaweza kutumiwa katika ujifunzaji wa lugha ya pili. Ametaja kwamba mkabala wa sarufi amba unahuishisha tafsiri ya sarufi kutoka L1 hadi L2 na matumizi ya sauti za L2, kusikia kinachozungumzwa na kujihusisha katika dayalojia hufanikisha ujifunzaji wa L2. Vile vile mkabala wa mawasiliano huhusisha aina yoyote ya mjifunzaji almradi mwanafunzi ana uwezo wa kukariri maneno, kurudia rudia maneno na kujihusisha katika dayalojia. Mkabala wa tatu amba ni wa utambuzi unatumia sana na wanafunzi amba wako katika mazingira ya darasa. Hivyo kuna uwezekano kwamba mikabala miwili iliwezesha ujifunzaji wa Kiswahili kama lugha ya pili kwa wafanyakibashara jijini Kampala.

### **2.3.2 Jinsi mitindo hutumiwa katika kujifunza lugha**

Kishe (2018) anasema kwamba Lugha ya Kiswahili inaweza kuitambulisha jamii ya nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki na kuifanya ijione ni kitu kimoja chenye lengo moja kwa maslahi ya maendeleo yao katika ile mihimili minne: umoja wa forodha, soko la pamoja, Fedha moja na shirikisho la siasa. Makala hii ina uhusiano lengwa na utafiti huu kwani dhima kuu katika matumizi ya Kiswahili kibiashara ni kukuza uchumi wa mtu binafsi,

nchi na kuleta utangamano. Hakuna namna kutakuwa na soko moja bila kuwepo kwa lugha moja ambayo inatumwiwa na watu wote. Hii ndiyo huenda ikawa shinikizo moja kuu la wafanyabiashara jijini Kampala kupata motisha wa kutaka kujifunza Kiswahili Kibiashara.

Gold na Rimmer (2000) wanasema kwamba motisha ni tamanio la kutaka kufanikisha lengo kwa kuhusisha nguvu za kufanya kazi ili kufanikisha lengo hilo. Mwanasaikolojia Kameerer (1990) anasema kwamba motisha ni msukumo unaodokeza tabia za mtu, kiwango cha utendaji na nguvu ambazo mtu hutumia katika taasisi fulani. Skehan (1991), Oxford (1990), Gass na Selinker (1994) wanasema kwamba tabia za mjifunzaji ni mtindo ambao hushtushwa na mwelekeo wa ndani kwa kutegemea motisha atakaoupata. Hivyo endapo mjifunzaji ni mzungumzaji na mchangamfu sana basi hujifunza L.2 kwa haraka lakini endapo ana hulka za unyamavu basi ujifunzaji wake utachukua muda mrefu.

Uhai wa lugha yoyote ile hudhihirika katika matumizi ya lugha hiyo. Hii inamaanisha iwapo lugha ya Kiswahili itaweza kuendelea kuwa na uhai, hatuna budi kuyapanua mawanda ya matumizi yake katika kila nyanja na taaluma (Mwansoko, 2016 na Kishe, 2018). Mchango wa Kishe na Mwansoko (washatajwa) uliangazia ufundishaji wa Kiswahili katika asasi ya elimu. Kwamba kinachofanya watu waongee Kiswahili ni kwa sababu ndiyo lugha iliyօ rahisi kueleweka na kutumiwa na watu wengi Afrika Mashariki na kwingineko. Pili ni lugha ya Kiafrika ambayo imekubalika na kutumika kimataifa. Hata hivyo Makala yao yaliyapa utafiti huu msingi thabiti katika kuangazia upanuaji wa matumizi ya Kiswahili katika nyanja nyingine ambayo ilikuwa nje ya mfumo rasmi wa ujifunzaji wa Kiswahili. Hali hii hutokea kutegemea upendo alionao mjifunzaji dhidi ya lugha hiyo. MacIntyre na Gardner (1991) wanasema kwamba kuwa kufurahia kitu fulani kunaweza kufanikisha chochote kile katika maisha ya binadamu. Upendo kulingana na Krashen (1987), Cohen (1996) ,Gardener (2010) na Krashen & Fahad (2020) unaojitokeza kama hisia ambayo mtu huwa nayo na humsukuma kutenda ama kufanikisha jambo fulani. Hamasa ambao ni mtindo ambao unatokana na hisia za mtu humfanya anavutiwa na kujifunza L.2 pasi kuwepo na vikwazo vyovypote. Kwa kushadidia Ehrman na Oxford (1990) wanasema kwamba hamasa hufanya mjifunzaji wa L.2 kupata umilisi wa L.2 kwa urahisi maana anafanya akipendacho.

Lalonde na Microsoft (1985) wanasema ujifunzaji wa L.2 ni mchakato ambao unahitaji mjifunzaji lugha kuwa tayari kujifunza lugha hiyo katika nafsi yake ili aweze kupata msamiati wa kutosha utakaomwezesha kuwasiliana. Ikiwa mjifunza L2 hatakuwa na msukumo kutoka ndani, uwezekano wa kuhifadhi lugha anayojifunza ni vigumu. Kwa hali

yoyote ile motisha ni muhimu katika ujifunzaji wa L2. Nicholson (2013) anajaribu kuelezea mwanafunzi ambaye anapewa motisha na mwalimu wake ili kujifunza lugha labda kwa ajili ya ujifunzaji tu darasani. Kwa wafanyabiashara, motisha wanayohitaji ni ile ya kuwafanya wabadilishe mwelekeo wao kuhusu lugha ya Kiswahili. Gardener (2010) na Gass (2022) wanasema kwamba mtindo wa mwelekeo kuhusu lugha yoyote ile huathiri ujifunzaji wa L2 . Mwelekeo unaathiri mjifunzaji L2 kwa namna mbili; mjifunzaji anaweza kuwa na mwelekeo hasi dhidi ya lugha ama jamii ya wazungumzao lugha lengwa. Mwelekeo chanya tu ndiyo unaofanikisha ujifunzaji wa L2. Ili wafanyabiashara wajifunze Kiswahili kibiashsara ilibidi baadhi yao kubadilisha mielekeo yao kuhusu lugha ya Kiswahili.

Savile-Troike (2012) anafafanua zaidi kwamba muktadha wa kujifunza L2 hauishii tu katika mazingira ya darasa ambamo ujifunzaji lugha hutendeka bali pia mazingira ambamo mjifunza L2 anakaa, kwa mfano nyumbani. Savile-Troike (Keshatajwa) alijaribu kuonyesha umuhimu wa mazingira ya nyumbani katika ujifunzaji wa L2. Kwa mujibu wa utafiti huu, mazingira yanayohitajika ni mazingira ambayo yanamsaidia mjifunzaji Kiswahili kujifunza kihalisia. Ujifunzaji kihalisia ujulikanao kama ujifunzaji fiche ni pale ambapo (Ehrman 1990; Gardener 2000) wanaeleza kuwa mjifunzaji L2 hujifunza lugha lengwa katika mazingira yanayomzunguka bila kuonyesha kwa wengine kwamba anajifunza lugha hiyo. Pale ambapo hali inamuhitaji kutumia lugha hiyo basi utamuona akijaribu kuzungumza katika lugha hiyo. Endapo hakuna mtu amemuhusisha kuongea katika L2 basi watu hao huishia tu kunyamaza lakini huwa tayari washapata umilisi wa lugha lengwa.

Gardener na Lambert (1972) katika utafiti ambao walishirikiana, hawakutofautisha kipaji na mwelekeo katika kazi zao za awali. Hili walilifanya kwa wanafunzi ambao ni wazungumzaji wa lugha ya Kiingereza lakini walikuwa wanajifunza Kifaransa kama L2. Walitambua vipengele viwili viliviyowajengea umilisi katika lugha ya Kifaransa. Kipengele cha kwanza kilikuwa ni kipaji halafu cha pili kilikuwa ni mwelekeo juu ya ujifunzaji wa Kifaransa. Ni vigumu kubaini kipawa katika ujifunzaji wa lugha ya pili kwa jamii ya wafanyabiashara ila mwelekeo ni rahisi kudhihirika endapo umewashirikisha katika mazungumzo ya Kiswahili. Ili kudhihirisha kwamba ujifunzaji ulifanikiwa ni pale ambapo mjifunzaji kwa kupitia mbinu tofauti za ukusanyaji data anakuonyesha kwamba mwelekeo chanya ulimfanya akajifunza lugha lengwa. Gardner (2000) anasema kwamba mwelekeo chanya huchangiwa na motisha wa ndani ambao unamsukuma mjifunzaji kufanikisha ujifunzaji. Mwelekeo hasi unakuwa kizungumkuti katika ujifunzaji wa Kiswahili. Hata hivyo ni mtindo wa kimsingi katika

ujifunzaji wa Kiswahili kwa ajili ya biashara. Mwingiliano ni mtindo maalumu ambao ni nguzo katika ujifunzaji wa L.2. (Oxford, 1990 na Broselow & Park, 2001). Mwingiliano unamsaidia mjifunzaji kujifunza mambo mengine kama utamaduni wa lugha hiyo ambao unamsaidia kuzungumza na kuwasiliana kiufasaha. Williams (1994) na Gardener (2010) wanasema kwamba mjifunzaji anapoingiliana na jamii ya wazungumzaji lugha L.2 huwa ni rahisi mjifunzaji kujenga umilisi kwa lugha hiyo. Asilimia tisini ya lugha ya Kiswahili imejengwa katika utamaduni wa Uswahilini. Mambo mengi yamefungika katika utamaduni huo. Hii inamsaidi mfanyabiashara kujifunza lugha ya Kiswahili na kujifunza msamiati wa Kiswahili.

Williams (1994) na Gardener (2010) wanasema kwamba mtindo wa mwingiliano hausimami peke yake. Kuna uwezekano kwamba, mwanafunzi anaweza kujifunza kimya kimya, kuthibiti wasiwasi alionao kuhusu ujifunzaji, viashiria ama njia ya kawaida. Ujifunzaji kupitia njia za kawaida ni kukubali kujifunza, mazingira ya kawaida ya mwanafunzi, kujisahihisha makosa, kutumia misamiati ya lugha lengwa na kujiendeleza katika lugha ya pili. Ujifunzaji kupitia njia ya mwingiliano haichagui ni mwanafunzi gani anajifunza ila uwezo wake wa kutumia, kufikiria na kufanya muhtasari, kujipanga, kuwa kwa makundi ya ujifunzaji, kutumia muziki, vichekesho, tafakari na kukubali maoni ya jamii. Kwa hiyo Williams na Gardener (keshatajwa) wanasema kwamba ujifunzaji kimyakimya unazua mtindo mwingine ambao unajitokea kama ujifunzaji kiuhalisia pale ambapo mjifunzaji mosi anakubali kuingiliana na jamii ya wazungumzao lugha lengwa na pili kujifunza bila wao kutambua kwamba huyu mwanafunzi anapiga hatua katika ujifunzaji wa L.2.

Gardener (2010) anasema kuwepo kwa mwelekeo changamani kunamsaidia mjifunzaji lugha ya pili kujifunza vizuri lugha hiyo na kujifunza utamaduni wake. Katika mwelekeo changamani kuna hoja tatu kuu anazositisiza. Kwanza ni mjifunzaji lugha kujuu historia ya lugha ilivyokuwa kwa mazingira yake, kwa sasa hiyo lugha ina nafasi gani wakati ujao. Mjifunzaji lugha akishatambua hizi hoja tatu, basi atakuwa na sababu ya kujifunza lugha ya pili maana kujifunza lugha ya pili. Gardener (keshatajwa) anaendelea kusema kwamba kipengele cha motisha kina mchango mkubwa wa kufanikisha mitindo ambayo inamsaidia mjifunzaji wa L.2 kujifunza lugha lengwa. Mitindo hiyo ni kama;

*Kipengele cha kwanza ni mwingiliano:* Katika hii modula, mwingiliano hupimwa kwa kuzingatia kujifunza lugha ya pili ili iwe rahisi kuwasiliana na wazungumzaji/wazawa wa

lugha hiyo. Huu ulikuwa ni mwelekeo wa wazungumzaji wa Kiingereza dhidi ya lugha ngeni. Kipengele cha mwingiliano kilisaidia sana wakati wa utafiti huu. Dhana ya mwingiliano ilisaidia kuchochea utafiti kubainisha ni kwa jinsi gani wafanyabiashara jijini Kampala hujifunza Kiswahili kupitia mwingiliano uliopo baina yao na ama wanunuzi au wafanyabiashara wenzao amba walikuwa na umilisi katika lugha ya Kiswahili.

*Kipengele cha pili ni mwelekeo:* Amesema mwelekeo unaangaliwa kwa upande wa mwalimu na mwanafunzi. Mwalimu aliyezungumziwa ni yule ambaye ana uwezo wa kumfundisha mjifunzaji wa lugha ya pili hata kama si katika mazingira ya darasa. Utafiti ulifaidika sana na hiki kipengele kwani ilikuwa bayana kuchunguza mwelekeo dhidi ya wanaojua kuzungumza Kiswahili wanavyopokelewa katika ufunzaji wa Kiswahili kwa ajili ya kufanikisha biashara jiji Kampala.

*Kipengele cha tatu ni hamu na kutaka kujifunza lugha ya pili:* Hii ni dukuduku mjifunzaji lugha anaweza kuwa nayo wakati anataka kujifunza lugha ya pili ama kuitumia ndani na nje mwa darasa. Dukuduku ni msukumo wa ndani wa mjifunzaji unaomshinikiza kusoma. Msukumo huu ndiyo anaoutumia kujifunza lugha ya pili. Lengo kuu la mfanyabiashara jijini Kampala la kujifunza Kiswahili ni kwa ajili ya kuwa na mawasiliano mazuri ya kibiashara kwa kutumia lugha ya Kiswahili. Dukuduku na mwelekeo vyote huenda kwa pamoja. Dukuduku ya chini humpa mtu motisha chanya halafu inayomsukuma kujifunza lugha ya pili. Utafiti huu ulielekea kushadidia kwamba ndiyo njia mwafaka ambayo ilikuwa bora kuwafanya, wafanyabiashara wajifunze Kiswahili.

Gardener na Tremblay (1994) anasema kwamba mjifunzaji ambaye anasema sana hupenda sana kuongea na wazungumzaji wa lugha lengwa ama katika mazingira ambamo lugha hiyo inatumia sana. Anasema kwamba kwa njia hii anapata msamiati wa kutosha katika L.2. Hufanya hivyo kwa kuweka msisitizo wa kurudia rudia neno hadi apate maana ya msamiati alioupara kutoka L.2. Hulka za mzungumzaji ni mtindo amba hufanya mjifunzaji ambaye anaongeaongea sana kupata umilisi kwani yeye mwenyewe hujitahidi kujifunza msamiati wa lugha hiyo. Huko kuongeaongea katika lugha lengwa ndiyo motisha inayofanya wajifunze lugha lengwa. Kwa kuongezea Oxford (2003) anasema kwamba mjifunzaji ambaye ni mzungumzaji sana hupenda kuwa na vijikaratasi ambavyo wameandika baadhi ya maneno halafu huuliza wazungumzaji wa lugha lengwa maana ya maneno hayo ama kuyatumia katika sentensi wakati wa kuongea.

Hoja nyingine iliyowasilishwa na Gardener (2000), ni njia ambayo itafanya mjifunzaji lugha apate motisha ya kujifunza L2. Je tuijulize mfanyabiashara anatoa wapi motisha ya kujifunza Kiswahili? Motisha inayomfanya kujifunza Kiswahili ni ufanisi anaopata baada ya kujifunza Kiswahili. Kwani huwa na matumaini kwamba lugha anayojifunza itamsaidia kufanikisha jambo fulani. Wafanyabiashara wanaweza kuwasiliana na wanunuzi wao wakiwa mbali, ambapo wao huagiza na kulipia bidhaa zao bila kusafiri. Hii ni motisha tosha ya wafanyabiashara kujifunza Kiswahili.

Ujifunzaji wowote wa lugha hutegemea msukumo wa mjifunzaji lugha. Msukumo husababishwa na motisha. Motisha ni tabia au msukumo katika kutimiza malengo fulani. Motisha unaweza kuwa kitu kama fedha inayotolewa ili kumtia mtu hamasa kujifunza jambo. Utafiti huu haukuangalia fedha kama kipengele cha hamasa ambacho mjifunzaji lugha anastahili kupata bali ulijikita kwa kufanikiwa kwa ujifunzaji wa Kiswahili kwa ajili ya mawasiliano ya biashara

Kwingineko Vigotsky (1978) anasema kwamba mjifunzaji lugha hufanikiwa kwa kuhusisha usikilizaji wa wanaozungumza L.2. Nyenzo ambazo anaweza kusukiliza ni kiwango cha uchaguzi ambacho mtu hufanya kuhusu lengo analotaka kufikia na jitihada atumiazo kufikia lengo hilo. Hoja yake Vigotsky (keshatajwa) inashadidiwa na Krashen (1987); Gardener (2010) na Gass (2022) kwamba mtindo wa kusikiliza ni muhimu sana katika ujifunzaji wa L.2. Mjifunzaji mwenyewe huamua ni nini anataka kusikiliza. Kwa mujibu wa utafiti wetu tunaamini kwamba kile mfanyabiashara angependa kusikiliza ni mazungumzo kutoka kwa wasemaji wa Kiswahili ama nyenzo za kusikiliza ambazo zinaweza kumsaidia kukuza umilisi wa kujifunza Kiswahili kwa ajili ya biashara. Wanauganda wana historia ndefu sana juu ya matumizi ya Kiswahili. Kuna wakati kulikuwa na matumizi mabaya ya Kiswahili. Hata hivyo hali hii imebadilika kwa kuititia uhamasishaji wa asasi tofauti tofauti. Ufunguaji wa mipaka na mwingiliano wa watu katika harakati tofautitofauti kumesaidia watu kuanza kukipenda Kiswahili. Ehrman na Oxford (1990) wanasema kwamba mwingiliano ni mtindo ambao humwezesha mjifunzaji lugha kuimarisha umilisi katika lugha lengwa. Hii ni kwa sababu mjifunzaji atakuwa na muda mwingi wa kutangamana na wazungumzaji wa L.2. Mwingiliano umepana mahusiano ya kuwafanya wafanyabiashara kusafiri nchi jirani kama vile Kenya na Tanzania kwa muda mchache ili wajifunze Kiswahili kwa Imani kuwa kuishi mionganoni mwa wazungumzaji wa Kiswahili kungeliwafanya wajifunze kwa haraka.

Dornyei (1994b), alisema kwamba kuna mambo mengi ambayo hutokea darasani wakati wa kujifunza lugha ya pili ambapo kanuni za motisha hazizingatiwi. Kwa hiyo ili kuelewa tabia za wanafunzi na mielekeo yao darasani, waliandaa kiunzi ambacho walitaja kama kiunzi cha ujifunzaji kwenye mazingira ya darasa ambapo motisha katika ujifunzaji wa lugha ya pili umeelekezwa katika mifumo mitatu. Alisema kwamba kiunzi hicho hakikuwa na nia ya kugawa motisha katika viwango tofauti ila ni kushadidia tu modula ya Gardener ya motisha (1985). Kiunzi chake kinafafanua kiwango cha jumla cha motisha wa ujifunzaji lugha ya pili. Hata hivyo utafiti wetu ulijikita sana katika modeli ya Gardener ya ujifunzaji wa lugha ya pili (2000) ambayo inaelekeza vizuri tabia za mwanafunzi kama mtindo mwafaka wa kujfunza L.2. Hivi kwamba umejengeka katika msingi wa ari na jitihada wakati wa kujifunza lugha ya pili, na hali ya ujifunzaji ambayo inaendana na athari za motisha juu ya ujifunzaji.

Anafafanua kwamba ari hutokana na hali ya motisha ya ndani kwa ndani na hulingana na mazingira yanayomzunguka mjifunzaji wa lugha ya pili. Ufaafu unategemea namna mwanafunzi anathamini anayojifunza kulingana na matakwa yake. Kisha matarajio ni namna mwanafunzi anafikiria atafanikiwa kukamilisha lile alilonuia kufanya na changamoto zilizoko mbele yake. Wakati wa kuchapisha kwa kiunzi hiki utafiti ulikuwa umeelekezwa tu kwa viwango vitatu yaani kiwango cha lugha, ukakamavu na kiwango cha mwanafunzi.

Kwa jumla wataalamu mbalimbali walionyesha namna wajifunzaji lugha ya pili hujifunza. Yaani kupitia tafsiri kutoka lugha chanzi hadi lugha ya pili, uchopekaji wa silabi katika maneno, urudiaji rudiaji, udondoshaji wa baadhi ya irabu ama silabi, kutumia masimulizi, uwasilishaji, mawasiliano baina yao na wazungumzaji wa lugha wanayojifunza, mkabala wa tafsiri, kutumia lugha mseto, utambuzi wa ujuzi, kuwasiliana na utambuzi. Vile vile mitindo mbalimbali kama motisha, jitihada, ragba, tabia za mwanafunzi na kupenda. Kulingana na tafiti mbalimbali za awali (O'Malley na Oxford 1990; Purpura 1999; Ehrman na oxford 1989,1995,1990,) ni dhahiri kwamba mikakati na mitindo (Hajimia,Sigh, na Chethiyar 2020) haiwezi kutenganishwa wakati wa kujifunza lugha ya pili ila zinakamilishana. Hali hii ni msingi thabiti wa kubainisha namna mikakati na mitindo hutumiwa na wafanyabiashara kujifunza Kiswahili kama lugha ya biashara jijini Kampala, Uganda.

## **2.4 Changamoto zinazotokana na ujifunzaji wa lugha ya pili**

Kimaro (2015) katika utafiti wake amefafanua kwamba mionganoni mwa changamoto zinazokumba lugha ya Kiswahili ni kukua, kusambaa ama kuenea kwa lugha za mitaani hasa Sheng. Anaendelea kusema shule zimejaa vijana ambao wanapenda lugha za mitaani ambazo

hazifungwi na kanuni za lugha. Lugha hizi hazizingatii mfumo wa ngeli wala kujali istilahi (msamiati maalumu) za lugha zinazotakikana. Ukuaji na usambaaji wa sheng hutegemea mazingira na umri fulani wa jumuiya fulani. Wafanyabiashara jijini Kampala hujumuika na watu tofauti wa umri na viwango tofauti. Huku kujumuika kunasababisha wajifunzaji lugha ya Kiswahili kuiga lugha ya wanunuzi ambao huenda si sahihi. Hivyo basi mfanyabiashara aliishia kujifunza msamiati usio kamili ama maneno ambayo si sahihi. Utafiti huu ulibainisha endapo mfumo usio rasmi kama huu uliathiri ujifunzaji wao wa Kiswahili ama kuna changamoto nyingine ambazo zilichangia katika ujifunzaji wa Kiswahili kwa ajili ya biashara.

Kimaro (2015) ameendelea kuelezea kwamba katika shule nchini Kenya wanafunzi wengi hawathamini lugha ya Kiswahili. Wengi wao wanaona kuwa ni lugha ya watu wa kiwango duni cha elimu. Yaani ni watu ambao hawawezi kujieleza vyema katika Kiingereza. Huu ni mfano wa changamoto kwa wenyeji ambao ni wazawa wa mazingira ambamo Kiswahili huzungumzwa. Tofauti na Uganda ambapo watu hujifunza tu Kiswahili kama lugha ya pili na kwa azma fulani. Utafiti wa Kimaro unazua hoja nyingine. Je, Uganda hasa wafanya biashara jijini Kampala bado wana mwelekeo hasi dhidi ya ujifunzaji wa Kiswahili au la? Je, sababu za mwelekeo hasi ni nini? Je, ujifunzaji wa Kiswahili kama lugha ya biashara ulisababisha changamoto za ujifunzaji au walichukulia kuwa lugha ya watu ambao hawakufanikiwa kimasomo?

Williams na Burden (1997) kama ilivyo katika Pigott (2008) walitoa kiunzi kingine ambapo walisema kwamba athari za motisha ndizo huchangia changamoto ambazo zinaweza kuibuka wakati wa kujifunza L.2. Wamegawa athari hizo mara mbili; yaani athari za ndani na athari za nje. Walidai kiunzi hiki kilitofautiana sana na cha Dornyei (1994b). Walitoa mfano mojawapo ukiwa kiwango cha ragba juu ya shughuli inayovutia. Katika kiunzi cha Dornyei (keshatajwa) ragba ni kama kipengele cha ujifunzaji (athari ya nje) ilhali katika kiunzi cha Williams na Burden (1997) ni athari ya ndani. Hivi viunzi vyote wataalamu wamevitumia kama mitindo ya kutambua motisha chanya katika mazingira ya ujifunzaji wa lugha ya pili darasani. Kwa minajili ya utafiti wetu viunzi hivi vilichunguzwa katika mazingira ya biashara na kutathmini endapo vilifanikisha ujifunzaji wa Kiswahili kama lugha ya biashara mionganoni mwa wafanya biashara na wala si wanafunzi waliojifunza Kiswahili darasani.

Reece na Walker (1997) walisema kwamba licha ya kuwepo kwa michango mingi juu ya ujifunzaji na upataji wa lugha ya pili, kwao walionelea kwamba motisha ina athari muhimu katika ujifunzaji wa lugha ya pili. Walisema kwamba mwanafunzi wa L2 aliye na utata wa kujifunza akipata motisha hujitahidi kujifunza lugha lengwa. Hii ni tofauti na mwanafunzi ambaye ana uwezo wa kujifunza lugha ya pili wakati hana motisha wa kujifunza lugha hiyo. Wanasisitiza kwamba mwalimu anayefundisha mwanafunzi lugha ya pili lazima amsaidie mwanafunzi kuwa na mwelekeo chanya dhidi ya lugha anayojifunza. Shulman (1986) alishadidia kwa kusema kwamba mwelekeo kwa wanafunzi wa ujifunzaji wa lugha ya pili hutokana na mazingira mazuri, uamuzi, ari na ufaafu wa kujifunza lugha lengwa. Kwa muktadha wa wafanya biashara nia ya kujifunza Kiswahili ni shughuli za mawasiliano kati yao na wanunuvi ambao walikuwa wakitumia Kiswahili kama lugha ya mawasiliano.

Comstock & Kamara, (2003) na Schwarz& Terrill, (2000) wanasema kwamba kujifunza lugha ya pili ni changamoto inayohitaji motisha nyingi, na kwa mtu mzima, changamoto za kujifunza lugha lengwa huwa na maana kubwa. Kwa mfano, kutofaulu, udhaifu, na matatizo katika kujifunza lugha mpya kunaweza kuwa na athari mbaya kwa: (a) kazi na shughuli za kitaaluma; (b) mwingiliano wa kijamii na mahusiano ya kibinagsi; na (c) kujistahi. Utafiti uliofanywa na Moss na Ross-Feldman (2003) ulibaini kwamba ili kuboresha motisha ya mjifunzaji walipendekeza kuwa mambo ya kijamii kama vile mazingira ya kujifunzia, mienendo ya kikundi, na hata motisha ya mzungumzaji wa lugha lengwa inafaa kumpa motisha mjifunzaji wa lugha lengwa. Vinginevyo huathiri mwelekeo wa mwanafunzi, juhudhi, tabia ya darasani na ujuzi wa lugha kwa mafanikio. Ifahamike kwamba nchini Uganda watu wengi waliathirika sana na matumizi mabaya ya lugha ya Kiswahili. Hivyo ikapelekea watu wengi kukichukia Kiswahili, hali ambayo imekuwa ikibadilika polepole. Endapo Kiswahili kinatumika katika maeneo ya biashara basi kuna uwezekano kwamba watu mwelekeo hasi kuhusu lugha ya Kiswahili umelegezwa.

Kando na motisha kuna dhana ya kupewa moyo. Gardener (2000) amezungumzia wazazi na walezi wengine. Mtu anapo jifunza lugha yoyote lazima akumbane na changamoto nyingi yakiwemo makosa ya kiisumu na lafudhi. Hata hivyo ni jukumu la yule anayetambua lugha hiyo kumpa moyo wakati wanawasiliana kwa kutumia lugha hiyo. Kipengele hiki kilichangia pakubwa uchanganuzi wa kipengele cha changamoto ambazo wafanyabiashara hukumbana nazo wakati wa kujifunza Kiswahili. Moja wapo ikiwa ni kipengele cha kuhimizwa na wazungumzaji wa Kiswahili ama kushutumiwa kwa nini walijifunza Kiswahili. Katika

mazingira ya biashara mambo mengi hutokea. Kuna wakati mtu anaweza kubezwa kwa kutumia vibaya lugha ama kucheklewa. Hali hii mara nyingi hutamausha hasa kwa mjifunzaji. Maoni ya Gardner (2000) yanaweza kuwa mwafaka kwa wanafunzi ambao wanachukulia Kiswahili kama sehemu moja ya masomo anayojifunza darasani ila kwa wafanya biashara kwao wanachokilenga ni namna watavutia wateja na kupata faida na wala siyo kuzamia katika ujifunzaji rasmi wa Kiswahili.

Ustadi wa kupokea L2 huwa haijitokezi waziwazi na mpokeaji lugha huwa hana ufahamu ulio wazi dhidi ya kanuni anazozipokea (Krashen, 1987). Kutokana na maelezo ya Krashen ni vigumu mwanafunzi anayejifunza Kiswahili kama lugha ya pili kujifunza vizuri sarufi ya Kiswahili hasa katika mazingira yenye ukiushi wa kaida alizozoea. Kuna namna ataongea jambo lione kane kuwa sahihi kwake lakini lisiwe fasaha. Hii ni changamoto ambayo haiwezi kuepukika mi ongoni mwa wafanyabiashara ambao wanajifunza Kiswahili kama lugha ya pili kwa ajili ya kuendeleza biashara jijini Kampala, Uganda. Mara nyingi mtu akizoea lugha yake ya kwanza, muda mwingi huwaza na kutafakari katika lugha ya kwanza kabla hajahamisha ujumbe huo katika lugha ya pili. Kuna uwezekano kwamba mjifunzaji huenda akachanganya sarufi ya L.1 katika L.2. Hali hii inapoendelea unajikuta kwamba mzungumzaji wa L.2 anaibuka na makosa mengi sana katika L.2. Makosa haya hutokea wakati mwingi katika udondoshaji na uchopekaji wa baadhi (Mgullu 1999; Massamba, 2012) ya sauti katika maneno ya Kiswahili.

Williams (1999) anasema kwamba umuhimu wa mawasiliano umefumbiwa macho wakati tunafikiri tuna tajriba ya kutosha ya mawasiliano bora kwa kuonyesha uhoodari wetu katika mambo ya mawasiliano, kutoelewana, ukalimani potofu kuwa ni jambo la kawa ida. Williams (1999) anaendelea kusema kwamba ni ukasumba kufikiria kwamba mtu atasafiri pembe zote za dunia na kutarajia kwamba kila mtu anaelewa lugha yake. Kusafiri ulimwengu iwe ni kwa ajili ya utalii ama biashara ni bora mtu awe amejifunza zaidi ya lugha moja zitakazomwezesha kuwasiliana na watu tofauti katika mazingira na hali tofauti. Umuhimu wa kuwa na tajriba zaidi ya lugha moja umekuwa wa kimataifa hasa katika jamii ya biashara za kimataifa. Gardener na Tremblay (1994) wanasema kwamba kinachomkwaza mjifunzaji lugha mara nyingi ni motisha inayomsukuma kujifunza L.2. Kwa wafanyabiashara ambao wameridhika na matumizi ya lugha yao tu huwa hawaoni sababu ya kujifunza lugha nyingine. Wafanyabiashara kama hawa huwa hawana motisha ya ndani ama hawana motisha yoyote ya nje ya kuwafanya wajifunze L2. Katika hali hii mjifunzaji anaishi katika maisha ya

kukwazika kwa sababu ya ufinyu wa lugha moja tu aliyonayo.

Kwingineko Williams (1999) amesema kwamba ujifunzaji wa lugha nyingi huwa na changamoto zake kwa sababu tayari huwa mtu mzima na ana mengi yanayomsibu ambayo yanaweza kukwamiza kuingiza mifumo ya lugha nyingine. Ameshadidiwa na kina Montano (2017) kwa kusema kwamba utata wa ujifunzaji hupatikana kupitia utambuzi. Katika utafiti walioufanya kwa wanafunzi watu wazima ambao walikuwa wanajifunza Kiingereza, Mwanafunzi alitaja mara kadhaa kumbukumbu mbaya ambayo ilionekana kuzuia uwezo wake wa kujifunza Kiingereza. Ingawa watu wazima wanahitaji kasi ndogo ya kufundishia kuliko watoto. Hii ni kwa sababu ya kupungua kwa uwezo wa kuchakata taarifa ambayo ina uwezekano kuwa inahusiana na kina cha uchakataji. Wanaendelea kusema kwamba Iwapo mwanafunzi huyu atapata kumbukumbu halisi au matatizo ya kuhifadhi maneno kwa lugha lengwa, huenda ikasababishwa na upungufu unaoweza kutambulika au baadhi ya tofauti za kisaikolojia ambazo zinaweza kudhibitiwa kupitia kumbukumbu au mazoezi ya kiakili, kama vile shughuli za kujifunza zenyewe. Anamatisha kwa kusema kwamba hili linasalia kuwa swali la ufuutiliaji au tathmini ya mtu aliyefunzwa katika maeneo hayo. Utafiti huu ulishughulikia watafitiwa ambao tayari ni watu wazima. Namna walijifunza Kiswahili kibashara huenda kulitokea baadhi ya changamoto ambazo kwa namna moja au nyingine ziliathiri ujifunzaji wao au hata kasi yao ya kufahamu lugha hii.

Monica (2003) anasisitiza kwamba lugha huunganisha jamii na kukuza uchumi wa nchi; Wingilugha huleta ushirikiano baina ya nchi au watu na kuwawezesha kuwa na soko moja kama vile soko moja la nchi za Ulaya. Mtu anapofika jijini Kampala ni kana kwamba mji mzima ni soko la Afrika Mashariki. Utakutana na watu wa aila tofauti tofauti katika ma-Ekedi na masoko wakinunua na kuuziwa bidhaa mbali mbali. Utofauti wa lugha unafanya Kiswahili kiwe lugha unganishi ambayo ilifanikisha asilimia themanini ya biashara zilizokuwa zinaendelezwa jijini Kampala. Kulingana na mazingira, kwa mara ya kwanza kweli utaona wauzaji wakitumia Kiganda ila wakati wanang'amua kwamba wanaowasiliana nao hawaelewi Kiganda mara moja wanabadilisha kwa lugha ya Kiswahili hasa kulingana na namna walivyomtathmini mnunuzi huyo. Kwa hali ya kuendana na wakati wafanyabiashara wanalazimika kubadili msimbo. Ubadilishaji msimbo huenda ukafanikisha lengo la uendelezaji biashara ama kukwaza shughuli za uendelezaji biashara. Mara nyingi ubadilishaji msimbo unahitaji mtu aliye na umilisi wa lugha zote mbili jambo ambalo ni gumu kwa wafanya biashara ambao walijifunza Kiswahili kama lugha ya pili kwa ajili ya kukitumia

kibiashara. Changamoto inajitokeza pale ambapo mfanyabiashara anataka kubadilisha msimbo akajikuta anabadilisha kwa lugha ambayo inafanana na Kiswahili na wala si Kiswahili chenyewe.

Lina (2017) anasema kwamba, mitazamo waliyonayo wanafunzi kuhusu somo la Kiswahili ambayo ilitokana na sera za elimu nchini Kenya imekuwa changamoto kubwa kwa walimu wa Kiswahili na wanafunzi ambao wanajifunza somo hili. Makala ya Lina (Keshatajwa) yalihusisha wanafunzi waliojifunza Kiswahili darasani na changamoto kutokana na sera za elimu juu ya somo la Kiswahili. Katika utafiti huu tuliangalia changamoto zinazotokana na ujifunzaji wa Kiswahili kwa kutumia mikakati na mitindo ya ujifunzaji lugha ambapo Gardener na Lambert (1959) wanasema kwamba mwanafunzi akiwa na mwelekeo chanya juu ya lugha basi itakuwa haraka kwake kujifunza L2. Changamoto zikiibuka humfanya kuwa na mwelekeo hasi, na hivyo basi huwa vigumu kwake kujifunza lugha lengwa. Mwelekeo unaorejelewa na Lina (keshatajwa) unaletwa na sera tena nchini Kenya. Mwelekeo nchini Uganda ultokana na hali tofauti. Katika harakati ya kisiasa matumizi ya lugha ya Kiswahili yalikuwa mabaya. Watu wanapojaribu kukitumia Kiswahili nje ya taaluma ya elimu, wanafanya hivyo kwa kujilazimisha huku waktilia maanani manufaa yaliyomo kwa mfano kupata wateja na faida na wala si kwa ajili ya kuendeleza Kiswahili.

Kuna mielekeo kadha wa kadha ambayo Macaro (2001) aliorodhesha kuwa huenda ziwe mionganoni mwa changamoto za kujifunza lugha ya pili. Mielekeo hiyo ni pamoja na; motisha, jinsia, umri, hulka na mazingira ya mwanafunzi. Mionganoni mwa hiyo mielekeo ametaja kwamba mwanafunzi aliye na motisha wa kujifunza lugha ndani mwake hufanikiwa zaidi ya yule ambaye anatarajia kupewa motisha kutoka kwenye mazingira yake. Vile vile anasema kwamba katika darasa, wanafunzi wa jinsia ya kike huelekea kushiriki kwa kuweka mikakati zaidi ya kujifunza lugha kuliko wa jinsia ya kiume. Endapo mikakati na motisha inayozungumziwa na Macaro (keshatajwa) ni katika mazingira ya darasa basi itakuwa vigumu zaidi kwa wafanya bishara ambao wanajifunzia Kiswahili katika mazingira ya uendelezaji shughuli zao za biashara. Vinginevyo hatuwezi kukadiria mazingira ambayo Macaro (keshatajwa) alirejelea. Mazingira tunayokoleza katika utafiti wetu ni yale mazingira ambayo mfanyabiashara anajifunza Kiswahili huku anaendeleza biashara zake kwa ajili ya kutumia Kiswahili hicho kibiashara.

Kuanzia miaka ya 1912 hadi 1925 wamishonari walianzisha mafunzo katika madarasa ya awali katika lugha ya Kiganda miongoni mwa shule ambazo zilikuwa zikifundisha lugha asili mukiwemo sehemu za Buganda, Tororo, Busoga na Bugisu na hata vitabu vya lugha na dini viliandikwa katika lugha za asili (Ssekamwa, 2000:245). Wakati huo watoto walikuwa wakishinda shuleni kutwa ama kanisani, mazingira ambamo lugha za asili na Kiingereza zilizingatiwa. Mackey (2006), Brown (2007) na Krashen (1987) wanasema kwamba watoto wa chini ya umri wa miaka kumi na miwili hujifunza lugha ngeni kwa rahisi kuliko watu wazima. Matumizi ya lugha ya kiasili miongoni mwa watoto huwatatiza ujifunzaji wa lugha nyingine baadaye. Hali hii imeshadidiwa na Corder (1967:1983) ambaye anasema kwamba makosa mengi ambayo hujitokeza kwa wanafunzi ambao wanajifunza L.2 hutokana na uhamishaji wa sheria za L.1 hadi L2. Mjifunzaji L2 huwa ashajizoesha kanuni za lugha awali aliyojifunza akiwa mdogo hivyo kubadilisha na kuanza kujifunza Kiswahili katika utu uzima hasa katika mazingira ya kufanya biashara kunakuwa na changamoto.

Uganda ni nchi ya wingilugha kwani ina zaidi ya lugha arubaini (Aidah, 2020) namna ilivyo katika nchi nyingine duniani. Kutegemea mazingira ambayo mtoto ameletelea anakuwa na uwezo wa kuzungumza zaidi ya lugha moja. Hoja hii imeshadidiwa na Gass (2022) kwamba kufikia miaka ya sitini wanasaikolojia walihusisha uwililugha na uwezo wa chini ya utambuzi ila baada ya kufanya uchunguzi zaidi iligunduliwa kuwa, wana uwililugha wana ujuzi wa lugha kimawazo na kimfumo. Utafiti huu unakuwa tishio katika utafiti wetu kwa sababu wanafunzi ambao ni wafanyabiashara huenda wakaibuka na kuchanganya ndimi ama kutumia msamiati usiofaa wakati wa kuendeleza biashara. Licha ya kuwa baadhi ya lugha za kibantu nchini Uganda ni lugha za nasaba moja na Kiswahili wafanyabiashara jijini Kampala siyo wabantu tu kwani kuna pia wanailoti ambao lugha yao si nasaba moja na Kiswahili. Ina maana kwamba changamoto zinaibuka pale ambapo mjifunzaji kwanza ajifunze lugha ya Luganda ambayo ni ya pili kwake halafu aongeze Kiswahili ambacho ni aidha lugha ya pili pia ama ya tatu.

Linda (2017), alifafanua mambo kama matamshi ya lugha ya kawaida kama changamoto ya ujifunzaji wa Kiingereza kama lugha ya pili. Inasemekana kuna kanuni nyingi na masharti mengi wakati wa kujifunza Kiingereza. Aidha, kuna fonimu ambazo zinatamkika sawa wakati zina maana tofauti. Mfano uliotolewa ni, “I will *read* the book today,” and “I *read* the book yesterday,” kwamba kwa maneno kama vile ‘*read*’ yameandikwa sawa lakini matamshi ni tofauti. Hata katika Kiswahili utakuta kwamba kuna foni ambazo

zinakaribiana na mtu asipojihadhari anajikuta anafanya makosa. Mfano ni kama (fua-vua, kula-kura, mimi niko- miminiko). Kufanana na kubadilishana sehemu za fonimu husababisha maana tofauti zikaibuka wakati mtu anajaribu kutamka neno na kutotofautisha neno kulingana na wapi shadda iliwekwa. Kuna maneno katika lugha za kiganda ambayo hutamkika sawa na Kiswahili lakini maana ni tofauti kabisa. Kwa mfano neno /choo!!!/ ni la mshangao katika Kikiga wakati katika Kiswahili ni sehemu za mtu kuenda haja. Kuna uwezekano msemaji kumuuliza mhusika wa lugha hiyo mahali kuna choo lakini mrejesho atakaoupata utakanganya mawasiliano.

Ellis (2003) amezungumzia mwelekeo kama mojawapo ya changamoto za ujifunzaji wa L2. Anasema mwelekeo ni imani kuhusiana na vitu fulani katika utamaduni wa lugha anayojifunza, dhidi ya utamaduni wa lugha ya mjifunzaji, madarasa ya kujifunza, walimu wake na shughuli kuhusu ujifunzaji ambavyo, kwake vinaathiri wajifunzaji na uwezo wao wa kumudu lugha hiyo. Swalii ni kwamba je wafanyabiashara jijini Kampala kwa jumla wana imani gani kuhusiana na lugha ya Kiswahili? Kwa kuongezea, Gardener na Lambert (1972) walichunguza imani mbalimbali za mwelekeo na kuainisha katika kategoria tatu kama ifuatavyo: Mwelekeo dhidi ya jumuiya na watu wanaozungumza L2, Mwelekeo dhidi ya ujifunzaji na kuhusiana na lugha na mwelekeo dhidi ya lugha na ujifunzaji lugha kwa jumla. Kwa hiyo, hali ya kuwa na imani hasi au chanya kuhusu lugha lengwa huathiri hali ya kujifunza lugha inayohusika. Hali ya hisia walizonazo dhidi ya lugha huibua ugumu fulani katika kujifunza lugha husika pamoja na utamaduni wake. Mwelekeo chanya umekuwa kizungumkuti katika ujifunzaji wa Kiswahili nchini Uganda. Si kwa wazungumzaji lugha lakini kuhusu lugha yenyewe. Hivyo huenda changamoto ambazo wafanyabiashara walikumbana nazo wakati wa kujifunza Kiswahili ilikuwa mwelekeo hasi dhidi ya lugha ya Kiswahili na sio wasemaji wa lugha ya Kiswahili.

William (1979) anasema, utambuzi na uendelezaji wa fonimu ndiyo changamoto kubwa katika ujifunzaji wa lugha ya pili. Ujifunzaji wa fonimu hutokea kwenye mazingira ambayo fonimu hizo zinasikika na kufundishwa. Fonimu zile ambazo hueleweka kwa urahisi ni zile ambazo zinatokana na L1. Hii inamaanisha tunajifunza sauti ambazo mwanzo zinasafirishwa katika ubongo kupokea ujumbe kutoka kwa lugha mahsus. Fonolojia ya Kiswahili ina sauti zake ambazo zimeainishwa kwa kuzingatia mahali pa kutamkia na jinsi ya kutamkia. Kwa wale ambao ni wabantu huenda ikawa rahisi kujifunza hizi foni. Kwa mfano huenda ikawa rahisi kwa Muganda kujifunza Kiswahili kwa sababu kuna foni ambazo pia kiganda

kunatokea mahali pamoja pa kutamkia tofauti na namna ujifunzaji unavyokuwa kwa Mnailoti. Mifano ni kama katika jedwali 2.1 hapa chini.

### **Jedwali 2.1: Mifano ya sauti zinavyotamkika**

<b>Jinsi ya kutamka Kiganda</b>		<b>Kiswahili</b>	<b>Kinailoti</b>
Vipasuo	P,b td c k	P b, td, kg	P, b td/th,dh c/c k, g
Vikwamizi	h ya glotaf, v, s, z ky	h ya glota f, v, th, dh	f,
Ving'ong'o	M, n, ny, mb, ng'	M, n, ny, mb, ng'	M, n ny, ng' Mb/nd
Viyeyusho	y,w, i	y,w	y, i,j
Vilainisho	L	L	L
Vimadende	-	R	

### **Chanzo cha data: Watafiti**

Mfano wa hapo juu unaonesha dhahiri kwamba ni rahisi mbantu kujifunza lugha ya Kiswahilikuliko mnailoti. Maneno mengi ambayo yanaanza na /s/ mara nyingi wao hutamka /ch/halafu mahali pana /ch/ wao huweka /c/ kwa mfano [chai] wao husema [eccai] wakati wabanu wanasema [chai]. Vile vile hawana sauti /h/ ya glota ndiyo maana katika maneno mengi ya Kiswahili ambayo hana sauti /h/ wao hutumia /a/. Hali kama hii huleta changamoto wakatiwa kujifunza Kiswahili kama lugha ya pili na lugha ya kibiashara. Mkude (2005) anasema kwamba lugha za kibantu huwa na vipengele vinne ambavyo vinafanana licha ya Kiswahili kuwa na misamiati mingi iliyokopwa kutoka lugha nyingine. Kipengele cha kwanza ni kwamba nomino zote lazima ziwe zimepangwa katika makundi tofauti kutegemea lugha bila kujali chimbuko lake. Kipengele cha pili ni kwamba vitenzi bila kujali chimbuko lake huruhusu uundaji wa vitenzi vingine ama nomino. Katika kipengele cha tatu Mkude (Keshatajwa) anaelezea kwamba kuna kubadilishana nafasi kati ya nomino na kitenzi halafu kipengele cha mwisho ni kwamba lugha zote za kibantu huwa na silabi wazi.

Arcand (1996) anasema changamoto ya pili katika ujifunzaji L2 ni kujifunza msamiati wa L2 kwa kutumia maelezo ya L1. Kujifunza maelezo ya muundo wa L1, dhana huwa inajijenga yenewe katika mzungumzaji kutokana na L1 ila ni vigumu kwa mtu mzima kufikiria katika L1 halafu azungumze katika L2 Anaendelea kusema kwamba ndiyo maana idadi kubwa ya watu wanaoshindwa kujifunza L2 ni mionganoni mwa watu wazima. Utafiti wa Arcand unakaribiana sana na utafiti wetu hasa tukiegemea katika jumuiya ya watafitiwa ambao

tayari ni watu wazima ambao wanafanya biashara jijini Kampala. Arcand (keshatajwa) alifanya utafiti kuhusu wanafunzi ambao walisoma masomo ya watu wazima katika mfumo rasmi wa ujifunzaji. Utafiti wetu unaangazia wanafunzi walio watu wazima lakini mafunzo yao hutokeea kwa ajili ya kazi wanayoifanya ambayo ni biashara.

Utafiti wa Arcand (1996), hautofautiani sana na wa Eckert (2003) ambaye alirejelea Charmot (1987) kwa kusema kwamba mtu hupata lugha katika umri maalum, umri huu mtu hupata lugha pasi na kukusudia. Inakisiwa kuanzia miaka miwili hadi umri wa kubalekhe kwake. Muda huo uwezekano wa kupata /kjufunza lugha ya pili inakuwa vigumu au haiwezekani kabisa. Wanasaikolojia wanasesma kwamba ubongo uliofika umri wa kubalekhe huwa unapoteza uwezo wa kupata lugha. Kama ilivyo kulingana na Katiba ya Uganda (1995) mtu mzima ni yule ambaye ametimiza miaka kumi na nane na wala siyo kujikita katika kigezo cha kubalekhe tu. Kulingana na maelezo ya wataalamu hawa hakuna mtaalamu ambaye ameibuka na hoja ya kisayansi kuthibitisha ukweli kwamba mtu akisha balekhe inakuwa vigumu kjufunza L2. Oxford na Nyikos (1989) walifanya utafiti juu ya wanafunzi 1,200 ambao walikuwa wakijifunza lugha tofauti katika Chuo Kikuu cha Midwest Merikani ambapo waligundua kwamba athari ya motisha ilikuwa mojawapo wa changamoto miongoni mwa wajifunzaji L2. Utafiti huu unawekea mkazo modeli ya Gardener (2000) anaposema kwamba motisha chanya hufanya ujifunzaji wa lugha kuwa rahisi ila motisha hasi hufanya ujifunzaji wa lugha ya pili kuwa mgumu. Oxford na Nyikos (1989) waligundua kwamba athari ya motisha iliathiri vigeugeu vya mikakati ya ujifunzaji wa lugha ya pili. Utafiti wa kina Oxford na Nyikos (Keshatajwa) ulichunguza wanafunzi wa kiwango cha juu amba ni wanafunzi wa chuo. Wanafunzi hawa walikuwa wakijifunza lugha tofauti. Malengo ya chuo ya kufundisha wanafunzi lugha tofauti ni tofauti na utafiti wetu ambao uliangalia jamii ya wafanyabiashara jijini Kampala bila kuhusisha viwango vya ujifunzaji katika mfumo rasmi wa elimu.

Hulka ya mtu binafsi huathiri namna ya kujifunza L2. Hulka hutokana na hali ya kukubali kitu au kuchukizwa kwa sababu ya kisaikolojia. Sababu hii hutokana na namna mtu yuko tayari kupokea ama kutenda jambo fulani. Utafiti wa Ehrman na Oxford (1989) kuhusu namna saikolojia huathiri ujifunzaji lugha kwa wanafunzi walio watu wazima ulionyesha kwamba kuna namna matumizi ya mikakati na hulka za mtu huathiri namna ya kujifunza L2. Utafiti huu una uhusiano lengwa na utafiti wetu kwani kundi ambalo lilifanyiwa utafiti ni watu ambao wana hulka tofauti na mwelekeo tofauti dhidi ya ujifunzaji wa lugha ya pili.

Kwa vile ni watu wazima ilikuwa bayana pia utafiti kubainisha namna waliweza kukabiliana na changamoto hizo ili kufanikisha ujifunzaji wa Kiswahili kibiashara.

Oxford na Nyikos (1989) waliendelea kusema kwamba, kuna changamoto za L2 ambazo pia ni kipingamizi katika ujifunzaji wa L2. Unajaribu kujifunza sarufi kuptitia maelezo ya lugha ya kwanza. Maelezo shadidifu yalitolewa na Chomsky (1988) ambaye alisema kwamba mtu mzima anapo jifunza lugha ya pili inabidi atumie mbinu nyingine kwa sababu sarufi bia ishatumika haimsaidii tena. Hapa inakuwa ni vigumu kwa sababu watu wazima hawawezi kuanza kufikiria kwa lugha ya kwanza halafu wakazungumza kwa lugha ya pili. Hili linafanya kunakuwa na idadi kubwa ya watu wazima ambao hawawezi kujifunza lugha ya pili. Kwamba watoto hujifunza L2 pasi kujuwa kufahamu wanajifunza lugha hiyo, wao hujikuta tu wanazungumza bila kukusudia. Maelezo ya Oxford na Nyikos (washatajwa) na Chomsky (keshatajwa) yaliongoza katika kukusanya data kuhusu changamoto zinazokabiliwa na wafanyabiashara katika kujifunza Kiswahili kibiashara na namna ya kutatua changamoto hizo. Fromkin na Rodman (1993), wanasema kwamba lugha ya kimama huathiri ujifunzaji wa L2 kwa sababu watu wengi huingiza sauti na kanuni za lugha zao za kimama katika ujifunzaji wa L2. Corder (1967) naye alikubaliana na kina Fromkin na Rodman (1993) na Fasold na Linton, (2006) kwa kusema kwamba makosa mengi ambayo hufanywa na wanafunzi hutokana na kuathiriana kwa lugha mama. Wataalamu hawa waliangalia wanafunzi ambao wanajifunza sheria za lugha kwa ajili ya kujifunza lugha sanifu. Pili utafiti wao ulijikita katika watoto ambao walikuwa wanajifundisha L2 ambayo si Kiswahili. Vile vile hawakutoa mwelekeo wa madhumuni na muktadha wanafunzi hawa walikuwa wakijifunzia. Hoja hizi zilitupa msukumo wa kutathmini ikiwa lugha za kiasili zili kuwa kipingamizi kwa wafanyabiashara wakati wa kujifunza Kiswahili kibiashara.

Gass na Selinker (1994), wanakubaliana na Benzier (1961) kwamba utendaji wa wanafunzi katika L2 huathirika na lugha moja ama nyingine ambazo wanafunzi wamekwisha kufahamu kwa mfano matamshi, fonolojia na sauti ya L1. Katika hali hii inakuwa rahisi kwa mwanafunzi kutumia njia hiyo hiyo wakati wa kujifunza lugha ya pili. Kwa mfano inakuwa rahisi kwa mwanafunzi kuoanisha mofimu zilizokaribiana ili kujuwa kutamka neno jipya katika lugha lengwa. Kwa mfano ni rahisi mjifunzaji lugha ambaye lugha yake ya kwanza ni kiganda kuweza kutamka (Mu-ntu) badala ya (M-tu) kwa sababu mofimu (MU) na (M) zote zinatokea katika nafasi moja kimofolojia, vile vile utapata neno chakula linatamkika kama kyakulya kwa sababu (cha na kya) karibu zinatokea katika mazingira sawa.

Gass na Selinker (1994) wametilia mkazo kwa kusema mjifunzaji L2 hujaribu kutoa mila zote za L2 kutokana na mambo teule matano ya mchakato wa akili. Miongoni mwa hayo mambo ni uwasilishaji wa lugha, yaani baadhi ya istilahi, mamlaka na utaratibu wa L2 unaweza kutokana na uwasilishaji kutoka L1. Hapa inadhihirika kwamba kuna vitu tofauti vinavyofanyika katika L1 kwa mfano kuakifisha sentensi ambapo hufanyika katika L2, kuwasilisha matumizi ya sintaksia yaliyomo pasi na utumiaji wa lugha sahihi. Cummins (1979) anasema pale ambapo kuna mazingira mazuri huongeza ubora wa utendaji na uzungumzaji wa L2. Cummins (Keshatajwa) anasisitiza kwa kusema kwamba mazingira mazuri ni pale ambapo mjifunzaji wa L2 anaweza kutiwa changamoto na wanaoifahamu lugha hiyo. Hali ambayo humfanya mwanafunzi kujitahidi kufanya mazoezi ya mara kwa mara katika L2. Utafiti wa kina Gass na Selinker na ule wa Cummins (washatajwa) hujaweka bayana wakati wa kuwasilisha na mazingira mazuri ya uzungumzaji wa L2. Watafitiwa wetu ni wale ambao wanafanya kazi zao sehemu za kuendesha biashara. Ni papo hapo ndipo wanajifunzia Kiswahili kama lugha ya biashara.

Umilisi wa kupata lugha ya pili miongoni mwa watu wazima hutofautiana na jinsi watoto hupata lugha. Hili limefanya watafiti kuunda nadharia nyingine ambayo inaitwa nadharia tete ya kipindi cha kuhakiki (CHP), (Garibaldi, 2013). Brown (2012) amefafanua zaidi kwa kusema hiki ni kama cha kibayolojia cha maisha wakati lugha inaweza kupatikana kwa urahisi zaidi ya kufikia ugumu wake wa kupatikana. Kulingana naye nadharia hii inaangalia wakati mgumu ambao lugha inaweza kupatikana, ambao ni wakati wa kubalekhe. Wataalamu hawa wanasema kwamba hali hii imechanganya wengi kwa kufikiria kwamba ukifika umri fulani tuseme kati ya miaka 12-13 huwa umechelewa kupata L2. Hakuna uthibitisho ulioonyeshwa kwamba mtu hubalekhe kati ya umri wa miaka 12 hadi 13. Vivyo hivyo ujifunzaji lugha ni mchakato ambao unaendelea kutegemea mtu anatangamana na jamii ya aina gani. Ni vigumu kushikilia hoja ya kubalekhe kama kigezo cha kujifunza L2 na kusahau kwamba kuna vigezo tofauti ambavyo hulazimu mtu kujifunza L2.

Kwa upande wake Gardner (2007) anasema ujifunzaji L2 huwezi kuwa unaathiriwa tu na kipengele kimoja ama viwili vyta umri. Mtoto ambaye amelelewa katika mazingira ya lugha mbili au zaidi huwa na uwezo wa kujifunza/kupata zaidi ya lugha moja. Wanaweza kuwa na uwezo wa kuandika na kusoma lugha zote. Anasema hata hivyo hili hutendeka kwa ajili ya kuwa na motisha ya kujifunza angalau lugha moja awe kwa watoto au watu wazima. Alisisitiza kwamba tuwe tukijiuliza kama kweli mjifunzaji L2 ana motisha ya kujifunza

lugha anayojifunza. Hivyo kwa muktadha huu alifikiria kwamba kando na kuangalia umri na labda uana, mazingira huchangia pakubwa katika ujifunzaji wa L2. Mwelekeo wa Gardener (2007) haukufumbiwa macho na utafiti huu kwani ulisaidia kuelekeza utafiti huu namna mazingira ya kibiashara na soko yalisaidia ujifunzaji wa Kiswahili kama lugha ya pili. Aidha mchango wa kazi ya Gardener (keshatajwa) ulisaidia kukusanya data iliyohusika na mazingira kama mojawapo ya changamoto zilizochangia katika kukwamiza ujifunzaji wa Kiswahili kama lugha ya biashara mionganii mwa wafanyabiashara jijini Kampala, Uganda.

Kwa muhtasari sehemu hii ilishughulikia tahakiki juu ya changamoto zinazokumba wanaojifunza L2. Tafiti mbalimbali zimeonyesha kwamba wanafunzi wanaojifunza L2 hukutana na changamoto nyingi mionganii mwazo zikiwa ni pamoja na, kuenea kwa lugha za mtaani ambazo hazifuati kanuni mwafaka za sarufi, kutothamini lugha ya Kiswahili, wengi hawana ustadi wa kupokea L2, mitazamo hasi dhidi ya L2, mielekeo tofauti ambayo inaweza kupelekea kudumaza ujifunzaji wa L2, utambuzi na uendelezaji wa fonimu, kujifunza misamiati ya L2, kujifunza msamiati wa L2, umri kwa kutumia maelezo ya L1, hulka ya mtu binafsi, uhaulishaji wa L1 katika L2 na changamoto za L2 zinazokwamiza ujifunzaji wake (Wang 1999; Ontieri, 2010; 2000; Mulei, Amukowa & Asiko, 2021; Wataalamu mbalimbali wamejadili namna wajifunzaji L2 hasa wanafunzi waliko katika mfumorasi wa ujifunzaji hukumbwa na changamoto wakati wa kujifunza L2 ambapo ni tofauti na utafiti ambao tuliofanya unaohusu changamoto zinazokumba wafanyabiashara wanaojifunza Kiswahili kama lugha ya biashara (Mukuthuria, 2006)

## **2.5 Mikakati ya namna ya kutatua changamoto zitokanazo na ujifunzaji wa lugha ya pili**

Nor-Farhana na Hamida (2003) walishughulikia changamoto ambazo ziliwakumba wanafunzi wa Taasisi ya Melaka ambao ni wa Malaysia wakati wa kujifunza Kiingereza, walipendekeza kwamba ni bora wanafunzi kuwekwa katika makundi madogo madogo ambayo yangeliwasaidia kujifunza Kiingereza. Kuna hali ambayo inawezekana na kuna hali ambayo ni tatanishi. Taasisi ya Melaka iliwfundisha wanafunzi wao Kiingeeza labda kwa ajili ya kuijiendelza baadaye masomoni. Kwamba wasije wakakwama endapo wamepata fursa za kuenda nchi zilizo nje ya bara la Afrika labda kwa kuijiendeza kimasomo ama kupata umilisi wa kuwasiliana katika kiingereza. Changamoto za wafanyabiashara jijini Kampala ni tofauti sana na za wanafunzi wa Melaka. Tena ni bayana itambulike kwamba kwa baadhi ya wafanyabiashara jijini Kampala, Kiswahili ni L.3 (Jjinga na Bakize, 2021) kwao. Hivyo kuna

uwezekano wa kukumbana na changamoto nyingi mno kuliko wanafunzi wa Melaka ambao tayari wana waelekezi.

Utafiti uliofanywa na Zehler (2005) kuhusu wanafunzi wa awali ambao walikuwa wakijifunza Kiingereza kama L2, alisema kwamba mara nyingine wanafunzi wenyewe hujaribu namna ya kusuluhisha changamoto za ujifunzaji wa L2 kwa kuomba wazungumzaji wa lugha lengwa kuwasahihisha kila wakati wanapokuwa katika mawasiliano. Anasema kwamba katika harakati ya muingiliano, mjifunzaji anakuwa na uhuru wa kuuliza wasemaji wa L.2 kuwafafanulia msamiati ambao ungeonekana kuwa mgumu. Dulay na Burt, (1973) Cook, (1994); & Schmidt, (1994) wamependekeza kwamba wanafunzi tofauti hukumbwa na changamoto tofauti. Pili huenda changamoto itokane na mwanafunzi mwenyewe (Gardener, 2000) kuwa na motisha hasi juu ya lugha ambayo anajifunza. Kwa mantiki hiyo kubadilisha mwelekeo (Krashen, 1987 na Gardener 2000) wa mwanafunzi kama huyo huwa vigumu.

Comstock & Kamara (2003) na Schwarz& Terrill (2000) wanasema kwamba ni muhimu wajifunzaji ambao hawafanyi maendeleo yanayotarajiwu kubaini sababu mbazo zinapelekea kutoendelea kimasomo. Mara nyingi changamoto zinazoibuka zinaweza kuhusisha ufinyu wa ujuzi, uwezo wa kuhimili ujifunzaji, mazoea ya kutumia lugha na kubaini nyenzo mbalimbali zinazowezekana katika ujifunzaji wao. Schwarz & Terrill (2000) wameshadidia kwa kusema kwamba mara nyingi wajifunzaji wa L2 huwa hawatambui matatizo yao ila kwa kuwasaidia ni vyema kuwashurutisha kuwa na mazoea ya kutumia lugha lengwa mara kwa mara. Wanaendelea kusema kwamba ni bora pia kupata nyenzo za kusikiliza na kuongea ambazo zinafanikisha ujifunzaji wa L2. Krashen (1987) katika mhimili wake wa tatu anasema kwamba katika mazingira asilia ambayo mjifunzaji L.2 anajaribu kujifunza kwa kuigiza wazungumzaji lengwa, hujikuta wanajitokeza na makosa. Hata hivyo makosa hayo huenda yakapotea kadri mzungumzaji anavyotangamana na wazungumzaji wa lugha lengwa. Gass na Selinker (1994) na Gardener (2000), wanasema wanafunzi kama hao wanastahili kupewa moyo na motisha kwamba baada ya muda si mrefu watakuwa washajifunza L2. Wataalamu hawa wanapendekeza kwamba ni vyema pia kuwaachia wajifunzaji wa L.2 kujichangulia nyenzo ambazo wanaona zitawafaa katika ujifunzaji wa L2 bila kuchaguliwa.

Gass (2022), wanakubaliana na maelezo ya awali ya Benzier (1961) kwamba utendaji wa wanafunzi katika L2 huathirika na lugha moja ama nyingine ambazo wanafunzi wamekwisha

jua kwa mfano matamshi, fonolojia na sauti ya L1. Katika hali hii inakuwa rahisi kwa mwanafunzi kutumia njia hiyo hiyo wakati wa kujifunza lugha ya pili. Kwa mfano inakuwa rahisi kwa mwanafunzi kuoanisha mofimu zilizokaribiana ili kujua kutamka neno jipya katika lugha lengwa. Kwa mfano ni rahisi mjifunza lugha ambaye lugha yake ya kwanza ni ni kiganda kuweza kutamka (Mu-ntu) badala ya (M-tu) kwa sababu mofimu (MU) na (M) zote zinatokea kwa nafasi moja kimofolojia, vile vile utapata neo chakula linatamkika kama kyakulya kwa sababu (cha na kya) karibu zinatokea katika mazingira sawa. Corder (1967-1983) pamoja na Zehler (2005) wanasema kwamba mara nyingine huwa ni muhimu kuwaacha wanafunzi kuendeleza kuhamisha sheria kutoka L.1 ili kuwasaidia katika ujifunzaji wa L.2.

Kulingana na Long (1990), anasema mtagusano na motisha wa kufunza lugha ndiyo hufanikisha ujifunzaji wa L2. Anatahadharisha wajifunzaji wa L2 kwamba siyo lazima wawe weledi wa fonolojia, mofolojia na sintaksia ya lugha hiyo ila washughulike na maana ya kisemantiki kulingana na mazingira ambayo wanatumia lugha hiyo. Anaendelea kusema ujifungaji katika kanuni na vipengele vya lugha hukwamisha ujifunzaji wa lugha hiyo.

Gardener, (1985, 2000, 2010a) ambaye katika modeli yake anasema kwamba mwelekeo kuhusu muktadha wa kujifunza lugha na mwelekeo kuhusu lugha hukwaza ujifunzaji wa lugha. Anasema kwamba pale ambapo mjifunzaji ana mweleko hasi inabidi apewe muda na kutiwa moyo. Aelezwe umuhimu wa kujifunza L2 kutegemea nini ambacho atanufaika na ujifunzaji huo na nini anaweza kupoteza wakati akikosa ujifunzaji wa L.2.

## 2.6 Hitimisho

Sura hii ilishughulikia tahakiki ya yaliyoandikwa kuhusu mada ya utafiti. Utafiti ultangulia na marejeleo ya jumla juu ya, mikakati ya jumla ya ujifunzaji wa lugha ya pili ilihakikiwa ambayo ni pamoja na kuonyesha maridhiano au pengo la kuzibwa na mada ya utafiti. Tahakiki hii ilienda sambamba na mitindo ya jumla ya ujifunzaji L2 na kuonesha namna vipengele vyote viwili hushirikiana katika ujifunzaji wa L2 vikielekea kukubaliana na mada na madhumuni ya utafiti. Mjadala wa mapitio ulionyesha namna mikakati kama; kuomba msaada ama waziwazi au kisirisiri, kuchanganya msimbo, utambuzi, mpango binafsi, kumbukizi, kufidia, mawasiliano, upatikanaji tena na mkakati wa mazoezi inaweza kufanikisha ujifunzaji wa L.2. Mikakati hiyo inavyoweza wezesha ujifunzaji wa L2 hasa Kiswahili kwa wafanyabiashara kuititia tafsiri kutoka lugha chanzi hadi L2, uchopekaji wa silabi katika maneno, urudiaji ruduijaji, udondoshaji wa baadhi ya irabu ama silabi, kutumia

masimulizi, uwasilishaji, mawasiliiano baina yao na wazungumzaji wa lugha wanayojifunza, mkabala wa tafsiri, kuwasiliiana na utambuzi kwa muegemeo wa nadharia ya Krashen na Gardener na pia wataalamu mbalimbali ambao walikaribia ama kubaliana na mawazo ya wananaadharia hizo. Mitindo mbalimbali kama dukuduku. nia, mwelekeo, hulka, unyamavu na uongeaji huweza kuchangia katika ujifunzaji wa L.2.

Sura hii vile vile ilihakiki mapitio ya maandishi kuhusu changamoto zilizoweza kutinga ujifunzaji wa lugha ya pili ikiwemo kuenea kwa lugha za mtaani ambazo hazifuati kanuni mwafaka za sarufi, kutothamini lugha ya Kiswahili, wengi hawana ustadi wa kupokea L2, mwelekeo hasi dhidi ya L2, mielekeo tofauti ambayo inaweza kupelekea kudumaza ujifunzaji wa L2, utambuzi na uendelezaji wa fonimu, kujifunza misamiati ya L2, umri na jinsia kama vigezo vya kujifunza L2, uhaulishaji wa L1 katika L2 wakati wa kujifunza L2.

Mjadala mkubwa ambao umejitokeza ni kuhusu yaliyoandikwa ya jumla kuhusu, mikakati na mitindo ya jumla ya ujifunzaji wa L2 mifano mingi ikitolewa kwa wanafunzi ambao walikuwa wakijifunza Kiingereza kama L2 na changamoto za jumla za ujifunzaji wa L2 hoja ambayo bado haijashughulikiwa ni mikakati, mitindo na changamoto za ujifunzaji wa Kiswahili kwa wafanya bishara jijini Kampala kama lugha ya biashara.

## **SURA YA TATU**

### **MBINU ZA UTAFITI**

#### **3.1 Utangulizi**

Sura hii ilishughulikia mpangilio na utaratibu wa mbinu za utafiti zilizotumiwa, muundo wa utafiti, eneo la utafiti, kundi lengwa, mchakato wa usampulishaji na sampuli, sababu za kuchagua sampuli, utaratibu wa kukusanya data, mbinu na vifaa vya kukusanya data, namna ya uwasilishaji na uchanganuzi wa data.

#### **3.2 Muundo wa Utafiti**

Utafiti huu ulizingatia muundo mseto. Muundo mseto kulingana na Creswell (2008) ni ule ambao unahusisha kwa pamoja muundo wa kithamano na kiwingi idadi. Katika utafiti huu takwimu elezi na kithamano zilifanikisha mikakati na mitindo mbalimbali ya L2 namna ilitumiwa na changamoto ambazo walikumbana nazo wakati wa kujifunza Kiswahili kama lugha ya biashara. Muundo huu unaafiki kupata data za kimsingi (Bryman 2015) kutoka kundi lengwa. Kwa upande mmoja wataalam ambao kwao wanashadidia muundo wa kithamano ni pamoja na (Maxwell, 1992; Crotty, 1998; Pring, 2000), Cohen na Weaver (2011) Denzin na Lincoln (2008). Imani yao ni kwamba watu ni wabunifu na hujenga jamii ya ukweli. Wanasema kwamba ulimwengu wa jamii unatakiwa kufanyiwa utafiti kwa hali ya kawaida kupitia kwa watafitiwa bila kuhitalifiana na watafiti. Kwa mujibu wa wataalamu hawa, mtafiti anastahili kuwapa watafitiwa uhuru wa kuelezea hali ilivyo kuliko mtafiti kushinikiza kile anachotaka mtafitiwa kusema. Wanafafanua kwamba unapotumia muundo elezi, utafiti huwa unazingatia historia ya mtu, usuli, uana jamii na utamaduni wa watu utafiti unapofanyika. Mbinu wanazotumia hasa katika usampulishaji, ni usampulishaji wa kimakusudi halafu wanachagua watafitiwa ambao watatoa data ya kuegemewa. Wao hutumia mbinu tofauti tofauti kukusanya data za kisifa.

Aidha, muundo wa takwimu elezi husaidia katika upatikanaji wa ufahamu mpya ulio tofauti na hali inayojulikana (Bryman, 2004). Data zinapatikana hupangwa kitakwimu. Fairclough, 2004 anasema kuwa uchanganuzi wa takwimu elezi huhuishwa kutimiza uchanganuzi wa kithamano huku uchanganuzi wa takwimu elezi hutumiwa kusitiza vipimo pamoja na vipengele vinavyokuwa vinatafitiwa.

Muundo huu uliwezesha utafiti huu kubaini kiwango cha utokeaji wa mikakati na mitindo kiidadi kuzingatia asilimia. Utafiti huu ultumia takwimu elezi na ya kithamano kutokana na

umuhimu wake kama ilivyoelezwa na Creswell (2008) na kushadidiwa na Denzin na Lincoln (2008) wanaosema kwamba hakuna mshiki wowote kutumia muundo mseto wakati wa utafiti wowote ule. Kwa kuhusisha muundo mseto ameainisha mbinu mwafaka ambazo zinaweza kutumiwa wakati wa kutumia muundo mseto katika utafiti. Mbinu zilizoanishwa na Tashakkori na Creswell (2007) ni pamoja na uchunzaji, (wahusika na wasiohusika), hojaji na dodoso (mahojiano ya ana kwa ana, vikundi viini, simu na mahojiano ya mtandaoni), majarida, picha, video na picha.

Muundo mseto ulishirikisha miundo miwili ya Kiwingiidadi na Kithamano. Muundo wa kiwingiidadi ulitumika kukusanya dada za kitwakimu kutoka nyanjani, kupanga data kiasilimia kuzingatia mara za kutokea kwa mikakati na mitindo ya kujifunza na kutumia Kiswahili, changamoto za ujifunzaji na matumizi na mikakati ya namna ya kutatua changamoto husika. Mikakati na mitindo, changamoto na mikakati ya utatuvi iliopatikana kiwingi idadi ilielezwa kutumia muundo wa kimaelezo kuonyesha hali jinsi inavyoelezwa na kufafanuliwa na wasailiwa wafanyabiashara nyanjani. Data hizi ziliwasilishwa kutumia majedwali na kumaelezo.

Aidha, muundo wa kithamano nao ulitumika kukusanya data kutoka nyanjani. Data za kithamano zilikusanywa kutoka kwa wasailiwa ana kwa ana kutambua mikakati na mitindo, changamoto na mikakati ya namna ya kutatua changamoto za ujifunzaji na matumizi ya lugha ya Kiswahili. Data za mikakati na mitindo ya ujifunzaji, changamoto na mikakati ya ujifunzaji na matumizi ya Kiswahili Kibiashara ndio iliyodondolewa kutohana na usaili wa ana kwa ana, uchunzaji na dodoso. Data iliopatikana nje ya madhumuni ya utafiti huu ilitupiliwa mbali na ile ya mikakati na mitindo ya ujifunzaji na matumizi, changamoto na mikakati ya utatuvi pekee ndiyo iliyozingatiwa. Kwa ajili ya kupata data za kimsingi zaidi mahojiano ya ana kwa ana yalifanyika kwa wasailiwa wafanyabiashara teule. Data hizo zilipangwa, zikachanganuliwa na kuwasilishwa kwa kutumia muundo mseto. Data za hojaji zilichanganuliwa kiwingi idadi na kufafanuliwa kimaelezo wakati data za mahojiano ziliwasilishwa kithamano. Data zilizopatikana zilihusu mikakati na mitindo ambayo wafanya biashara hutumia wakati wa kujifunza Kiswahili kama lugha ya biashara. Vile vile changamoto zilizo wakumba wafanyabiashara wakati walijifunza Kiswahili kama lugha ya biashara na namna ya kutatua changamoto hizo.

### **3.3 Eneo la Utafiti**

Eneo la utafiti liligawanyika katika sehemu mbili. Eneo la kijiografia ambapo ni jijini Kampala katika Ekedi ya Mukwano, Simlaw International Limited na soko la Kikuubo. Eneo la jijini Kampala lilichaguliwa kwa sababu ni eneo ambalo lina biashara nyingi na maduka makubwa mengi pamoja na wafanyabiashara wengi wanaotoka nje ya Kampala na mataifa jirani yanayotumia Kiswahili kama lugha ya kibiashara. Utafiti huu ulichagua Ekedi mbili za Ekedi ya Mukwano na Simlaw Uganda Limited na Soko moja la Kikuubo. Masoko haya yalichaguliwa kutokana na umaarufu wake, ukubwa, bidhaa na huduma zinazopatikana katika maeneo haya na uanuwai wa wafanyabiashara wanaofika na wanaofanya biashara katika eneo hili. Mbali na kuchunguza mikakati na mitindo ya matumizi ya Kiswahili, utafiti huu ulichagua wafanyabiashara wala sio biashara au wahusike wengineo. Wafanyabiashara hawa walichaguliwa kwa sababu wao ndio wanaohusika na shughuli za ununuzi na uuzaji wa bidhaa na huduma. Aidha, ni wafanyabiashara hawa wanaotangamana mionganoni mwao pamoja na wateja wanaotoka maeneo mbalimbali ya nchi na ujirani wa nchi. Ni wao wanaochagua lugha ya kutumia katika biashara na athari zinazotokana na matumizi hayo huwakumba wao. Data zilikusanywa kwa kuhusisha wafanyabiashara ambao walikuwa wakifanya biashara zao katika maeneo hayo.

Mbali na eneo la kijiografia utafiti huu ulishughulisha pia eneo la kiakademia ambapo ujifunzaji wa Kiswahili kama lugha ya pili katika kufanikisha biashara uliangaziwa. Data ilikusanywa kulingana na madhumuni ya utafiti kuhusu mikakati, mitindo na changamoto za kujifunza Kiswahili kama lugha ya biashara mionganoni mwa wafanyabiashara jijini Kampala, Uganda. Aidha, mikakati ya utatuza ilishughulikiwa. Utafiti huu upo katika taaluma ya isimu ya ujifunzaji na ufundishaji wa lugha ya pili na isimujamii. Data iliyokusanywa ilishabiki namna wafanyabiashara hutumia mikakati na mitindo ya ujifunzaji L2 kujifunza Kiswahili kwa ajili ya biashara. Vile vile kuangazia changamoto walizokumbana nazo wakati wa kujifunza Kiswahili kibiashara na namna ya kuzitatuwa.

### **3.4 Idadi lengwa**

Cooper (1989) kwa kumrejelea Mugenda na Mugenda (2003) anasema kundi lengwa ni wahusika wote, mtu mmoja, kikundi au elementi ambazo mtafiti alikusudia kuzihusisha katika utafiti wake. Kundi lengwa ni jumla ya watu wote ambao huhushishwa katika utafiti. Kundi lengwa katika utafiti huu ni wafanyabiashara wote wanaofanya biashara jijini Kampala. Kundi hili liliteuliwa kulingana na sifa ya kuwa wao

wanatangamana mionganini mwao pamoja na wateja wanaotoka maeneo mbalimbali ya nchi na nchi jirani wanaotumia lugha ya Kiswahili. Ni wao wanaochagua na kuathirika na lugha ya kutumia katika biashara. Mathalani, Mikakati na mitindo ya kujifunza na kutumia lugha ya Kiswahili kibiashara pamoja na changamoto za ujifunzaji wa Kiswahili kama lugha ya biashara hutokana na utangamano na wateja wao wanaotumia Kiswahili.

Utafiti huu ulizingatia rekodi ya data za wenyekiti wa Ekedidi 13 na masoko 3 ya eneo la jijini Kampala ya kati ya mwaka 2021, KACITA (2019), iliyotambua kuwa idadi ya wafanyabiashara katika Ekedidi na masoko kwa mujibu wa usajili wa eneo hili ni 7302. Jijini Kampala ya kati, utafiti huu ultambua Ekedidi 2 kati ya 13 na soko 1 kati ya 3. Kwa hivyo, idadi lengwa ya wafanyabiashara waliohusika katika utafiti huu ni wafanyabiashara 1500 kutoka Ekedidi 2 na Soko moja. Ekedidi ikiwakilishwa na idadi ya wafanyabiashara 673 na soko likiwakilishwa na idadi ya wafanyabiashara 827 Ekedidi na soko iliyohusika ni ile inayoshirikisha wafanyabiashara wa ndani na wale wanaotoka nje ya nchi za Afrika mashariki wanaokuja kuuza na kununua bidhaa na huduma anuwai. Kwa jumla, kundi lendwa lililoteuliwa kwa ajili ya utafiti huu, ni wafanyabiashara elfu moja na mia tano (1500) ambaao waliwakilisha kundi zima la wafanyabiashara jijini Kampala Uganda kutoka Ekedidi mbili na soko moja.

### **3.5 Usampulishaji na Sampuli**

Usampulishaji na Sampuli ni mchakato wa kuchagua idadi ndogo ya watu (Barbie 1992, Field, 2005 Mugenda na Mugenda 2012, Cooper na Schindler 2001) ambaao watawasilisha idadi kubwa katika utafiti. Usampulishaji ndiyo kitendo chenyewe cha kufanya uteuzi wa sampuli ya utafiti husika (Myers na Mitchel, 2004). Kwa hivyo, sampuli inafasiriwa kama kundi dogo la watafitiwa lililochaguliwa kutoka katika idadi kubwa ya wanajamii ama vitu vyovvyote vile ambavyo mtafiti anataka kuvitafiti (Adam na Podmenik 2005, Babbie 1992). Sampuli ni sehemu ya idadi ya watu ama vitu ambavyo mtafiti anavutiwa navyo katika kukusanya taarifa zitakazotoa hitimisho la utafiti wake (Babbie, 1992). Gomm (2000) ameshadidia kwa kusemakwamba ni heri kuwa na sampuli ndogo ambayo itakupatia taarifa zilizokusudiwa kuliko kuwa na sampuli kubwa ambayo haitakupa taarifa sahihi. Ili kuwezesha uteuzi wa kundi hilo dogo kutoka katika kundi kubwa zipo (Gay, Mills na Airisian, 2006) mbinu za aina mbalimbali za usampulishaji. Muhimu zaidi ni kuwa na idadi kubwa halafu baadaye mtafiti anaibuka na sampuli husika ya utafiti itakayo fanikisha ukusanyaji data. Usampulishaji katika utafiti huu ulifanywa kwa kutumia mbinu ya

usampulishaji dhamirifu kwa kurejelea aina yake ya usampulishaji wa mpokezano ambapo uteuzi dabwa ulitumiwa kuteua wasailiwa.

Katika utafiti huu, wahusika wa jumla waliohusika ni wafanyabiashara wanaotumia Kiswahili katika kuendeleza biashara zao. Wasailiwa hawa ni wale wanaofanya biashara katika Ekedи na masoko ya jijini Kampala. Utafiti huu ulihusisha wasailiwa wafanyabiashara 306 kutoka kundi nzima la wafanyabiashara 1500 waliochaguliwa kutumia mchakato wa uteuzi wa sampuli kwa kurejelea chati ya Krejcie na Morgan (1970). Sampuli hii ni ya jumla ya Ekedи 2 kutoka kwa Ekedи 13 na soko moja kutoka kwa masoko 3 ya jijini Kampala ya kati. Mbinu ya usampulishaji mpokezano kifu ambayo hutumia kundi dogo kushawishi wengine kuhusika katika utafiti ili kupanua idadi ya sampuli kama ilivyoelezwa na Suri, (2011) ilitumika kuwateua wasailiwa wafanyabiashara. Katika aina hii ya sampuli mtafiti alianza kwa kumtambua mfanyabiashara ambaye angalau alikifahamu Kiswahili, msailiwa huyo alielekeza mtafiti kwa msailiwa mwininge ambaye alifahamu Kiswahili hadi kufikia idadi toshelevu ya utafiti. Jumla ya wasailiwa wafanya biashara 260 walikubali kushiriki katika utafiti huu kutoka kwa jumla ya wasailiwa 306. Hali hii ilitokana na baadhi ya wafanyabiashara kutokubali miadi ya kuhojiwa kwa ajili ya shughuli zao. Mbinu ya usampulishaji wa mpokezano kifu ilitumika kwa sababu kuna wafanyabiashara ambao licha ya kuwepo kwa wateja wanaotumia Kiswahili, kuna wale ambao bado wanajifunza kutumia Kiswahili kuendeleza biashara zao. Aidha, kuna wale ambao wana misimamo hasi lakini kwa sababu ya kibiashara, wanajifunza kutumia Kiswahili.

Utafiti huu uliteuwa wafanyabiashara ambao licha ya kuwa wanatumia Kiswahili ama kujifunza Kiswahili, hawana elimu ya kimsingi ya Kiswahili waliyopokea shulen. Mbinu hii ilikuwa mwafaka ya kuweza kupata watu tofauti tofauti kwa wakati tofauti hasa wakati utafiti ulikuwa unaendelea. Pia kwa vile utafiti ulijishughulisha na Kiswahili, ilikuwa ni njia mwafaka ya kukusanya data kwani siyo kila mmoja angekuwa na muda wa kutosha kutoa hoja kuhusu matumizi ya Kiswahili. Idadi ya wasailiwa ni kama inavyorejelewa katika Jedwali 3.1.

### **Jedwali 3.1: Idadi ya wasailiwa**

<b>Na</b>	<b>Ekedi</b>	<b>Idadi Lengwa</b>	<b>Idadi Teuliwa</b>	<b>%</b>
1	Mukwano	86	70	81
2	Simlaw Uganda Limited	100	80	80
3	Soko la Kikuubo	120	92	81
<b>Jumla</b>	<b>03</b>	<b>306</b>	<b>260</b>	<b>242</b>

*Chanzo cha data: Nyanjani 2022*

Kwa kutumia mchakato wa kimaksudi jedwali 3.1 laonyesha Ekedi (02) na soko moja (01) zilichaguliwa. Utafiti ulidhamiria kusaili watafitiwa mia tatu na sita (306) hata hivyo waliokubali kushiriki katika utafiti walikuwa wasailiwa mia mbili sitini (260). Wasailiwa sabini (70) kutoka Ekedi ya Mukwano, themanini (80) kutoka Ekedi ya Simlaw International halafu tisini na mbili (92) kutoka soko la Kikuubo.

Kwingineko sampuli kusudio ilitumika ili kuteuwa wasailiwa wafanyabiashara ambao hutumia Kiswahili katika shughuli zao za kuendeleza biashara. Brewton na Millwood (2001); Suri (2011) na Sealle (2000) wanasema kwamba madhumuni ya kutumia sampuli kusudio ni hali ya kumakinika kwenya kundi iliyo mahsusni ambalo husaidia kutoa majibu ya maswali ya utafiti. Wanaendelea kusema kwamba siyo lazima sampuli hii iwakilishe idadi lengwa lakini husaidia kupata data iliyokusudiwa. Kwa mujibu wa madai ya watalaamu hawa, mbinu hii ni ile ambayo hulenga tu wale ambao wanahusiana na swala la utafiti. Wahusika walioteuliwa ni wale wanaoendeleza biashara katika Eneo la utafiti. Kwa kutumia mbinu ya usampulishaji mpokezano dhamirifu, watafiti waliteua msailiwa mfanyabiashara katika eneo la utafiti na kuwaongoza kuwateuwa wasailiwa walengwa wengine wenye sifa za kutumia Kiswahili katika shughuli za Kibiashara. Jumla ya wasailiwa 260 waliteuliwa kushiriki katika utafiti huu kutohana na sifa zao za kuwa wafanya biashara wanaojifunza na kutumia Kiswahili katika shughuli za kuendeleza biashara. Kwa kutumia usampulishaji dhamirifu kufikia kiwango toshelevu cha mahitaji ya utafiti huu ambapo hakuna jambo lingine jipya lilijitokeza, wasailiwa wafanya biashara walio eleza mikakati na mitindo ya ujifunzaji na matumizi ya Kiswahili, changamoto na mikakati ya namna ya kutatua changamoto husika ndio walioteuliwa.

### **3.6 Mbinu za ukusanyaji data**

Ukusanyaji data ni sehemu ya utafiti. Ukusanyaji wa data ni ujumbe mahsusni unaokusudiwa au kukubaliana ama kupinga dhana. Mtafiti lazima awe na uelewa nini ananuia kukusanya na

ajue vifaa atakavyotumia kukusanya data, wasailiwa na eneo la utafiti (Punch, 2009, Kombo na Tromp, 2016). Data zilikusanywa, zikachunguzwa na kuwasilishwa ili kufanikisha malengo la utafiti. Ukusanyaji wa data kwa ajili ya utafiti huu kwa upana ulitumia mbinu kama vile Hojaji, usaili na Uchunzaji. Mbinu hizi zilifanikishwa na vifaa mbalimbali mkiwemo hojaji, mwongozo wa mahojiano na ratiba ya uchunzaji. Hojaji ilitumika katika kupata data za kiwingiidadi wakati mwongozo wa mahojiano na ratiba ya uchunzaji ulisaidia kukusanya data ya kithamano. Kwa kuongezea kulikuwa na vifaa visaidizi kama kalamu, shajara simu na tarakilishi. Mbinu na vifaa hivyo vimejadiliwa kwa mapana katika sehemu inayofuata.

### **3.6.1 Hojaji**

Hojaji ni mbinu ambayo inahusisha uundaji wa maswali ambayo hutolewa kwa minajili ya kuibua majibu kuhusu mada ya utafiti Timothy na Forns (2003). Mtafiti huorodhesha maswali ambayo alitumia kupata data kutoka nyanjani. Kwa mujibu wa utafiti huu majibu yaliyokusanywa kutoka nyanjani kutokana na hojaji zilizosambazwa yalikusanywa na kuchanganuliwa kiwingiidadi wakati wa kuwasilisha tasnifu. Komp na Tromp (2006) wanasema kwamba matumizi ya hojaji ni njia ya majibizano ambayo inaweza kufanyika kwa njia ya ana kwa ana ama kwa kutumia simu kati ya watu wawili au zaidi kwa ajili ya kukusanya taarifa kuhusu jambo fulani. Mbinu hii hutumika ili kupata uthabiti wa majibu ya watafitiwa.

Mtafiti aliandaa hojaji kwa wasailiwa wafanyabiashara kupima mikakati na mitindo ya ujifunzaji na matumizi ya Kiswahili, changamoto na mikakati ya namna ya kutatua changamoto za ujifunzaji na matumizi ya Kiswahili. Watafiti wasaizi wawili amba walikuwa na umilisi wa Kiswahili walihusishwa katika mchakato mzima wa ukusanyaji data. Awali ya hapo, waliombwa kujaza dodoso na hojaji, halafu wakapangiwa kikao na mtafiti ili kupata ufanuzi zaidi kuhusu mbinu na vifaa vilivyotumiwa kupata data. Kwa kusaidiwa na watafiti wasaidizi, hojaji hizi zilisambazwa kwa wasailiwa wafanyabiashara walioteuliwa kutumia njia ya mpokezano dhamiri kwa ajili ya kujibiwa. Matokeo ya hojaji yalirekodiwa na kunukuliwa kithamano. Taarifa hizi zilichanganuliwa ni mikakati na mitindo ya ujifunzaji na matumizi ya Kiswahili, changamoto na mikakati ya namna ya kutatua changamoto za ujifunzaji na matumizi ya Kiswahili kunukuliwa na kupangwa kiwingiidadi na kuwasilishwa kutumia majedwali na kuelezwu kudhihirisha matokeo ya mikakati na mitindo ya ujifunzaji na matumizi ya Kiswahili, changamoto na mikakati ya namna ya kutatua changamoto za

ujifunzaji na matumizi ya Kiswahili.

### **3.6.2 Usaili**

Usaili ni utafutaji wa taarifa kwa njia ya kuuliza maswali. Aidha, ni utafiti wa kugundua ujuzi au taaluma anayofanyiwa mtu kwa kuulizwa maswali ana kwa ana (Kothari, 2003) naye kutoa majibu papo hapo. Kvale (1996) anafasili usaili kama mbinu ya kisifa inayokusudia kueleza maana ya dhana kuu katika kazi ya utafiti. Usaili huundwa kwa ushirikiano wa ana kwa ana (Mertens, 2008) kati ya mtafiti na msailiwa. Mtafiti hukusanya data kulingana na ushirikiano kati yake na msailiwa. Kila msailiwa hujibu maswali hayo hayo yaliyowekwa katika lugha moja hivyo inakuwa rahisi mtafiti kupata majibu yanayoweza kurejelewa (Jonathan, 2013). Jonathan (keshatajwa) anaendelea kusema kwamba mbinu hii inamsaidia mtafiti kubadilisha swali kutegemea jibu analolihitaji ama kubadilisha muundo wa swali hilo hilo ili kupata majibu yaliyokusudiwa.

Kwa mujibu wa utafiti huu, watafiti waliomba na kupanga miadi ya kuwasaili wasailiwa wafanyabiashara walioteuliwa kimpokezano kueleza mikakati, mitindo na changamoto za kujifunza Kiswahili na namna ya kutatua changamoto husika wakati wa kujifunza na kutumia Kiswahili kama lugha ya biashara. Watafiti kwa kusaidiwa na watafiti wasaidizi, waliwasaili wasailiwa wafanyabiashara kulingana na miadi, msailiwa kwa msailiwa na katika vikundi, taarifa za mikakati na mitindo, changamoto na mikakati ya namna ya kutatua changamoto kurekodiwa kutumia simu, na kunakiliwa katika daftari. Baada ya usaili kukamilika, Kila mtafiti msaidizi kwa kuongozwa na watafiti, walielekezwa kudondoa na kunukuu data zilizorekodiwa, kupanga na kueleza matokeo ya usaili kithamano. Data iliyojitokeza ilipangwa kithamano na kiwingi idadi na matokeo kuwasilishwa kutumia majedwali na kuelezwu kutumia mbinu ya kimaelezo kuchambua mikakati na mitindo, kutathmini jinsi mikakati na mitindo mbalimbali huwezesha ujifunzaji na matumizi ya Kiswahili. Vile vile hupambanua changamoto na kufafanua mikakati ya namna ya kutatua changamoto za ujifunzaji na matumizi ya Kiswahili kama lugha ya kibashara.

### **3.6.3 Uchunzaji**

Mbinu ya Uchunzaji katika utafiti hushughulikia dhana kwa undani wake, hali halisi, eneo halisi na hulka za watafitiwa katika mazingira halisi ya utafiti (DeWalt na DeWalt, 2011). Uchunzaji unasaidzia kutambua watu wanafanya nini, nafasi zao na tabia zao na namna inavyoweza kuathiri matokeo ya utafiti (Walshe, Edwing, Grifths, 2011). Mazungumzo

yaliyorekodiwa yalifanyiwa unukuzi na ni kutokana na nukuzi hizo ambapo data inayohusiana na madhumuni ilipatikana. Orodha ya uchunzaji ilitumiwa kukusanya data za kimsingi katika mazingira halisi ambamo shughuli za biashara hufanyika. Watafitiwa wakiwa nyanjani walishiriki moja kwa moja ambapo walinakili mikakati na mitindo, changamoto na mikakati ya namna ya kutatua changamoto za ujifunzaji na matumizi ya Kiswahili. Baada ya kunakili waliweza kunukuu maelezo ya wasailiwa kwa mujibu wa madhumuni kudhihirisha mikakati na mitindo, changamoto na mikakati ya namna ya kutatua changamoto za ujifunzaji na matumizi ya Kiswahili.

### **3.7 Vifaa vya kukusanya data**

Vifaa vya kukusanya data ni vifaa ambavyo mtafiti hutumia katika mchakato wa ukusanyaji wa data. Vifaa hivi ni pamoja na dodoso, hojaji, kushiriki na kusoma (Cooper na Schindler 2013). Kwa ajili ya utafiti wetu, mbinu za kukusanya data ziliwa ni dodoso, usaili na Uchunzaji. Vifaa vilivyohusishwa vilikuwa hojaji, dodoso, mwongozo wa uchunzaji, simu na tarakilishi.

#### **3.7.1 Hojaji lililo na maswali ya kujaza**

Kwa mujibu wa Kothari (2003) hojaji huwa ni maswali ambayo yameandikwa katika karatasi yanayohusu swala linalotafitiwa. Maswali hutolewa kwa minajili ya kuibua majibu kuhusu mada ya utafiti ambayo yanamuelekeza mtafiti namna atakusanya data (Timothy na Forns, 2003). Mtafiti huorodhesha maswali ambayo atatumia kupata data kutoka nyanjani. Hojaji mia moja na tatu (103), kiambatisho E. zilisambazwa kwa watafitiwa. Data zilizokusanya kutoka nyanjani zilichanganuliwa na kuwasilishwa kiwingiidadi. Kombo na Tromp (2016) wanasema kwamba matumizi ya hojaji ni njia ya majibizano ambayo inaweza kufanyika kwa njia ya ana kwa ana ama kwa kutumia simu kati ya watu wawili au zaidi kwa ajili ya kukusanya taarifa kuhusu jambo fulani.

Kwingineko, hojaji ni rahisi kujibu kwa ajili ya kujaza tu mapengo, rahisi kwa mtafiti kudhibiti sampuli kwa usahihi zaidi. Vile vile humfungia msailiwa ndani ya mipaka ya muda na matokeo ni rahisi kujedwalishwa na kuchanganuliwa (Buliba, Mayaka na Riro, 2014). Utafiti huu ulitumia hojaji iliyo wazi katika kukusanya data kuhusiana na mikakati na mitindo ya lugha ya pili ilivywasaidia kujifunza Kiswahili kama lugha ya biashara, jinsi walivyotumia mikakati na mitindo waliyotaja kujifunza Kiswahili. Maswali katika hojaji yalipangwa kwa mujibu wa malengo manne ya utafiti kwa ajili ya kujibiwa na wasailiwa

wafanyabiashara kuhusu mikakati na mitindo ya lugha ya pili ilivyowasaidia kujifunza Kiswahili kama lugha ya biashara, jinsi walivyotumia mikakati na mitindo waliyotaja kujifunza Kiswahili kama lugha ya biashara na changamoto za ujifunzaji na matumizi ya Kiswahili kama lugha ya biashara.

### **3.7.2 Dodoso**

Timothy na Forns (2003) na De vaus (2001) wanaeleza kwamba dodoso ni mfumo wa maswali yanayoandaliwa kuongoza mtafiti nyanjani kwa kumuuliza mtu ili kupata data inayokusudiwa kuhusu mada fulani. Kombo na Tromp (2016) wanasema kwamba, dodoso ni mfumo wa maswali yaliyoandaliwa na yanaulizwa na mtafiti ili kupata data kuhusu mada fulani. Wanaendelea kusema dodoso huwa za aina mbili yaani ile ya usaili lengwa ambayo madhumuni yake ni kuchunguza mada mahsus halafu kuna dodoso ya uchunguzi kifani ambayo ni ya kuchunguza juu ya kisa fulani kwa undani. Utafiti huu ulitumia dodoso la usaili lengwa ambalo lilikuwa na orodha ya maswali ambayo yalielekezwa na maswali ya utafiti na madhumuni ya utafiti.

Kulikuwa na seti moja ya dodoso (mwongozo wa mahojiano) ambayo ilikuwa na maswali wazi (kiambatisho F). Maswali haya yaliulizwa ana kwa ana huku mtafiti akirekodi majibu. Hii ilitumika sana kwa wasailiwa ambao walikuwa na utata wa kuandika katika hojaji. Wasailiwa mia moja hamsini na saba (157) kushirikishwa katika mahojiano ya ana kwa ana. Kutokana na mikakati na mitindo ya kujifunza Kiswahili kibiashara iliyopendekezwa, mtafiti aliweza kubaini jinsi wafanyabiashara hutumia mikakati na mitindo ya kujifunza Kiswahili kibiashara. Kifaa hiki kilikuwa na vipengele vyote ambavyo viliegemea madhumuni ya utafiti.

Kifaa hiki kilikusanya taarifa za mikakati na mitindo ya ujifunzaji na matumzi ya Kiswahili, jinsi mikakati na mitindo ilivyosaidia katika ujifunzaji na matumizi ya Kiswahili, changamoto na mikakati ya kutatua changamoto za ujifunzaji na matumizi ya Kiswahili kama lugha ya kibiashara. Vile vile watafiti walikuwa na uhuru wa kuuliza maswali zaidi ili kupata data zilizofaa sana utafiti ambapo ilikuwa vigumu kufanyika kwa kutumia hojaji ambayo awali iliwachiwa wasailiwa na kukusanya baadaye. Kifaa hiki kilikuwa na maswali wazi ambapo kilitumika kukusanya data za kithamano kushirikisha mahojiano. Mwongozo ulikuwa na vipengele mbali mbali ambavyo vililenga data kuhusu mikakati na mitindo na namna ilivyyotumiwa katika ujifunzaji wa Kiswahili kama lugha ya biashara pamoja na

changamoto walizokumbana nazo.

### **3.7.3 Simu mahiri**

Simu mahiri/tamba imekuwa kifaa cha elektroniki bora cha kukusanya data (Pakhare na Kaira 2013). Pakhare na Kaira wanaendea kusema kwamba mtindo wa kukusanya data kutumia vitabu, karatasi na kuandika ni mtindo wa zamani na unachosha. Kwake anasema simu za kisasa husaidia kukusanya data kwa kutumia muda mfupi na ulio bora zaidi. Simu ilitumika kunasa picha na mazungumzo halisi ya shughuli za uchuuzi zilizokuwa zikiendelezwa kati ya wanunuzi na wauzaji. Ileweke kwamba asilimia kubwa ya watafitiwa hawakuwa wanajua kwamba kuna mikakati na mitindo ya kujifunza L2 hivyo siyo kila msailiwa alijua namna ya kuifafanua lakini katika harakati ya kuendeleza shughuli ya biashara mikakati na mitindo ilibainika. Kifaa hiki kilisaidia sana kufanikisha mbinu ya ukusanyaji wa data ya uchunzaji.

Aidha, utafiti huu ulirekodi usaili ambao uliendelea baina ya wasailiwa na wasaidizi au mtafiti mkuu kwa ajili ya kupata data za madhumuni matatu; kuchambua mikakati na mitindo ya ujifunzaji, kutathimini jinsi mikakati na mitindo ilivyotumika katika ujifunzaji na Kufafanua changamoto za ujifunzaji wa Kiswahili kama lugha ya kibiashara jijini Kampala, Uganda.

### **3.7.4 Mwongozo wa uchuzaji**

Kuna njia mbalimbali ambazo mtafiti anaweza kutumia wakati wa uchunzaji. Kwa mfano mtafiti anaweza kuwa mshiriki katika hadhira ambayo anafanya utafiti, ama (DeWalt na DeWalt, 2011) ama mtu anaweza kurikodi kwa kurikodi kwa video ama kunasa mazungumzo ambapo ni uchunzaji wa moja kwa moja. Kwa hali hii mtafiti alifika uwanjani kufanya uchunguzi wa moja kwa moja kwa sampuli iliyoteuliwa kushiriki katika utafiti. Hivyo kilichokuwa kinazingatiwa katika mazingira maalum ya wafanya biashara ilikuwa ni mikakati na mitindo ya ujifunzaji lugha ya pili namna ilikuwa ikitumiwa na wafanya biashara kujifunza Kiswahili kwa ajili ya biashara. Mtafiti alizuru maeneo ya uchunzaji sio kama mshiriki lakini alinakili data ambazo zilipatika maeneo ya Simlaw International Limited, eneo la soko la Kikuubo na Ekedo ya Mukwano. Data zilizopatikana zilinukuliwa na kuchanganuliwa baadaye. Mwongozo wa Uchunzaji umewekwa kama Kiambatisho G, uk.

### **3.7.5 Ufaafu na utegemezi wa vifaa vyakukusanya data**

Joppe (2000) anafasili udhabiti kama kiwango cha matokeo na uwasilishaji mahsus ikuhusu idadi lengwa ya wasailiwa na kama huo utafiti unaweza kurejelewa kwa kutumia mbinu hizo na vifaa mwafaka vilivytumiwa wakati wa utafiti.

Ufaafu na utegemezi wa kukusanya data kwa mujibu wa Mugenda na Mugenda (2003) Mogere (2018) na Eisner (1991) ni kiwango cha kifaa kutoa matokeo ya kuegemewa au data baada ya majoribio kadhaa. Maelezo haya yanashadidiwa na Grix (2010) anayeeleza kuwa ufaafu hutegemea uhusiano wa taarifa zilizotolewa na wahojiva teule katika muda tofauti wa matumizi ya vifaa. Utaratibu na mbinu za utafiti kutokana na matumizi ya kifaa. Utafiti huu uliandaa vifaa vyakukusanya data kwa kutegemea madhumuni ya kupata data kuhusu mikakati na mitindo ya kujifunza Kiswahili kibiashara pamoja na changamoto wanazopata wafanyabiashara wanapojifunza na kutumia Kiswahili jijini Kampala. Ubora wa kila kifaa na ufaafu wake katika kupata kila data inayowiana na madhumuni ultokana na uteuzi wa kifaa na majoribio awali kuhakikisha kuwa kila kifaa kinatimiza malengo yaliyokusudiwa.

Utafiti huu ultumia kifaa cha hojaji. Kifaa hiki kilitumika kwa mujibu wa Kothari (2003) ambao wanaeleza kuwa maswali yanayohusu swala linalotafitiwa huandikwa katika karatasi. Maswali hutolewa kwa minajili ya kuibua majibu kuhusu mada ya utafiti. Aidha ufaafu na udhabiti wa kifaa hiki hutokana na mijadala awali kilifanywa baina ya mtafiti, wasimamizi na watafiti wasaidizi kupima ufaafu wa matokeo ya kifaa.

Vile vile utafiti huu ultimia kifaa cha dododso. Kwa mujibu wa De vaus (2001); Timothy na Forns (2003) na Kombo na Tromp (2016) wanaeleza kwamba dodoso ni mfumo wa maswali yanayoandalialiwa kuongoza mtafiti nyanjani kwa kumuuliza mtu ili kupata data inayokusudiwa kuhusu mada fulani. Ufaafu na udhabiti wa kifaa hiki ultokana na mijadala awali baina ya mtafiti, wasimamizi na watafiti wasaidizi kupima ufaafu wa matokeo ya kifaa.

Kwingineko utafiti huu ultumia simu mahiri. Pakhare na Kaira (2013) wanasema kwamba mtindo wa kukusanya data kutumia vitabu, karatasi na kuandika ni mtindo wa zamani na unachosha. Hivyo waansema kwamba mtindo wa kutumia simu mahiri ni faafu unaotumua muda mfupi na ulio bora zaidi. Ufaafu na udhabiti wa kifaa hiki ultokana na mijadala awali baina ya mtafiti, wasimamizi na watafiti wasaidizi kupima ufaafu wa matokeo ya kifaa.

Orodha ya uchunzaji ultumiwa na utafiti huu kukusanya data kulingana na mada ya utafiti na madhumuni ya pili. Kifaa hiki kulingana na (Walshe, Edwing, Griffiths, 2011) wanasema

kwamba kinasaidia kutambua watu wanafanya nini, nafasi zao na tabia zao na namna inavyoweza kuathiri matokeo ya utafiti. Ufaafu na udhabit na kifaa hiki ultokana na mijadala awali baina ya mtafiti na wasimamizi, mijadala baina ya watafiti wasaidizi na mtafiti kuhusu ufaafu wa kifaa katika ukusanyaji na upimaji wa matokeo ya data zilizokusanywa nyanjani.

Kuaminiwa kwa data za utafiti huu kulitokana na ufaafu na udhabit na mbinu za utafiti kuzalisha matokeo yaleyale kutoka kwa wasailiwa. Kutokana na matokeo ya majibu yaliyotolewa kwenye hojaji na usaili kuendana na orodha ya uchunzaji ya utafiti huu.

### **3.8 Uchanganuzi na uwasilishaji wa data**

Shamoo na Resnik (2003) wanasema kwamba uchambuzi wa data ni mchakato wa kisifa unaohusisha takwimu/mikakati mantiki, kuchambua, kuonyesha, kukusanya, kuainisha na kupanga data na kuzichanganua ili kufanikisha lengo kuu na madhumuni ya utafiti. Kwa mujibu wa Suri (2011) uchambuzi wa data ni mchakato wa kukusanya, kuainisha na kupanga data. Grix (2004) anaeleza kuwa uchanganuzi ni mchakato wa kutathmini data kwa kutumia sababu za kiuchambuzi na kimantiki kwa kuangalia kila kipengele cha data zilizokusanywa. Naye Kothari (2003) anaeleza kwamba, uchambuzi wa data ni kitendo cha kufupisha na kupangilia vizuri data zilizokusanywa kwa namna ambayo zitakusaidia kujibu maswali ya utafiti husika. Uchambuzi wa data ni hatua muhimu sana katika kutafuta majibu ya tatizo la utafiti. Hivyo basi utafiti huu ulizingatia uchanganuzi kimaelezo na kuwasilishwa kwa mfumo wa kinathari na kwa majedwali.

Baada ya kukusanya data kuitia hojaji na dodoso, uchunzaji mtafiti alizipanga kwa kuzingatia madhumuni ya utafiti, maswali ya utafiti, mapitio ya maandishi na nadharia zilizotumika halafu zikachanganuliwa kwa kuzingatia mfumo huo. Data ilikusanywa kutokana na mbinu na vifaa ambavyo viliteuliwa kwa ajili ya utafiti huu. Uwasilishaji wake ulifanywa kwanjia majedwali na maelezo. Maelezo ambayo yalipatikana kwa kupanga data za kiwingi idadi na za kithamano zilizokusanywa kwa kuhusisha maswali ya utafiti na nadharia za utafiti. Data zisizohusiana na utafiti hazikurejelewa. Data iliyochanganuliwa ilikuwa mikakati na mitindo inayotumiwa kujifunza Kiswahili kama lugha ya biashara, jinsi wafanyabiashara hutumia mikakati na mitindo kujifunza Kiswahili kibiashara, changamoto zinazokumba katika ujifunzaji wa Kiswahili kibiashara na namna ya kuzitatua.

### **3.9 Maadili ya utafiti**

Mukuthuria (2006) anasema maadili ni kaida (Kitetu 2003, Okombo na Tromp (2016)) zinazoelekeza tabia zetu katika mahusiano yetu ya kila siku na wenzetu. Hoja yake ame ilinganisha na ya Mathooko (2007) kwamba katika utafiti maadili ni uwajibikaji na uwelekevu kitabia kuhusiana na haki za wale wote tunaotangamana nao katika utafiti, uelekevu katika nia na malengo ya utafiti na jinsi ya kutumia matokeo kwa uadilifu ili yaweze kuwa faida kwa jamii ya binadamu.

Cherry (2019), kwa kurejelea kanuni za maadili ya utafiti ya APA anasema utafiti yafaa uzingatie ubora na ufaafu wa kazi inayotafitiwa. Mtafiti anastahili kutaja majina ya waandishi mbalimbali wa kazi iliyorejelewa namna tulivyofanya na utafiti wetu. Mtafiti anastahilikufahamisha wasailiwa kiini cha utafiti au sababu mwafaka wakati na namna utafiti unavyoendelea. Awaeleze watafitiwa umuhimu wao katika utafiti na kwamba maoni yao yatatumiwa tu kwa ajili ya utafiti na wala sio mambo mengine ambayo yatakiuka maadili ya utafiti. Watafitiwa wana haki ya hiari ya kuridhia endapo watahusika katika utafiti ama la. Watafitiwa walihakikishiwa kwamba ushiriki wao ulikuwa ni wa usiri na mawazo yao yangetumika tu kwa ajili ya utafiti na si mahali pengine katika umma.

Pia uoneshe kwamba utafiti wako ni wa kiakademia unaolenga tu kuongeza maarifa katika asasi ya kiakademia. Aidha, Cherry (keshatajwa), anasema utafiti usiwe ni wa kumdhuru mtafitiwa endapo madhara yatatokea basi lazima kuwepo na mipango maalum ya kuonesha namna madhara hayo yataepukwa na namna ya kuhifadhi data ambayo ilikusanywa. Madhara yanaweza kuwa ya kisaikolojia, kimwilii, kihela, ama kumuingilia katika maisha yake binafsi hivyo kuepukana na hayo yote mtafiti anastahili kuomba ruhusa kwa mtafitiwa kabla ya kumhoji ama kukutana naye, kumuonesha kwamba maoni yake yatahifadhiwa kwa ajili ya utafiti na pia utafiti haulengi kumdhuru kivyovyote. Kwa kuongeza, kazi zilizorejelewa ziliweza kunukuliwa na waandishi wake kutajwa moja kwa moja. Kwa mantiki hii, utafiti huu ulipewa kibali kutoka Chuo Kikuu cha Maseno, cha kuruhusu mtafiti kuingia nyanjani kukusanya data. Kibali kingine cha kukagua pendekemo kwa ajili ya maadili na kuruhusu ukusanyaji data kilipatikana kutoka ofisi kuu ya (REC) ambayo iko chuo kikuu cha kimataifa cha Clarke nchini Uganda.

### **3.10 Hitimisho**

Sura hii ilieleza bayana muundo wa utafiti ambao ulikuwa wa muundo mseto, eneo lililofanyiwa utafiti lilikuwa jiji kuu Kampala katika Ekedo ya Mukwano, Simlaw Uganda Limited na soko la Kikuubo. Kundi lengwa la utafiti lilikuwa idadi ya wafanyabiashara 260 kati ya 1500 ambao waliwakilisha asilimia 85% kulingana na uteuzi wa sampuli wa Krejcie na Morgan 1970.

Ukusanyaji wa data ulielekezwa na nadharia ya Krashen (1987) pamoja na ile ya Gardener (2000). Mbinu ambazo zilitumiwa kukusanya data zilikuwa ni hojaji, usaili na uchunzaji. Hojaji ilifanikishwa kwa kutumia mwongozo wa hojaji kwa wasailiwa ambao walikuwa na uwezo wa kulijaza, halafu dodoso ilitumiwa kwa wasailiwa ambao walipendelea kusailiwa ana kwa ana na wala si kwa kujaza hojaji . Data za dodoso zilikuwa za kimsingi sana kwa kuegemea kwamba Kiswahili kama lugha ya biashara ilikuwa L2 kwao kujifunza katika mazingira yasiyo rasmi. Njia ya uchunzaji nayo ilitumiaka ili kupata mikakati na mitindo iliyjitekeza wakati wafanyabiashara. Wanunuzi na wauzaji walishirikiana katika mawasiliano kupitia mpangilio wa kubadilishana zamu. Data ilipatikana kwa kutumia simu na daftari katika mazingira halisi ya uendelezaji biashara katika Ekedo ya Mukwano, Simlaw International Limited na soko la Kikuubo. Licha ya wasailiwa kufafanua jinsi walivyotumia mikakati na mitindo kujifunza Kiswahili kibashara kupitia hojaji na dodoso, ukakasi wake ulihitaji watafiti watazamwe namna mikakati na mitindo ilivyojitekeza katika mchakato wa kufanya biashara. Mifano ya data za uchunzaji zimechananuliwa sambamba katika mikakati na mitindo iliyotokana na hojaji na dodoso.

Takwimu zilizotokana na hojaji zilichanganuliwa kiwingiidadi na kufanyiwa ufanuzi kimaelezo halafu data za usaili ambazo zilitokana na dodoso zilieleza kithamano . Wasailiwa waliohusishwa ni wafanyabiashara ambao wanapatikana katika Ekedo ya Mukwano, Simlaw International Limited, na soko la Kikuubo. Utaratibu wa kukusanya data ulieleza kupitia namna mtafiti alipata kibali kutoka chuoni cha kumruhusu kuenda nyanjani kukusanya data, mchakato wa kuenda nyanjani, kukutana na wasailiwa na kukusanya data. Sura hii ilieleza upangaji wa data uwasilishaji na uchanganuzi wa data kulingana na mada ya utafiti, madhumuni ya utafiti, mapitio ya maandiko na nadharia zilizo elekeza ukusanyaji wa data. Sehemu ya mwisho ilionyesha maadili mtafiti alizingatia wakati wa kukusanya data.

## **SURA YA NNE**

### **UCHANGANUZI, MJADALA NA UWASILISHAJI WA MATOKEO**

#### **4.1 Utangulizi**

Sura hii inawasilisha matokeo ya data ambazo zilitokana na madhumuni matatu ya utafiti huu. Madhumuni ya kwanza yalifanua mikakati na mitindo iliyotumiwa na wafanyabiashara kujifunza Kiswahili kama lugha ya biashara kwa wafanyabiashara jijini Kampala, Uganda. Madhumuni ya pili yalitathmini jinsi mikakati na mitindo mbalimbali huwawezesha wafanyabiashara kujifunza Kiswahili kama lugha ya biashara jijini Kampala, Uganda. Madhumuni ya tatu yalipambanua changamoto zinazowakumba wafanyabiashara wakati wa kujifunza Kiswahili kama lugha ya biashara jijini Kampala, Uganda. Hatimaye, madhumuni ya nne yalichanganua mikakati ya namna ya kutatua changamoto zinazowakabidhi wafanyabiashara ili kufanikisha ujifunzaji na matumizi ya Kiswahili kibiashara. Data ya utafiti imechanganuliwa kwa kutumia takwimu za kiwingiidadi na kauli mbalimbali zilinukuliwa kutokana na nukuu za mazungumzo ya mahojiano kati ya mtafiti na matafitiwa pamoja na yaliyotokana na uchunzaji.

#### **4.2 Mikakati na mitindo mbalimbali ambayo ilitumiwa na wafanyabiashara kujifunza Kiswahili kama lugha ya biashara**

Sehemu hii imejadili kwa mapana kuonyesha mikakati na mitindo mbalimbali ambayo wafanyabiashara wa Ekedi ya mukwano, Simlaw International Limited na soko la Kikuubo walikuwa wakitumia ili kujifunza Kiswahili kama lugha ya kuendelezea biashara zao. Kwa kutumia mhimili wa kwanza wa Krashen amba ni nadharia tete ya upataji/ujifunzaji pamoja na mhimili wa kwanza na wa pili wa Gardener (2000) wa jitihada na nia ilisaidia katika kuelezea mikakati na mitindo mbalimbali ambayo ilitumiwa kujifunza Kiswahili kama lugha ya biashara.

Matokeo kutokana na hojaji na dodoso yalijadili data zilizotoka na kuridhia ama kutoridhia mafunzo ya Kiswahili kibiashara. Mikakati ifuatayo katika aya zitakazojadiliwa ambayo wafanyabiashara walitumia katika ujifunzaji Kiswahili kama lugha ya biashara jijini Kampala. Kwa sababu ya maadili ya utafiti, majina ya wasailiwa hayakutumiwa hivyo msimbo uliotumiwa ulihuisha tu nambari kwa mfano MS 000 (MS) ni akronimu inayosimamia msailiwa kutokana na uchanganuzi wa umaratokezi kutoka kwa hojaji na nukuu za mahojiano namna walikuwa wakitoa ufanuzi wao zilibainishwa kama MS.1,

MS.2 mtawalia.

#### Jedwali 4.1: Kupata mafunzo ya Kiswahili kibiashara

Ujifunzaji	Asilimia
Ndio	02
La	101
Jumla	103

Asili :Data ya umaratokezi kutokana na hojaji- Februari,2022

Kutokana na hojaji 103 zilizosambazwa, Kwa kuzingatia umaratokezi wa majibu, wasailiwa 02 ambao waliwakilisha ailimia 1.9 % walikiri kwamba waliwahi kupata mafunzo ya Kiswahili kibiashara. Wasailiwa 101 ambao waliwakilisha asilimia 98.0 % jibu lao lilikuwa ‘la’ kumaanisha kwamba hawajawahi kupata masomo yoyote ya Kiswahili kibiashara.

Kutokana na mahojiano kati ya mtafiti na msailiwa, wasailiwa watatu mionganini mwa wasailiwa mia moja hamsini na saba walikiri kwamba waliwahi kupata masomo ya Kiswahili kibishara kama inavyoitokeza katika nukuu zifuatazo

#### MS.018

*Mimi nasoma chiswahili chidogo. KACITA na fundisha mambo ya Kiswahili.Najua kusabua katika swahili,najua siku za wiki ,najua hata mwaka. Nawea ongea chiswahili chidogo kama bakastoma banakuja.*

Nilisoma Kiswahili kidogo. KACITA ilitufundisha masomo ya Kiswahili. Najua kuhesabu katika Kiswahili, najua siku za wiki na hata mwaka.Nawea kuongea Kiswahili kidogo kama wateja wamekuja. (TY)

Kwa kuegemea nadharia ya Krashen (1987) katika muhimili wa kwanza hatua ya pili ambayo ni ya kuongea, mjifunzaji lugha huwa anatumia maneno na virai vifupi vifupi. Kutokana na nukuu 1 tunaona kwamba msailiwa anajitahidi kuonyesha kwamba kwa kweli alijifunza Kiswahili kwa kutamka sentensi zake katika Kiswahili. Hata hivyo sentensi zenyewe zinajitokeza kama virai vifupi vifupi ambavyo aliimarika kujifunza wakati wa mafunzo ya KACITA. Vile vile Krashen (keshatajwa) anaendelea kusema kwamba wakati huu huwa kuna makosa mengi ambayo hutokea. Tunaona vilevile makosa ya kisarufi yakijitokeza kama vile *nasoma* badala ya **nilisoma chiswahili chidogo** badala ya **Kiswahili kidogo nafundisha** badala ya **tulifundishwa** mambo ya Kiswahili. *Najuwa kusabua swahili* katika badala ya **Ninajua kuhesabu katika Kiswahili , banakuja** badala ya **wakija/wanapokuja**. Kwingineko, kuna kunajitokeza uchanganyaji msimbo pale ambapo msailiwa anasema *bakastoma* badala ya **wateja** yaani amejaribu kuhawilisha dhana ya *customer* katika Kiingereza na kuweka katika Kiswahili. Juhudi ambazo aliziweka katika

ujifunzaji wa Kiswahili zimeshadidiwa na Gardener (2000) kwamba nia huwa kama msukumo hasa wa ndani ambao humsaidia mjifunzaji wa L.2 kujifunza lugha hiyo. Licha ya kuwa kuna wataalamu kama kina Coder (1983), Selinker (1972) ambao wameshikilia kusahihisha makosa yanayotokana na ujifunzaji wa L.2, Anderson na Elioumi (2004) na Palma na Madirgal (2021) wanasema kwamba katika ujifunzaji wa L.2 makosa hayaepukiki. Kwa hivyo mwanafunzi hastahili kukashifiwa ama kulazimishwa kusahihisha makosa hayo kwani (Krashen 1987) huenda yakipungua kadri mwanafunzi anapomudu L.2.

### **MS 031**

*Nilijua Kiswahili kidogo kutoka shule langu la uko Rakai. Mwalimu yetu alitusomesa Kiswahili muzuri sana. Wakati mimi naanza busuubuzi apa KACITA ilituleteya mwalimu wa Kiswahili. Tena mimi nafurahia kabisa. Najifunza namna ya kuongea na basubuzi kutoka Kenya na hata Tanzania.* Asili:

Krashen (1987) katika hatua yake ya nne ya mhimili wa kwanza anasema kwamba katika hatua hii mjifunzaji wa L.2 huwa anaimarisha mawasiliano yake kwa kuzingatia baadhi ya sheria za lugha bila kujali makosa ambayo yatajitokeza. Huwa ana uwezo wa kutumia maneno katika lugha lengwa. Hoja mbayo imeshadidiwa na Ehrman na Oxford (1995) kwamba wanafunzi kama hawa huwa wanajiona kwamba wameimarika katika L.2 na wanaweza kutangamana na wazungunzaji wa lugha lengwa. Naye Gardener (2000) katika mhimili wake wa kwanza anasema kwamba uvumilivu na kumakinika ambavyo hutokana na jitihada na ari aliyonayo mjifunzaji wa L.2 humsaidia kuchochaea ujifunzaji wa L.2.

#### **4.2.1 Mikakati iliyotumiwa na wafanyabiashara kujifunza Kiswahili kama lugha ya biashara jijini Kampala, Uganda**

Japo kuna mikakati anuai ya kujifunza L2 kama vile; mawasiliano, kumbukizi, kuuliza maswali Kufidia, utabiri kuomba msaada na upatikanaji tena kama ilivyowasilishwa na wataalamu kama; Wanyanya 2020, Mkwinda 2013, Cohen na Weaver 2011, Hassan 2000, Oxford 1990, Tarone 1989, O'Marley & Chamot 1990, Cohen 1998 na Chomsky 1968. Kujibu swalii la mikakati ipi ya ujifunzaji L2 ambayo wafanyabiashara walitumia kujifunza Kiswahili kama lugha ya biashara, data zifuatazo zilipatikana kutokana na hojaji zinawasilishwa katika jedwali lifuatalo;

**Jedwali 4.2: Mikakati ya ujifunzaji lugha ya pili ambayo ilitumiwa kujifunza Kiswahili kibiashara**

Ujifunzaji	Asilimia
Ndio	02
La	101
Jumla	103
	100%

**Asili: Data ya umaratokezi kutokana na hojaji (Februari,2022)**

Matokeo katika jedwali hili yanaonyesha kwamba kutokana na hojaji 103 zilizosambazwa, Kwa kuzingatia umaratokezi wa majibu, wasailiwa 02 ambao waliwakilisha ailimia 1.9 % walikiri kwamba walitumia mikakati ya ujifunzaji L2 kujifunza Kiswahili kibiashara. Wasailiwa 101 ambao waliwakilisha asilimia 98.0 % jibu lao lilikuwa ‘la’ kumaanisha kwamba hawakujua mikakati yoyote ya ujifunzaji wa L.2. Takwimu hizi zimetokana na hojaji zililotumiwa kupata data za kimsingi. Kutokana na mahojiano kati ya mtafiti na wasailiwa watatu walikiri kwamba kuna mikakati ya ujifunzaji L.2 ambayo iliwasaidia katika ujifunzaji wa Kiswahili kibiashara.

Waliokiri kwamba walitambua mikakati ya ujifunzaji Kiswahili kama lugha ya biashara kutokana na nukuu za hapo chini, walitaja tu mafunzo ya awali ambayo walipata kama katika viwango vya chini vya ujifunzaji ambapo Kiswahili kama somo la hiari kilifundishwa k a t i k a shule walizohudhuria. Data hizi zinadhihirika kutokana na mahojiano kati ya mtafiti na mfanyabiashara namna inavyoonyeshwa hapa chini;

**Mtafiti:** *Ssebo ogambye walio obukuggu bwewakozesaanga kwesomesa luswali lwo” busubuzi. Obukuggu obwo bwe buli waaa?*

Bwana umesema kuna mikakati ulikuwaukitumia kujifunza Kiswahili kama lugha ya Kiswahili. Mikakati hiyo ni ipi? (TY)

**Msailiwa 029 :** *Eeeh mwatu! mimi lisoma mambo kidogo kama kyakulya, abari, minenda nyumbani. Ebyo bye batusomesa nga ndi musinia esooka ne yokubiri. We twatuka musinia yokusatu ne tulekeelao anti akaseera ako nga tetulabba mugaso gwo’ Oluswaili. Siluigangako bulungi nakoma awo. Na”abasiinga ffena wano abasubuuzi tuyiiye luswaili. Naye walio abagezaako okulogera. Mwatu singa twaiga ebigaambo bbinji naye katti tutetekeny a bimu bimu.*

Ehhe hakye! Mimi nilisoma msamiati kidogo kidogo kama chakula, habari, naenda nyumbani. Hayo ndio walitufundisha tukiwa kidato cha kwamza na cha pili.Tulivyofika kidato cha tatu tuliwacha maana wakati huo hatukuona umuhimu wa Kiswahili. Sikuwahi kujifunza vizuri niliishia hapo. Na wengi wetu wafanyabiashara twabambanya tuu. Laiti tungejifunza msamiati mwingi lakini sasa tunajaribu kidogo kidogo(TY).

### **MS.033**

*Oluswaili twalusomako katono musinia esooka halafu sisi natoroka nga tulabba bitumaliira bidde. Twafunnako habari, jambo siku za wiki ebilala kati mbyelabidde. Kakati wano kweimirizaawo kubusuubuzi luswaili tuyiiye luyiiye ne tuiga kuva mu "abalogeera nga tuwaya.*

Tulisoma Kiswahili kidogo kidato cha kwanza halafu tukatoroka madarasa hayo. Tuliona inatumalizia wakati. Tulipata msamiati kama habari, jambo siku za wiki mengine nimesahau. Hivyo hapa ili kufaulu katika biashara tunababanya babanya Kiswahili nakujifunza kutoka kwa wanaokiongea wakati wa mawasiliano. (TY).

Mahojiano haya yanaonyesha kwamba idadi kubwa ya wafanyabiashara hawakutambua kwamba kulikuwa na mikakati ya ujifunzaji wa L2 ambayo walitumia kujifunza Kiswahili kama lugha ya biashara. Kwa hali hiyo waliomba kutajiwa mikakati ya ujifunzaji wa L2 ambapo ilikuwa rahisi kwao kutaja ile ambayo walifikiri kwamba ndiyo iliwasaidia kujifunza Kiswahili kama lugha ya biashara. Matokeo haya yanawiana na maelezo ya kina Krashen (1987), Oxford, Tarone 1990, Ellis 2003, O'Marley na, Chamot 1990 na Gardner 2000 wanoeleza kwamba wakati wa ujifunzaji wa L2 mara nyingi mjifunzaji lugha hujikuta amejifunza lugha bila kutambua kwamba kuna mikakati ya ujifunzaji L2 ambayo ilimsaidia kujifunza lugha hiyo. Hoja ambayo imeshadidiwa na Gardener (2000) ambaye anakubaliana na mhimili wa Kwanza wa Krashen (1987) unaohimiza kwamba ujifunzaji lugha ni swala la kisaikolojia ambalo hujitokeza kama motisha ambayo humshnikiza mjifunzaji kujifunza lugha hiyo.

Katika swali la kutaka kutambulishiwa mikakati ya ujifunzaji L2, wasailiwa wote 260 kutokana na hojaji na mwongozo wa mahojiano walikiri kwamba walihitaji kutambulishiwa mikakati ya ujifunzaji L.2 ili kubaini kama ndiyo walitumia kujifunza Kiswahili kibiashara. Baada ya kutambulishwa baadhi ya mikakati na mtafitiwa, walitaja ile ambayo walifikiri ndiyo iliwasaidia kujifunza Kiswahili kibiashara. Data zilizopatikana na umaratokezi wa hojaji ipo kwenye jedwali 4.3;

#### **Jedwali 4.3: Mikakati iliyokuwa ikitumiwa na wafanyabiashara kujifunza Kiswahili .**

<b>SN</b>	<b>Mikakati</b>	<b>Mukwano</b>	<b>Simlaw Int.</b>	<b>Kikuubo</b>	<b>Jumla</b>	<b>%</b>
1.	Nyimbo/Ukariri	08	03	05	16	15.5
2.	Mwanafunzi kwa mwanafunzi	02	--	04	06	6
3.	Matumizi ya lugha chanzi	04	06	04	14	13.5
4.	Kuongea	--	03	07	10	9
5.	Mawasiliano	08	07	05	20	19
6.	Mitagusano ya ukuruba kati ya wanunuzi na wauzaji	02	10	05	17	17
7.	Teknolojia	03	03	04	10	9
8.	Mpango binafsi	03	--	--	03	3
9.	Kufidia	02	--	--	02	2
10.	Utambuzi	--	06	--	06	5
11.	Upatikanaji tena	--	--	01	01	1
<b>Jumla</b>		<b>32</b>	<b>38</b>	<b>33</b>	<b>103</b>	<b>100%</b>

Asili: *Data kutokana na hojaji.(Februari,2022)*

##### **4.2.1.1 Nyimbo/ Ukariri**

Matokeo ya hojaji yalionyesha kwamba wafanyabiashara walikuwa wakitumia mkakati wa nyimbo/ ukariri katika kujifunza Kiswahili kwa ajili ya kuendeleza biashara zao. Wasailiwa nane (08/32) kutoka Ekedu ya mukwano, watatu (03/38) kutoka Ekedu ya Simlaw Internatioal na watano (05/33) kutoka soko la Kikuubo kwa jumla wasailiwa kumi na sita (16/103) ambapo ni jumla ya asilimia (15.5%) walisema kwamba walikuwa wakisikiliza nyimbo za Kiswahili na wakati mwingine kuzikariri hivyo kujikuta wanapata kujua Kiswahili.

Nyimbo/ ukariri ni mojawapo wa mikakati iliyo bora katika ujifunzaji wa lugha yoyote ile. Mkakati huu ulipendelewa sana na wafanyabiashara amba walipatikana katika sehemu teule zilizofanyiwa utafiti. Data zilizopatikana kwa kutumia hojaji zilionyesha kwamba kukariri kuliwasaidia kuimarisha lafudhi ya matumizi ya msamiati amba walikuwa wakitumia katike kuendeleza biashara zao. Walisema kwamba mkakati wa ukariri uliwafanya wawe na mfumo fulani amba walikuwa wakitumia ili kuwavutia wanunuzi. Aidha, walisema kwamba ukariri uliwafanya wahifadhi maneno mengi ambayo wangetumia bila kusahau. Kila mara walipoyatumia ndivyo walivyoishia kuyatamka vizuri na kupata misemo ya kiutani utani katika kuendeleza biashara zao jijini Kampala. Hali hii imepigiwa upatu na hatua ya pili ya mhimili wa upataji/ujifunzaji wa lugha ya pili wa Krahen (1987). Tunafahamishwa kwamba mwanafunzi hukariri msamiati amba alijifunza katika hatua ya kwanza ambayo ni ya unyamavu. Kwamba baada ya kuhifadhi baadhi ya maneno basi anaweza kuyakariri na kuyatumia katika mazingira ambamo maneno hayo yanahitajika.

Matokeo kutokana na mahojiano yalihuisha wafanyabiashara kumi na tisa ambao walikiri kuhusika sana katika usikilizaji wa nyimbo tofauti tofauti za Kiswahili. Hoja hii iliwekewa uzito wakati wa mahojiano na mfanyabiashara 023 ambaye alitoa mfano wa wimbo wa Chameleon kwamba;

### MS 023

*Anaomba bitu bya pei kali kama hajui mimi sina mali. Si unaona pei kali....Mutu kama nasema pei kali mimi nasema pei muzuri.*

Anaomba vitu vya bei ghali kama hajui mimi sina mali. Si unaona bei ghali..  
Mtu akisema bei ghali mimi nasema bei nzuri (TY).

Tahajia zinazojitokeza katika mahojiano haya ni kwa ajili ya athari za lugha asili. Japo kuna makosa kama hayo, Krashen (1987) anasema kwamba baada ya muda huwa yanapotea wakati mzungumzaji anamudu kuongea kwa kutumia lugha lengwa.

Kwa kushadidia, utafiti wa Xian (2010) alioufanya Uchina akirejelea (Peter, 1998; na Stock, 1978) unaonyesha kwamba kukariri kunasaidia mjifunzaji wa lugha ya pili kuelewa zaidi lugha hiyo. Kwamba kutumia mkakati huo, kunawafanya wahifadhi msamiati, sentensi na misemo yoyote ambayo inatokea katika lugha lengwa. Matokeo haya yameelezwa na Krashen (1987), Ellis (1997) na Gardener (2010) wanaoshikilia kwamba katika hatua za Kwanza za ujifunzaji lugha, mwanafunzi hutumia sana urudiaji rudiaji na kukariri msamiati na virai ambavyo amesikia kutokana na lugha anayojifunza. Aidha, Gardener (2000) katika mhimiili wake wa kwanza, anasema kwamba mchakato wa uradidi wa maneno huhitaji mjifunzaji wa L.2 kuwa na nia na kuweka jitihada nyingi katika kujifunza lugha hiyo ndiyo apate msamiati wa kutumia. Wasailiwa walisema kwamba wanunuvi kutoka nje ya nchi walitumia ‘viswahili’ tofauti tofauti. Hivyo, ilikuwa ni bora kila mara kukariri kila msamiati ambao walikutana nao ili kuwasaidia kutumia vizuri Kiswahili kibashara kulingana na wanunuvi ambao waliwafikia. Naye mfanyabiashara 026 alikiri kwamba maneno yanayokaririwa huwa ni vigumu kuyasahau, na ni mojawapo ya mbinu za kuwavutia wanunuvi. Baadhi ya maneno aliyotaja ni kama; *karibu boss!, bei muzuri! Tafanya muzuri, kalibu lafiki, ona pesa/mafaranga ngapi?* n.k Matokeo haya yanaendana na fikra za kina Skehan (1991); Stern (1992); Griffths (2004), Rubin (1987) wanaosema kwamba kukariri kunasaidia kujenga uelewa wa lugha lengwa na kujenga msingi bora wa kumbukizi mionganoni mwa wajifunzaji lugha.

#### **4.2.1.2 Mkakati wa ujifunzaji kati ya Mwanafunzi na mwanafunzi**

Kutokana na umaratokezi wa hojaji, wasailiya wawili (02/32) kutoka ekedi ya Mkwano na wasailiya wanne (04/33) kutoka kwa soko la Kikuubo walisema kwamba kwao hujifunza kutokana na ama wanunuzi watumiao Kiswahili ama wafanyabiashara wenzao ambao kwa kiasi fulani walijua Kiswahili. Jumla ya wafanyabiashara sita (06/103) ambapo ni asilimia sita (06%) walisema kwamba licha ya kuwepo mikakati mingine ambayo walitajiwa kwao waliona kwamba ujifunzaji mionganoni mwao na wanunuzi ndio ulikuwa wa kimsingi sana kwao kujifunza Kiswahili kama lugha ya biashara. Kupitia mkakati huu walijikuta mara nyingi wakiomba msaada ama waziwazi au kisirisiri kutoka kwa wanunuzi wenzao wanaofahamu Kiswahili ama kuwasaidia kuwafafanualia zaidi. Kuomba msaada kunaweza kujitokeza kama mkakati, kulingana na Gardener (2000) kwa kukubaliana na hatua ya pili ya ujifunzaji lugha ya Krashen (1987) ni hulka ya mjifunzaji lugha ya pili ambayo imechochewa na motisha unaosaidia ujifunzaji lugha pale ambapo anaona kwamba atakapomuuliza mjifunzaji mwenzie ataelewa zaidi. Hivyo wanaendelea kusema kwamba mjifunzaji wa L.2 anaweza kujifunza lugha hiyo kutoka kwa mwanafunzi mwenzake ambaye ameonesha kwamba yuko katika kiwango cha tatu na nne cha ujifunzaji wa L2. Walikiri kutambua kuwepo kwa mikakati mingine lakini walisema kwamba kwa kiasi kikubwa walifanya mipango ya kujifunza wao wenyewe kwa wenyewe. Maana waliona hili liliwafanya kuepukana na hali ya kuwa na uoga wakati wa kuongea na kupunguza kubezwa na waliojiita wamilisi wa lugha ya Kiswahili. Wakati wa mahojiano na wasailiya nane mmoja wao alisema;

#### **MS.016**

*Banaange oluswahili lwa basomesa ne lwetuuliza lusi luzibbu .lwekyo oyigira kumunno alumanyi obulungi nakunyonyola ebigambo.Obba siekyo noolinda omusubuuzi efafuuka mkwano gwo nakunyonyolako kuebimu nga mulimumboozi ekyamula kyamula.*

Jamani Kiswahili cha walimu na kile tuasikia ni vigumu .Hivyo unajifunza kutoka kwa mwenzako aliyekifahamu vizuri ambaye anakufafanulia machache wakati wa maongezi ya mapumzikoni.(TY)

#### **M.S 031**

*Nze nninda omusubuzi bwaba azze.Olwo neng'amba munaange nti ojjakunyambako okuvunula. Omusubuzi oluvaao nemubuuza abinyonyole mbitegeere buluungi. Alafu mimi tavijua muzuli.*

Mimi husubiri mnunuzi anapofika. Hapo Ninaomwomba mwenzangu kuja kunisaidia kutafsiri. Mnunuzi kuondoka tu ninamuuliza anifafanulie nielewe

vizuri. Halafu mimi nitakuwa ninayafahamu maneno hayo vizuri.(TY).

Matokeo haya yanawiana na watetezi wa mkakati huu kama kina Vygotsky (1978), Towell na Hawkins, (1994) Scollon na Scollon (2001) ambao wanasema kwamba kuna pale ambapo hapastahili utaalamu wa mwalimu kuwepo ndipo mwanafunzi ajifunze L2, ila anaweza kushirikiana na mwanafunzi aliye na umilisi zaidi kujifunza lugha lengwa. Ezat (2015) ambaye alikuwa akifundisha wanafunzi wa Uarabuni Kiingereza kama L2 ameeleza kwamba, mionganoni mwa changamoto alizokumbana nazo kutoka kwa walimu wenzake ni kuwepo na tabia ya kufundisha wanafunzi kupita mtihani kwa kutumia njia ya kukariri na walimu kulazimisha mafunzo yao kwa wanafunzi wa L2. Anaeleza kwamba wanafunzi wanastahili kuendeleza ujifunzaji wao kwa mikakati ambayo wanafikiri itawafaa na mojawapo ilikuwa wanafunzi kuendeleza ujifunzaji mionganoni mwao wenyewe.

Kwa kuongezea wataalamu wa L2 kama Palma na Madirgal (2021), Anderson na Elioumi (2004), Oxford (2003), na Rock (2012) wanasema wakati wa kujifunza L2 mwanafunzi hukumbwa na changamoto nyingi za ujifunzaji L2. Mionganoni mwa hizo changamoto zaweza kusuluhishwa kwao wenyewe mionganoni mwa wanafunzi hasa katika mazingira ambayo mwalimu hayupo.

Utafiti huu vile vile umekubaliana na (Brown 2012, Skehan 1989 na Ellis 2003) wanaoeleza kwamba mwanafunzi anaweza kuomba msaada kutoka kwa mwanafunzi mwenzake pale ambapo amekwama, kutoka kwa mzugumzaji wa lugha lengwa ama mwalimu anayefundisha lugha hiyo kama itahitajika. Gardener (2010a) anasema kwamba mwanafunzi anapokuwa na nia ya kujifunza L.2 anajitafutia yeye mwenyewe hali ambayo itamwezesha kujifunza lugha hiyo. Katika mazingira ya uendelezaji biashara katika jiji la Kampala ujifunzaji wa Kiswahili uliendelezwa katika hali ya kutaniana na kufanya mizaha kutumia lugha ya Kiswahili mionganoni mwa wafanyabiashara wenyewe ama wanunuzi ambao walinunua bidhaa kutoka kwa wafanyabiashara wenza.

#### **4.2.1.3 Mkakati wa Matumizi ya lugha chanzi**

Massamba (2012) anasema kwamba Kiswahili ni lugha ambayo iliathirika na lugha nyingine za Kibantu. Kwa hali hii inakuwa rahisi sana mjifunzaji L2 ama kuhamisha sheria za lugha mama kutoka L.1 hadi L.2 na pia kutamka neno katika lugha yake chasili. Watafitiwa ambao walikuwa Wabantu walithibitisha kwamba Kiswahili kina maneno ambayo yalifanana na lugha mama zao. Hivyo wasailiwa wanne (04/32) kutoka ekedi ya Mukwano, sita (06/38) kutoka Simlaw International Limited na wanne (04) kutoka soko la Kikuubo ambao ni

wasailiwa kumi na nne (14/103 ) ambapo kwa jumla ni asilimia kumi na tatu nukta tano (13.5%) walikiri kwamba kushirikisha lugha mama katika ujifunzaji wao Kiswahili kama lugha ya biashara kuliwasaidia kujifunza kwa haraka Kiswahili. Kwamba walijaribu kuoanisha msamiati waliowahi kusikia katika mazingira ya biashara kutoka kwa wasemaji wa lugha ya Kiswahili. Walikiri kwamba lugha ya Kiswahili ina msamiati amba o unafanana na baadhi ya maneno ya lugha zao mama. Lugha ambazo huwa zimetokana na L.1 moja huathiriana kwa namna moja ama nyingine. Hivyo ilikuwa rahisi kwao kuhawilisha maneno mengine kutoka L.1 hadi Kiswahili. Wakati wa mahojiano na wasailiwa ishirini na tatu ilibainika kwamba L.1 zilikua na sehemu kubwa katika ujifunzaji wa Kiswahili kama lugha ya biashara. Kutokana na nukuu zifuatazo tunaona mchongo mkubwa wa L1 katika ujifunzaji wa L2 ambapo kulingana na utafiti wetu ni lugha ya Kiswahili.

#### **M.S 045**

*Chiswaili ni kama chiluga yetu chabagaanda.Oyinza okugamba muntu yangu kalibu. Ama oyagala engoye.Ndaba nabo baziita nguwo. Kakati engoye ne nguwo tebyaukana nyoo.*

Kiswahili ni kama lugha yetu Waganda.Unaweza kusema mtuwangu karibu. Ama unataka nguo. Naona nao (wazungumzao Kiswahili) wanaziita nguo. Hivyo neno engoye na nguo maneno hayo hayatofautiani sana.(TY)

Kauli ya mfanyabiashara 045 inakubaliana na Chomsky (1968), Ladefoged (1971) na Selinker na Gass (2008) amba o wanasema kwamba ujifunzaji wa L2 huwa na msingi thabiti katika lugha ya asili. Watu hujaribu kuhamisha muundo, maana na usambazaji wa muundo wa maana ya lugha yao ya asili na utamaduni kwa lugha lengwa. Huwa wanajaribu kuzungumza na kutenda katika utamaduni wao wanapajaribu kujifunza, kuelewa lugha na utamaduni wa lugha nyingine.

#### **M.S 050**

*Luswaili siyo ngumu.Walio ebigaambo ebifaanana ne ebyoluganda. .*

*Mulimo nga ebbasi, maama, okugenda .Tollaba nga bifanana nenbya luswaili.*

Kiswahili sio kigumu. Kuna maneno yanayofanana na ya luganda.Kuna kama basi, mama, kuenda. Si unaona yanafanana na ya Kiswahili (TY).

Kauli ya mfanyabiashara 045 na 050 zinaonyesha kwamba lugha chanzi huwa na mchango mkubwa sana katika ujifunzaji wa L2. Kauli hizi zinakubaliana na hatua ya pili ya Krashen (1987) mhimili wa kwanza ambapo anasema kwamba wakati mjifunzaji lugha anaanza kuongea L.2 huibuka na makosa machache. Makosa haya mara nyingi hutokea kwa ajili ya

kuathirika kwa L.1. Selinker na Gass (2008) wanakubaliana na Krashen (1987) kwamba wakati huu mjifunza lugha hujaribu kutoa mila zote za L2 kutokana na mambo teule ambayo ni; Uwasilishaji wa lugha ambapo baadhi ya istilahi, mamlaka na utaratibu wa lugha ya pili unaweza kutokana na uwasilishaji katika lugha ya kwanza.

#### **4.2.1.4 Mkakati wa Kuongea**

Wasailiwa watatu (03/38) kutoka Simlaw International Limited na saba (07/33) kutoka sokola Kikuubo ambapo waliwakilisha asilimia tisa (09%) ya wasailiwa walisema kwamba wao huwa wanaongea ongea maneno kwa kubahatisha maneno ya Kiswahili yale ambayo walifikiri yaliendana na Kiswahili cha biashara. Hii ni idadi wastani sana ya wasailiwa lakini huenda kuna pia wengine waliotumia lakini hawakutambua kwamba ni mkakati wa kujifunza L2. Walitaja kwamba wao huongea ongea maneno ya Kiswahili kwa namna wanavyoyasikia kutoka kwa wazungumzaji. walikiri kwamba walikuwa wakitumia mkakati wa kuongea tuseme kimushtukizo. Tafakuri nyingi zinafafanua kwamba kuongea ni stadi ya ukuzaji wa lugha hivyo, ni vigumu kuendeleza biashara yoyote ila bila kuwa na hulka za kuongea ongea.

Katika hali ya kutafuta wanunuizi lazima kuwepo maneno shawishi ambayo yanamfanya mnunuizi kuchagua muuzaji X badala ya muuzaji Y. Ikumbukwe kwamba kuzungumza huenda sambamba na ujifunzaji wa lugha husika. Matokeo kulingana na mahojiano baina ya mtafitiwa na watafitiwa kumi na saba yalidhihirisha kwamba baadhi ya wafanyabiashara walijifunza Kiswahili kama lugha ya biashara kutokana na kuongeaonjea kimshtukizo maneno ya Kiswahili. Katika mjadala wa mahojiano na mfanyabiashara 122 na 130, walisema kwamba;

#### **M.S :122:**

*Onaona sasa mimi nasungumza sungumza. Ebyo byetusiibamo. Twogerayo bitono tono. Omanyi olulimi booba tonaluyiga obulungi tekyikwetagisa atte oyasamme yasamme oinza kwogeera ebikyaamu. Mfuubako okgoogeera yogeera ebyo byensobodde.*

Unaona mimi nazungumza zungumza. Twashinda kwa hali hiyo-yaani kuongea ongea maneno machache.Twaongea machache. Wajua kabla hujajifunza lugha vizuri haitakikani kuruia rukia unaweza kuongea mambo ambayo hayafai.Najitahidi kuongea yale naweza (TY)

**Naye mfanyabiashara 130 alisema :**

*Nze mfubakko okulabba ndina kenjogedeeo. Wesanga mukusaaga okwo ndi kuiga oluswairi. Olulimi luno si luzibu booba oyogeera buli lunaku.*

Mimi hujitahidi kuona kuna kitu nimeongea. Utakuta katika huo utani najifunza Kiswahili. Lugha hii (Kiswahili) si lugha ngumu endapo unaongea kila siku (TY).

Kauli hizi mbili zinaonyesha kwamba wafanyabiashara wana juhudzi za kutaka kujifunza Kiswahili kama lugha ya biashara. Gardener (2000) anasema kwamba ari na juhudzi alizonazo mjifunzaji lugha ya pili humsaidia katika ujifunzaji lugha hiyo kwa kutumia muda mfupi.

Walitaja kwamba wao huongeaongea maneno ya Kiswahili kwa namna wanavyoyasikia kutoka kwa wazungumzaji. Hili linatokea kwenye mazingira maalumu pale ambapo mwalimu anakuza stadi za kujifunza lugha. Hakuna ithibati kwamba stadi hizo ni za kujifunza Kiswahili kwa ajili ya biashara. Hata hivyo, wataalamu wa ujifunzaji L2 kama kina Krashen (1987), Weaver na Cohen, (1994) na Cook (2001) wanasema kwamba ili mwanafunzi ajifunze lugha ya pili, huanza kwa kusikiliza lugha hiyo halafu baadaye akaiongea. Kulingana na Krashen (1987) kuongea ni hatua ya pili katika ujifunzaji wa L.2. Yaani mjifunzaji huwa ameanza kuunda sentensi fupi fupi na tena makosa huanza kupungua kadri anapopata umilisi wa lugha lengwa. Cohen, (1996), Cohen na Weaver (1994) wameeleza sababu kwa nini kuongea kunakuwa mkakati wa kujifunza L2 na sio tu stadi ya ukuzaji wa lugha. Katika maelezo yao wamedadavua kwamba mjifunzaji L2 huanza na kutambua malengo na sababu ya kuongea lugha hiyo, atanufaika vipi na hayo maarifa? Je, kuna maarifa katika hali halisi ambayo yatamwezesha kujifunza L2, nini kitafanyika akianza kuongea katika lugha hiyo? Wakati wa mahojiano kati ya mtafiti na mzungunzaji katika nukuu ifuatayo;

### **M.S 063**

*Mimi napenda ongea sana swaili. Lugha ii inafanya mimi napata bakasitoma mingi sana. Kale lwangu lutwanguila okuluigga.*

Mimi ninapenda kuongea Kiswahili. Lugha hii inanisaidia kupata wateja wengi sana. Ni nyepesi na ni rahisi kujifunza (TY)

Gardener (2000) anasema kwamba kinachomshinikiza mjifunzaji huyo kuongea lugha hiyo ninia ya kutaka kujifunza kwa ajili ya malengo fulani. Malengo hayo huwa ni motisha kwa ajifunzaye L.2. Kwa wafanyabiashara, kinachowapa motisha kujifunza Kiswahili ni kwa ajili ya kukitumia katika kuendeleza biashara zao. Hivyo, huwa wanakuwa tayari kukabiliana na matokeo ya kuongea kwao bila kujali makosa ya sarufi yatakayojitokeza almradi ajikute akiongea maneno katika lugha lengwa.

#### **4.2.1.5 Mkakati wa Mawasiliano**

Uwezo wa kuwasiliana na kubadilishana maarifa na taarifa ni muhimu sana kwenye ulimwengu wa biashara. Hakuna njia yoyote mwafaka ambayo inaweza kufanikisha kubadilishana mawazo na kushawishi wanunuzi bila mawasiliano. Data zilizokusanywa kwa kutumia hojaji zilionyesha kwamba wasailiya nane (08/32) kutoka Ekedi ya Mukwano, saba (07/38) kutoka Simlaw International Limited na watano (05/33) kutoka soko la Kikuubo ambalo ni jumla ya asilimia kumi na tisa (19%) walikiri kutumia mkakati wa mawasiliano katika ujifunzaji Kiswahili kwa ajili ya biashara. Walikiri kwamba wao kwa kupitia mawasiliano na wanunuzi kutoka sehemu mbalimbali ambao hawajui Kiganda mara nyingi waliishia kutumia Kiswahili. Huu ni mkakati ulioibuka kutumiwa sana na wafanyabiashara jijini Kampala. Wafanyabiashara ambao walishirikishwa katika mahojiano walisema kwamba katika kule kuwasiliana kupitia ubadilishanaji zamu, walijikuta wanapata misamiati ambayo iliwasaidia kuwasiliana na wanunuzi wao kulingana na bidhaa ambazo walikuwa wakiiza. Walisema kwamba hawakujua Kiswahili kwa upana wake ila walichokijua kilikuwa kile kidogo kidogo cha kuuza bidhaa zao na labda kusalimiana tu, kwani hawangelewa ikiwa mazungumzo ya ndani yangeendelea.

Wakati wa mahojiano wafanyabiashara ishirini na wawili walikiri kwamba mawasiliano baina yao na wazungumzaji wa lugha ya Kiswahili kuliwafanya wapanue weledi wa misamiati mingi ambayo ilitumiwa katika biashara. Walieleza kwamba mawasiliano yalistaa milisha mazungumzo kati yao na wanunuzi.

#### **M.S 029 alisema**

*Tubaluddemu abbasubuuzi abakozesa luswaili nga bajja kugula ebiintu. Kati togeera nab "o bwetugatamu oluganda. Mwanyinanzie communication mmumakati waffe etuyambye nnyo kukozesa luswaili.*

Tumekuwa nao wanunuzi wanaotumia Kiswahili wakija kunua vitu. Huwa tunaongea nao tukichanganya Kiganda. Dadangu mawasiliano kati yetu imetusaidia sana kutumia Kiswahili (TY).

Katika hatua ya tatu ya mhimili wa kwanza Krashen (1987) anasema kwamba mjifunzaji wa L.2 huwa anastaamili mazungumzo kati yake na mzungumzaji wa lugha lengwa. Kwamba wakati huu mjifunzaji wa L.2 ana uwezo wa kutumia sentensi sahili na changamani katika mawasiliano na watu wengine. Umilisi ambao atakuwa amepata unamsaidia yeze mwenyewe kutambua kwamba sehemu fulani amefanya makosa na kuna jinsi anaweza kujisahihishia makosa hayo. Watetezi wa ujifunzaji wa L2 wanaoshadidia mkabala wa kimawasiliano kama

Dornyei (1994b), Lam (2010), Nakatani (2010), wanasema kwamba huwa kuna manufaa kemkem wakati wa kutumia mkakati wa mawasiliano kujifunza L2. Wanaendelea kusema kwamba mkakati huu huwa ni nyenzo ambayo huhusisha mantiki kwa namna ya kuwasilisha ujumbe. Tarone (1989) anakubaliana nao kwa kuweka ufanuzi zaidi kwa kutaja kategoria tano ambazo zinajenga mkakati wa mawasiliano yaani: kutafakari, kukopa, kuomba msaada na kuiga. Hoja ambazo Palibakht (1985) Poulisse (1990), Bialystock (2001) na Rubin na Thompson (1994) wamepingana nazo kwa kusema kwamba hawaoni umuhimu wa kutumia mkakati wa mawasiliano wakati wa kujifunza L2 kwani huwa tayari walishapata umilisi wa L1. Hata hivyo, ili kuweka wazi kwa nini mkakati wa kimawasiliano ni faafu, ufanuzi zaidi umetolewa na Taksiran (2010 ), Tarone (1984), Willims (1987), O'Malley (1987) Tarone na Yule (1989) kwamba mkakati wa mawasiliano huchangia katika ukuzaji wa umilisi wa mawasiliano na kuhamisha stadi za lugha ya kwanza hadi lugha ya pili. Hili limethibitishwa na:

### **M.S 096**

*Its very easy for one to create a sentence in your language and use it in Kiswahili while communicating to a customer. Reason is Kiswahili is not hard. For example if you want to respond to a customer who wants shoes . You ask onataka biatu.*

Ni rahisi sana mtu kuunda sentensi katika lugha mama na kuitumia katika Kiswahili wakati unwasiliana na mnunuzi. Sababu ni kwamba Kiswahili si kigumu. Unauliza unataka viatu?. TY)

Willims (1979), O'Malley (1987) Tarone na Yule (1989) Wamesema kwamba japo kuna uhusiano kati ya mawasiliano katika L1 na L2, pale ambapo mjifunzaji anahamisha baadhi ya miundo ya L1 hadi L2 hakuna ithibati kwamba alitumia mkakati wa kuwasiliana kujifunza L1. Wanaendelea kusisitiza kwamba utumiaji wa mkakati wa mawasiliano hutofautiana kulingana na wajifunzaji na namna wanajifunza lugha wanayokusudia kujifunza. Tafakuri ya maandishi haya ilipatia utafiti wetu uhuru wa kuhusisha dhana ya mawasiliano na ujifunzaji wa Kiswahili kama njia mwafaka ya kufanikisha biashara mionganii mwa wafanyabiashara jijini Kampala. Lengo la namna ya kuwasiliana kati ya wanunuzi na wauzaji ni kufanikisha shughuli za biashara na siyo mawasiliano ya jumla tu.

#### **4.2.1.6 Mtagusano na ukuruba kati ya wanunuzi na wafanyabiashara**

Taarifa iliyotokana na hojaji zilionyesha kwamba Wasailiwa wawili (02/32) kutoka Ekedo ya Mukwano, kumi (10) kutoka Simlaw International na watano (05) ambao kwa jumla ni asilimia kumi na saba (17%) walikiri kutumia mkakati wa mtagusano na ukuruba kati yao na

wanunuzi ambapo ilipekea wao kujifunza Kiswahili kibiashara. Binadamu hujikuta wametagusana kulingana na shughuli mbalimbali ama sehemu wanakoishi ama kutendea shughuli zao za kazi za kila siku. Kwa kutumia usaili wafanyabiashara 13 walikiri kutagusana na wazungumzaji wa Kiswahili waliokuwa ama wakiishi nao ama ambao walishirikiana kwa muda mrefu katika harakati za kufanya biashara. Walisema kwamba katika jamii walimokuwa wakiishi kulikuwa na mtagusano na makabila mbalimbali. Hili liliwafanya wawe wakikopa baadhi ya msamiati kutokana na jamii walizokuwa wakitangamana nazo. Cohen (1996) anasema kwamba mtagusano huhusisha hatua ambayo wanafunzi huchagua vipi watagusana na wanafunzi ama wazungumzaji wa lugha lengwa kuititia kushauriana, kuuliza ufanuzi wa maswala fulani na kupata msamiati mpya kutoka kwa wanaozungumza lugha lengwa.

Mfanyabiashara 005 alikiri kujifunza Kiswahili kutokana na kutangamana kwake na wamama wafanyabiashara ambao ni wa kutoka nchi ya Demokrasia ya Kongo. Alisema kwamba

*bako kina bamama wengi kutoka Kongo lafiki yangu. Banaongea namimi swaili.* Krashen (1987) anasema kwamba katika kiwango cha hatua ya nne ya mhimili wa kwanza mjifunzaji L.2 ana uwezo wa kutangamana na wazungumzao lugha lengwa. Hapa mjifunzaji wa L.2 ana uwezo wa kuwasiliana kwa kutumia sentensi sahili na changamani huku akisawazisha sehemu ya kiima na yambwa. Ana uwezo wa kuhusisha maneno mingine wakati wa kutunga sentensi kama; vielezi, vivumishi, viwakilishi nk. Ellis (1994), Rahimi,Riaz na Salf (2008), Oxford (1990), Oxford (2011) Oxford na Chamot (2004), wamefafanua kuwa jamii ambayo mjifunzaji lugha anamoishi ama kutagusana nayo humsaidia kujifunza kaida, utamaduni na mila za lugha lengwa.

Mjifunzaji lugha hujitahidi kujaribu kuzungumza namna wazungumzaji wa lugha hiyo wanavyoizungumza. Hili hutokea mionganoni mwa watoto na hata watu wazima wanaojifunza L2. Mara nyingi hujikuta wanajihuisha na wenyeji wa lugha wanamoishi. Walipoulizwa kwa nini waliacha mikakati mingine ambayo pia ni muhimu katika ujifunzaji wa L2, walisema kwamba kuishi kwao na watu wanaozungungumza Kiswahili hasa katika maeneo kama Nakivubo, Mukwano, Burkeley na Kisenyi (haya ni maeneo ambayo mionganoni mwayo ni sehemu ua biashara zinazoendelezwa; Kwa mfano eneo la Mukwano) ambapo kuna makabila tofauti kama vile Wanubi, Chotara, Somali ambao hutumia Kiswahili kuliwasaidia

kujifunza Kiswahili.

#### **4.2.1.7 Mkakati wa Teknolojia**

Maendeleo ya teknolojia kuititia TEHAMA hasa matumizi ya simu yalianza tangu matumizi ya simu ya kukoroga hadi simu mahiri za mkononi. Mawasiliano na uendeshaji biashara unafanikishwa ndani ya sekunde chache tu kati ya wahusika walio sehemu mbalimbali. Luga za ulimwenguni zimekuwa zikitumia teknolojia kwa kuhusisha istilahi tofauti tofauti. Matumizi ya teknolojia yamekuwa kiungo kikubwa katika maendeleo ya watu ulimwenguni katika kurahisisha mawasiliano, kufanya biashara na mambo mengi ya kimsimgi.

Matokeo yaliyotokana na hojaji yalionyesha kwamba wafanyabiashara watatu (03/32), watatu (03/38) kutoka ekedi ya Simlaw International pamoja na wafanyabiashara wanne (04/33) ambapo ni asilimia tisa (09%) walichagua matumizi ya teknolojia kuwa ilichangia ujifunzaji wa Kiswahili kama luga ya biashara. Licha kuwa mkakati huu haukuwa kwenye orodha ambayo watafitiwa walitambulishiwa, ilibainika kwamba ni mojwapo ya mikakati iliyopendelewa katika ujifunzaji wa Kiswahili kwa ajili ya biashara.

Mahojiano kati ya mtafiti na baadhi ya wasailiwa yalithibitisha kwamba teknolojia imekuwa njia mwafaka kwao kuendeleza biashara hasa katika kuhusisha watu ambao hawakujua luga ya Kiganda. Walisema kwamba kuititia simu wanajifunza msamati mbalimbali, wanasikiza matangazo ya biashara kutoka redio mbalimbali. Walifuatilia pia vipindi vyta baadhi ya redio, youtube, BBC na mafunzo ya televisheni ya idara ya UBC namna ilivofafanuliwa na

#### **MS 079 kwamba,**

*Sisi pana enda kwa dalasi kusoma swaili. Mimi Napata chiswahili yangu kutoka kwa redio BBC haa safi sana na You Tube. Apo iko mambo mingi sana ya chiswahili.*

#### **M.S 083 anasema kwamba**

*Baba wangu likua na radio na kila jioni yeye litoa kitiii fupi nje kusikiliza BBC na Redio Uganda namna leo wanaita UBC kusikiliza maneno ya Amini . Yeye likua lafiki wa wajeshi .Namna iyo pia sisi nasikiliza na kuongea swaili. Mimi sasa natumia muzuri na basubuzi ii nakuja kunua manguo kwa pei ya wholesale.*

Kauli ya mfanyabiashara 79 na mfanyabiashara 083 zinaonyesha kwamba matumizi ya redio yalichangia pakubwa katika kujifunza Kiswahili. Ingawa walikubaliana na mikakati ambayo mtafiti aliwatajia, kwao waliona kwamba redio zinazotoa taarifa kutumia luga ya Kiswahili ziliikuwa bora sana kuegemewa katika ujifunzaji wa Kiswahili. Motisha ya mjifunzaji luga

anapopata nafasi ya kutumia mkakati kama huu ni jinsi ambavyo anajikuta amehifadhi baadhi ya msamiati (Gardner 2000) kutohana na juhudhi na ari alizoweka katika kusikiza yanayosemwa. Naye Krashen (1987) katika ujifunzaji anasema kwamba hatua ya kusikiliza ni kiwango muhimu sana ambapo mjifunzaji lugha hutumia kuhifadhi msamiati wa lugha lengwa. Wakati huu mjifunzaji anaweza kuhifadhi angalau maneno mia tano.

Kwa kuongezea utafiti huu unakubaliana na Herman (2015) kwamba matumizi ya teknolojia katika ulimwengu wa sasa ni dhihirisho la maendeleo hasa katika uwanja wa mawasiliano jambo ambalo linarahisisha utekelezaji na uendeshaji wa sehemu nyingine za maendeleo kama vile uendeshaji biashara, ushiriki wa kisiasa, Mtagusano na ukuruba kati ya wanunuza na wauzaji kiuchumi. Ameeleza kwamba wakati wa kutumia tafsiri huwa kuna ukopaji. Anasema kuwa ndiyo njia ilio bora zaidi kwani kuna kukopa maneno kutoka lugha asilia katika lugha lengwa yaani lugha moja kutumia usemi kutoka lugha nyingine. Kwa kuongezea matokeo ya utafiti wetu yanawiana na mchango wa Garfinkel 1972, Wipf 1984, Cook 1994, Holland, Kaplan na Sams 1995, Levy 1997 wanaodai kwamba matumizi ya redio humsadia mjifunzaji lugha kujifunza lugha yoyote na katika mazingira yoyote yale hata kama ni kijiji ambacho ni masikini zaidi ulimwenguni. Kwamba redio huwa na masafa mapana ambapo mjifunza L2 anaweza kujifunza lugha hiyo almradi ana uwezo wa kuwa na redio.

#### **4.2.1.8 Mkakati wa Mpango binafsi**

Kuna njia mbalimbali ambazo mtu anaweza kuijandaa kwa ajili ya kufanikisha kitu fulani. Alimradi mtu ana motisha ya kufanya kitu/shughuli basi atatafuta namna ya kufanikisha shughuli hiyo. Kutumia hojaji wafanyabiashara watatu (03/103) ambapo inawasilisha idadi ya silimia tatu (03%) peke yao ndio walikiri kutumia mpango binafasi kujifunza Kiswahili kama lugha ya biashara. Ila mahojiano kati ya mtafiti na watafitiwa yalionyesha kwamba kutumia mpango binafsi kujifunza Kiswahili kama lugha ya biashara ilikuwa njia rahisi. Walitaja kwamba walianza kwa kupata orodha ya maneno ambayo walifikiri yatawasaidia katika kutumia Kiswahili. Pili, kabla ya kuwasiliana na mnunuzi waliandaa kwa kupanga maneno kutoka lugha yao chasili halafu maneno hayo yakanukuliwa katika Kiswahili.

Matokeo ya mahojiano ambayo yalihuisha wasailiwa 15 walikiri kwamba kwa muda mrefu walijipangia namna wangeliedeleza ujifunzaji wa Kiswahili kama lugha ya biashara.

#### **Mfanyabiashara 008 alisema kwamba,**

*.....In order to get Swahili words you need just to note down some basic terms of business so long as you know the start up abari and kalibu. It takes*

*some time but in a long run you learn how to use them.*

Ili kupata msamiati wa Kiswahili unahitaji tuu kuandika maneno ya kimsingi ya biashara almradi unajua ya kimsingi kama habari na karibu. Inachukua muda lakini baadaye unajifunza kuyatumia (TY).

Wanafunzi wa L2 wakati mwingine hutumia ufasaha wa L1 kujifunza L2 (Ghalebi, Sadighi,na Bagheri, 2020). Huwa inakuwa rahisi mwanafunzi kuunda sentensi fupi fupi katika vijikaratasi kwa kurejelea msingi wa lugha chanzi halafu anazihawilisha katika lugha lengwa. Mchakato wa aina hii umefafanuliwa na Krashen (1987) kwamba katika kiwango cha tatu na nne katika ujifunzaji L.2 mwanafunzi huanza kuunda maneno na sentensi fupi fupi ambazo zinaweza kumsaidia katika kuwasiliana bila uoga. Nao kina Vyotsky (1978), Gass na Selinker (1994), Suri(2010) wanakubaliana kwamba mjifunzaji wa L2 mwanzo hujenga mawazo na kuyapanga halafu akayawasilisha katika lugha lengwa. Motisha unaotoka na mrejesho anaopata kutoka kwa walengwa unampa ari ya kuendelea kujifunza lugha hiyo

#### **4.2.1.9 Mkakati Kufidia**

Kuna wakati mjifunzaji lugha hutumia lugha hiyo kwa kupata msamiati amba o unatokana na kubahatisha tu. Katika bahatisha bahatisha anajikuta kwamba ama amesema lililosahihi ama alilokosea. Kwa wale amba o walibahatika kutumia kubahatisha na kufanikiwa, wamekuwa wakihifadhi misamiati ya Kiswahili hasa inayohusiana na biashara. Hii ilitokana na majibu yalitolewa na wafanyabiashara wawili (02/103) kutokana na hojaji zilizojazwa. Kwamba walijaribu kuoanisha msamiati waliowahi kuusikia katika mazingira ya biashara kutoka kwa wasemaji wa lugha ya Kiswahili. Hili lilifanyika kila wakati walipofikiwa na wanunu zi amba o walionyesha kwamba hawakuweza kuzungumza baadhi ya lugha za wenyeji. Krashen (1978), Gardener (2010a), Vygotsky (1978) wanashikilia kwamba mwanafunzi wa L2 huweza kuzungumza katika lugha lengwa endapo ana tajriba ya kukumbuka aliyo yasoma katika mazingira ya darasa, aliyo yasikia kutokana na wazungumzaji wa lugha lengwa ama kubahatisha maneno kutoka lugha lengwa. Hoja ambayo Gardener (2010b) amesema kwamba kubahatisha hujengeka kwa misingi ya nia/ari aliyonayo mjifunzaji lugha kama nafsi yake ina mruhusu kuhifadhi kile ambacho alibahatisha na kikawa cha ukweli. Anasititiza kwamba kwa hali kama hii mwanafunzi hastahili kulazimishwa kujifunza katika mazingira rasmi ya darasani ila waachwe katika mifumo na mazingira halisi ya lugha ambayo anatangamana nayo kumwezesha kujifunza lugha husika. Kupitia mahojiano ya wafanyabiashara 03, utafiti huu ulibaini kuwa mkakati wa kufidia ulikuwa mkakati rahisi

uliowasaidia kujifunza lugha. Waliweza kutangamana na wazungumzaji katika mazingira yao na baada ya muda fulani walijikuta wakiwa wameimarika kutumia Kiswahilikutokana na msamiati ambao walibahatisha na kuishia kuutumia mara kwa mara katika mazingira ya biashara.

#### **M.S 051**

*Mimi nakubatisha maneno.Mi nasema boss kalibu, bosi mimi tabadilisha pesa muzuri.Wewe nataka ya Kenya, Congo, Rwanda ama Tanzania.Yote iko mimi tapatia wewe kwa pei muzuri.Namna iyo.*

O'Malley na Oxford (1990) Griffths (2004) wanasema kuwa mkakati huu wa kufidia husaidia mwanafunzi wa L2 wakati wa kuunganisha sauti na ujenzi wa sentensi. Matokeo haya yanakubaliana na tafiti za wataalamu wa ujifunzaji L2 ambao wanapendekeza kwamba mwanafunzi akionyesha dalili za kuimarisha umilisi wake katika lugha lengwa basi huwa hauhitaji tena kwani huwa tayari umetimiza lengo la kufanikisha kuzungumza kwa kutumia lugha lengwa (Chamot, 1987, Cohen, 1996 na Nick, 2008).

Kwa mantiki ya utafiti huu hatukusudia kujadili mwanafunzi yejote ajifunzae L2 bali wafanyabiashara ambao walihitaji kuitumia Kiswahili kwa ajili ya biashara. Kubahatisha baadhi ya msamiati ya biashara kuliwasaidia kuendeleza umilisi katika matumizi ya Kiswahili kibiashara. Kupitia mahojiano na kujibu swali kuhusu mikakati ambayo walitumia kujifunza Kiswahili kibiashara, wasailiwa walijitetea kwa kukubali kwamba takribani mikakati yote ya ujifunzaji na matumizi ya lugha iliyotajwa na mtafiti ilikuwa faafu. Ilibainika kuwa wafanyabiashara walitumia mikakati hiyo katika kujifunza na kutumia lugha katika shughuli zao za kibiashara. Hivyo kwa kuwa mikakati mingine inahitaji kusoma na kuandika, muda wao wa kusoma na kuandika ni mchache mno kwa ajili ya shughuli walizonazo. La muhimu ni ama kubahatisha baadhi ya maneno ama kutumia Kiswahili kimshutukizo. Wakati wa mahojiano na wasailiwa watatu kutoka Mukwano walikiri kwamba mkakati huu wa kufidia uliwasaidia sana kuhifadhi akilini mwao baadhi ya misamiati ambayo waliitumia katika kufanikisha biashara zao.

#### **4.2.1.10 Mkakati wa Utambuzi**

Wasailiwa walikiri kutumia mkakati wa utambuzi kwa muda mrefu kuliko mikakati mingine. Kutokana na hojaji walikuwa (06/103) idadi inayowakilisha asilimia tano (05%). Wasailiwa hawa walikiri kuwa na ujuzi mdogo wa ujifunzaji wa Kiswahili. Hata hivyo, waliweza kujifunza Kiswahili kama lugha ya biashara kwa kutumia makakati huu.

Mjadala kati ya mtafiti na wahojiwa 9 ambao walipendelea mkakati wa utambuzi, waliutumia

sana katika kujifunza Kiswahili kibashara. Walisema kwamba alimradi mtu ana uwezo wa kusoma basi inakuwa rahisi kujifundisha Kiswahili mwenyewe hasa kupatia misamiati inayohusu biashara. Kutokana na mahojiano,

**M.S 090 alisema,**

*Chairman wa KACITA yalileta mwalimu wa swaili. Ailifundishanga sisi luswaili. In my former school too we started abit of swaili. It was abit tough manya these things of ngeli we didn't understand .I pulled out. But here we have these small books "Akatabo akayigiriza olulimi oluswayiri' it really helps us traders. It has some basic words that have been translated from Luganda to swaili.*

Mwenyekiti wa KACITA alileta mwalimu wa Kiswahili. Alinitufundisha Kiswahili. Katika shule yangu ya awali tulisoma Kiswahili kidogo .Ilikuwa vigumu haya mambo ya ngeli hatukuelewa .Nilijitoa. Lakini tuko hapa na hivi vitabu vidogo 'Akatabo akayigiriza olulimi oluswayiri' vinatusaidia sisi wafanya biashara. Viko na maneno rahisi ambayo yametafsiriwa kutoka Luganda hadi Kiswahili (TY)

Katika mahojiano hoja zaidi zilijitokeza kama inavyojitokeza katika Msailiwa 120:

*Watembeyi wanapitisa apa bitabu ya Swahili/Luganda. Sisi tumepata hiyo bitabu. Ipo maneno mingi yasaidia sisi kusoma luswaili apa kikuubo. Mimi nasema na wasubuzi swaili ile yetu ya apa Uganda alafu wao nasema na mimi ile ya Kenya na Kongo. Okyitegeela!*

Wachuuzi wanaouza vitabu hupitisha hapa vitabu vya Kiswahili/Luganda. Baadhi yetu tumenunue vitabu hivyo. Yapo maneno mengi yanayotusaidia kusoma Kiswahili hapa Kikuubo. Mimi ninaongea na wanunuzi kile Kiswahili cha kwetu hapa Uganda halafu wao wanasema na mimi kile cha Kenya na Kongo. Unaelewa!(TY).

Kauli za wahojiwa hawa zinaingiliana na mapendeleko ya Oxford (1990) na Cohen (1998) wanaofafanua kwamba ni vyema kumpa mjifunzaji L2 uhuru wa kuchagua vifaa ambavyo vinaweza kumwezesha kujifunza lugha hiyo. Licha ya Hajimia na wenzake (2020) kupendelekeza mkakati huu kutumika katika mfumo rasmi wa ujifunzaji L2 kwa mfumo wa mkabala wa utambuzi. Brown (1994), Ellis (1994), Larsen-Freeman na Long, (1991) wametetea kwamba mwanafunzi ana uhuru wa kuhamisha ujuzi alionao kutoka L1 ama popote pale na akautumia katika kujifunza L2. Krashen (1987), Gardener (2010a), Galloway na Labarca (1991), Ellis (1994); Oxford na Cohen (1992); Chamot (1987); Oxford (1990), wanaeleza kwamba ujifunzaji lugha kwa kutumia mkakati wa utambuzi unaweza kutokea pale ambapo mwanafunzi amejipanga mwenyewe kwa kupata motisha na ari ya kujifunza na namna anavyofutilia ujifunzaji wake wa kupata msamiati, virai na elementi zingine bila

kufungwa na masharti ya ujifunzaji L2.

Mara nyingi wanafunzi ambao wanatumia mkakati wa utambuzi huwa angalau wamepitia mfumo wa elimu na wana tajriba ya kutumia akili yao kujifunza L2. Hajimia na wenzake (2020) wanasema kwamba wanafunzi wanaotumia mkakati wa utambuzi hutumia uelewa walio nao kutoka L1 ama matini tofauti tofauti kujifunza L2. Wanafunzi hawa huwa na mbinu za kuwafanya wao wenyewe wakadirie ni wakati gani watajifunza lugha na nyenzo zipi zitumike wakati wa kujifunza. Kupitia mahojiano wasailiwa walisema kwamba ili ujifunze lugha yoyote ile unastahili kuijandaa na kuandaa yale ambayo unataka kujifunza. Kwa jumla matokeo ya hojaji na dodoso yanaonyesha kwamba wafanyabiashara kumi na tano (15/260) walikuwa na uwezo wa kuijandalia nyenzo ambazo zingefanikisha ujifunzaji wa Kiswahili kama lugha ya biashara. Waliweza kutumia nyenzo kutoka lugha lengwa ama kutuma ujuzi wa ujifunzaji kutokana na maarifa waliyonayo kujifunza lugha ya pili. Chamort (2005), Oxford (2003) na Gardener na Cohen (1996) wanasema kwamba nyenzo zinazotumiwa huenda zisiwe katika mazingira maalumu ya kujifunza ila mazingira ambayo mwanafunzi amejiandalia kujifunza. Wafanyabiashara huwa na muda wa kutafuta nyenzo za kujifunzia Kiswahili. Ujifunzaji wao unatokea palepale ambapo wanaendeleza biashara zao jijini Kampala.

#### **4.2.1.11 Urejeshaji**

Mkakati wa urejeshaji hutumika pale ambapo mjifunzaji lugha anakuwa na muda wa kurejelea mambo ambayo aliyasikia kwenye mazingira yake ama wakati fulani alipokuwa anatagusana na wazungumzaji wa lugha lengwa. Matokeo ya hojaji yalionyesha kwamba mfanyabiashara mmoja (01/103) ndiye aliyekubali kwamba mkakati wa upatikanaji tena ulimsaidia kujifunza Kiswahili kama L2. Waliokubaliana naye kutokana na mahojiano walitanabahi kwamba mikakati yote ya ujifunzaji L2 ilikuwa mizuri. Hata hivyo, Walisema kwamba ili mtu kuweza kutumia na kuhifadhi lugha lengwa ni muhimu awe anafanya mazoezi ili kujizoesha na lugha anayojifunza. Walisema kwamba usipofanya mazoezi katika lugha ambayo umejifunza ukubwani utaisahau kwa haraka pia. Hivyo urejeshaji ni namna ya kurejelea kumbukumbu kwa yale uliyowahi ama kusoma au kusikia kutoka kwa wasemaji L.2 na kuyafanya mazoezi ili kukuza ufasaha wa lugha hiyo.

Mazoezi hayo yaliwafanya kuwa na uendelezaji wa matumizi ya lugha ya Kiswahili kibiashara na kuonekana kana kwamba walikijua Kiswahili. Walisema kwamba mkakati huu

ulifanya lafudhi yao katika kutamka maneno ya Kiswahili kuboreshwa. Krashen (1987) anasema kwamba mwanafunzi ambaye anajifunza L2 hujaribu kwa kufanya mazoezi kufahamiana na kanuni za lugha anayojifunza, kwa kujifanyia mazoezi ama kupata mtu ambaye anaweza kumuelekeza. Aidha, Vigotsky (1978), Gardener (2000: 2010b) nao wanaeleza kwamba mwanafunzi hahitaji mfumo halisi wa ujifunzaji wa L2 ila anaweza kujifanyia hivyo katika mazingira asilia kwa kusukumwa na motisha ya ujifunzaji L2. Msisitizo wa kisaikolojia kuhusiana na wazo hili umetolewa na Krashen (1976, 1982, 1987), Dornyei (1994b), Gardener (2000) na Rock (2012), wanaofafanua kwamba mazoezi hufanya mwanafunzi anayejifunza lugha kupata ukakamavu na kujiamini wakati anavyoongea lugha ambayo amejifunza. Swala la mazoezi halikuwekwa bayana na wanasaikolojia ila wasailiwa wa utafiti huu waliangalia hali ya mazoezi kama njia ya kufahamiana na msamiati wa lugha ya Kiswahili katika kufanikisha biashara. Katika mazungumzo yao walijaribu kurejelea msamiati na virai ambavyo vimetumika katika hali ya uradidi.

#### **4.2.2 Mitindo iliyotumiwa na wafanyabiashara kujifunza Kiswahili**

Wasailiwa wote hawakujua kwamba kulikuwa na mitindo ambayo walikuwa wakitumia kujifunza Kiswahili kama lugha ya biashara. Baada ya kutajiwa mitindo ya ujifunzaji lugha ya pili na mtafiti, walitaja na kufafanua mitindo ambayo waliyofikiri walitumia kujifunza Kiswahili kibiashara. Mitindo waliyotaja imeonyeshwa katika jedwali 4.2. Mitindo kulingana na Gardener 2000, Williams na Burdens (1997), Dornyei (1994b), Cohen(1998) Keefe (1979) ni hali ya kisaikolojia ambayo mjifunzaji lugha hupata msukumo wa ndani kwa ndani na ari ya ujifunzaji wa L2. Ili kupata data iliyokusudiwa, ilikuwa bayana watafiti kuwatajia wasailiwa mitindo ambayo ilitumiwa kujifunza L2 ili iwe rahisi kwao kutambua mitindo ambayo walitumia kujifunza Kiswahili kama lugha ya biashara. Mwelekeo huu ultokana na ufafanuzi wa Gardener (2010) na Cohen (1996) wanaosema kwamba wanafunzi wengi ambao hujifunza L2 hujikuta wamepata umilisi wa L2 bila kutambua kwamba kulikuwa na mitindo ambayo iliwawezesha kujifunza lugha hiyo. Baada ya kutajiwa baadhi ya mitindo ya ujifunzaji L2 kutokana na hojaji na usaili walikiri kwamba walikuwa wakitumia mitindo ya ujifunzaji L2 wakati wa kujifunza Kiswahili kama lugha ya biashara. Mitindo mbalimbali ambayo walikubali kuitumia kujifunza Kiswahili ni kama inavyojadiliwa katika jedwali (4.4).

**Jedwali 4.4: Mitindo iliyokuwa ikitumiwa na wafanyabiashara kujifunza Kiswahili kama lugha ya biashara kutoka kwa hojaji**

SN	Mtindo	Mukwano	Simlaw Int.	Kikuubo	Jumla	%
1.	Mwingiliano	04	05	04	13	13
2.	Dukuduku	02	--	--	02	02
3.	Kusikiza	06	07	07	20	19
4.	Ujifunzaji asilia	--	06	04	10	09
5.	Mwelekeo	09	07	06	22	21
6.	Hamasa	06	05	05	16	16
7.	Kuashira	03	03	03	09	09
8.	Hulka za mzungumzaji	02	05	04	11	11
<b>Jumla</b>		<b>32</b>	<b>38</b>	<b>33</b>	<b>103</b>	<b>100%</b>

Asili: *Data kutokana na dodoso. Februari, 2022*

#### **4.2.2.1 Mwingiliano**

Nadharia ya elimu ya Gardener inashikilia kwamba mwingiliano ni kipengele muhimu katika ujifunzaji wa L2. Mtindo huu ulibainika kuwa katika msamiati wa mbele katika ujifunzaji Kiswahili kwa ajili ya biashara. Watafitiwa walioupendelea walikuwa wanne (04/32) kutoka ekedi, watano (05/38) kutoka ekedi ya Simlaw International na wanne (04/33) kutoka soko la Mukwano. Kulingana na data zilizopatikana kutokana na hojaji jumla ya watafitiwa kumi na watatu (13/103), asilimia kumi na tatu (13%) waliupendelea mtindo huu. Matokeo haya yanathibitisha mawazo ya kina Ehram na Oxford (1990) katika utafiti wao wakati wa kushughulikia mitindo ya ujifunzaji L2 kuhusu wanafunzi ambao walikuwa Waingereza na walikuwa wanajifunza lugha zingine za Kigeni. Walipendekeza kiwango cha juu cha kujumuika. Kwamba katika hiki kiwango mwanafunzi hifuata kile anataka na hupenda kujumuika na wengine katika shughuli za mazungumzo, mahali wanaweza kuzungumza wakasikika bila kujali makosa ya kisarufi. Huwa wako sawa hata kama hawana ujumbe wa kutosha na hupenda kukisia yale yanayozungumzwa na wengine.

Matokeo ya utafiti kutokana na mahojiano ya wasailiwa 27 yalionyesha kwamba wasailiwa walijumuika sana na wasemao lugha ya Kiswahili. Maeneo yote matatu kupitia mahojiano yalionyesha kwamba mwingiliano ni sehemu kubwa ya mitindo ambayo ilifanikisha ujifunzaji wa Kiswahili kama lugha ya biashara. Wasailiwa wafanyabiashara walikiri kwamba kuingiliana na watu waliokuwa wakiongea Kiswahili kuliwashinikiza kujifunza Kiswahili. Katika soko la Kikuubo ambapo utafiti ulisaili wasailiwa 13 walikiri kwamba mtagusano wao na wanunuzi waliokifahamu Kiswahili kuliwasaidia kujifunza Kiswahili. Kwa hiyo, katika sehemu tatu zote wasailiwa walionyesha kwamba mwingiliano

ndiyo ulikuwa mtindo mkuu ambao uliwawezesha kujifunza Kiswahili kibiashara.

### **M.S 060 alisema kwamba**

*Sisi tunazaliwa Masaka Lwera lakini wakati wa vita vya Amin wakombozi walikuwa wanajificha kwa baba yangu halafu walikuwa wanatumia Kiswahili neno ambao nilikuwa nakumbuka ni nje iko safi? Sikujua wanamaanisha nini lakini baadaye nilimuuliza baba akasema walikuwa wanauliza kama huko nje hakuna adui ili watoke nje kidogo.*

Kwa mujibu wa (Richard na Eunice 1985, Gardener, 2010, na Wittrok, 1977) wanafunzi wanaweza kujifunza L2 kwa urahisi kwa kuingiliana na ama wanafunzi wenzao wanaozungumza lugha hiyo ama jamii ambayo inayo umilisi wa kuzungumza lugha lengwa. Japo Nicholson (2013) na Williams na Burden (1997) wamesisitiza kwamba hili hutokea kama mwanafunzi mwenyewe ameweka juhudu katika kujifunza. Hilo lisipokuwepo hata pawepo na mtagusano kiasi gani bila nia (Gardener, 2000) ya kujifunza itakuwa vigumu mwanafunzi kujifunza L2. Baadhi ya wasailiwa walisema kwamba walijifunza Kiswahili cha Kenya na Congo ila cha Tanzania kilikuwa kigumu sana namna. Msailiwa 122 alikuwa na ya kusema kuhusu ‘viswahili’ tofauti .

*Luno oluswaili lulimu ebbika nebbika, abakongoli bwogera bifanana Lingala, abbo abbava ekenya oluswaili labbwe lwangu lwangu ebimu obotegeera mangu. Mh naye batanzania baanange olwabwe luzibbu nyoonyo. Kati ffe tugeenda nekyitwanguira.*

Kuna viswahili tofauti tofauti, wakongo wanaonhea ambacho kinafanana na kilingala, wanaotoka Kenya Kiswahili chao ni rahisi mambo mengine yanaeleweka haraka. Mh lakini Watanzania jamani Kiswahili chao kigumu sana sana. Sisi huendana na kile kilicho rahisi kwetu (TY).

Kwao hawakuwa na uwezo wa kutambua na kutafautisha Kiswahili sanifu na cha kuzungumza pamoja na sheng ambayo ilitumiwa na baadhi ya wanunuvi. Walisema mradi walipata wanunuvi wa bidhaa zao. Swala la usanifu wa lugha halikuwa muhimu kwao. Kiango (2002) katika makala yake kuhusu nafasi ya Kiswahili katika ujenzi mpya wa Afrika Mashariki amejadili viwango tofauti tofauti vya mwingiliano. Mmojawapo ukiwa ni mwingiliano unaotokana na mkusanyiko wa watu kutoka kwa tamaduni tofauti tofauti wakiwa na lugha moja ya kuwaunganisha. Hoja hii imesisitizwa pia na (Gardener, 2010; Brown, 2000), walioeleza kuwa mjifunzaji wa L2 anaweza kujifunza kwa kawaida tu kulingana na watu anaoingiliana nao na siyo lazima kulazimishwa kutumia lugha sanifu almradi anaweza kuwasilisha ujumbe anaonua kuwasilisha katika lugha tumizi.

#### **4.2.2.2 Dukuduku**

Dukuduku ni hali ya kuhofia kwingi ama kuwa na wasiwasi kuhusu swala fulani. Mchakato wa ujifunzaji L2 huhusisha mambo mengi mkiwemo kupata maarifa, ujumbe, mwelekeo uwezo na stadi za lugha anazoweza kupata mjifunzaji lugha. Hata hivyo wakati mwanafunzi anapopitia mchakato huu mara nyingi huathirika kisaikolojia (Witrock, 1977; Tobias, 1983; MacIntyre, 1995) na kiwango cha dukuduku.

Kulingana na matokeo ya hojaji, ilibainika kwamba wasailiya wawili (02/32) ndiyo waliouelewa mtindo wa dukuduku kama hali ya kisaikolojia ambayo inayomwezesha mjifunzaji kufanikisha ujifunzaji wake wa lugha. M.S 011 katika kutoa majibu katika hojaji ili kujibu mtindo mionganini ya aliyotajiwaa ambayo ilimsaidia kujifunza Kiswahili kwa ajili ya biashara, aliishia kuweka alama ya kukubali katika dukuduku kwenye kijisanduku na kuacha mengine ambayo yalikuwa yameorodheshwa. Kutokana na mapitio ya maandishi, Brown (2020) amependekeza aina tatu za dukuduku ambazo huibuka wakati wa kujifunza L2.; namna ya kuwasiliana pale ambapo mjifunzaji lugha anashindwa kujieleza ama kutoa hoja katika mazingira ya kawaada, uoga wa kutathminiwa na jamii inayozungumza lugha lengwa wakati wanapotaka wakubalike na jamii ya lugha lengwa, uoga wa kujifunza katika mazingira rasmi. MacIntyre (1995) anasema kuwa ujifunzaji wa L2 ni mchakato unaohusisha akili ambapo ushirikishwaji wa dukuduku huwa mstari wa mbele katika kufanikisha ujifunzaji wa lugha lengwa.

Kulingana na Gardener (1991), MacIntyre na Gardener (1991) wanasema kwamba kinachopelekea mwanafunzi kuwa na dukuduku ni hali ya kuwa na uoga, kutojamini, wasiwasi wa kujistahi, na mwanafunzi kumudu mawasiliano. Jambo ambalo MacIntyre na Gardener (1991) wanasema kuwa watafiti hawajapata fasili moja ya kuelezea haya mambo yote kutumia dhana moja kuonyesha hali ya dukuduku na jinsi inavyojitokeza mionganini mwa wajifunzaji lugha.

Wakati wa mahojiano kati ya mtafiti na watafitiwa 08, utafiti huu ulibani walikiri kwamba dukuduku hasa yajuu ndiyo iliyowasaidia kujifunza Kiswahili kama lugha ya biashara namna mfanyakishwaji (M.S 028) alivyoeleza kuwa;

*obba oliao entunusi ne zikukuba nti obba byengeenda okogeera bituufu, obba  
si bituufu, obba bajjakunseklera. Olulimi booba tolumanyi obeeramu  
okutya...*

Unakuwa hapo hivyo halafu moyo unakudunda, yaani sijui ninachoenda

kuongea kikiwa sahihi ama si sahihi, ama watanichekelea. Lughu ambayo hujui ama ambayo huna umilsi wa kutoksha hukuogopesha kuongea....(TY)

Hivyo mjifunzaji L2 akiwa na dukuduku ya juu huwa kuna uwezekano wa kujifunza kwa urahisi lakini akikumbwa na dukuduku ya chini huenda kujifunza kusitokee. Hata hivyo Felder na Henriques (1995), Fathman (1975), Gardener (2000) na Ellis (2008) wanasema kwamba dukuduku haistahili kuchukuliwa katika mwelekeo hasi ambapo wanaamini kwamba hili litamuwezesha mwanafunzi kujifunza L2. Wanapendekeza kwamba mjifunzaji L2 anastahili kupuuza dhana kwamba atatathminiwa na wanaozungumza lugha lengwa. Mjifunzaji huyu anastahili kutambua kuwa muhimu zaidi ya udhaifu alionao ni ujumbe ama hoja anazowasilisha kueleweka wala sio kujali jinsi atakavyowasilisha ujumbe. Katika kufanya hivi atakuwa anajifunza lugha iliyopo kwenye mazingira yake. Hali hii ya kutojali endapo kuna usahihishaji wa makosa umewashadidia wafanyabiashara kujikuta wanajifunza L.2 popote walipo. Wao hushiriki katika mazungumzo almaradi yatawasaidia kupata wateja. Kwao sio usanifu wa lugha na hata mara nyingi huenda wasitambue sheria za lugha lengwa. Kile wanacholenga ni jinsi ya kuwasiliana na wateja wao, kuuza bidhaa zao na upataji wa faida. Ufanisi wa haya yote ni motisha ya kujifunza lugha husika na kuendelea na biashara yake siku nyingine.

#### **4.2.2.3 Kusikiliza**

Kusikiliza ni uwezo anaokuwa nao mtu unaomuwezesha kupokea ujumbe kutoka kwa msemaji kuuelewa na kuweza kufasiriwa akilini mwake. Ni kutokana na ujumbe uliofasiriwa ambapo msikilizaji anaweza kuongea kwa ufasaha na kwa njia inayoelewaka. Matokeo ya utafiti yaliyotokana na hojaji yalonyesha kwamba wafanyabiashara sita (06/32) kutoka Ekedi ya Mukwano, saba (07/38) kutoka Ekedi ya Simlaw International Limited na saba (07/33) kutoka soko la Kikuubo, hivyo jumla ya wasailiya ishirini (20/103) amba waliwakilisha asilimia kumi na tisa (19%) walisema kwamba walipata baadhi ya msamiati kutokana na namna walivyokuwa wakisikia kutoka kwa wasemaji ama nyimbo za Kiswahili. Walisema kwamba wale amba wanauzu bidhaa kama simu, diskii mweko, kadi sakimia na kadiwia walikua wakiimbisha muziki wa Kiswahili katika maeneo yaliyotajwa ya kufanya biashara. Msailiwa 044 alisema kwamba yeche aliwa akisikiliza muziki wa Bongo na Genge na kufuatilia tamthiliya za Kiswahili kwenye televisheni.

Krashen (1978) anasema kwamba katika hatua ya kwanza katika ujifunzaji lugha huwa msikilizaji anamakinika kusikiliza ujumbe wowote unaotokana na L.2. Msamiati amba anaupata wakati huo ndio unaomwezesha kuanza kuongea maneno katika lugha lengwa.

Binadamu ana uwezo wa kusikia na kusikiliza kile ambacho nafsi yake imemkubalia kusikia. Hakuna namna mtu anaweza kumchagulia mtu nini cha kusikiliza kiwe kibaya au kizuri. Krashen (1987) anasema kwamba katika hatua ya kwanza ya ujifunzaji lugha, mjifunzaji katika kipindi cha ukimya huruhusu nafsi yake kuingiza ubongoni anachotaka. Ari na jitihada humsukuma kusikiliza kile ambacho kinampa motisha (Gardener, 2000). Katika hatua hii mjifunzaji lugha huwa anasikiliza kile kinachoimbwa, kuzungumzwa kutokana na lugha lengwa. Yale ambayo huwa anayasikia huyatumia baadaye katika maongezi. Matokeo ya usaili wa ana kwa ana yalibainisha wasailiwa 31 waliopendelea sana mtindo wa kusikiliza. Idadi hii ilikubalika sana na wafanyabiashara jijini Kampala. Takriban wasailiwa 51 walipenda sana kusikiliza nyimbo, muziki, filamu mbalimbali za Kiswahili na maongezi ya Kiswahili kutoka kwa wazungumzao Kiswahili.

### **M.S 051 alisema kwamba**

*Mimi nasikiliza maneno toka youtube .Hata naweza sabua moja mbili tatu namna iyo. Iko pia kusalimiya namna abari, wewe iko..Pia iko nyimbo ya chameleon jamila analia bwana yake amemuacha, halafu anapenda bitu ya pei kali.Iko nyimbo mingi sana.*

### **M.S 068 alisema**

kwamba nafundisha luswahili na ii nyimbo yajambo,jambo bwana abari gani muzuri sana. Halafu na ii ya chameleon valuvalu,vumilia , acha kulia shida za duni yote iko katika youtube. Si unaona hapa tunapatikana na biashara ngumu sana (TY).

Kauli ya msailiwa 051 na 068 ni ithibati kwamba kwa kupitia kusikiliza fasihi, maneno mbalimbali kutoka vifaa mbalimbali vya kusikiza kumewafanya wajifunze Kiswahili. Katika kauli zao wamejitahidi sana kushiriki kwa kutumia Kiswahili licha ya kuwepo makosa ya kitahajia. Utafiti huu haukuwa na dhamira yoyote ya kukosoa makosa yaliyoibuka kutoka kwa wasailiwa ila ilikuwa namna mitindo tumikizi ya ujifunzaji L.2 ilivyowasaidia kujifunza Kiswahili kama lugha ya biashara. Krashen (1978), na Vygotsky (1978), Ehraman na Oxford (1990), Gold na Rimmer (2000), Gardener (2000, 2010a) wanasema kuwa makosa ambayo huibuka wakati wa kujifunza L.2 ni sehemu moja ya hatua za ujifunzaji L.2. Hivyo mjifunzaji hastahili kukosolewa kwani baada ya muda fulani akimudu lugha hiyo makosa nayo hupungua. Dhana ya kusikiliza katika taaluma ya ujifunzaji ni pana na inategemea unaskiliza nini. Wataalamu kama Vygotsky (1978) na Gardener (2010a) wanakubaliana na Krashen (1987) kwamba kabla mwanafunzi wa L2 kuanza kusema hiyo lugha lazima awe amesikia kutoka kwa wanayoisema. Hiki ni kipindi ambacho kimerejelewa kama kipindi cha

unyamavu. Krashen, 1987 na Gass 2022, wanasema wakati huu mwanafunzi anapata msamiati, anahifadhi halafu anatafakari juu ya matumizi yake na wapi atautumia. Msamiati ambao ulifikirika kwa ajili ya utafiti huu ni msamiati wa Kiswahili ambao ulifanikisha kupata msamiati wa kibiashara.

#### **4.2.2.4 Mtindo wa Ujifunzaji asilia**

Ujifunzaji asilia ni pale ambapo mjifunzaji lugha anatumia fursa ya mazingira asilia kujifunza L2. Huwa hakuna muda, wakati na mkazo wowote unaowekewa katika ujifunzaji. Ujifunzaji huu hudhihirika tu pale ambapo mjifunzaji L2 anashtukia amepata umilisi wa lugha hiyo kutokana na shughuli na lugha inayotumiwa katika mazingira alimo. Kutokana na hojaji, wasailiwa sita (06/38) kutoka Simlaw International na wanne (04/33) kutoka Kikuubo walikiri kwamba walijifunza Kiswahili kutokana na kujizoesha kwao na ye yote aliye kuwa akitumia lugha ya Kiswahili. Takwimu hii ni asilimia (10/103) waliowakilisha asilimia tisa (09%) ya jumla ya wasiliwa 103 (10/103). Aidha, inaaminika kwamba mtindo wa ujifunzaji asilia unaweza kutokea ama kama mtindo au mkakati hasa pale ambapo kuna kuzoeana na wazungumzaji wa L.2 ama lugha ambayo hutumiwa katika sehemu za shughuli za mjifunzaji. Kinacholeta tofauti ni mazingira ambamo dhana inadhahirika. Katika utafiti wetu ujifunzaji asilia ulijitokeza kama mtindo kwa sababu huwa ni ari na jitihada aliyonayo mjifunzaji kujifunza L.2 (Gardener, 2000). Kuna uwezekano mjifunzaji asijifunze L.2 hata kama yuko katika mazingira asilia ya wazungumzaji wa hiyo lugha. Kulingana na Oxford (2009) ujifunzaji asilia unatokana na mazingira asilia na hudhihirika kama mkakati wa ujifunzaji lugha yapili. Hata hivyo, Ellis (2008) Cook (1994), na Gardner (2000) wamesisitiza kuwa ujifunzaji asilia hutokea kama mtindo hasa pale ambapo mjifunzaji anajishughulisha mwenyewe katika ujifunzaji fiche bila kuonyesha kwamba anajifunza kutokana na hali asilia aliyomo ya ujifunzaji.

Hivyo wale ambao wanatumia mazingira asilia ya darasa kulingana na (Elis, 2008; Cook, 1993; na Gardner, 2000) huwa ni mkakati ila katika mazingira yasiyo rasmi basi huwa ni mtindo. Waliendelea kufafanua kwamba ujifunzaji rasmi unaoweza kujitokeza kwa mfano (tukitumia mazingira ya Kampala) kati ya wanunuzi na wauzaji. Ujifunzaji unahushisha kujifunza kutoka katika jamii inayozungumza lugha tumizi, kushauriana kuititia majibzano ya kibiashara na walengwa wa lugha hiyo. Kujaribu kuwasiliana na walengwa ili mjifunzaji aonyeshe kwamba anafaa katika jamii anamojifunzia lugha.

Kutokana na mahojiano, kati ya mtafiti na wasailiya 32, wanajadili kwamba wao wamenufaika sana na mfumuko wa wanunuzi kutoka nchi jirani ambao siku hizi wamekuwa sehemu ya uendelezaji biashara jijini Kampala. Wengi kutoka Kenya, Tanzania na Kongo huja hata kipindi cha siku kuu kununua bidhaa nyingi mno. Kipindi hiki huwa ni kizuri sana katika kuchangamkia maongezi katika Kiswahili. Aidha, kuna wale ambao ni wazawa wa Kenya lakini wanaendeleza biashara zao Kampala. Hivyo mara nyingi hutumia Kiswahili wakichanganya na Luganda. Hii imekuwa fursa ya wafanyabiashara ambao ni wazawa wa Uganda kujifunza Kiswahili kibiashara katika mazingira asilia ya kufanya biashara.

### **M.S 099 alisema.**

*Walio akaseera nga basubuuzi bangi nyooo. Atte bwe batuka bakozeesa luswaili. Ababiluddemu batabulamu luganda luffu. Naye fenna twetegeera. Ekyiraara walio banakenya kati bafuuka banayuganda. Olwo bwaba nga yakaja ayogera nyo oluswaili bwa ggatamu oluganda. Kati nafee tubaigirko. Tuiga oluswaili lwabwe nga nabbo bwe baiga oluganda.*

Kuna wakati wanunuzi huwa wengi sana. Tena wakifika hutumia Kiswahili. Kwa wale wamefanya biashara kwa muda mrefu huchanganya Kiganda kibovu. Hata hivyo huwa tuna elewana. Kwingineko kuna wakenya ambao sasa walishakuwa wanauganda. Kipindi akiwa ndiyo amefika hutumia sana Kiswahili huku akichanganya Luganda. Nasi twajifunza kutoka kwao. Twajifunza Kiswahili chao na wao wanajifunza Luganda (TY)

Ufanuzi wa wasailiya kutoka nyanjani umejikita katika hatua ya nne ya mhimili wa kwanza wa ujifunzaji wa Krashen (1978) kwamba mjifunzaji wa L2 katika hiki kiwango huongea bila uoga. Mjifunzaji hutumia fursa yoyote ile kujifunza kutokana na chochote kinachozungumzwa kutokana na lugha lengwa. Kulingana na ari na jitihada alizonazo kuhusu ujifunzaji wa L.2 motisha ya ndani huonyesha kwamba naye anaweza kuwasiliana katika lugha lengwa. Mfano wa nukuu ifuatayo ni ithibati kwamba kuna baadhi wameanza kufahamu Kiswahili ila husubiri wakati mwafaka (mazingira) ya matumizi yake.

### **M.S 083 alisema**

*Olooza luswaili tetulimanyi. Tusilikila muli naye banakenya bwebajja tuluingizaa. Boogera nga tubaadamu. Kati wanno ozze nga oyogera Luganda. Singa weffude nti tomansi luganda nandikugambye sister wewe nataka nguwo gani. Omanyi bakongo bagula nyoo engaoye zino mpya bwebatuletela ebitengye okutunda enno ewaffe.*

Wafikiri hatujui Kiswahili. Tunanyamaza tu lakini Wakenya wakija tunakiingiza. Wanaongea huku twawajibu. Hapa umeongea Luganda. Ungejifanya eti hujui Luganda ningekeuuliza dada wataka nguo gani. Wajua Wakongo hununua nguo hizi mpya huku wakileta vitenge vyao kuuza huku kwetu (TY).

Hoja ya mfanyabiashara 099 na 083 walionyesha namna hawakuona ugumu wa kujifunza Kiswahili kama lugha ya biashara. Katika hali ya kuendeleza biashara zao mumo humo ndimo wamepata fursa ya kujifunza Kiswahili. Mazingira wanayofanyia kazi hasa wale wa Simlaw International kuna wafanyabiashara wengi ambao hutumia Kiswahili. Hali hii inafanya ujifunzaji kwa wanaojifunza kurahisishwa.

#### **4.2.2.5 Mtindo wa Mwelekeo**

Utafiti uligundua kwamba mwelekeo ulichangia katika ujifunzaji Kiswahili mionganoni mwa wafanyabiashara. Mtindo huu ulijitokeza katika kuelezea namna baadhi ya wasailiwa walikuwa wakijibu hojaji na dodoso. Mionganoni mwa wafanyabiashara waliojaza hojaji, Wasailiwa tisa (09/32) kutoka Mukwano, saba (07/38) kutoka Simlaw International na sita (06/33) kutoka soko la Kikuubo jumla ya wasailiwa ishirini na mbili (22/103) walikubali kwamba mwelekeo chanya uliwafanya wajifunze Kiswahili kwa haraka. Kwa wale ambao walikuwa na mwelekeo hasi iliwachukulia muda kujifunza Kiswahili. Takwimu hii ni asilimia Ishirini na moja (21%) ya jumla ya wasailiwa walengwa 103 (22/103).

Matokeo ya mahojiano mionganoni mwa wasailiwa 25 yilibaini kwamba kuwepo na mwelekeo chanya kuliwafanya wakubali kutangamana na lugha ya Kiswahili hasa kwa ajili ya biashara. Mtafiti aliwaauliza k u t a m b u a kwa nini wao walishikilia kwamba mwelekeo ndio ulikuwa mtindo mkuu kwo katika ujifunzaji wa Kiswahili kwa ajili ya biashara kama ilivyoelezwa na (MS. 013) kuwa .

#### **MS. 013 alisema ;**

*Olwooza buliomu ayagala luswaili.Tonyumiza tonyumiza bakombozi kyebakola ewaffe mmh.Baatukyaiisa luswaili.Ebigambo ebimuu mbitegeera naye sagala bwagazi kuloogera.*

Wafikiri kila mtu anataka Kiswahili. Usiniambie tena usiniambie. Walichokifanya Wakombozi kwetu mmh... Walifanya tuchukie Kiswahili. Kuna maneno nayaolewa lakini sitaki kuongea (TY)

#### **Naye M.S 034 alisema kwamba;**

*I do like swaili if at one time I get some classes I can improve. I can try a little but am not like these Kenyans and Tanzanians. Its high time we change attitude because we need to trade with people from all East Africa.*

Napenda Kiswahili ikiwa wakati mmoja nitapata mafunzo nitaboresha. Najaribu kidogo kidogo lakini siko kama Wakenya na Watanzania. Ni wakati tubadilishe mwelekeo kwa sababu watastahili kufanya biashara na watu wote kutoka Afrika Mashariki (TY)

Hoja za mfanyabiashara 013 kwa kiasi zinakinzana na za mfanyabiashara 034. Mfanyabiashara 013 zinaonyesha kwamba kuna Kiswahili kidogo anachokifahamu ila kwa sababu ya mwelekeo hasi anabaki na msamiati finyu. Mfanyabiashara 034 anaonyesha kwamba anakipenda Kiswahili, yuko tayari kukisoma. Vile vile kinamsaidia kujifunza Kiswahili kwa ajili ya kuendeleza biashara zake. Wananaadharia wa ujifunzaji L2 kama (Nick, 2008; Gardener, 2010; na Gass, 2022), wamasema kwamba mwelekeo chanya humfanya mtu akawa na maisha mema na kupunguza changamoto ambazo zingeathiri maisha yake. Aidha, wanasema kwamba mweleko chanya hupanua utambuzi amba unakuza fikra za kimwili na kimawazo. Kuwa na mwelekeo chanya kunafanya mtu kuwa na hisia chanya dhidi ya kitu ama shughuli ambayo anastahili kukamilisha. Mwelekeo hasi ni hulka za mtu ambazo mtu mwenyewe anaweza kutambua kama anazo au la. Hali kama hii huathiri utendaji na maendeleo katika jamii. Gardener (2000, 2010b) amefafanua kwamba mwelekeo dhidi ya hali yoyote ile katika mazingira ambamo lugha inafunzwa huwa ni mwelekeo dhidi ya hali ya ujifunzaji. Kulingana na Gardner (2000, 2010a, 2010b) kinachosababisha mwanafunzi kuwa na mwelekeo kuhusu kile anachojifunza, hutokana na motisha na ari aliyonayo mwanafunzi kuhusu ujifunzaji wa lugha lengwa.

Kwa mantiki hii Gardener (2000) amegawa motisha katika sehemu tatu. Hamu ya kutaka kujifunza lugha, mwelekeo dhidi ya ujifunzaji lugha na msukumo wa ujifunzaji lugha. Anaendelea kusema kwamba vipengele vya motisha vinavyomsukuma mwanafunzi kujifunza lugha ni, lengo, hamu ya kufanikisha lengo, mwelekeo na juhudhi mwanafunzi huweka katika ujifunzaji lugha. Japo hakuthibitisha namna vipengele vya awali vinajenga motisha, (Stern, 1983; Cook, 1993; Williams na Burden, 1997 Ellis, 2008) wametetea kwa kueleza kwamba modeli ya Gardener (2000) imekuwa msingi wa kurejelewa hasa pale ambapo amedadavua maswala ya ujifunzaji ambayo utafiti mwingi ulikuwa umeacha nje. Wanasema kwamba tafiti za wananaadharia wengi zilishughulikia tu mikakati na ujifunzaji lugha bila kutambua kwamba hiyo mitindo hujengwa na hisia za mtu ambazo zimejengeka kupitia motisha na mwelekeo wa ujifunzaji wa lugha. Kwa namna ya kukubaliana nao, Gardener (2010a) na Hajimia, Sigh na Chethiyar (2020) wanasema kuwa ufanisi katika ujifunzaji lugha una mashiko katika motisha ambayo ndani mwake imejengwa na vigeugeu kama usuli wa lugha anayojifunza, uwezo wake wa kujifunza na utamaduni wa lugha. Mazingira ambamo mwanafunzi anajifunzia yataamua imani ya mjifunzaji lugha. Namna vigeugeu hivyo vinavoathiri mwelekeo itakuwa msingi mkubwa wa kupata motisha wa ujifunzaji lugha

lengwa. Wakati wa mahojiano wasailiwa walipoulizwa kwa nini walitaja mitindo hiyo na kuacha mingine, walisema kwamba kitambo mtu aamue kufanya jambo huwa kuna kilichomvutia ama kumsukuma kufanya hivyo. Waliendelea kusema kwamba katika mazingira ya Uganda, Kiswahili kilitumika vibaya na hawakupenda kuzungumza Kiswahili ila baadaye walivyobadilisha mwelekeo wakaanza kujifunza baadhi ya maneno namna inavyoelezwa hapa chini;

### **M.S 081**

*Economic situation has really changed .You cannot rely on buyers from one setting or region. We do business in East Africa and beyond. So which language will you communicate with buyers from Kenya or Tanzani. Today we are in the digital era. A customer will give a call and request for the merchandise which you are supposed to load in the bus and rich wherever he/she is. The language you use will not necessarily be Luganda.Some are not good at English.Will you force them to speak Luganda.We need to embrace swaili in order to go forward with business.*

Hali ya kiuchumi kwa kweli imebadilika. Huwezi kutegemea wanunuzi kutoka kwa mazingira mamoja au eneo moja tu. Tunafanya biashara Afrika Mashariki na kwingineko. Kwa hivyo ni lugha gani utawasiliana na wanunuzi kutoka Kenya au Tanzani. Leo tuko kwenye zama za kidijitali. Mteja atakupigia simu na kuagiza bidhaa ambazo unastahili kupakia kwenye basi na kumpata mahali popote alipo. Lugha utakayotumia si lazima iwe Kiganda.Wengine hawana umilisiwa kutosha katika Kiingereza.Utawalazimisha kuzungumza Kiganda. Siku hizi mambo yamebadilika. Tunahitaji kutumia Kiswahili ili tuendelee na biashara (TY).

Mwelekeo huwa na mchango mkubwa sana katika kushawishi hulka za mtu. Hili hutokea sana katika mazingira ya ujifunzaji. Mambo yanayotokea hupelekeea mwanafunzi ama kuwa na mwelekeo chanya au hasi. Mwelekeo chanya na kutokuwa na motisha hukwamisha ujifunzaji wa lugha. Gong, Gao na Lyu (2020a); Li (2021) wanakubaliana na utafiti kwa kusema kwamba mwelekeo unaweza kubadilishwa kutoptana na matukio na mazingira ya ujifunzaji. Hali na matukio ya utafiti huu ilikuwa shughuli za biashara katika jiji la Kampala. Baadhi ya wasailiwa kuititia mahojiano walisema kwamba Kiswahili kiliwasaidia kupata wanunuzi. Hivyo iliwabidi wabadili namna walikuwa wanakichukulia na kuanza kujifunza kwa kupata maneno machache machache.

#### **4.2.2.6 Mtindo wa Hamasa**

Wasailiwa walikiri kwamba hawakutambua kwamba mtu anaweza kujifunza L2 kwa kutumia mitindo ya ujifunzaji lugha. Kwao walifikiri kwamba ujifunzaji lugha ni hiari kwa mtu yeoyote ambaye alitaka kujifunza ama kufundishwa akiwa shulen. Kwamba mtu anaweza pia

kujifunza L2 endapo masilahi yanahitaji afanye hivyo. Hivyo hawakutambua kwamba walikuwa wakitumia mitindo ya ujifunzaji L2 kujifunza Kiswahili kama lugha ya biashara.

Hata baada ya kutambulishiwa baadhi ya mitindo ya ujifunzaji L2, walikiri kwamba waliskumwa na upendo kwa lugha ya Kiswahili ili kujifunza kwa ajili ya biashara. Matokeo ya hojaji yalionyesha kwamba wasailiwa (06/32) kutoka ekedi ya Mukwano, (05/38) kutoka Simlaw International Limited na (05/33) kutoka soko la Kikuubo kutokana na hamu ya kukipenda Kiswahili kulifanya waweke nguvu katika ujifunzaji wa Kiswahili kama lugha ya biashara.

Wasailiwa 13 ambao walihusishwa katika mahojiano walisema kwamba kilichowafanya wajifunze Kiswahili bila wasiwasni kwamba walikipenda. Maoni ya mfanyakibashara mmojawapo;

### **M.S 130 alisema kwamba;**

*Oluswaili ndwagaliira bwerere. Omanyi ntiwalio abalwogeera jooli bali mukuimba?atte ebigaambo sibigumu enyoo ekyili awo. Bwobiuliliza kale oyiga. Kye ekyiluungi kyalo.*

Napenda tu Kiswahili. Wajua kuna wanaokizungumza utadhani wanaimba? Tena maneno si magumu hivyo. Ukisikiza unajifunza. Ndio uzuri wake (TY).

Northwood (2014) anasema kwamba hamasa na motisha wa ujifunzaji wa L2 vinahusishwa na nadharia ya Gadrner (2000) ambaye katika modeli yake ya elimu amefafanua elementi tatu ambazo zaweza kufanikisha ujifunzaji wa L2. Elementi hizi ni hamu ya kujifunza L.2, na mwelekeo chanya kuhusu L.2 ambapo kwa pamoja vinazua dhana za uthamanishi, juhudzi za kila wakati na kuhamasika. Anaendela kusema kwamba hamasa huonyesha hali ya kipekee ambapo inaunganisha shughuli na ufananisho na katika uwili wa hamasa (usawa na utambuzi). Kwingineko dhana hizi zinamaanisha kwamba kujishughulisha na shughuli ambazo zimetokana na hamasa husaidia kujikuza kwa kuhusisha katika utambulishaji uzoefu wa matokeo chanya.

Hoja ya mfanyakibashara 130 inadhihirisha kwamba kujifunza lugha ni kutokana na sifa za mtu na anachokipenda. Wasailiwa walisema kwamba walikipenda tu Kiswahili hivyo polepole walikuwa wakijifunza. Waliendelea kusema kwamba walikichukulia Kiswahili kama lugha ambayo wangeweza kusikiliza ama kusoma kwa muda wao na wanaweza kuzungumza na watu kutoka makabila tofauti tofauti. Cohen (1996), Krashen (1978) na

Gardener (2000, 2010a) wanaeleza kuwa hamasa inadhibiti hisia za mtu ili ashawishike kujifunza L2. Hisia hutokana na ari/nia aliyonayo na jitihada ambazo anaweka katika kujifunza L.2. Hoja ambayo William na Burden (1997), Taksiran (2010), Wittrok (1977)) Brown (2007) walikubaliana nayo kwamba kushawishika pia kunajengeka kwa msingi wa kutaka kujuu manufaa ya lugha wanayojifunza. Hata kama hoja hizi hazikuhusisha lugha yoyote mahsususi, Utafiti wetu ulikubaliana nazo kwani wakati utafiti wetu ulibainika kwamba Kiswahili kilipendwa kama lugha ya kufanikisha biashara jijini Kampala.

#### **4.2.2.7 Kuashiria**

Kuashiria hujitokeza kutegemea na uwezo mahsususi. Kuashiria kunaweza kutokea wakati wa kutaka kuonyesha kitu, kuonyesha umbali wa kitu, kuona na kufasili mazingira kitu kinapopatikana. Ni kutokana na matumizi mapana ya viashiria ndiyo yaliwasaidia kuweka kumbukumbu za baadhi ya msamiati wa Kiswahili kuwasaidia kuitumia kati yao na wanunuzi waliokuwa wakitumia Kiswahili. Wakati wa kuashiria ubongo hujenga dhana na maana ya nini kinachoashiriwa. Kutokana na hojaji wasailiwa (03/32) kutoka ekedi ya Mukwano, (03/38) kutoka Simlaw International Limited na (03/33) kutoka Kikuubo walisema kwamba kwa hali ambayo wangejikuta hawawezi kutaja kitu, waliashiria halafu mnunuzi angelitaja kilichoashiriwa. Katika hali ya kutaja, mfanyabiashara angejitahidi kuhifadhi neno alilotajiwa ili wakati mwagine asitumie ishara. Kwa kutumia mahojiano wasailiwa 21 walionyesha kwamba kuashiria iliwasaidia kuficha staha yake asikose wateja. Kuficha hali ya kwamba hawezi kutamka anachokiiza katika lugha ya mlengwa ambaye ni mzungumzaji wa Kiswahili. Namna ilibainika kutokana na maelezo haya ;

#### **M.S 150**

*Nze ekyigambo kyaluswaili bwe kibula nsoongamu. Olumalla okusongamu aggula ajjakung'amba elinya lyekintu kyayagalaokugulla. Bwentyo naange mba ndimukuiga kyaba ayogedde. Kuba nga bbwotaluiga mukyiibiina, olina okulufuniira wanno ngotuunda ebintu.*

Kwangu neno la Kiswahili likipotea naashiria. Nikisha ashiria mteja ataniambia jina la kitu anachotaka kunua. Hivyo ndivyo nami nakuwa najifunza kutegemea kile ambacho ameongea. kwa sababu usipojifunza darasni basi wastahili Kupata Kiswahili hapa ukiuza vitu (TY).

Lindsay (1999) na Saranray na Meenakshi (2016) wanasema kwamba ujifunzaji wa L2 hufanikishwa na matumizi ya hisi zote za binadamu. Hivyo kwa kutumia ishara ya mikono ama kubadili uso kwa ajili ya kutoa ujumbe fulani ni mojawapo mtindo wa ujifunzaji wa L.2. Hoja hizi zinakubaliana na Oxford (2003) katika makala yake kuhusu mitindo na mikakati ya

ujifunzaji wa L2, ameordhesha vipengele vinne vya kimitindo ambavyo humwezesha mjifunzaji wa L2; Kuona kile kinachofundishwa, kusikia anayoyasoma, kutembea na kuona kile kinachofundishwa na kugusa kile kinachofundishwa. Vile vile utafiti huu unakubaliana na Fleming (2001) katika mapitio ya maandishi pale ambapo alifanya utafiti wake miaka ya themanini kwa kuelekeza mitindo mbalimbali ambayo hufanywa na wajifunza L2. Anaelezea kwamba mjifunza lugha anaweza kutumia viungo vya mwili kwa mfano, mikono yake kugusa kitu, kuandika ama kuchora majedwali yaani chochote kile uwezo wa viungo vya mwili vyaweza kufanya.

#### **4.2.2.8 Mtindo wa Tabia za mjifunzaji**

Matokeo ya hojaji yalionyesha kwamba wasailiwa (02/32) kutoka ekedi ya Mukwano, (05/38) kutoka Simlaw International Limited na (04/33) kutoka soko la Kikuubo walikubali kwamba hulka walizokuwa nazo ndizo zilizowawezesha kujifunza Kiswahili kwa ajili ya biashara. Tabia za mjifunzaji ni kipengele ambacho huenda tafiti nyingi hazikutilia maanani. Pia ni vigumu kutambua kwamba tabia huchangia katika ujifunzaji L2 hadi unapopata maoni kutoka kwa wahusika. Tabia za mjifunzaji lugha huchangiwa sana na mwanafunzi anayejifunza lugha hiyo. Hulka zake zaweza kufanikisha ama kutofanikisha ujifunzaji wa lugha. Ehrman (1996) anafafanua kuwa kuna uhusiano mkubwa sana kati ya tabia za mjifunzaji na ujifunzaji lugha. Tabia ni dhana ya kisaikolojia ambayo imeelezwa na wataalamu kama Krashen (1987) Skehan (1991) Gas na Selinker (1994), Gardener (2000, 2010b) kwamba katika mazingira yoyote yale kinachompelekea mjifunzaji lugha kujifunza L2, ni tabia zake mwenyewe ambazo huathiri vigeugeu vya ujifunzaji lugha. Tabia za mjifunzaji lugha zinamfanya achague namna atakavyojifunza lugha na kwa njia zipi atakavyojifunza lugha hiyo.

Kulingana na Anderson (2002) mojawapo ya tabia ambayo inaathiri ujifunzaji L2 imefafanuliwa kwa njia mbili; wenyewe hulka za kuongea hawapendi kukaa peke yao, hupenda kutagusana na watu, hupenda kufanya mizaha bila kuonyesha kwamba kuna jambo limewakera, na huongeaongea bila mipaka, wanaweza kuthubutu jambo lolote. Wale wanyamavu nao hupenda kuwa peke yao, na hawapendi kutagusana na watu katika jamii waliyomo. Watu kama hawa hupenda kujifanya shughuli zao kwa kujitenga ama sivyo kufanya na kundi dogo sana. Katika kukinzana na maelezo haya utafiti wa awali wa mwana saikolojia Hans (1990) alisema kwamba unyamavu hauhusiani na ujifunzaji wa L2 ila huwa ni kemikali ya kifenomena katika ubongo wa binadamu. Kwa hiyo kwake unyamavu na

asiyekuwa mnyamavu wote wana uwezo wa kujifunza lugha yoyote ile. Hata hivyo wananaadharia wa ujifunzaji wa L2 kama kina Krashen (1985), Gardener (2000), Cook (2001), Swain (1985) na McDonough (1986) wanashikilia msimamo waokwamba wanafunzi wanaozungumza sana hujifunza kwa haraka lugha. Kwamba wanapata kiwango kikubwa cha kuingiza dhana mpya (Krashen, 1987), wanapenda mkakati wa mawasliano (Cook, 2001) na wanapenda kutangamana na jamii wanamojifunzia lugha na kujijengea umilisi wa lugha hiyo.

Kwa kuongezea tafiti nyingi zimeonyesha kwamba hakuna namna ujifunzaji unaweza kukamilika bila kugusia swala la staha. Staha ni tathmini ya mtu binafsi au kufanya uamuzi kutegemea kujiamini alikonako ambapo hujengeka kwa misingi ya mwelekeo. Gardener na Lambert (1972), Gardener (2000), Brown (2007), Amfast na Holmen (2010) wanajadili kuwa kujiamini na kuwa na staha ni athari muhimu katika ujifunzaji wa L2. Mjifunzaji L2 asiposhughulikia nafsi yake na kukazia kujistahi huenda asijifunze kwa mwendo wa wastani. Mjifunzaji kama huyo huchukua muda mrefu kutamka maneno ya lugha lengwa.

Kwa jumla data iliyopatikana kuititia hojaji na mahojiano kuhusu mitindo iliyotumiwa na wafanya biashara kujifunza Kiswahili kibiashara yalionyesha kwamba wasailiwa (40/260) walitumia mtindo wa mwiningiano kujifunza Kiswahili kibiashara, (10/260) dukuduku ndiyo ilipelekea wao kujifunza Kiswahili kibiashara, idadi kubwa sana ya wasailiwa amba ni (51/260) walipendelea sana kusikiza nyimbo, matangazo, na filamu za Kiswahili na hata wanaozungumza Kiswahili ili wao kupata umilisi wa lugha ya Kiswahili. Wasailiwa arubaini na wawili (42/260) walikiri kwamba uzoefu wa mazingira asilia ya ufanyaji shughuli za biashara yaliwasaidia kujifunza Kiswahili kibiashara, aruaini na saba (47/260) walisema kwamba mwelekeo hasi ulikuwa kizuizi cha ujifunzaji Kiswahili kwa sababu za athari za awali. Hata hivyo kubadilisha mweleko kuliwasaidia kujifunza Kiswahili. Wasailiwa ishirini na tisa (29/260) walisema kwamba hamasa ilikuwa msukumo amba ni uliwasaidia kujifunza Kiswahiliki biashara. Kwingineko wasailiwa thelathini (30/260) walikiri kwamba kwa hali ambayo hawakujua jina la bidhaa waliishia kuashiria ili mzungumzaji wa Kiswahili angetaja jina la kitu. Msamati huo ungehifadhiwa kwa matumizi ya baadaye katika kufanikisha biashara na wasailiwa kumi na moja (11/260) walisema kwamba hulka walizokuwa nazo na kujumuika na wasemaji wa Kiswahili na kujaribu kukiiongea kuliwasaidia kujifunza Kiswahili kibiashara.

#### **4.3 Jinsi mikakati na mitindo mbalimbali iliwezesha kujifunza Kiswahili**

Data zilizopatikana zilijibu swali la kwa jinsi gani mikakati na mitindo waliyotaja iliwasaidia katika ujifunzaji wa Kiswahili kibiashara. Data tutakazojadili katika kipengele hiki zilifanikishwa na mhimili wa pili na nne wa Krashen (1978) pamoja na mhimili wa pili na tatu nne wa Gardener (2000). Mbinu zilizofanikisha ukusanyaji data ziliwa hojaji kwa kuhusisha maswali ya kujaza, usaili kwa kuhusisha dodoso yaani mahojiano ya ana kwa ana pamoja na uchunzaji kwa kunasa baadhi ya matumizi ya Kiswahili katika mazingira halisi. Sehemu hii vile vile imegawika katika sehemu mbili; sehemu ya kwanza ni mikakati na sehemu ya pili ni mitindo.

##### **4.3.1 Mikakati iliyowezesha ujifunzaji wa Kiswahili kama lugha ya biashara**

Katika kujibu swali la ni kwa jinsi gani wafanyabiashara walitumia mikakati na mitindo ya ujifunzaji L2 kujifunza Kiswahili kama lugha ya biashara. mtafiti aliwapa wasailiwa uhuru wa kujaza hojaji kudhihirisha namna walivyotumia mikakati kujifunza Kiswahili. Kupitia mahojiano, wasailiwa waliombwa kufafanua jinsi mikakati waliyotaja ilivyowawezesha kujifunza Kiswahili kama lugha ya biashara. Aidha, uchunzaji ulishirikishwa ili kupata data katika mazingira halisi ya mpokezano zamu ya mazungumzo kati ya wanunuvi na wauzaji. Katika jedwali 4.5 mikakati inayowasilishwa ilitokana na hojaji ambazo zilisambazwa katika eneo la Ekedi ya Mukwano, Simlaw International Limited na soko la Kikuubo.

##### **Jedwali 4.5: Namna mikakati iliviyotumiwa na wafanyabiashara kujifunza Kiswahili kibiashara.**

<b>SN</b>	<b>Mikakati</b>	<b>Jumla</b>	<b>Asilimia</b>
1.	Nyimbo/Ukariri	16	15.5
2.	Mwanafunzi kwa mwanafunzi	06	06
3.	Matumizi ya lugha chanzi	14	13.5
4.	Kuongea	10	09
5.	Mawasiliano	20	20
6.	Mitagusano ya ukuruba kati ya wanunuvi na Wauzaji	17	17
7.	Teknolojia	10	09
8.	Mpango binafsi	05	05
9.	Utambuzi	03	03
10.	Upatikanaji tena	02	02
<b>Jumla</b>		<b>103</b>	<b>100</b>

*Asili: Data ya nyanjani kutokana na hojaji, Februari 2022*

##### **4.3.1.1 Nyimbo/Ukariri**

Miongoni mwa wafanyabiashara waliojaza hojaji wasailiwa kumi na sita (16/103) walikiri kwamba walituma nyimbo kujifunza Kiswahili kama lugha ya biashara. Hata hivyo waliofanikiwa kueleza namna nyimbo zilivywawezesha katika ujifunzaji walikuwa sita

(06/16) ikiwa asilimia mbili (2%) ya jumla ya idadi ya wasailiwa 103. Wasailiwa hawa walijaribu kuelezea namna nyimbo walizotaja zilivyowawezesha kujifunza Kiswahili. Walitaja misamiati mbalimbali ambao ultokana na nyimbo ambazo waliskiliza. Misamiati hiyo ni kama; *pesa, chakula, bei, njoo, karibu sana, nikusaidiaje, jambo, fanya na nguvu na kusema*. Ufafanuzi zaidi ultokana na mahojiano kati ya mtafiti namna nyimbo zilichangia katika ujifunzaji wa Kiswahili kama lugha ya biashara. Wasailiwa walisema kwamba, nyimbo nyingi huchezwa katika Ekedo, soko na maduka kwa ajili ya kuuza CD za nyimbo na filamu, za wasanii fulani. Hivyo ni kawaida kusikia pia nyimbo za wasanii waliotumia Kiswahili. Nyimbo zina sifa moja na mkakati wa ukariri kwani kuna urudiajirudiaji wa maneno hivyo kujenga msisitizo fulani.

Licha ya nyimbo nyingi kutumika kama burudani, wafanyabiashara walipata fursa ya kujifunza msamiati ambao uliwasaidia katika kuendeleza biashara zao. Baadhi ya nyimbo ambazo zilitia fora na kusaidia ujifunzaji wa Kiswahili ni zile za Joseph Mayanja ambaye anajulikana kwa brandi ya jina lake kama *Doctor Chamelion*. Mfano wa nyimbo ambazo zilitokana na umaratokezi kupitia hojaji ni pamoja na ***Beyi Kali, Rafiki yangu, Shida za Dunia***, na badilisha.

Kupitia mahojiano ya ana kwa ana na wasailiwa, waliweza kuimba baadhi ya nyimbo na kufafanua misamiati ambayo walipata kutokana na nyimbo hizo namna inavyojitokeza katika nyimbo zifuatazo

#### **Wimbo 1: namna ilivyowasilishwa na :M.S 023,029**

##### **Bei Kali-Jose Chamellion**

Kibwagizo

*Anapenda vitu vya bei kali*

*Kama hajui ati sina mali*

*Ananiomba vitu vya bei kali*

*Nikiwa sina yeye hanijali*

##### **Ubeti 1**

*Kutano la kwanza likua Mombasa*

*Rohoni niliskia nimempata sasa*

*Kumbe hata yeye alininoki pia*

*Jioni tukaenda pamoja out for beer*

*Nilishangaa alianza kuomba whisky*

*Na vinyaji vya bei bila kua tipsy*

*Niliamua twende dance floor tucheze*

*Akakataa ati hapendi nyimbo za lingala.*

## **Ubeti 2**

*Siku nyininge alikuja Kampala  
Tuka "anza kutafuta hoteli ya kulala  
Nikampeleka **hoteli** nje ya Kampala  
Hiyo ndio nilikua naweza lipia  
Tukafikepo akaanza kunicheka  
Nikatafuta **rafiki yangu** anisaidie  
Kwa bahati mbaya ata yeye nilimkosa  
Kibwagizo*

## **Ubeti 3**

*Nilipanga tuende pamoja Kigali  
Tukale hepi kwa sababu nilikua na **mali**  
Akafurahika penzi letu kufika mbali  
Kumbe kuenda Kigali ndio ilikua **hatari**  
Nilimpeleka restaurant akakataa **ugali**  
Ati hawezi kula alikatazwa na daktari  
Nilijifanya mjinga kama simjali  
Kumbe kesho **namtoroka** nimwache Kigali  
Kibwagizo  
Kibwagizo*

***Muape fasi** Kampala-Uganda **Muape fasi**  
**Muape fasi** Daesalaam-Bongo **Muape fasi**  
Kigali –Rwanda ndabakunda  
nimuze tubyine Olobi ndege nini Kongo  
bapewe fasi Nairobi, Mombasa, Kisumu, Kenya yote wape fasi  
Sita sahau Bururundi Bujumbura wote **wape fasi**  
**Amuka basi** umepewa fasi amuka basi x2  
Kampala mulungi nyoo naye ajjudde abateesi  
Kampala muzuri sana naye ajjudde abateesi  
Atooba bakaye, nange nsazeewo nkaaye.....*

*Asili: Data kutokana na mahojiano (Fabruari 2022)*

Katika huu wimbo kuna baadhi ya maneno ambayo yamekolezwa ambayo ni ya kibiashara namengine ya kawaida lakini nayo yanachangia katika matumizi ya Kiswahili. Kwa mfano vitu vya **bei kali, sina mali**, vinyaji, akakataa, kulala, **hoteli, rafiki yangu, mali, hatari, namtorooka, muape fasi, wape fasi** na vyakula kama ugali. Kwa kawaida Uganda ugali/sima/sembe huitwa kaunga ka posho (ugali wa mahindi). Ila katika baadhi za hoteli pale ambapo waliuza vyakula kwa ajili ya wasafiri wafanyabiashara waliweza kutumia maneno ugali na hata pilau. Mumo humo pia kuna vielezi vya wakati kama **kesho** na hata maneno ya tahadhari endapo mtu anataka kukutaperi **nilijifanya mjinga** kama simjali. Kwa wale ambao walijifunza Kiswahili kupitia nyimbo kama za Chameleon waliathirika sana na

namna ya kutamka msamiati ya Kiswahili kama walivyoipokea kutoka kwa wimbo. Kuna udondoshaji wa baadhi ya maneno kama katika (*vinyaji-Vinywaji, nilkua-nilikua, ata-hata fasi-nafasi*) na uchopekaji wa irabu katika neno kama (*muzuri-mzuri*).

Krashen (1978) kwamba kuegemea mhimili wake wa pili yaani nadharia tete ya mfumo halisi na mhimili wa nne halisi nadharia tete ya dhana mpya, ujifunzaji huanza na muundo wa maswali ya neno moja moja: Nini? Wapi? Lini? Nani? nk. Matumizi ya viunganishi kwa mfano: *nakula posho na nyama?* Matumizi ya njeo-wakati uliopo, ujao na uliopita, kama vile *vilijfanya* mjinga matumizi ya vimilikishi kama vile *changu, chako, chake*; Matumizi ya vivumishi kama vile ***muzuri*** na vielezi kama ***kesho***. Kwingineko mjifunzaji anachuja dhana ambazo anastahili kuzitumia katika mazingira husika. (Krashen, 1978 na Cohen ,1996). Kwa kuongezea Gardener (2000, 2010a) anasema kwamba nia ya kutaka kujifunza ambayo ni mhimili wa pili wa Modeli ya jamii humshawishi mjifunzaji lugha kutumia msamiati wa lugha lengwa na kutangamana na wazungumzaji wa lugha hiyo. Kuwa na nia huthibitisha kiwango cha motisha mjifunzaji L2 alichonacho kinachompa uwezo wa kujifunza L.2.

Mara nyingi huenda makosa yakajitokeza wakati wanajifunza msamiati unaotokana na nyimbo na namna tulivyoona hapo awali. Hata hivyo, mionganoni mwa hatua za ujifunzaji L2, katika hatua ya pili ya Krashen (1978) mwanafunzi huwa anafanya makosa mengi ila si sababu yakekutuhumiwa kwa makosa hayo ila kumpa motisha (Gardener na Lambert 1959; Gardener, 1985; Gardener, 2000; MacIntyre na Gregerson, 2012; Rock, 2012) kwa kumsifu kwamba yuko sawa na atarekebisha baada ya muda fulani alimradi anaweza kuongea katika muktadha wa lugha anayojifunza.

## Wimbo 2: Shida za dunia-Jose .M.S 023,040,047 na 053.

Ubeti 1

**Rafiki yangu**  
alikuja  
nyumbani  
Kunielezea  
*shida fulani*  
Ati alifikuzwa *kazi na hajui atafanya nini*,  
Ati alifikuzwa *kazi na hajui atafanya nini*,  
Mke wake amemutoroka  
Rafiki zake wanamcheka  
Shida amepata nyingi amechoka  
Dunia anajuta

*Kibwagizo*

*Acha kulia shida za dunia  
Hebu tulia mungu alakujali piax2  
Ubetai.2*

*Maisha mwendo ni pole Ukipata  
shida leo usikonde Wengi wako  
kama wewe usijali  
Acha kulia ni maisha makali  
Tazama kwanza uone  
kesho Usikonde uwape kichekesho  
Maisha itakuwa na matatizo Uombe mungu  
Atakupa uwezo*

*Asili :Data zilizopatika kutoka na mahojiano.Februari,2022*

Katika wimbo wa shida za dunia kuna maneno kama **rafiki yangu** ambacho ni kirai kinatumwiwa sana kuvutia wanunuzi wakati wa kunadi biashara na pia kutoa salamu. Mara nyingi salamu huwa kama dhana ya kuanzisha mawasiliano. Pia maneno ambayo yanamsaidia mfanyabiashara kutumia endapo amepata changamoto zozote katika biashara zake. *Ukipata shida leo usikonde. Acha kulia maisha ni makali*

Katika huu wimbo wa shida za dunia kuna maneno walisema kwamba yaliwasaidia kuwasongeza karibu na wanunuzi ambao baadaye waliibuka kuwa wanunuzi wa kudumu. Kwa mfano katika kila biashara lazima uwe na marafiki. Ni mara kadhaa kwa hali y a kawaida ukiwa unapita katika maduka ya Emedi za Kampala utasikia mfanyabiashara akikuita rafiki njoo, pale ambapo **rafiki** imetumiwa tu kama dhana ya kukuvutia kununua bidhaa zake. Matumizi ya wakati mfano **njoo kesho** na usijali japo mara nyingi wanasema wewe **apanajali**. Matokeo haya yanakubaliana na mapendekezo ya Krashen (1987) kwamba mjifunzaji lugha ya pili anastahili kupewa pembejeo zenye sifa za kisarufi ambazo wanaweza kupata mbapo ni hali ya kupata dhana mpya kutokana na lugha anayojifunza. Mara nyingi huibuka na msamiati wa maneno mafupi mafupi hali ambayo wana uwezo wa kufanikiwa endapo wana nia ya kujifunza L.2 kwa kusukumwa na motisha changamani ambapo huweza kuwa ya ndani ama nje. (Gardener, 2000).

Kwingineko ujifunzaji wa Kiswahili kupitia nyimbo za wasanii kumeibua uchanganyaji ndimi mionganoni mwa wafanyabisahara. Utakuta wanatoa kauli kama **mpatikana kutoka pata-hali ya kupata matatizo, Nsaba Mungu-Naomba Mungu, Maali ya dunia-mali ya**

**dunia** kwa mfano kutokana na wimbo wa shida za dunia. Krashen (1987) anasema kwamba wakati wa kuhusisha dhana mpya pamoja na mfumo halisi hufanya mjifunzaji lugha aathirike na uchanganyaji ndimi kwa ajili ya kuathiriwa na L.1.

Nyimbo ama ukariri husaidia mwanafunzi kuhusisha dhana moja na dhana nyingine hata kama haihusishi uelewa wa kina. Katika mazingira halisi uchunzaji ulisaidia kushuhudia baadhi ya mikakati namna ilikuwa ikitumiwa. Mfano 1 unaonyesha mazungumzo yaliyokuwa yakiendelea kati ya wauzaji. Mazungumzo hayo yalidhihirisha namna ukariri ultiwezesha ujifunzaji wa Kiswahili kibiashara.

### **Mfano:1 Ukariri**

1. Muz. 4: *Bei dondolooo! Bei Laisi! (anarudia rudia kama wimbo)*
2. Muz. 5: *Omuyaye nkuulira.(Taperi nakusikia)*
3. Muz. 4: *Owaye, mbeera mukilasi:Ebiintu bya kuyiya (owaaye niko darasni .Mambo ni ya kubabanya)*
4. Muz.5: *Kyiki kyotegeeza ?(Unamaanisha nini?)*
5. Muz:4 *Anti ulinokusika omusubuuzi wa buli gwanga.*  
*(Naam yastahili uvutie mfanyabiashara kutoka kila nchi)*
6. Muz:5 *(Anacheka) ate awo nze sivijua.Naye nja kuiga .Oluswaili lulungi.*  
*(Hhhm mimi hapo sikiju.Lakini nitajifunza.Kiswahili ni kizuri*

### **Asili: Data ya nyanjani kutokana na uchunzaji (Februari ,2022)**

Ukariri ni mkakati muhimu katika uhifadhi wa maneno. Kadri msailiwa anavyoyarudiarudia ndivyo anavyojifunza. Kukariri ni tabia ambayo wauzaji hawawezi kuepukana nayo. Muz. 4 anasikika na Muz. 5 na hata watu wengine ambao wanapitapita mahali anakouzia nguo za watoto. Mwenzie anamtania kwa kumwambia bwana nakuona umechacha na kuimba. Muz.4 anamjibu kwa kumwambia namna hali ilivyo lazima atafute mbinu ya kuvutia wanunu. Hivyo inabidi arudierudie kuitana almaradi wanapopita wasogee karibu alipo wanunu. nguo.

Hali ya kuvutia wanunu imefanya wafanyabiashara kuibuka na njia zingine za kuelewana kimawasiliano. Kwa mfano baadhi yao wanarekodi sauti zao halafu wanatumia vipaza sauti kuvutia wanunu. Huu ni mkakati ambao unatumika sana na wauzaji simu. Hali ilivyokuwa ilibainika kwamba kufanya mazoezi ya kuimba yalitokana na motisha changamani wasailiwa walikuwa nao. Krashen (1987) na Ellis (2005) wanasema kukariri kunamfanya mjifunzaji wa L.2 asisahau alichohifadhi akilini mwake. Vile vile Muz. 4 ana motisha chanya (Gardener, 2000) juu ya lugha ya Kiswahili. Hii imemfanya ajivunie matumizi ya Kiswahili

katika Kiswahili na pia ana uwezo wa kumudu kile anachorudiarudia.

Mikakati mingi inayohusiana na ukariri husaidia wanafunzi kuunda maneno kama akronimu halafu ujuzi mwagine husaidia kukumbuka na kutumia sauti (kwa mfuatano wa mdundo), (McDonough 1986, O’Malley 1995; Gardner, 2000 na 2010a, 2010b; Rock 2012) na taswira (picha inayojengeka akilini asikiapo neno). Nyimbo ilikuwa mkakati ambao kila mfanyabiashara alijivunia kwamba ulimsaidia katika ujifunzaji wa Kiswahili kibashara.

#### **4.3.1.2 Mwanafunzi kwa mwanafunzi kufanikisha mawasiliano**

Wasailiwa sita (06/103) ambao waliwakilisha asilimia tano nukta nane (5.8%) ndio walitaja kwamba walijifunza Kiswahili kwa kupitia kwa kushirikiana kwao na wanunuzi ama wafanyabiashara wenzao ambao walikuwa wanakifahamu Kiswahili. Kutokana na hojaji walisema kwamba unamuuliza mwenzako ama mnunuzi halafu anakusaidia kupata msamiatu mwafaka. Ufafanuzi zaidi umetolewa kupitia mahojiano kuelezea namna kusaidiana kulifanikisha ujifunzaji wa Kiswahili kwa ajili ya biashara kupitia nukuu ifuatayo;

##### **M.S 016 akifafanua,**

*Kasitoma bwajja nga sisobola kubinyonyola ngamba munange nti owaye sooka oleete luswaili wano. Awo bwakyikola nfuunda eziwela nga satu mba nayizeemu abiigambo nga bisaatu. Olaaba naiga kalibu bosi hii handibag pei muzuuri.*

Mnunuzi akija kama siwezi kufafanua namwambia mwenzangu kwamba wewe mwanzo leta Kiswahili chako hapa. Akifanya hivyo mara kama tatu hivi nitakuwa nimejifunza maneno kama matatu hivi. Waona nilijifunza karibu bosi hili begi ni bei nzuri (TY)

Walielezea namna wamekuwa wakisaidiana yaani wakati kuna mteja ambaye ni mzungumzaji Kiswahili angefika, basi mfanyabiashara ambaye alijua Kiswahili angemfikia mwenzake ambaye hajui Kiswahili hivyo kujaribu kumtafsiria baadhi ya maneno au kuendeleza mchakato wa makubaliano. Baadaye yule ambaye hajui Kiswahili angeuliza afafanuliwe zaidi maneno ambayo yalikuwa yaktumiwa. Krashen (1987) anasema kwamba wakati mjifunzaji L.2 anakumbana na dhana mpya wakati mwagine hupenda kujisaidia kwa kutumia tafsiri ama kuomba msaada kutoka kwa mzungumzaji wa L.2. Ambapo Gardner (2000) anasema kwamba hali hiyo hutokea wakati mjifunzaji yuko tayari kujifunza na amejipima na kuona kwamba ana uwezo wa kujifunza lugha lengwa. Kulingana na Anderson na Elioumi (2004), Oxford (2003), Richard na Schmidt (2010) na Li (2021) wakati wa ujifunzaji lugha siyo lazima mwalimu awe kipaumbele katika kumsaidia

mwanafunzi, kulingana na changamoto anazokumbana nazo, anaweza kushirikiana na mwanafunzi mwenzake kufahamu lugha anayojifunza.

Mkakati wa mwanafunzi kwa mwanafunzi kufanikisha mawasiliano unakaribiana sana na mkakati wa Mtagusano na ukuruba kati ya wanunuzi na wauzaji. Tofauti iliyopo ni kwamba mkakati wa Mtagusano na ukuruba kati ya wanunuzi na wauzaji ni mpana wakati mkakati wa mwanafunzi kwa mwanafunzi ni pale ambapo mwanafunzi asijejua lugha lengwa hunyemelea anayeijua lugha lengwa na kujaribu mawasiliano ya mara kwa mara huku akijifunza msamiati michache kwa wakati wake. Mkakati huu kwa kiasi unaonekana kuwa mgumu maana unafanya mjifunza lugha kuchukua muda mrefu kujifunza kwa sababu lazima kuwepo msaиди. Ugumu wake ndiyo ulifanya data za kimsingi zifikirike kupitia hali halisi namna wanafunzi wanasaidiana wenyewe kwa wenyewe katika ujifunzaji Kiswahili kwa ajili ya biashara. Mtafiti alishuhudia maongezi haya katika mazingira halisi pale ambapo biashara ya nguo mpya ilikuwa inaendelezwa. Uchunzaji ulionyesha hali mbalimbali ambazo ujifunzaji kati ya mwanafunzi kwa mwanafunzi ultokea kama ilivyowasilishwa kwa mifano ifuatayo;

## **Mfano 2.kuomba msaada**

1. Mnz 1: *Ssebo hujambo!*
2. Muz 1: *Muzuli*
3. Mnz 1: *Nguo ni pesa ngapi?*
4. Muz 2: *Mitwalo tano*
5. Muz 1: *(Akitizama Mnz 1) Kwati lwaki tomugamba uliswaili*  
*(Mbona humwambii katika Kiswahili)*
6. Mnz 3: *Ndiyo nini ssebo?*
7. Muz 2: *(Anachukua kijikaratasi na kuandika ) 50,000/-*
8. Muz 1: *Omugambye bikyi –(umemwambia nini?)*
9. Muz 2: *Nyabbo ni pei muzuri njoo nkuguze*  
*(Bibi ni bei nzuri njoo nikuuzie)*
10. Mnz 3: *(anawatazama wauzaji lakin anaongea na Munz1) Hapa tutamaliza*  
*muda hebu twende kwa dukalingine.*
11. Muz 1: *Nyabbo wait.(anamuita mwingine upande wa pili) Gwe mkonjo jangu*  
*otuyambe ne luswaili*  
*(We mkonjo njoo utusaidie na Kiswahili.*

### **Asili: Data ya nyanjani kutokana na kushuhudia maongezi. (Februari 2022)**

Haya ni mazungumzo ambayo yanaendelea baina ya wauzaji na wanunuzi katika duka la nguo. Muz.1 amepata wanunuzi ila kustaamili mapatano katika lugha ya Kiswahili imekuwa vigumu. Katika hali hii Muz.1 kwa kuhofia kwamba Muz. 2 anaweza kuwachukua wanunuzi anaomba msaada wa mwenzake Mkonzo kumsaidia. Aidha, mara nyingi, wafanyabiashara jijini Kampala huwa na fikra kwamba yejote ambaye anazungumza kikonzo huwa anakijua Kiswahili. Kabilalau Wakonzo hutokea sehemu ambazo zimepakana na Kongo. Hata kuna nadharia kwamba Wakonzo walio Kongo ni wengi mno kuliko walio Uganda. Naiman et al. (1975) wanasema kwamba wanafunzi wapewe uhuru wa kutumia mikakati ambayo inawawezesha kujifunza lugha tumizi kwa mazingira yao wenyewe bila mwalimu kuingilia. Kwa kuongezea (Krashen 1987, Krashen, 1994; Gardener, 2000; Nelly, 2009, Nakatani 2010 na Saville-Troike, 2012) kwamba kuna wakati mjifunzaji lugha anajifunza kupidia mkakati fulani amba hata yeye mwenyewe huenda asifahamu kwamba anatumia mkakati huo kujifunza L.2. Hivyo huenda waliona ni hali ya kawaida ya kusaidiana katika mazingira ya biashara japo utafiti wetu ultambua kwamba mkakati wa mwanafunzi kwa mwanafunzi uliwezesha ujifunzaji wa Kiswahili kibiashara.

### **Mfano wa 3: kupata usaidizi wa papo hapo**

Mama wawili wanaingia kwa duka la vipodozi. Wauzaji wawili wanawaona na kuwakaribisha kutumia lugha shawishi ya biashara.

1. *Muz:6* *(anamnog'onezea mwenzake)Mwana bakongolee baingideo*  
*(Wakongo wameingia)*
2. *Muz:7* *Bakasitoma bamekuja*
3. *Mnz:Mkongo 1* *Leo we iko na bintu bingi.Unapata mafaranga*  
*mingi(anamfanyaia muzaha Muz.7)*
4. *Muz:6* *Abali ya Kongo lafiki*
5. *Mnz:Mkongo 2* *Hahaha pia wewe sebo natumiza Kiswahili?*
6. *Muz:6* *(anamkodelea macho Muz.7) Nyamba nawe nzilamu ntya? (we*  
*pia nisaidie najibu vipi)*
7. *Muz:7* *(Anamjibu Muz.6) bagambe kyitoko kyitoko*  
*(wambie kidogo kidogo)*
8. *Muz:6* *Leo tachukua nini lafiki yangu*  
*(leo utachukua nini rafiki yangu?)*

Muz. 6 amepata wanunuzi ilhali kustaamili mazungumzo kunamletea shida. Hivyo, anamuomba Muz.7 kumsaidia ni kwa jinsi gani atajibu katika Kiswahili. Kuomba msaada hutumika sana kwa wanafunzi ambao wanataka msaada kutoka kwa wale ambao wanaweza kuongea L.2. Baada ya kukwama anaweza kumgeukia yule aliye karibu na kuomba msaada Ellis (1997).

#### **Mfano. 4 Usaidizi kutoka kwa mnunuzi**

1. *Muz: B Nyabbo jangu wano nkuguze (Bibi njoo hapa nikuuzie)*
2. *Mnz: D (Anamwangalia halafu anarudisha macho sehemu nyine)*
3. *Muz: B Madam jangu siseera (madam njoo siuzi bei ghali)*
4. *Mnz: D You cannot speak any other language? (Huwezi ukaongea lugha nyine)*
5. *Muz: B Oh! Sorry luzungu lwange luzibu. (Sorry kizungu change si kizuri)*
6. *Mnz: D Which language can you try because I can understand Luganda but can not speak*
7. *Muz: F oyo knows some luswaili (huyo anajua Kiswahili kidogo)*
8. *Mnz: D Okay hiyo bagi we nauza pesa ngapi?*
9. *Muz: F Pozi bagi is what in Kiswahili*
10. *Muz: B Bagi zibeera nsawo. (Begi nsawo katika kiganda)*

Mfano wa 3 na 4 yote yanaonyesha namna mjifunzaji wa Kiswahili ana nia na motisha wa (Gardener, 2000) kutaka kujifunza Kiswahili kibashara. Anaonesha ari ya kutaka kujifunza meno mapya katika Kiswahili (Krashen, 1987) ili yamsaidie kujijengea umilisi katika matumizi ya Kiswahili kibashara.

#### **Mfano 5 . Kuuliza Maswali kupata uhakika**

1. *Muz:X Umeingizana lafiki*
2. *Mnz: Eeeh! Sijakuelewa*
3. *Muz:X Like what am I supposed to say in Kiswahili , 'you are welcome friend)*
4. *Mnz: Unasema karibu rafiki*
5. *Mnz:X Asanti lafiki*

Katika mfano wa 5 Muz. D anajaribu kupata jina kamili katika Kiswahili la bidhaa ambazo anauza. Vivyo hivyo katika mfano wa 5 Muz. X anauliza ni kwa jinsi gani atamkaribisha mnunuzi. Kuuliza maswali ni sifa moja ya ujifunzaji wa lugha ya pili. Hii ni nia moja ya

kutaka kupata dhihirisho kwamba unachokisema kiko sahihi na kama kuna kubahatisha basi unaomba msaada kutoka kwa mtu mwingine. (Gardener na Lambert, 1972; Gardener, 2000, 2010; Cook, 2001) wanasema kwamba kuomba msaada hutokea kwa wale ambao wana motisha ya kujifunza lugha lengwa. Huwa wanajitahidi iwezekanavyo kuomba msaada kwa wazungumzaji wa lugha hiyo ama wale ambao wanajua lugha hiyo ili kufanikiwa.

#### **4.3.1.3 Matumzi ya Lugha chanzi**

Wasailiwa thelathini na tano (35/103) ambapo waliwakilisha asilimia kumi na tatu nukta tano (13.5%) kwa kushirikisha hojaji walitaja matumizi ya fomula; Hizi ni fomula ambazo hasa zilibuniwa na wasailiwa ambao ni wabantu. Miongoni mwazo zilitumiwa kutaja siku za wiki, miezi, na kupanga akronimu za maneno ili kuibuka na sentensi. Walisema k a t i k a mfumo wa kuunda sentensi kuna fomula ambayo (kutokana na mfumo wa lugha asili) wangetumia ili kuibuka na sentensi katika Kiswahili ambazo kwao waliona ni rahisi na sahihi kwao kutumia. Chomsky (1968) na Ladefoged (1971) wanasema kuwa ujifunzaji wa lugha ya pili huwa na msingi mkubwa katika lugha ya asili. Watu hujaribu kuhamisha muundo na maana na usambazaji wa muundo wa maana ya lugha yao ya asili na utamaduni kwa lugha lengwa. Huwa wanajaribu kuzungumza na kutenda katika utamaduni wao wanapajaribu kujifunza, kuelewa lugha na utamaduni wa lugha nyingine.

Sambamba na hayo mahojiano kati ya mtafiti na watafitiwa yaliibua dhana za kimsingi kuelezea namna lugha chanzi iliwezesha ujifunzaji wa Kiswahili kama lugha ya biashara. Data za sehemu hii ambazo zilipatikana kutokana na hojaji pamoja na dodoso ziliwasilishwa kithamano. Mifano hiyo imeonyeshwa katika majedwali mbalimbali yafuatayo.

#### Jedwali 4.6: Matumizi ya fomula katika sentensi

Fomula	Kutoka Lugha Chanzi	Kiswahili
3J+A+I+2J	<i>Sande, bbalaza, lwakubiri, Jumatatu, Jumanne, Jumatano, lwakusatu, lwakuna, lwakutano, Alhamisi, Ijumaa, Jumamosi, Jumapili lwamukaaga</i>	Jumatano, Jumanne, Jumapili Agosti, Septemba, Oktoba, Novemba, Desemba
JAFEMA+JUJUA+ SEPONODE	<i>Gatonya, Mukutulansanja, Mugulan sin go, Kafumuulampawu, Muzigo, Sseb as eka, Kasamabula, Muwakanya, Mutu nd a, Mukulusabitungotungo, Musenene , Ntenu (Luganda) Biruuru, Katambuga, Nyaiakoma, Kya b ahezi, Kahingo, Nyairurwe, Kicurans i/ Nyakanga, Kamena, Kashwa, Musen ee ne Muzimbeesi (Lunyakore/Lukiga)</i>	Januari, Februari, Machi, Juni, Julai, Agosti, Septemba, Oktoba, Novemba, Desemba
N+KN+NJ+KT	<i>-John ajakuletaa leero emigugu -John yalesse jjo emigugu -John ajakuleta nkya emigugu</i>	John analeta leo mzigowakati uliopo John alileta jana mzigowakati uliopita John ataleta keshomzigo-wakati ujao
N+KO+KN+KT	<i>-ensau zilli ziingidde leero -Ssuuti zino ziva edubai -Emottoka eno etuleteera jora zzeDubai engoye</i>	Begi zile zimeingia leo Suti hizi zatoka Gari hili linatuletea jora za nguo
N+KN+NJ(KI)+KT +NM	<i>-Lule bwebamuwereza ssenteajjagulamaali -Meneja bwanasasula nja kukkubilanitakupigia simu Nakazi ssimu -Nakazi bwanatunda bulungi ajjakufuna amagoba</i>	Lule akitumiwa pesa atatumamali Meneja akilipa Nakazi akiuza vizuri atapata faida

Asili: Data Kutokana na hojaji na mahojiano : Februari-machi 2022

Wasailiwa walidai huo uundaji wa fomula uliwasaidia kupunguza makosa wakati wanatumia Kiswahili kibiashara. Ila hii fomula iliwezekana tu kwa wasailiwa ambao ni wabantu. Ilibainika kwamba msailiwa anaunda kutoka lugha chanzi vivyo hivyo kuhawalisha (Chomsky, 1968; Krashen, 1986; Cook, 1993; Gass 1979; Benzehat 2021) katika lugha ya

Kiswahili. Krashen (1987) anasema kwamba wakati huu mwanafunzi anajaribu kutangamana na sheria za lugha lengwa hivyo makosa huibuka kwa sababu ya athari za lugha mama. Hivyo muhimu ni kwamba mwanafunzi kupewa mwoyo kuendelea na matumizi ya lugha katika mawasiliano alimradi ameeweleweka. Kwa kuongezea Gardener (2000) anasema kwamba mjifunzaji akionyesha nia ya ujifunzaji lugha ya pili basi kumsifia kwamba anawasiliana vizuri ni motisha ambayo inamfanya aendelee kujifunza.

Kwa upande wa kutaja miezi ya mwaka, walisema kwamba kwao walihesabu miezi kutegemea utaratibu wa matukio katika utamaduni wao. Hivyo kuhesabu kwao hakukuwa kama katika Kiswahili ila walibidi wapange akronimu ya miezi katika Kiswahili kuwasaidia kukumbuka miezi katika Kiswahili. Kisarufi huu muundo wa formula hausaidii katika sentensi za kukanusha hata hivyo unawapatia msingi bora wa kujenga umilisi wao katika lugha ya Kiswahili kibiashara. Katika huo mkakati ilibainika kwamba kuna dhana ya utafsiri kutoka lugha chanzi hadi lugha lengwa ambayo ni ya Kiswahili; Mfano mzuri uko katika hizi sentensi. Cook (1993) anasisistiza kwamba wakati wa ujifunzaji lugha ya pili huwa hakuna uhakika kwamba uhawalishaji wa miundo ya lugha mama itasaidiana na ya lugha ya pili. Hivyo kutegemea nini kinahawilishwa miundo mingine huenda isiwezekane. Hata hivyo anatoa mawaidha kwamba pale ambapo uhawalishaji wa muundo hauwezekani, utohozi na tafsiri yaweza kufanikisha ujifunzaji lugha ambayo mwanafunzi anajifunza. Hoja ya utohozi na tafsiri imeshughulikiwa katika utafiti huu kama vipengele muhimu ambavyo vilitumiwa kujifunza Kiswahili kama lugha ya biashara.

#### **Jedwali 4.7: Matumizi ya maneno katika sentensi**

<b>Kutoka lugha chanzi ya kibantu</b>	<b>Kiswahili</b>
1.. <i>John ajakuletaa leero emigugu-(wakati uliopo)</i>	John analeta leo mzigo- (wakati uliopo)
2. <i>John yalesse jjo emigugu-(wakati uliopita)</i>	John alileta jana mzigo-(wakati uliopita)
3. <i>John ajakuleta nkyu emigugu-(wakati ujao)</i>	John ataleta kesho mzigo-(wakati ujao)
4. <i>ensau zilli ziingidde leero</i>	Begi zile zimeingia leo
5. <i>Ssuuti zino ziva edubai</i>	Suti hizi zatoka Dubai
6. <i>Emottoka eno etuleteera jora zze engoye</i>	Gari hili linatuletea jora za nguo
7. <i>Lule bwebamuwereza ssente ajjakugula maali</i>	Lule akitumiwa pesa atatumua mali
8. <i>Meneja bwanasasula nja kukkubila ssimu</i>	Meneja akilipa nitakupigia simu
9. <i>Nakazi bwanatunda bulungi ajjakufuna amagoba</i>	Nakazi akiuza vizuri atapata faida

**Asili: Data kutokana na mahojiano (Februauri- Machi 2022)**

Sentensi zilizo hapo juu katika jedwali zinaonyesha namna sentensi zilitafsiriwa moja kwa moja kutoka lugha chanzi hadi lugha ya Kiswahili. Ndiyo maana Krashen (1987); Hassan, 2000; Lucy, 2014, na Hajimia et.al 2020 wanasema kwamba tafsiri ina mwezesha (Baker 2001; Jilala 2014; Sarah na Leonard, 2019) mwanafunzi kujifunza lugha ya pili kwa mkabala wa kisemantiki yaani maana. Kupitia tafsiri mwanafunzi anajua uhusiano wa kuunganisha sentensi na kulinganisha na sentensi inayowiana katika L1. Pia atabaini kuwa, msamiati wa lugha fulani hauorodheshwi tu kama faridi pekee, bali unapangiliwa katika eneo au uga ambalo neno linaingiliana na kuelezewa kila moja tofauti. Wanaendelea kusema kwamba tafsiri katika ufundishaji wa L2 huwasaidia wanafunzi kujua vipengele vya sarufi, kwa mfano katika kiwango cha fonolojia. Tafsiri imekitambulisha Kiswahili ulimwenguni (Sarah na Leonard, 2019), kuwa miongoni mwa lugha kubwa na muhimu duniani. Upanuzi wa msamiati na istilahi zake umechangia pakubwa katika maendeleo. Biashara ni asasi mojawapo ambayo inakuza na kuendeleza uchumi wa nchi. Utafiti uligundua kwamba wasailiwa walitafsiri sentensi kisisisi kutoka lugha chanzi hadi lugha tumizi ambayo ilikuwa lugha ya Kiswahili.

Wafanya biashara wanaweza kujua tofauti na kufanana kwa sauti katika lugha mbili yaani L1 na L2. Mifano kama hii iliibuka wakati wa kukusanya data wakati baadhi ya wasailiwa wakati wa mahojiano walisema kwamba walipokuwa wakijifunza lugha ya Kiswahili walikuwa ama wakichanganya au kuhamisha baadhi ya sauti kutoka lugha mama hadi Kiswahili katika maneno kadhaa ambayo yalitolewa na msailiwa 014 katika mifano ifuatayo katika jedwali 4.8

#### **Jedwali 4.8: Kuhamisha sauti kutoka lugha chanzi hadi Kiswahili**

<b>Lugha asili</b>	<b>Kiswahili</b>
1. <i>Kyakulya</i>	/chakula/
2. <i>Anafundisa</i>	/anafundisha/
3. <i>Kali</i>	/ghali/
4. <i>Pei</i>	/bei/

**Asili: Data kutokana na mahojiano. (Machi 2022)**

Katika maneno ambayo yaliwasilishwa katika jedwali 4.5 ni namna sauti zilitumiwa kutoka lugha mama hadi Kiswahili. Yaani /kya/-/Č/, /S/-/Š/, /K/-/়/, /p/-/b/. Wakati wa kuyatumia kuna hizo tofauti ambazo huwa zinajitokeza kwa ajili ya muathiriano wa lugha mama. Krashen (1987) anaeleza kuwa mjifunzaji lugha anapojifunza L.2 hukumbana na matatizo mengi ya sauti, sheria na muundo wa L.2. Matatizo hayo hutokana na L.1 ambapo mjifunzaji huenda asilielewe ndiyo chanzo cha utokeaji wa makosa hayo. Ni rahisi sana mtu kusema nataka kyakula kuliko nataka chakula katika mazingira ya Kampala kwa sababu ya

athari ya kuhamisha mfumo wa L.1 na kuuingiza namna ilivyo katika lugha chanzi. Wakati biashara ziliendelea athari hizi hazikuzingatiwa sana ila lililokuwa la muhimu lilikuwa ni kufanikisha mawasiliano ya kibiashara.

#### **Jedwali 4.9: Baadhi ya maneno ya biashara ya kiasili na Kiswahili**

<b>Kiganda/Lusoga</b>	<b>Kinyankore/Kukiga</b>	<b>Langi/Japadhola</b>	<b>Kiswahili</b>
<i>Duuka</i>	<i>Duuka</i>	<i>Duk(h)a</i>	Duka
<i>Banka</i>	<i>Banka</i>	<i>Benk</i>	Benki
<i>Emaali</i>	<i>Emaali</i>	<i>Dami</i>	Mali
<i>Beeyi</i>	<i>Beeyi</i>	<i>Cilingi</i>	Bei
<i>Emiggugu</i>	<i>Emiguguni</i>	<i>Jami</i>	Mizigo
<i>Looni</i>	<i>Looni</i>	<i>Den</i>	Loni

#### **Asili: Data kutokana na mahojiano; Machi 2022**

Kutokana na maneno kwenye jedwali la 4.9 kwa kiasi lugha chanzi ilichangia katika ujifunzaji na matumizi ya Kiswahili. Ukiona neno kama [duu-ka] lina silabi mbili. Vivyo hivyo katika Kiswahili neno [**du-ka**] lina silabi mbili licha ya kuwa neno asili lilikuwa na irabu mwambatano. Kuna wakati maneno yanawahlilishwa kulingana na mazingira na matumizi yake. **Den** na **benk** katika lugha ya kinailoti ni kwamba walikosa msamiatii mwafaka na kutumia tafsiri kisisi. Den ni deni yani kuwa unadaiwa. Maana kwamba ukiwa ulichukua loni basi uko na deni la kulipa. Kwingineko Krashen 1987 anaeleza kwamba mjifunzaji huchuja dhana ambazo anastahili kuzitumia katika mazingira husika. Wittrock (1977) Cohen ,1996) na Gardener (2000) wanafafanua kwamba nia ya kutaka kujifunza ambayo ni mhimili wa pili wa Modeli ya jamii humshawishi mjifunzaji lugha kutumia msamiat wa lugha lengwa na kutangamana na wazungumzaji wa lugha hiyo. Kuwa na nia huthibitisha kiwango cha motisha mjifunzaji L2 alichonacho kinachomjengea uwezo wa kumudu lugha na kuitumia katika mazingaira yanayofaa. Kwa wafanyabiashara msamiat kama /**benki/**, **bei/** na **/loni/** ambapo wanashinda wakipata mikopo kuendeleza biashara zao inakuwa ni msamiat zoefu mno. Kuna uwezekano akawa anatamka msamiat huo na lafudhi ya L.1 lakini mwisho wa siku hayakuwa yanaeleweka katika Kiswahili.

#### Jedwali 4.10: Matumizi ya msamiati wa biashara katika sentensi

Luganda/Lusoga	Lunyakole/Lukiga	Langi/Japadhola	Kiswahili
<i>Nnoonya edduuka lye'ngoye</i>	<i>Ninoonda eduuka lye Ebyenda</i>	<i>Akwayo duk(h) a ne dong</i>	Natafuta duka la nguo
<i>Ssasula mu'banka ya Equity</i>	<i>Sasula mu banka ya Equity</i>	<i>Cul I benk equity</i>	Lipa kwa benki ya Equity
<i>Emaali yaingidde</i>	<i>Email zatahamu</i>	<i>Dami dong</i>	Mali imeingia
<i>Byoona wammu beeyi kyi</i>	<i>Zoona hani ni zinka</i>	<i>Duchuti cente nene</i>	Vyoote pamoja bei gani
<i>Alina loni</i>	<i>Alina looni</i>	<i>In den</i>	Yuko na loni

**Asili ya data.Nyanjani kutokana na mahojiano; Machhi,2022**

Matokeo ya utafiti yalionyesha kwamba mfumo wote wa sentensi ulifuatwa kwa kuzungatia aina za sentensi kileksia na kimaumbo. Kando na Luganda, Lusoga, Lunyakole na Lukiga sehemu ya Kinailoti ilibainisha sentensi ambazo zilitokea katika lugha ya Lango, Japadhola na Acholi. Lugha hizi zinakaribiana sana na kiluo cha Kenya. Kwa kutumia mbinu ya usaili sentesi zilizotokana na msailiwa 062 wa kiganga, zilikuwa msingi wa kuuliza wasailiwa 068 na 070 waliokuwa na uasili wa Lusoga Kinyakore na Kikiga amba walitoa mifano; ***Nnoonya edduuka lye'ngoye, Ninoonda eduuka lye ebyenda, Ssasula mu'banka ya Equity, Sasula mu banka ya equity*** ni baadhi ya sentensi arifu halafu ***Kasitooma waffe omulingi, Emigugu jange*** zinadhihirisha muundo wa kiima na kiarifa ambapo inawarahisishia kujifunza Lugha ya Kiswahili kibiashara kwa kufuata muundo wa Kiswahili. Krashen (1987) anasema kwamba wakati wa kupata dhana mpya sio lazima kwamba mjifunzaji atafuata sheria zote za lugha na muundo kwa wakati mmoja. Kwamba uimarikaji katika umilisi wa L.2 hutegemea muda na kiwango ambacho mjifunzaji amefikia kujifunza lugha hiyo. Gardener na MacIntyre (1992) na Ghalebi, Sagithhi na Bagheri (2020) wanasema kwamba kujifunza sheria ni kitu kimoja na kuwa na uwezo wa kutaka kufanikiwa na nia ni vitu viwili tofauti. Wanasema kwamba mjifunzaji huenda awe anataka tu kujifunza lugha kwa ajili ya kuwasiliana. Hutamfungia mjifunzaji kama huyo katika sheria za ujifunzaji lugha. Hivyo nia ya ujifunzaji lugha lengwa hutofautiana na malengo ya mtu binafsi ya ujifunzaji.

Matokeo hayo ya utafiti yanaonyesha bayana namna ilivyo rahisi kwa wabantu kujifunza Kiswahili kuliko namna ilikuwa kwa wanailoti kimuundo. Aidha, dhana ya ukopaji na ulughamamaishi ulifanya hata khabila za kinailoti zimamaishe na kukopa misamiati ambayo haikuwa katika lugha yao asili. Ukiangalia neno duka na benki ambalo nalo lilikuwa ka mkopo katika Kiswahili limeendelea kutumika vivyo hivyo hata katika lugha za Kiasili.

Katika kiluo tunaona kwamba loni limetumika kama den ambapo kwa mantiiki yake katika Kiswahili, mtu akichukua mkopo huwa ni deni ambalo anastahili kulipa kutegemea na wakati. Mwingiliano wa lugha mama na matumizi ya L1 yalichangia pakubwa katika kufanikisha ujifunzaji wa Kiswahili kwa mawasiliano ya kibiashara.

#### **Jedwali 4.11: Msamiati wa mavazi katika Lugha asili na Kiswahili**

<b>Kiganda/Kisoga</b>	<b>Kinyankore/Kikiga</b>	<b>Lango/Japadhola</b>	<b>Kiswahili</b>
<i>Esaati</i>	<i>Esaati</i>	<i>Cati (chari)</i>	Shati
<i>Sikaati</i>	<i>Skaati</i>	<i>Cikati</i>	Sketi
<i>Ekooti</i>	<i>Ekoti</i>	<i>Kori (koti)</i>	Koti
<i>Esweeta</i>	<i>Esweeta</i>	<i>Cweta</i>	Sweta
<i>Sitookisi</i>	<i>Sokisi</i>	<i>Cokci</i>	Sokisi

**Asili :Data kutoka na hojaji:Machi ,2022**

Kulingana na jedwali 4.11 inaonekana bayana kwamba maneno ya kibantu yalikaribiana sana na maneno ya Kiswahili. Hii inafanya mjifunzaji lugha ya Kiswahili ambaye ni mbantu kujifunza kwa haraka. Tukiangalia maneno ya kinailoti neno shati wanatamka kama /ca: ti/ ila kimaandishi inaanidika kama cha: ri. Katika lugha ya Kilango ama Japadhola konsonanti /t/ ikiwa kati kati mwa irabu mbili hasa /a/ na /i/ ukaakaishaji unatokea halafu sauti hiyo inabadilika na kuwa /r/. Lugha hii vile vile haina sauti /s/ na /sh/ ndiyo maana utakuta mtu akisema *chacha* badala ya sasa. Hata hivyo mpangilio wa kisilabi unasaidia mjifunzaji lugha kuboresha matamshi yake hata kama atakuwa wamefuata muundo wa L.1. Kwa mfano

*Esa:ti Esa:ti ca:ti sha:ti yote yana silabi mbili  
 Si:ka:ti s:ka:ti ci:ka:ti: s:ke:ti yote yana silabi tatu*

Katika maneno ya kwanza huwa sauti /e/ huwa ni nyamavu hata mtu akitamka kwa haraka huenda isisikie. Nadharia tete ya mfumo halisi ya Krashen (1987) hueleza namna mjifunzaji hupata sheria za lugha kwa mfumo maalum wa kiasili ambao unatabiri sarufi sahihi hadi sarufi tata. Mfumo huu halisi wa upataji lugha ni sawasawa kwa wote wanaojifunza L1 na L2. Mfumo huu hurejelewa kama mfumo wa umilisi mkuzi ambapo ujifunzaji huanza na muundo wa virai vifupi vifupi halafu baadaye kuimarika katika kuunda sentensi.

#### Jedwali 4.12: Msamiati katika matumizi ya sentensi

Kiganda/Kisoga	Kinyakore/Kikiga	Kinailoti	Kiswahili
<i>Esaati bbiri seente</i>	<i>Essati ibiri ebbey yazo</i>	<i>Cati ario ti</i>	Shati mbili pesa
<i>Meeka</i>	<i>neingana kyi</i>	<i>cente neene</i>	ngapi
<i>Nnaguzzekooti</i>	<i>Nikagura ekooti ikumi</i>	<i>Awilo kori</i>	Nilinunua koti kumi
<i>Kumi</i>		<i>apar</i>	
<i>Esweeta</i>	<i>Esweetaza baantu</i>	<i>Cweeta ne ojee</i>	Sweta za watu
<i>Za'abbakulu</i>	<i>Abakuzire</i>		wazima
<i>Sitookisi za'abana</i>	<i>Ninenda sokisi eza abaana</i>	<i>cokci me odino</i>	Sokisi za watoto

#### Asili :Kutokana na mahojiano nyanjani (Machi, 2022)

Sentensi za hapo juu zilitokana na data ambazo zilikusanywa kutokana na jedwali 4.9 kwa kuhusisha mahojiano kati ya mtafiti na wasailiwa. Kuibuka na sentensi hizi ilikuwa kwa ajili ya kujibu swali la namna wasailiwa walivyotumia mikakati kujifunza Kiswahili kibiashara. Mkakati ambao unaelezwa hapa ni mkakati wa matumizi ya L.1 katika ujifunzaji wa Kiswahili kibiashara. Katika sentensi ya kwanza kuna neno ambalo linadhihirisha kiwango cha kwamba hata kwa yule ambaye anaweza kutatizika anaweza kutumia ujuzi wake kuelewa nini kinachorejelewa. Neno hilo ni /shati/. Kwa hali yoyote ile mnunuzi akiuliza bei ya shati hata kwa mnailoti ataeleweka kwa sababu licha ya kuwa neno katika maandishi yake ni /cati/, katika matamshi ni /chati/. Ni rahisi mtu kuhusisha shati na chati na kuelewa nini kilichokuwa kinarejelewa. Neno kama /cokci/ katika matamshi ya kawaida ni /soksi/. Hivyo utafiti huu uligundua kwamba L.1 ilikuwa na mchango mkubwa sana katika ujifunzaji wa Kiswahili hasa wakati wa kuzingatia lugha ya wasemaji. Krashen (1987) anaeleza kwamba mjifunzaji hupata sheria za lugha kwa mfumo maalum wa kiasili ambao unatabirika sarufi sahihi hadi sarufi tata. Mfumo ambao hurejelewa kama umilisi mkuzi hueleza namna mjifunzaji hujizoesha na mfumo wa lugha lengwa. Dhana mpya zinazojitokeza zinaweza kuathirika na L.1 kwa sababu ya uhawalishaji. Aidha, Gardener (2000) na Krashen (1987) wanaelekeza kwamba ni bora mjifunzaji aanze na dhana nyepesi halafu kadri anavyoijiimarisha anaweza kutumia sentensi changamano katika matumizi ya L.2

Data iliyotokana na uchunzaji ilionyesha kwamba wafanyabiashara bila kuju walihuisha matumizi ya L.1 katika matumizi ya lugha ya Kiswahili kibiashara namna inavyoonyeshwa katika mazungumzo yaliyojitokeza katika maeneo ya kufanya biashara katika ekedi ya Mukwano katika sehemu ya mkahawa

Mnz: Umepika chakula gani?

Mh1: *Iko kaunga,mchele,matoke, nyama,kuku na samakyi*

- Mnz: Hamna mboga. Nilitaka Ugali na kuku lakini weka mboga.
- Mh1: *Iko ugali ya kaunga na kalo mimi letea wewe ipi*
- Mnz: nimesema ugali na kuku na mboga kwani kuna pia aina ya ugali
- Mh.2 *Bano baagala kaunga kati olikumubuzaabuza. Customer wacha mimi taletea wewe posho ile ya Uganda.*
- Mh.1 *Haya ugali ndiyo hii. Sisi naita kaunga*

### **Asili : Data kutokana na uchunzaji (Machi 2022)**

Katika lugha nyingi za kibantu hasa Wabantu ambao walio katikati mwa Uganda hawakuwa na jina mwafaka katika ethnolojia yao kuhusu chakula kinachotokana na unga. Wallita ugali *kaunga* kwa sababu chakula hicho kinatokana na unga. Katika kabilalau Wagisi walioko karibu na mipaka ya mashariki mwa Uganda kukaribia Kenya huita *busuma* ama *liposo*. Hata hivyo katika mazungumzo haya tunaona tayari Mh.2 alikuwa na ufahamu kwamba Ugali ndiyo kisawe cha *kaunga*. Mh.1 naye alionyesha ukubalifu wa kujifunza msamati mpya kutoka na kumhudumia mteja ambaye asili yake ni tofauti na wateja ambao huwa anawahudumia mara kwa mara.

Hali ya kujifunza dhana mpya huhitaji uvumilivu na kujitolea sana. Hapa ndipo Gardener (2000) katika mhimili wake wa pili anasema kwamba lazima mjifunzaji aonyeshe nia ya kujifunza L.2 ndiyo afanikiwe kujifunza lugha hiyo. Vile vile amehusisha mhimili wa tatu katika kiwango hiki kwamba ujifunzaji lugha hutokana na motisha changamni alionao mjifunzaji lugha ya pili. Motisha wa mtu binafsi (Gardener, 2000; Gardener, 2007; Rock, 2012 na Hardach 2018) huhuishwa na vigeugeu vitatu ambavyo ni ujumuishaji, mwelekeo kuhusu muktadha wa kujifunza na mwelekeo kuhusu lugha. Ujumuishaji unasaidia mjifunzaji lugha ya pili kukubali kuwa mwanajamii wa jumuiya fulani na kukubali utamaduni wao. Tunaona kwamba MH.1 anaridhia kwamba watu hutoka tamaduni tofauti na ni muhimu kuheshimu tamaduni za watu tofauti na kujifunza misamati yao endapo ungetaka kuendeleza biashara vyema. Kwa mfanyakishara kujifunza Kiswahili, lazima awe amekubali lugha hiyo na utamaduni wake. Hili litafanikiwa tu endapo mjifunzaji lugha ya pili ana uwezo wa kujifunza lugha hiyo. Dornyei (1994b) anasema kwamba kiwango cha mwanafunzi cha kufanikiwa pia huwa muhimu katika ujifunzaji. Kupata dhana mpya kutokana na mazingira halisi ya matumizi ya L.2. na mwanafunzi kuwa na sifa za kiutambuzi na kujiamini. Katika madhumuni ya pili wafanyakishara walionyesha ari, motisha

changamani na uwezo walio nao kutumia dhana mpya katika ujifunzaji wa Kiswahili kama lugha ya kibiashara.

#### **4.3.1.4 Kuongea**

Matokeo ya hojaji yalionyesha kwamba Wasailiya kumi (10/103) ambao ni asilimia tisa (9%) walikiri kubahatisha baadhi ya maneno ambayo walijikuta wanaongea kimushtukizo kujifunza Kiswahili kibiashara. Walisema hii njia ni kupitia kusikiliza baadhi ya msamati ambayo ilitokana na kutagusana. Kubahatisha bahatisha kulisaidia katika kuelekeza na kupokea wanunuzi ambao waliotangaman nao katika mazingira ya kufanya biashara.

Kupitia mjadala wa mahojiano kati ya mtafiti na wafanyabiashara kumi na saba, mfanyabiashara 063 alisema kwamba kuna baadhi ya maneno ambayo ye ye huongeaongea kutegemea alivyomtathmini mnunuzi na mahitaji yake. Kuanzia kwa wale waliotaka kuelekezwa, hadi kununua bidhaa. Alisema;

*Nje njogera byange luusi byemba mpulidde. Tugeze walio ababuuza ii barabaranakwenda wapi; njilamu ku William, kuMtaasa. Aba tategeede? saa ngapi, walio bino; karibu dada, njoo bosi, njoo kasitoma, nitafanya muzuri, huyu hapa, leo bei muzuri, oh rafiki umerudi. kasitoma onakusafika: leo tachukua mali ya gani; siyo pei kali leo: mimi nafanya muzuri' eeeh luswaili si lwangu.*

Mimi huongea tu mambo yangu wakati mwengine yale ambayo nimesikia. Kwa mfano kuna wale ambao wanauliza barabara hii inakwenda wapi? Nawajibu inaelekea barabara ya William ama Mtaasa. Kwani anakua hajaelewa? Saa ngapi, kuna haya kama karibu dada, njoo bosi, njoo mnunuzi, nitakufanya vizuri, huyu hapa, leo bei nzuri, Oh umerudi rafiki, mnunuzi umefika, leo utachukua mali ya kiasi gani, sio bei ghali, nitakufanya vizuri- eeh Kiswahili si kirahisi.TY)

Walisema huu mfumo uliwapa maneno machache mno wakati wa kutumia Kiswahili kibiashara. Ilibainika kwamba walitumia kubahatisha katika kuwashawishi wanunuzi wao ili wawavutie kununua bidhaa zao. Wenden na Rubin (1987), Bachman (1990), Bailystock (1990) wanaeleza kwamba mwanafunzi anaweza kubahatisha kwa kuzungumza kile anachokizungumza bila kufahamu kama alichozungumza ni kweli ama la. Krashen (1987), Vygotsky (1978) na Gardner (2000, 2010a) wanaeleza kuwa mjifunzaji lugha hutapatapa na kuongea msamati ambao huenda wakati mwengine asijue maana yake lakini akilini mwake anajua amewasilisha ujumbe. Wanaendelea kusema kwamba wajifunzaji wa aina hii huruka ruka mambo mengine au mengine huyaeleza kwa kukisia tu au hata kuyarahisisha zaidi mradi tu waendeleze mazungumzo ama wawasilishe ujumbe waliokusudia. Kwa mfano

maneno haya mawili ***kuWilliam, kuMtaasa*** yana muelekeza mhusika katika maeneo mawili tofauti ila katika kuelekeza mfanyabiashara anaruka mengine ili kufupisha dhana ambayo kwake itakua rahisi kutamka. Huu ni wakati mjifunzaji L.2 anapata mfumo halisi wa lugha kwa kutilia maanani dhana mpya zinazoibuka wakati wa kujifunza lugha lengwa. Hali hii imeshadidiwa na mhimili wa pili wa Gardener (2000) wa nia na mhimili wa nne ambapo mjifunzaji L.2 anatumia uwezo wake wa kufanikiwa katika kufanikisha ujifunzaji wa L.2 .

#### **4.3.1.5 Mawasiliano**

Matokeo ya hojaji yalionyesha kwamba matumizi ya mawasiliano ndiyo yalipendelewa sana kutokana na wasailiya ishirini (20/103). Idadi hii iliwakilisha asilimia kumi na tisa (19%) . Walisema wao walikuwa na mawasiliano ya hapa na pale na wanunuzi katika sehemu za kufanyia biashara Kampala. Walitaja kuwasiliana ana kwa ana kati yao na wanunuzi, kuwasiliana na wanunuzi ambao walikuwa mbali kwa mfano wakati mnunuzi aliagiza bidhaa fulani, alituma jumbe fupi kupitia simu mahiri. Kutokana na mahojiano na wasailiya takriban ishirini walikuwa na mchango tofauti tofauti kuonesha namna mawasiliano yaliwasaidia kumudu Kiswahili cha kibiashara.. Msailiwa 029 alisema,

*Omanyi ne booba olulimi tolumanyi naye ollaba baalwo nga webogere, walio ebigambo byotegeeramu mululimi lwo .Kinooyinza kumanya kyiki omusubuuzi kyayagala. Nawe nogatamu ebyolugaanda aaah nemugengeeramu awo.*

Wajua hata kama lugha haujui halafu unaona wenyeji wa lugha namna wanaongea, kuna maneno kutoka kwa hiyo lugha ambayo unaweza kuelewa. Unaweza kuelewa mnunuzi anachohitaji halafu nawe unaongezea kiganda aaaah na kumalizana hivyo hivyo .(TY)

Nukuu: M.S 096 alisema kwamba kilichomshawishi kuchagua mkakati wa mawasiliano ni ule wepesi wa matumizi kupitia simu .

*Now days phones have made life easy. You just go to google find a word translate it in Kiswahili then use that word with a customer in Kiswahili.*

Siku hizi simu zinafanya maisha kuwa rahisi. Unaenda google unatafuta neno halafu kupitia google unalitafsiri katika Kiswahili halafu neno hilo unalitumia na mnunuzi (TY)

Waliongezea kwamba kwa kuchagua mkakati huu wakati wa mawasiliano, inakuwa rahisi mno kuwa na uzoefu wa kufuatilia maneno yanayotumika na hivyo kujifunza msamiati tofauti tofauti. Mara nyingi wao huiga msamiati tofauti wa wazungumzaji wa Kiswahili na

kujifunza namna ya kuutumia. Stadi za mawasiliano humuwezesha mwasilianaji kuchagua mbinu stahili ya mawasiliano ili aitumie kuhawilisha ujumbe kwa mujibu wa muktadha husika. Mwasilianaji anafanya hivi ili aweze kutimiza malengo yake katika mchakato wa mawasiliano, bila kumdhuru mwasilianaji mwenza. Licha ya kwamba Krashen (1987) anasema kwamba katika hatua ya nne katika ujifunzaji, mjifunzaji huimarisha sheria na muundo wa lugha lengwa na kuimarisha umilisi katika L.2, kiwango cha kupata dhana mpya, Gardener (2000) anasisitiza kuwa siyo lazima mwanafunzi aimarike katika sheria na mfumo wa L.2 almradi anaweza kumudu mawasiliano. Gardener (keshatajwa) anaendelea kusema kwamba wakati wa kujifunza L2 nia na uwezo wa kujifunza unajengeka katika nguzo kuu nne yaani hekima, maarifa, motisha na muktatha. Simiyu na Kavoi (2013) wanasema mtu anayezimudu stadi za mawasiliano ni yule anayeweza kutamka kile anachotaka kukisema na kukimaanisha kile anachokisema bila kupoteza maana.

Tafakuri za watetezi wa mkakati wa mawasiliano kama wanautambuzi, wanamuwingilano na wanamtaguasno lugha wanasema kwamba mawasiliano yanasaidia sana katika ujifunzaji wa L2. Selinker (1972) alipendekeza dhana ya mkakati wa mawasiliano kuwa mionganini mwa taratibu tano ambazo hushuhulisha mchakato mzima wa mawasiliano. Japo hajataja hizo taratibu, nia ya mkakati huu ni kujifunza lugha na kuitumia katika mazingira ambayo yanahitajika. Jambo ambalo (Faerch na Kasper, 1980; Coder, 1983 Tarone, 1989,) wamekubaliana nalo. Canale na Swain (1980) wameendelea kutoa ufanuzi kwamba mkakati huu unakuza umilisi wa kuwasiliana. Kwa kuongezea mkakati wa mawasiliano umeendelea kuwa stahiki kwa wanafunzi wenyewe umilisi finyu katika L2 ambayo huishia kutumia mkakati wa mawasiliano unaohusisha uhamishaji miundo, tafsiri, na kuchanganya ndimi.

Simiyu na Kavoi (keshatajwa) wanaendelea kusema mawasiliano hutokea katika muktadha maalum; kati ya mtu mmoja au zaidi au kati ya kikundi kimoja au zaidi; kati ya mtu au kikundi au vikundi vya watu wenyewe tajriba na mahusiano mbalimbali. Mahusiano yaliyorejelewa na utafiti huu ni ama kati ya mfanyabiashara na mnunuzi au wafanyabiashara wenyewe.

Mtafiti pia alishuhudia mazungumzo kati wa muuzaji na mnunuzi kwa kutumia mbinu ya uchunzaji kuona namna waliendeleza mawasiliano yao katika mazingira halisi ambapo mpokezano zamu kati yao ulikuisha mawasiliano.

## **Mfano 6.mazungumzo kati ya muuzaji na mnunuzi**

1. Mnz:X      *Umefungua mapema*
2. Muz:Y      *Mi najua basi taingiya subui*
3. Mnz:X      *Umefunguliwa vizuri hata mimi leo nataka kununua vitu mapema*
4. Mnz:M      *(Naye anafikia kwa duka la Muz.X). Afadhalii hapa pamefunguliwa. Habari yako?*
5. Muz:X      *Oh karibu boss! kiketi hii apa kama nangojea bengine kufungua*
6. Mnz:P      *Ni saa tatu na maduka mengi hayajafunguliwa?*

## **Mfano 7 Mazungumzo ya simu (muuzaji anajibu simu)**

*Muz:N (Anapokea simu huku akicheka) hahaha boss  
Bakasitoma bangu banapotea wote  
Oh!! Kweli season mbaya kapisa  
Namna gani utalipia ile mali (Utalipia lini ile mali)  
Aya ngoja mimi nisabue na calculator  
Nilituma muzigo mara mbili .iyo sente kidogo boss*

### **Asili: Data kutokana na uchunzaji (Marchi,2022)**

Mawasiliano hutokea kati ya watu wawili, kundi ama zaidi. Kuna mawasiliano ya ana kwa anana mawasiliano kuitia njia za teknolojia kwa mfano kutumia simu. Mfano wa kwanza wa mawasiliano unaonyesha mawasiliano kati ya wauzaji na wanunuzi. Ni kwamba walikuwa wamefika mapema zaidi na baadhi ya maduka yalikuwa bado hayajafunguliwa. Katika mfano wa pili Muz. N anawasiliana na mnunuzi ambaye yuko mbali naye kufuatilia mzigo ambao alishawahidi kutuma na bado hajalipwa. Huu ujumbe ni kiashiria kwamba mjifunzaji lugha ya Kiswahili amepiga hatua katika ujifunzaji wake (Krashen,1987). Krashen (keshatajwa) anasema kwamba katika kiwango hiki kuna uwezekano wa mjifunzaji L.2 kuweza kujibu maswali katika L.2 wakati wa mawasiliano. Anaweza kutumia sheria za lugha kwa mfumo maalum wa kiasili ambao anaweza kutumia sentensi sahili hadi changamano katika matumizi yake ya kawaida. Gardener (2000) anasema kwamba mjifunzaji lugha anapoonyesha dalili za kufanikiwa huwa amejitahidi kwa kuhusisha motisha changamani ambayo ilimpa ari ya kustahimili hali hiyo.

Kiswahili ni lugha ya Kiafrika inayozungumzwa na watu wengi Afrika Mashariki na hata

kwagineko. Lugha hii hutumiwa kama lugha ya mawasiliano mapana katika takriban maeneo yote ya Afrika Mashariki na kati huku ikiwa na matumizi machache katika sehemu za kusini na kaskazini mwa Afrika (Mukuthuria, 2006; Bwege, 2012 ). Mutembei (2016) anasema kwamba kutokana na mawasiliano baina ya Waafrika kuitia Kiswahili, iwe katika biashara, mwingiliano wa utamaduni, ujenzi wa utambulisho wa Uafrika, leo inaweza kusemwa kuwa watu wameendelea kuwa karibu zaidi. Matumizi ya simu za mkononi, mawasiliano kwa intaneti na matumizi ya vyombo vya habari yamefanya usambazwaji wa Kiswahili uwe rahisi na wepesi zaidi kuliko ilivyokuwa awali.

Mahojiano kati ya mtafiti na watafitiwa yalionyesha kwamba wasailiya waliwekea mkazo namna mawasiliano yalikuwa sehemu pana ya kuwezesha ujifunzaji wa Kiswahili kwa ajili ya biashara. Msailiwa 014 ambaye ana umilisi wa Kiswahili alisema kwamba ,

**M.S 014 aliyekuwa na umilisi katika Kiswahili alisema;**

*Wajua biashara haiwezi kuendelezwa na mtu mnyamavu, hivyo huwa hatuoni aibu kuzungumza Kiswahili na wanunuzi wetu; mahali tunafanya makosa wanatusaidia kutukosoa; kuitia njia hiyo tunafanya fanya mzaha na ujanja ujanja wa kujifunza halafu baadaye unajikuta tu unazungumza.*

Msailiwa 014 alifafanua namna walitumia mkakati wa kimawasiliano katika kutumia Kiswahili ili kufanikisha biashara zao. Hali ya ushirikiano pia iliwezesha wafanyabiashara kutumia sana mkakati wa kimawasiliano: Katika hoteli ya Uhuru mfanyakishaa alionyesha maongezi yake na mteja ambaye alitaka kuhifadhiwa nyama choma wakati bado anafanya shughuli za kununua bidhaa zake. Msailiwa alijaribu kumjibu kwa kuonyesha hali ilivyokuwa. Jibu lake likuwa hivi;

*Haaa! Twasikitika sana kwa sababu ya hatuna mahali au chombo kinachofaa ambayo tungeweza kukuwekea nyama choma kwa muda huo. Lakini wewe ukifika sisi tatafuta njia muzuri ya kuchoma nyama araka araka.*

Msailiwa 014 ni mionganini mwa wajifunzaji lugha ambao wana uwezo wa kumudu muundo na sheria za L.2. Mhimili wa pili wa (Krashen, 1987) unajibu swali la lini Mjifunzaji lugha hukuza umilisi na kwa muda ngani ambapo jibu ni kwamba mjifunzaji ambaye yuko katika kiwango cha  $i$  anastahili kupata dhana mpya ambayo ni kiwango cha  $i+1$ . Kwamba tunafanikiwa katika L.2 kama tunaelielewa lugha hiyo ambayo iko na muundo changamani. Kuelewa lugha kuna maana kwamba tunaweza kuisikia, kuisoma na kuiandika. Hoja za Krashen (keshatajwa) zimeshadidiwa na modeli ya elimu ya Gardener (2000) kwamba

binadamu wana namna tofauti tofauti ya kuchakata data na kila mmoja yuko huru na uwezo fulani katika kipawa kimojawapo. Kipawa kinaweza kuwa cha kimamatshi ama kiisimu namna tumeona katika Msailiwa 014.

**M.S 053 alisema kwamba;**

*Bbwooba tomanyi enim ezi suuka munimi bili tosobola kukola obusuubuzi wano mkampala. Atte tetuli na budee obwo kugeenda mukibiina okusoma oluswaili. Nze njogera na abasubuuzi kuva Kenya ne Tanzania obba na bano abanaffe abamanyi oluswaili. Byokubba mbogo walioobukodyo bwokola tugeze nga akamwenyumwenyu nga tolina kyoyogeede, okukwatamukoku muuka nga towangaade mukogeera awo nga ofunna obuyambi. Bwetutyo bwe tukoola .Mpola mpola tusaba obuyambi mukyama.*

Usipojua zaidi ya lugha mbili huwezi kufanya biashara hapa Kampala; Tena hatuna muda wa kuenda darasani kujifunza Kiswahili. Mimi huwa nazungumza tu na wale wanunuzi kutoka Kenya ama Tanzania ama na hawa wenzetu ambao wanakijua Kiswahili; Ukipiga mbogo, unatoa ishara fulani kwa mfano kutoa machoya tabasamu bila kusema kitu, kupumua kidogo bila kuendelea na mazungumzo halafu unapata usaidizi; hivyo ndivyo tunavyojifunza; Kwamba mfumo uliotumiwa ni mfumo wa kuomba msaada kisirisiri.(TY)

Kwa vile hawatambui kwamba wanatumia mkakati, wao wanafikiri kwamba ni hatua tu ya kawaida ya matumizi ya Kiswahili katika biashara. Griffiths (2004), Myles na Mitchel (2004), wanakubaliana kwamba katika mazungumzo mikakati mwafaka wa kuzungumza L2 ni kutumia visawe au maelezo ya kufaa. Griffiths (keshatajwa) anaendelea kusema kwamba wakati wa kujifunza L2, licha kuwa mawasiliano huchukua mkondo mkubwa hali ya ujifunzaji ni ya kawaida kuliko ujifunzaji wa mfumo wa sarufi, ujumbe kupitia muziki au sanaa na hulka za mjifunzaji lazima huwa zilichangia katika mawasiliano ya lugha lengwa. Hoja hii tayari imeshughulikiwa katika muhimili wa tatu na nne wa Gardener (2000).

**4.3.1.6 Mitagusano ya ukuruba kati ya wanunuzi na wauzaji**

Wasailiwa kumi na saba (17/103) ambao ni asilimia kumi na saba (17%) ya wasailiwa walisema kwamba kutagusana kati yao na wanunuzi kuliwezesha ujifunzaji wa Kiswahili kwa ajili ya kuendeleza biashara. Namna walikuwa wakitumia mkakati huu ni kwamba walikuwa wakijaribu kuzungumza na wazawa wa lugha ya Kiswahili katika mazingira wanamofanya kazi. Kwamba wanapajaribu kujifunza lugha ya Kiswahili hujaribu kuigiza uzungumzaji wa wafanyabiashara wenzao katika Ekedo na hata wanuuzi ambao wanatoka nje ya Uganda hasa Kenya, Tanzania na Kongo.

Wasailiwa walitaja kwamba walijitahidi kuzungumza na wazawa wa lugha ya Kiswahili na kupeleleza tamaduni na kanuni za jamii ya lugha ya waswahili kutoka hizo sehemu tofauti.

Waliendeala kusema kwamba wanapojaribu kutumia Kiswahili, hujaribu kuigiza uzungumzaji wa wazaliwa wa lugha ya Kiswahili, tabia na desturi na mila zao. Kutohana na hojaji kuna wale ambao walitaja maneno wayolijifunza wakati wa kipindi fulani cha siasa. Maneno hayo yalikuwa kama; *fungua mlango, toa pesa, nataka nini, naenda wapi*. Hata kama kipindi hicho kiliwafanya kuwa na picha mbaya ya matumizi ya Kiswahili na kukichukia kila mmoja ambaye ama alijihusisha au kuzungumza lugha ya Kiswahili, kuna msamiati ambao walichota ambao kwa sasa unawasaidia kuendeleza biashara zao.

Mjadala kutohana na mahojiano kati ya mtafiti na wasailiwa kumi na watatu (13) ambao walitaja kwamba kutagusana kuliwasaidia katika ujifunzaji wa Kiswahili kama lugha ya biashara.

#### **M.S 036. Katika Ekedi ya Simlaw alisema;**

*Apa katika ii Ekedi ya Simlaw iko wafanyabiashara wengi wanatoka Kenya, Tanzania, Kongo amba ni marafiki wetu na banatufundisa luswaili muzuri sana. Banasema apana penda sana misumari ya Uganda alafu naambiya wao ata iko nyininge muzuri .*

Alichomaanisha msailiwa 036 ni kwamba kuna wafanyabiashara ambao wanatoka Kenya, Tanzania na Kongo amba ni marafiki zao na wanakiswahili kizuri. Hivyo hubeza na kuwaambia kwamba misumari ambayo inatengenezwa nchini Uganda si mizuri. Halafu anamjibu mnunuzi kwamba kuna mingine mizuri. Wanafanya hivi ili wanunuzi wakifika wapate misumari tofauti tofauti kulingana na kampuni na bei ya kila kampuni.

#### **M.S 005 kutoka Ekedi ya Mukwano alisema;**

*Hawa kina mama kutoka Kongo bakija kununuwa nguwo bao banatumia Swahili. Hii ya Tanzania inakuwa ngumu kabisa hata unawambia translate kidogo kesho kama banarudi sisi natumia ile balitumia. Batu ba Kongo iko na bitenge muzuri muzuri na ndiyo banaleta halafu mimi nasaplaya hapa Kampala.*

Huyu mfanyabiashara alikuwa ameathirika na Kiswahili cha Kongo. Ni kana kwamba kwa muda mrefu amekuwa akijishughulisha sana na kuwauzia wakongo nguo mpya hasa za kina mama. Kwa ajili ya kutangamana na wazungumzaji wa Kiswahili kutoka Kongo kwa ajili ya

biashara na mazingira tulivu yaliwafanya wapate motisha wa kutumia Kiswahili katika kufanikisha biashara. Ehram na Oxfrod (1990) pamoja na Kiango (2002) wanasema kwamba kiwango cha juu cha kujumuika na watu wengi wa lugha mbalimbali husababisha kuteuliwa kwa lugha moja ambayo itawezesha mawasiliano. Gardener (2000) katika mhimili wake wa pili anasema kwamba nia ya mtu kujifunza huchangia katika kuimarisha motisha changamani ambayo inampa fursa ya kuchagua nini cha kujifunza na ni katika jumuiya ipi mjifunzaji anataka kujifunza lugha yake. Vile vile Krashen (1987) na Gardener (2000) wanasema kwamba almradi mjifunzaji ameonyesha uwezo wa kumudu L2, ina maana kwamba atajifunza mila na desturi za utamaduni waliochagua kujifunza na kuitumia. Utafiti wetu pamoja na maelezo ya wataalamu unakubaliana na Minti (2012) ambaye alifanya utafiti wake wa maingiliano kati ya Wasomali na Waigembe kwamba ushirikishaji wa wahusika katika shughuli moja huwepa uwezekano wa kutumia lugha moja.

#### **M.S 068: kutoka ekedi ya Mukwano alisema**

*Kabla sijaanza biashara hapa Mukwano tulikuwa na duka kubwa ya godoro huko Iganga ninako zaliwa. Tulipata watu mingi walikuwa wanazungumza Kiswahili. Iganga iko na watu mingi wanajua Kiswaili tena wengi kutoka Tanzania na Kenya. Nilipata pesa na kufungua duka ii ya mafuta hapa Mukawano. Niko na wakasitoma wangu wanakuja kununua mafuta ama wakinituma mimi napeleka. Iko duka ya rafiki yangu huko Westlands huko Kenya mimi napelekeea yeye mafuta ya warembo.*

#### **M.S 092**

*Ffe abasubuuzi muziakedi tulina ebibiina byaffe ate tukoleera wamu. Okwogerezana kutwala ekyifa kya agullu enyo lwekyo bwetuba twogerezaganaya nadalla nabo abamanyi oluswaili tufunna ebigambo ebyo oluswaili ebituyaamba naffe bwetuba mu luswaili. Wali ngatuli mukuuliliziganya na abasuubuzi , okwogera fe ku fee, okukayana kwetubeeramu tufuna ebigaambao abituyamba kukozesa mukukola obusuubuzi.*

Sisi wafanyabiashara katika hizi Ekedи tuna vyama vyetu na tunashirikiana sana. Mawasiliano huchukua nafasi kubwa mno hivyo, wakati wa kuwasiliana hasa na wanaojua Kiswahili tunapata msamiati mipya ambayo inatuwezesha kuwasiliana katika Kiswahili. Pale kwenye mapatano na wanunuzi, dialojia kwetu sisi kwa sisi, ubishi unatufanya tunapata matamshi ambayo yanatusaidia kufanya biashara.(TY)

Ilibainika kwamba hali hii humwezesha mfanyabiashara kuwa na ukakamavu wakati anapozungumza, kuimarisha matamshi bora na kumtayarisha kuwa mzungumzaji mzuri wa lugha ya Kiswahili kibiashara. Ubishi waliorejelea katika utafiti huu haukuwa wa malumbano ila uwezo wa kumshawishi mnunuzi anunue bidhaa zao.

Utafiti pia uligundua kwamba wasailiwa ambao walikuwa wamelelewa katika kambi za askari polisi na jeshi, kutangamana na Wachotara na Wanubi pamoja na Wasomali na makabila mengine ambayo wakaazi walikuwa wakitumia Kiswahili kuliwasaidia kupata umilisi wa kutumia Kiswahili. Ni kwa ajili yakuwa na tajriba hiyo ndiyo iliwasaidia kutumia umilisi walioupata kupitia utangamano wao uliowasaidia kujifunza Kiswahili na kuendelea nacho katika kufanya bishara. Mchakato wa utagusanaji na muingiliano ni hoja ambayo Krashen (1987) amesema kwamba huchangia katika uamiliasi katika L2 ambapo ingizo tambuzi ndilo sehemu muhimu ya ujifunzaji L2. Gardener (2000) ambaye katika mhimili yake hasa wa tatu wa motisha changamani unaowezesha ujifunzaji L2 na uwezo wa kuwa na kipawa cha mtagusano na walengwa wa L2. Gardener (keshatajwa) anasema kwamba mtagusano na ujifunzaji L2 siyo kwamba lazima vitokee kwa wakati mmoja maana kuna yule ambaye anaweza kutagusana na wazungumzaji wa L2 na wala asijufunze lugha yao. Hivyo amesisitiza kwamba ili mjifunzaji kujifunza L2 kupitia mtagusano lazima awe na ari ambayo ilimsukuma kujifunza lugha hiyo.

#### **4.3.1.7 Matumizi ya Teknolojia**

Matokeo ya hojaji yalionyesha kwamba wafanyabiashara kumi (10/103) ambao ni asilimia tisa (09%) ya wasailiwa walitumia sana vyombo vyta teknolojia kujifunza Kiswahili kibiashara. Vyombo vilivyotajwa kutumika kutokana na umaratokezi wa majibu ya hojaji ni pamoja na runinga, tarakilishi, mitandao ya kijamii ya *whatsApp*, *Youtube*, *Facebook*, rununu na kanda za video tofauti tofauti. Kupitia kipindi cha ‘jifunze Kiswahili na jicho la vijana’ katika runinga ya UBC (Uganda Broadcasting Coporation) wameweza kujifunza maneno ya Kiswahili kwa ajili ya mawasiliano na msamiati katika Kiswahili. Waliweza kutaja baadhi ya msamiati ambao wanatumia kuendeleza biashara kwa jumla kama; bima, rahani, kodi, pesa, bei kali, uchumi, kuuza, ushuru, faida, losi nk. Ujifunzaji kwa kupitia teknolojia ni mkakati ambao ultajwa na wasailiwa katika kujibu swali la kutaja mikakati mingine ambayo walikuwa wakitumia kujifunza Kiswahili kama lugha ya biashara ambayo haikuwa kwenye orodha ya mtafiti. Hoja ambayo Krashen (1987) katika mhimili wake wa pili anasema kwamba mwanafunzi ambaye katika mazingira halisi alionyesha kiwango kidogo cha ujifunzaji anaweza kuimarika kidogo katika kujifunza msamiati wa lugha lengwa katika mazingira halisi. Hoja ambayo imepingwa na Reid (1998) ambaye amependekeza kwamba ujifunzaji sio lazima utokee katika mazingira halisi ila mjifunzaji anaweza kujitafutia njia ambazo zinaweza kurahisisha ujifunzaji wa lugha lengwa. Gardener

(Keshatajwa) naye amekubaliana na Reid (keshatajwa) kwa kusema kwamba wajifunzaji huwa na uwezo tofauti tofauti wa ujifunzaji. Kuna wale walio na kipawa cha muziki; kucheza na kuimba, kipawa cha mazingira halisi; kuona na kutenda na kipawa cha kutazama ambapo vipawa hivi huweka msingi thabiti wa kujifunzia kutegemea nyenzo ambazo mjifunzaji L.2 huamua kutumia.

Herman (2015) na Montana wanasema kwamba matumizi ya teknolojia katika ulimwengu wa sasa ni dhihirisho la maendeleo hasa katika uwanja wa mawasiliano jambo ambalo lina rahisisha utekelezaji na uendeshaji wa sehemu nyingine za maendeleo kama vile uendeshaji biashara, ushiriki wa kisiasa, kutagusana kwa wanunuzi na wauzaji na kiuchumi. Simu za mkononi nazo zilitumika kwa kiasi kikubwa kutafsiri baadhi ya maneno kutoka Kiingereza hadi Kiswahili ili kurahisisha mawasiliano. Wakati wa kutumia tafsiri, kulibainika kuwepo kwa ukopaji ambapo anasema ndiyo njia iliyobora zaidi kwani kuna kukopa maneno kutoka lugha asilia hadi lugha lengwa. Herman (2015) anasema kwamba tafsiri inaweza kuwa na matokeo kadhaa, kwanza kusharabu bila kubadili maumbo na maana, ukopaji kwa kubadili maumbo lakini kudumisha maana ama ukopaji ambapo sehemu moja ya istilahi ni asilia na nyingine imesharabiwa nayo maana ikawa yote imekopwa.

Dhana ya tafsiri katika muktadha wa utafiti huu iliingiliana katika mikakati tofauti tofauti. Tafsiri imetumika kama njia moja ambayo inaweza kusaidia katika ujifunzaji wa Kiswahili katika muktadha wa biashara. Wafanyabiashara wengi wamekuwa wakitumia simu za mikono kutembelea *google*, *Youtube* na mitandao mingine ya kijamii kufanikisha matumizi ya Kiswahili katika biashara. Aidha, wasailiwa walitumia teknolojia kutafuta msamiati kutoka kamusi ya mtandaoni ili kupata neno mwafaka la kutumia. Vile vile walitumia teknolojia kuzuru madhara ya *Youtube*. Katika *Youtube* kuna programu za kujifunza Kiswahili kwa namna ya kuzungumza kutegemea muda husika kwa dakika moja, mbili , tatu, na kadhalika.

Wakati wa mahojiano, wafanyabiashara ishirini (20) kutoka sehemu tatu ambazo zilishughulikiwa katika utafiti yalionyesha kwamba kuwepo kwa teknolojia kuliwapatia motisha wa kujifunza Kiswahili kwa wakati wao na mahali popote almaradi walikua na simu za mkononi. Hoja zao ukiziunganisha na zile za hojaji utakuta kwamba zina ama fanana au kukaribiana. Nao walikiri kwamba programu za *Youtube*, *Facebook*, *Twitter*, *Instagram* na *Google* zimewasaidia kujifunza Kiswahili ili kuwasiliana kwa ufasaha. Wafanyabiashara 079, 083,095 na 116 walisema kwamba walifuatilia sana mafunzo ya *swahilipod*

101.com.www, swahiliclass.co.tz na learn Swahili business. Mafunzo ambayo yanatolewa na ama mwalimu Medina au Mwalimu Saayi Michael ambao huwa wanafundisha namna ya kutamka Kiswahili na kutunga sentensi fupifupi. Mifano ya data iliyotokana na mahojiano ya kutumia teknolojia kujifunza Kiswahili ni kama ifuatavyo:

### Mfano ya data 8. Kujifunza salamu mtandaoni

<i>Habari</i>	<i>-Hello</i>
<i>Habari ya asubuhi</i>	<i>Good morning?</i>
<i>Habari ya leo-</i>	<i>How is your day today</i>
<i>Habari ya mchana</i>	<i>Good afternoon?</i>
<i>Uko mzima</i>	<i>-are you well</i>

**Asili:** *Data kutoka nyanjani za mahojiano (Machi, 2022)*

### Mfano ya data 9: Salamu kutokana na wimbo

<i>Jambo!</i>	<i>Jambo bwana</i>
<i>Habari gani nzuri</i>	
<i>sana</i>	<i>Wageni</i>
<i>mwakaribishwa</i>	
<i>Kenya yetu hakuna</i>	
<i>matata</i>	

**Asili:** *Data nyanjani kutokana na mahojiano (Machi, 2022)*

Salamu ni moja wapo ya sehemu ya kujenga uhusiano mionganini mwa watu wanaotaka kuwasiliana. Siyo kila mtu ataaelewa tofauti kati ya muda wa salamu kama siyo mzungumzaji wa lugha hiyo. Shughuli ya biashara ni ya kila siku na kila wakati ambapo tunatarajia wafanyabiashara kujifunza moja kwa moja kupitia shughuli zao. Hata hivyo huwa kuna wakati wa uhaba na wakati biashara zinapamba moto (*dry and peak business times*). Karne hii ya ishirini na moja, unapozungumzia biashara huwezi kuwacha kuihusisha na TEHAMA. Kwa hiyoilibainika kwamba wafanyabiashara walitumia fursa ya uhaba wa wanunuzi kutumia mitandao ya kijamii kujifunza msamiati tofauti tofauti wa Kiswahili kama inavyoonyeshwa katika mfano wa data 10;

### Mfano ya data 10: Msamiati kuhusu usafi na vyakula.

<i>Kujitolea</i>	<i>-to volunteer</i>
<i>Napenda kujitolea</i>	<i>-I like to volunteer</i>
<i>Kinga</i>	<i>-to protect</i>
<i>Kutumia tena</i>	<i>-to re use</i>

<i>Kuhifadhi</i>	-to conserve
<i>Punguza uchafu</i>	-to reduce trash
<i>Enda ulaya</i>	-to travel abroad-am going abroad
<i>Kupimzika katika bichi-to relax at the beach</i>	-I like to relax at the beach
<i>Kujifunza kupika chakula cha Kenya</i>	-to learn how to cook Kenyan food
<i>Kuandaa nyama choma</i>	- to have a barbecue

### **Asili: Data kutokana na hojaji na mahojiano (Machi, 2022)**

Kulingana na data ya 10, ni bayana kwamba kuna msamiati ambao uliwasaidia waliokuwa katika sehemu ya hoteli. Kuna msamiati wa vyakula kutoka nchini Kenya na namna ya kuhifadhi usafi. Uganda, nyama choma hutambulisha Mkenya. Hivyo wanaoendesha biashara za hoteli ambao walipatikana sehemu za Mukwano na Kikuubo wanapotagusana na wanunuzi kutoka Kenya wanajua tu wataitisha nyama choma, samaki kaanga kwa ugali. Hii inawapatia motisha wafanyabiashara kutambua kwamba biashara wanayoifanya ni yenye kunufaisha.


Gardner (2000, 2010b) na Ellis (2003) wanaeleza kuwa mwanafunzi akionyesha uwezo wa kujifunza ambao unatokana na motisha na mwelekeo huwa hahitaji tena kwenda darasani ili ajifunze lugha lengwa. Wana uwezo wa kujifunza na kutumia Kiswahili katika sehemu zao za kazi ama mahali ambapo watajichagulia wao wenyewe. Kuna wengine waliopakua APP ujifunzaji wa kimtandao ya (*CALL-Computer-Assisted Language Learning*) ambayo inafundisha lugha kuititia mitandao ya kielektroniki. Mitandao hii humsaidia mjifunzaji L2 kujifunza lugha yoyote pasi kuwa na mwalimu na kutumia ujifunzaji huo kutumia lugha katika mazingira yanayostahili. Kwa wale waliokuwa na tajriba ya mitandao ya kielektroniki waliweza hata kusaidika pale ambapo wanakumbwa na matatizo ya kutamka. Waliendela kusema, kuna televisheni nyingi ambazo zina vipindi vya Kiswahili mkiwemo; Citizen, Maisha Magic, NTV-Kenya, KTN, TBC, AZAM na UBC ambavyo hutumia Kiswahili. Hivyo, kipindi cha mapumziko, wao huweza kufuutilia baadhi ya vipindi katika Kiswahili na kujifunza namna wanavyozungumza. Hali hii iliwasaidia kujifunza Kiswahili kwa wakati wao wenyewe. Hivyo inawawezesha kujua namna ya kujitambulisha, kusalimia na kutumia maneno machache ya Kiswahili kwa ajili ya mawasiliano.

#### **4.3.1.8 Mkakati wa Mpango binafsi**

Wasailiwa watano (05/103) ambao waliwakilisha asilimia nne nukta nane (4.8 %) kutokana na hojaji walikiri kutumia mpango binafsi katika ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili kwa ajili ya biashara. Walisema kwamba hawakuhitaji Kiswahili kingi sana. Hivyo walipanga ni kwa jinsi gani watakavyojifunza na kwa njia ambayo ilikua rahisi kwao kutumia. Hivyo njia

iliyokuwa rahisi kwao ni kujipangia wao wenyewe ujifunzaji wa Kiswahili.

Kutokana na mahojiano kati ya mtafiti na watafitiwa, wafanyabiashara kumi na watano nao walikiri kamba walijipangia namna walivyofanikisha biashara zao kwa kutumia Kiswahili. Walieleza namna walivyokuwa wakitumia mpango binafsi hasa wakati wa kuhusisha lugha chasili na lugha ya Kiswahili. Mfanyabiashara 016 alikuwa na maneno ambayo yalikuwa yameandikwa katika daftari. Maneno hayo aliyaandika katika L.1 halafu hapo hapo aka tafsiri maneno hayo katika Kiswahili namna aya kuyatumia akiwa na mteja wake anayekuwa kununua bidhaa. Huu hapa chini ni mfano wa data kuonyesha namna wafanyabiashara wanaanza kwa kupanga mawazo kuititia lugha chanzi na kuyahawilisha katika lugha lengwa.



#### **Muchoro 4.1: Kupanga maneno kutoka Kiganda hadi Kiswahili**

**Asili:** *Data kutokana na mahojiano .(Machi, 2022)*

Huu ni mfano wa data ambayo msailiwa alitupa kuonyesha namna anavyoanza na kupanga anachokihitaji kwa kutumia lugha chanzi halafu anayanukuu katika Kiswahili. Huyu ni mfanyabiashara jijini Kampala ambaye anashughulikia uuzaji wa simu. Purpura (1999) anasema kwamba kuititia mpango binafsi wakati mwingine mwanafunzi huenda akaandika maneno katika vijikaratasi ambavyo atarejelea wakati anapotaka kuvitumia au sivyo kuandika maneno machache mkononi mwake ili iwe rahisi kwake kuyatumia. Gardener (2000) anasema kwamba kila mjifunzaji L.2 huwa ana uwezo wa kujifunza lugha ila uwezo huo ndio unaokuwa tofauti. Kwa mfano huo mfano wa 11 unaonyesha kwamba mjifunzaji ana uwezo wa kipawa cha kuandika na ukokotozi. Picha hiyo ilichukuliwa wakati wa kukusanya data kuonyesha namna wasailiwa walivyokuwa wakitumia mpango binafsi kushirikisha biashara zao katika lugha ya Kiswahili. Wengi wao walipatikana na vijikaratasi kama hivyo ambavyo walisema kwamba waliandika baadhi ya msamiati kulingana na mahitaji ya wanunuzi kwa ajili ya kuwasiliana nao. Mfanyabiashara 028 alikuwa na orodha

ya maneno ambayo alikuwa ameandika miongoni mwa yale aliyokuwa akijifunza huku akiwa anapata muda wa kujifunza.

### **Mfano.12 ujizoeshaji na msamiati tofauti tofauti**

<b>Lugha asilia</b>	<b>Kiswahili</b>
<i>Ssente ze emaanja</i>	<i>Pesa mimi nadai</i>
<i>Omwaka guno</i>	<i>Mwaka ii</i>
<i>Kyange</i>	<i>Kyangu</i>
<i>Olulimi</i>	<i>Luga</i>
<i>Wandiika wano</i>	<i>Wandiika apa</i>
<i>Tutuunda</i>	<i>Tunawuza</i>
<i>Bino biluungi</i>	<i>Ii muzuri</i>

**Asili:** *Data kutokana na mahojiano nyanjani (Machi,2022)*

Walisema kwamba kuna wanunuzi ambao hutuma ujumbe kwa simu kuagizia bidhaa wanazotaka. Kwa kupokezana mawasiliano iliwabidi wawe na mpangilio wa maneno ambayo walitumia kuwasiliana na wanunuzi wa bidhaa zao. Uwekaji wa kumbukumbu kama hizi mara mara uliwasaidia wasailiwa kuwa na kumbukumbu ambazo walirejelea kila wakati walitaka kutumia lugha ya Kiswahili au wakati wowote wa matumizi ya lugha ya Kiswahili kibiashara. Katika mpango binafsi vile vile mtumiaji lugha hujifanyia mipango yake na kufuatilia yale ambayo amejifunza. Hupanga yepi yatatangulia (Gardener, 2000: 2010b: Montano, 2017) na yepi ya kufuatia. Ufanisi wa mpango binafsi ni pale ambapo mjifunzaji lugha anakuwa na mwelekeo chanya na kujifanyia mambo yake mwenyewe. Kwa wale ambao walipata mafunzo ya Kiswahili kuititia KACITA walidai kuwa, Kwa sababu ya ukosefu wa muda wa kutosha wa kupata mafunzo hayo na kila mara madarasa yalikuwa makubwa, iliwabidi wajipange namna watakavyokuwa wakihudhuria mafunzo kulingana na mada ambazo zingeliwasaidia kujifunza Kiswahili kibiashara. Wanafunzi wa L2 hutumia ufasaha wa L1 kujifunza (Griffths, 2003). Huwa inakuwa rahisi mwanafunzi kuunda sentensi fupi fupi za Kiswahili kwa kurejelea msingi wa L1. Kwa wale waliokiri kutumia njia hii walisema kwamba iliwasaidia sana katika kujijengea msamiati wa Kiswahili kibiashara kutumia L1 kama inavoonyeshwa katika jedwali 4.13.

#### **Jedwali 4.13: Matumizi ya mpango binafsi katika sentensi**

<b>Kiganda</b>	<b>Kinyakole</b>	<b>Kiswahili</b>
<i>Jesca yateka ebitoche Nttunda engoye</i>	<i>Jesca afumbye amatooke za Ninguza ngeyo za Bakyalala</i>	<i>Jeska amepika matooke Nauza nguo za</i>
<i>Abakyalla</i>		<i>Wanawake</i>
<i>Nja kukusindikira ssente</i>	<i>Nikueindikira sente</i>	<i>Nitakutumia pesa</i>
<i>Olin ne banja lyange</i>	<i>Olina ibanja lyawe</i>	<i>Uko na deni langu</i>
<i>Mwana tetwakoze ssente</i>	<i>Mwana titwakozire sente</i>	<i>Bwana hatujafanya pesa</i>
<i>Edoola ebuzze</i>	<i>Doola yabuzire</i>	<i>Dola imepotea</i>
<i>Ebinti byalinye beyi</i>	<i>Bintu byalinya beyi</i>	<i>Vitu vimepanda bei</i>

**Asili : Data ya nyanjani kutokana na mahojiano, Machi 2022**

Utafiti uligundua kwamba muundo wa baadhi ya lugha za Kibantu nchini Uganda ulifanana na ule wa Kiswahili. Hivyo ilikuwa ni rahisi kwa wafanyabiashara kutumia Kiswahili kibiashara. Krashen (1987) anasema ujifunzaji wa L2 ni mchakato wa ufahima ambapo mjifunzaji lugha anajifunza miundo na maumbo ya lugha kama vile matamshi, msamiati, sarufi na sheria zote za matumizi ya lugha mahsusni akijua ya kwamba anajifunza lugha hiyo anapojifunza L1 na L2. Haya maelezo yalisadifu ya utafiti huu kwamba lugha chanzi ina mchango mkubwa kufanikisha mpango binafsi wakati wa kutumia Kiswahili kibiashara. Lugha (Fromkin na Rodman, 1993; Wanzira, 2002) kama ulivyo katika ujifunzaji wa L1 husaidia katika ujifunzaji wa L2 (Chomsky 1988) anasema kwamba lazima ieleweke kwamba kila mjifunzaji lugha huwa ana yale anayoyajua na huenda asijitambue kwamba kuna dhana anazozitambua. Hicho kipawa kinamsaidia kupata msamiati wa kutumia bila utata wowote na kiwango cha kisintaksia ndicho kiini cha kuwezesha kuwepo mawasiliano. Hoja zilizotolewa pamoja na utafiti wetu unaafikiana na Gardener (2000) ambaye anasema kwamba kiwango cha uwezo wa mwanafunzi katika ujifunzaji wa L2 hufanikishwa na kiwango cha motisha alichonacho kilichomfanya apate ushawishi wa kujifunza lugha hiyo. Mawasiliano yanayorejelewa ni namna mfanyabiashara na mnunuzi hutumia lugha kimapatano wakati wa biashara.

#### **4.3.1.9 Utambuzi**

Mkakati wa utambuzi huchukua nafasi kubwa sana katika uelewaji wa yaliyomo katika lugha lengwa. Utambuzi unampa mjifunzaji L2 uwezo wa kutafakari, kuhamisha ujumbe, kusoma na kuandika maneno kadhaa na hata ikiwezekana kufanya ufupisho.

Matokeo ya hojaji yalionyesha kwamba wafanyabiashara sita (03/103) waliokuwa na sifa za kiutambuzi walitumia vifaa mbalimbali ambavyo viliwawezesha kujifunza Kiswahili kwaajili ya biashara. Wanafunzi hawa huwa wanasisa za utayari wa kujifunza na husukumwa

na motisha ya hali ya juu. Hili limekubalika na Oxford (1990), Skehan (1991) Gardener (2000) na Schmitt (2010). Kwamba uwezo wa kuandika (Gardener,2000) ni mojawapo wa vipawa mjifunzaji lugha huwa amesheheni katika ujifunzaji L.2. Hata hivyo mjadala wa mahojiano kati ya mtafitiwa na watafitiwa wanne ambao walijibu swali la jinsi wanatumia mkakati waliochagua kujifunza Kiswahili kibiashara, walipendelea mkakati wa utambuzi. kwamba mkakati huwawezesha kujaribu kuchanganua nyenzo za lugha kupitia kuwaza, kutafakari, kufanya muhtasari sahihi, kuorodhesha na kupanga ujumbe ili kuibuka na msamiati ambao uliwasaidia kujifunza Kiswahili kibiashara. Hawa ni wale wafanyabiashara ambao walikuwa wamepata kidogo mafunzo ya awali ya Kiswahili kupitia KACITA. Walihusisha ujifunzaji wao na namna walijifunza lugha zao asili. Mkakati huu uliwasaidia kupanga vizuri sheria za lugha ya Kiswahili ili kuwarahisishia uelewaji wao katika kujifunza na kutumia Kiswahili kibiashara.

### **Mfano 13: Kuhawilisha sentensi kutoka lugha asili hadi Kiswahili.**

<b>Kiganda</b>	<b>Kiswahili</b>
<i>Onno yabbye sente zaafe</i>	<i>Uyu anaiba pesa yetu</i>
<i>Jjuuzi namulabye wano</i>	<i>Juzi nilimuona apa</i>
<i>Agamba nti</i>	<i>Anasema ati</i>
<i>Kitegeeza oyaggala kyakulya</i>	<i>Kinamaanisa onataka kyakula</i>
<i>Omusuubuzi azze</i>	<i>Muchuuzi nakuja</i>
<i>Ssindika sente kusimu enno</i>	<i>Sindika pesa kwa ii simu</i>
<i>Tujja</i>	<i>Kuja</i>

**Asili:***Data kutokana na mahojiano nyanjani (Machi,2022)*

Tunaona kwamba kuna kanuni za kisintaksia ambazo zinatokea katika lugha asili ndizo hizo hizo zinabainika katika lugha ya Kiswahili. Pia kuna maneno ambayo yanatokana na kudondosha sauti ya awali ya L.1 na kuchopeka sauti ya Kiswahili kama katika /tujja/na /kuja/. Udondoshaji ama uchopekaji ni sehemu mojawapo ya hatua za ujifunzaji L.2. Krashen (1987) anasema mwanafunzi ambaye ameonyesha uwezo wa kuongea katika L.2 mara nyingi kuna makosa ambayo hujitokeza katika kudondosha baadhi ya sauti, kuongeza sauti ama kuchanganya nyakati. Anasema kwamba anavyojizoesha na msamiati mpya katika L.2 ndivyo makosa nayo hupungua. Bachman (1990) anasema wajifunzaji lugha wa aina hii huruka mambo mengine au kuyarahisisha zaidi mradi tu waendeleze mazungumzo au wawasilishe ujumbe waliokusudia. Mazungumzo haya huwa ni watu wa kawaida ama wale wanatarajia kuijendeleza katika ujifunzaji wa lugha lengwa. Cohen na Olshtam (1993)

wamelipigia upatu kwa kusema kwamba wanafunzi hawa hutamka msamiati kiholela mradi tu unajitokeza katika lugha lengwa na sentensi za kisarufi bia bila mpangilio kamili.

Vile vile kwa kushirikisha uchunzaji katika mazingira ambamo biashara ziliendelezwa, mtafiti alishuhudia maongezi kati ya wafanyabiashara ambao hata wao wenyewe hawakujua kwamba mkakati waliotumia ulikuwa ni wa utambuzi namna inavyobainika katika data ifuatayo;

#### **Mfano 14: Kusoma matini za Kiswahili**

1. *Muz:J (anaongea na muuzaji mwenzake). Gwe kanyankole mpa akatabu kaange*
2. *Muz:Z Wabula okaagala akatabo ako. (Unapenda hako kakitabu)*
3. *Muz:J Nawe tekakuyaambye (Kwani na wewe hakajakusaidia?)*
4. *Muz:Z Nzija kuguula akaange mwana (Nitanunua kangu yakhe)*
5. *Muz:J Kalimo obugambogambo obulungi obwo luswaili (kuna maneno mazuri ya Kiswahili)*

#### **Asili: Data kutokan na uchunzaji (Machi, 2022)**

Ukiona mtu anatajriba ya kusoma kitu, basi aliwahi kupitia mfumo halisi wa ujifunzaji. (Krashen,1987). Muz. J ana kitabu ambacho Muz. Z amechukua na kukipitia. kitabu hicho kina maneno ya Kiswahili ambayo yamewafurahisha na wanaendelea kujifunza. Kuna matini ndogo ndogo amazo huuzwa jijini Kampala ambazo zilizotafsiriwa kutoka Kiganda hadi Kiswahili. Wafanyabiashara wanaojua kusoma huzitumia sana.

#### **Mfano 14. Kujistahi**

1. *Muz:S Karibu! Karibu.....*
2. *Mun:H Habari yako!*
3. *Muz:S Pole safari....*
4. *Mun:K Mkahawa uko wapi .Njaa yatuuma*
5. *Muz: Oh !we nataka kahawa tanunua tu kwa duka.*
6. *Wanuz:H na K (Kwa pamoja) twataka mahali pa kunywa chai.*
7. *Muz:S (Anacheke) taonyesha wewe.*

#### **Asili: Data kutokana na uchunzaji (Machi, 2022)**

Muz: S anawasiliana na wanunuzi H na K. Ni kana kwamba wana mazoea. Wanataka kuelekezwa mahali pa kupata chai. Muz: S hatambui kwamba aliulizwa mkahawa kama

mahali pa kupata kiamsha kinywa alifikiri wanunuzi walitaka kununua kahawa. Kwa vile anajiamini anaficha kutofahamu kwake kwa kucheka halafu anakubali kuwasaidia. Coopersmith (1969) anafasili kujiamini kama uamuzi mjifunzaji lugha hufikia kupima nafasi yake katika lugha anayojifunza kutegemea mwelekeo (Garderner, 2000) alionao katika lugha tumizi. Kwa kuongezea Cook (2001) anasema kwamba kujiamini kunajengea ukubalifu wa kuwasiliana kikamilifu katika lugha lengwa. Ule ukakamavu na uwezo wa kuongea katika lugha hupatikana kutokana na kujiamini. Uwezo wa kujiamni vile vile unafanya mtu kila mara kuzingatia namna anawasiliana na wengine. Mara nyingi hapendi kuona kwamba amekosea kwa kile alitaka kuwasilisha.

#### **4.3.1.10 Mkakati wa urejeleaji**

Matokeo ya hojaji yalionyesha kwamba wafanyabiashara wawili (02/103) ndio walichagua mkakati wa upatikanaji tena. Hata hivyo kuitia dodoso wafanyabiashara nane walikiri kushirikisha mkakati wa urejeshaji katika kutumia Kiswahili kibashara. Huu ni mkakati ambao kwa kufahamu au kutofahamu hufanya wanafunzi wa L2 wasionekane kama hawaelewi lugha wanayoizungumza. Kutokana na mazungumzo na mfanyabiashara 148 alisema wana namna wanatumia lugha kuwateka wanunuzi wao. Yaani alimradi awe na maneno kama *bosi, bei muzuri, njoo nitafanyia wewe pei nzuri, nitawekea wewe kwa basi, nitapatia basi ilete, tuma pesa na M-pesa, Nitafunga vizuri wasilikalewasisumbue wewe na tasabulia mimi bitu wewe nataka* yalimtosha kuwasiliana na wanunuzi maana nao kila wakati wakija huwa wanakuwa na haraka ya kuondoka. Hivyo mazungumzo ni ya kukatiza katiza ili biashara iendelee.

M.S 047 alisema;

*Mimi nikiwa shule ya msingi tulifundishwa Kiswahili kuanzia kidato cha kwanza hadi cha tatu. Kwa bahati mbaya wazazi wangu walipohama, shule ambayo walinipeleka Kiswahili kilikuwa hakifundishwi; Hata hivyo baada ya kuanza biashara nilijaribu kurejelea na kukumbuka msamiati mwalimu wetu alitufundisha namna ya kusailimiana, siku za wiki, tarehe na alama za barabarani. Najaribu kutumia maneno kidogo ambayo tulifundishwa wakatu huo; Maneno mengine yalipotea lakini menginebado nayatumia;*

Krashen (1987) na Cohen (2011) wanasema kwamba mwanafunzi anafanya mazoezi kulingana na dhamira tegemezi kwa unyambuaji wa vitenzi tofauti tofauti ili kukamilisha lengo la mawasiliano. Mikakati ya urejeleaji huambatana na hali ya kufanya mazoezi na kukariri baadhi ya msamiati ambayo walikuwa wamehifadhi awali ili kuwasaidia kuyatumia wakati walikuwa wakiwasiliana na wanunuzi wa bidhaa zao.

Kwingineko mnunuzi na muuzaji walishirikiana katika kupata dhana ambayo ilitakikana. Shughuli ya mfanyabiashara Y kuandika kile ambacho mnunuzi amemwambia ni ishara kwamba anataka kuhifadhi msamiati huo ili aweze kuutumia wakati mwingine. Mfano huo umeonyeshwa hapa chini

### **Mfano. 15 Uhifadhi wa maneno**

1. Muz: Y (*Ameshika kalamu na kitabu) theres a word you have said I don't understand*
2. Mnz: *Nauliza hapa unauza vocha ama simu tu.*
3. Muz: Y *Yes I have written simu what is the other thing*
4. Mnz: *Vocha nyinyi mnaita (scratch card)*
5. Muz: Y *Wait I first write on my paper.*

### **Asili: Data ya uchunzaji (marchi, 2022)**

Kuna mambo mengi ambayo hutokea wakati wa ujifunzaji wa L2. Urejeleaji ni pale ambapo mjifunzaji wa L2 anaandika matini kidogo kidogo halafu kwa muda wake anafanya mazoezi ya namna ya kutumia aliyoandika. Huwa hana sehemu maalum pa kuandika popote pale anapata anaandika neno. Ama hata labda siandike lakini mnunuzi anapomfikia anawaza kidogo halafu anakumbuka baadhi maneno aliyojifunza. Bachman (1990) anasema kwamba huu ni mkakati ambao hauna mfumo maalum. Mjifunzaji lugha tumizi anaweza kuandika ama kuhifadhi msamiati mfupi mfupi halafu akautumia mahali inahitajika. Bachman (keshatajwa) ameshadidiwa na Gardner (2000) kwamba mchakato huu unadhihirisha uwezo wa kipawa alichonacho mjifunzaji lugha na motisha changamani ambao unampa ari ya kujitahidi iwezekanavyo kujikuta anajifunza L.2. Wafanyabiashara wa jiji la Kampala pia hujikuta wakibadilisha msimo ili kustamili mawasiliano kati yao na wanunuvi. Hivyo hujikuta wakiwa na hulka ya kuchanganya na kubadilisha msimbo. Kwao labda waliona ni kitu cha kawaida kuwasaidia katika kuendeleza biashara pasi kujua kwamba shughuli kama hiyo ilikuwa ni mkakati ambao kwa kutumiwa kwa kipindi kirefu ungewasaidia katika ujenzi wa umilisi wa matumizi ya Kiswahili kibiashara. Walisema wao hubahatisha kutookana na yale walikuwa wanasikiza na yale yanasemwaa na kutumia sinonimu na ishara ili kuwasaidia kuzungumza.

**M.S 041** alisema,

*Anti walio waluulira omu agamba nguo yawatoi ni pesa ngapi. Nosooka newebuuza obba ayagalla kugenda mutoilet. Kati osooka nosilikirira wano ngogobeleza amaso kyiki kyatunulidde awo mubiloozo byo newegamba nti*

*ndooza ayagalla engoye za abaato. Nogobelezaayo ku kati .Bwakiriza nga omuguzza.*

Yaani kuna wakati unasikia mmoja akisema nguo ya watoi ni pesa ngapi. Mwanzo unajiuliza sijui anataka kuenda chooni. Unanyamaza huku ukifuata kwa macho kuona nini anaangalia hapo katika fikra zako ukajisema kwamba nadhani anataka nguo za watoto wadogo. Hapo unaafuutilisha kijiti kuonyesha palipo nguo za watoto. Akikubali unamuuzia. (TY)

Cohen, (1998) anakisia kwamba kipindi cha upatikanaji tena sio lazima iwe ile ya sarufi mahsusni ya kujifunza lugha maana mtu anaweza tu kuhifadhi maneno ambayo anafikiri yatamfanikisha kile anachokusudia. Hivyo wasailiwa walisema kwamba katika ile hali ya kuhifadhi na kutumia maneno baadaye wangejikuta wanatamka maneno ambayo yanawasaidia kuzungumza Kiswahili; Akikumbuka neno na likabainika kwamba lilikuwa la kweli basi angeweza kulitumia kila wakati anapopata mnunuzi. Kuhifadhi na kutumia maneno baadaye kuna karibiana na kubahatisha ila tofauti iliyopo ni kwamba mkakati upatikanaji tena mwanafunzi anatamka kile aliwahi kusikia wakati wa kubahatisha mwanafunzi anataja chochote ambacho kinamjia akilini mwake. Hali hii imeshadidiwa na (Tarone na Yule,1989; Oxford,1990; Bialystok ,1991; Wenden,1991; Green na Oxfrod, 1995) kwamba njia yoyote ile mwanafunzi anatumia kufanikisha ujifunzaji na matumizi ya L2 unakubalika almradi unamkuzia umilisi wake wa kuzungumza. Krashen (1977, 1987) naye anasema kwamba ujifunzaji na matumizi ya lugha kimawasiliano unaweza kufanikishwa kupitia mawasiliano ya kawaida ama njia yoyote ile ambayo imekuwa rahisi kwa mjifunzaji wa lugha tumizi. Hivyo mkakati wa Kufidia huwezi kufumbiwa macho kwa namna unawezesha matumizi ya Kiswahili kibiashara. Kwa jumla wafanyabiashara walijitahidi kupitia mahojiano kuonyesha namna mikakati iliyotajwa katika 4.2 namna iliawezesha kujifunza Kiswahili katika 4.3

#### **4.3.2 Jinsi mitindo ilivyotumiwa na wafanyabiashara kujifunza Kiswahili kama kibiashara jijini Kampala Uganda**

Hii ni sehemu ya pili ya mhimili wa pili ambao ni kutathmini jinsi mikakati na mitindo ilivyowezesha ujifunzaji na matumzi ya Kiswahili kama lugha ya kibiashara. Data zilizotokana na hojaji na usaili zilijibu swali la jinsi mitindo hutumika kujifunza Kiswahili kibiashara. Mitindo iliyopatikana kulingana na umaratokezi imewasilishwa katika jedwali 4.14. Data zilizotoka na mahojiano na uchunzaji zilipambanuliwa sambamba na data za hojaji.

**Jedwali 4.14: Jinsi Mitindo iliwezesha Kujifunza Kiswahili kama lugha ya biashara**

Mtindo	Wasailiwa	Asilimia
1. Mwingiliano	13	13
2. Dukuduku	02	02
3. Kusikiza	20	19
4. Ujifunzaji kihalisia	10	09
5. Mwelekeo	22	21
6. Hamasa	16	16
7. Kuashiria	13	05
8. Hulk za mjifunzaji	07	6.7
<b>Jumla</b>	<b>103</b>	<b>100</b>

**Asili ya data: Nyanjani kutokana na hojaji ,Machi 2022**

#### **4.3.2.1 Mwingiliano**

Kutokana na hojaji wasailiwa kumi na tatu (13/103) waliowakilisha asilimia kumi na mbili nukta sita (12.6%) walisema kwamba mtagusano kati yao na wafanyabiashara wenzao, wanunuzi na wazungumzaji lugha ya Kiswahili uliwasaidia kujifunza Kiswahili kama lugha ya biashara. Mfanyabiashara 011 katika kujaza hojaji aliandika kwamba wanunuzi waliokuwa wakitoka nje ya Uganda mara nyingi walitumia Kiswahili na kwa vile ilikuwa vigumu kuwambia wasitumie Kiswahili ilimbidi awe akijifunza maneno machache machache kutokana na wanunuzi hao.

Krashen (1987) katika mhimili wake wa pili anasema kwamba ujifunzaji ulio bora ni ule ambaao mjifunzaji L.2 anajifunza katika mfumo halisi pale ambapo lugha hiyo inatumika. Ameendelea kusema kwamba wakati wa utangamano basi mjifunzaji hujikuza kwani anajifunza dhana mpya ambazo zinaongezeka kwa umilisi alionao. Kia na Zahed (2010) walishughulikia mitindo ya ujifunzaji wa L2. Walisema kwamba mwingiliano hutokea pale ambapo mjifunzaji L2 hutangamana na jamii ambayo anajifunzia lugha. Hoja ambayo inafafanuliwa kwa upana katika modeli ya Gardener (2000) kwamba katika motisha changamani mjifunzaji L.2 akipenda lugha basi atapenda pia kujumuika na wazungumzaji lugha hiyo. Anaendelea kusema endapo atachukuzwa na lugha lengwa basi kuna uwezekano wa kuchukizwa na wazungumzaji wa lugha lengwa na hivyo ujifunzaji hautatokea.

Ekedi zilizotajwa zina kila aina za biashara na kwa mara nyingi huwa na mfumko wa wanunuzi kutoka sehemu mbalimbali za ndani na nje ya nchi. Wakati wa mahojiano, wasailiwa ishirini na saba (27) walisema kwamba kuingiliana kwao na watu kutoka mataifa mbalimbali na wengine kuishi katika mazingira ambayo yalikuwa na mchanganyiko wa

makabila uliwafanya wajifunze Kiswahili. Kwa mfano;

### **M.S 029**

*Obusuubuzi bwe bubeera wagullu abasuubuzi bajja bangi kuva empenda za njaullo. Walio abogeera mangu mangu naye ate walio abagomvu ate baombefu ate bbo abeKongo tosoobola na kutegeera luswaili kyi lwebalina. Naye okubeera wammu nabbo kutuyamba okuffunako ebigambo nga;;njoo, nauza biatu, nataka pesa ngapi nebilaara bingi.*

Msimo ambao biashara zinakuwa juu wanunuvi wengi huja kutoka sehemu mbali mbali. Kuna wale huwa wanazungumza kwa haraka haraka halafu kuna wale wanazungumza vizuri pole pole halafu wale wa Kongo hujui wanakiswahili gani. Hata hivyo tunapata baadhi ya masmiati kama; njoo, nauza viatu, unataka pesa ngapi na mengine mengi. (TY)

Lahaja nyingi zimechangia ukuzaji wa Kiswahili sanifu. Hata hivyo isimu jamii inaangazia matumizi ya lugha kulingana na sehemu ambapo watu wanatumia lugha. Inakuwa vigumu kuweka jamii zote kutoka Afrika Mashiriki katika mfumo mmoja wa Kiswahili kimatumizi. Hivyo wafanyabiashara huchota kutoka kwa hao wanunuvi Kiswahili ambacho wanatumia kuendeleza biashara zao. Mathalan utakuta mnunuvi kutoka Kongo badala ya kusema pesa anasema mafaranga;

### **Nukuu: M.S. 060 alisimulia haya kutokana na kipindi cha wakombozi**

*Mwaka 1979 ulikuwa mwaka wa vita vikali vya kuondoa Idi Amini Dada. Wakombozi walikuja kufukuza yeye. Iii wakati sisi balijifunza Kiswahili ndiyo tuongee vizuri na wajeshi. Hata wasichana wa kwetu waliolewa na wakombozi kutoka Tanzania. Hata sasa iko dada yangu iko Kahama. Nilipoanza biashara mwaka 1987 mimi alikuwa anaweza kuongea Swahili nzuri sana. Hata sasa mimi hapana pata shida na wachuuzi kutoka Kenya na Tanzania. Bado ntatumia ile mimi nilipata kwa wakombozi.*

### **Nukuu: M.S Katika mjadala wa mahojiano mfanyabiashara 062 alisema,**

*Sisi tunazaliwa Masaka Lwera lakini wakati wa vita vya Amini wakombozi walikuwa wanajificha kwa baba yangu halafu walikuwa wanatumia Kiswahili neno ambao nilikuwa nakumbuka ni nje iko safi? Sikujuwa wanamaanisha nini lakini baadaye nilimuuliza baba akasema walikuwa wanauliza kama huko nje hakuna adui ili watoke nje kidogo. Mimi sina shida na Kiswahili. Nakijua sana tena nafundisha hawa wenzangu*

Alisema picha ambayo wakombozi walionyesha ilibainisha kwamba Kiswahili kilistahili kutumiwa katika mazingira ya vita. Wakati huo alijifunza Kiswahili kwa sababu sio kwamba alikuwa anakipenda Kiswahili lakini alikitumia kama kinga ambayo ingelimsaidia dhidi ya kuteswa na jeshi la wakati huo

Krashen (1977, 1987), Sulz (1991); Chien (2010) na Savile-Troike (2012) wanasesma, mtu huanza kujifunza L1 kutoka kwa wazazi wake halafu baadaye anajifunza L2 kutoka kwa jamii lengwa kwa kukopa namna wanavyozungumza na mienendo yao. Ujifunzaji huu unatokea pale ambapo mjifunza L2 anakuwa na mwingiliano na mzungumzaji wa lugha lengwa. Ujifunzaji lugha siyo tu kuzungumza ila pia kujifunza utamaduni, itikadi na mienendo ya lugha lengwa. Durojaye (1976) anaamini kwamba mwingiliano humpa mjifunzaji fursa na motisha changamani (Gardener, 2000) kujifunza lugha lengwa. Yaani anayejifunza lugha mara nyingi hurudia yale amesekia ya kizungumzwa na kuyatumia mara kwa mara anapopata fursa ya kuyatumia. Gardener (keshatajwa) anaongezea kwa kusema kwamba kila mmoja anapozaliwa ana uwezo wa kujifunza L2 almradi mjifunzaji huyo aonyeshe kwamba ana nia ya kujifunza lugha hiyo. Hoja ambazo zinaleta upanuzi wa mawazo yanayopigwa upatu na kina Goold na Rimmer (2000) kwamba, tajriba na motisha huchangia pakubwa katika kumpa mtu jazba ya kujifunza lugha. Weaver na Cohen (1998) kwa kurejelea utafiti wa Oxford na Chamot (1990) waligundua kwamba ujifunzaji L2 hautegemei maarifa tu ila mwelekeo na mwingiliano wa mtagusano na ukuruba kati ya wanunuzi na wauzaji husaidia sana kukuza umilisi wa ujifunzaji wa L2.

Msingi kutokana na mijadala na mawazo ya wataalmu hawa ni kwamba licha ya kuwa tunajadili mikakati na mitindo kama vipengele anuwai, ni vigumu vipengele hivi kufanya kazi pekee. Ndiyo maana katika hali ya mwingiliano, mtagusano na ukuruba kati ya watu ambao wanashughulika katika mazingira mamoja hayaepukiki. Msailiwa 120 alieleza kwamba ;

#### **M.S 120 Alieleza kwamba**

*Kwetu ni karibu na mpaka wa Uganda na Tanzania, hata lugha zetu zinakaribiana muhaya akizungunza hata tuyankole utaelewa hivyo wakati wa vita vya Amini wakombozi kutoka Tanzania walikua wakitumia sana Kiswahili. Katika hali ya kuogopa ama wakati mmoja tungekuwa Uganda au Tanzania kulingana na hali. Hali hii ilitufanya tujifunze Kiswahili. Nilijifunza tuuu hivyo sikujua kwamba kulikuwa na mkakati lakini kuongea na marafiki wangu pale mpakani kulinyoosha Kiswahili change. Naweza kuita wanunuzi, kuwapa maarifa.*

Mukuthuria (2006) anasema kwamba Kiswahili nchini Uganda kilikita mizizi kupitia biashara. Biashara za misafara mirefu ilifanya wata watangamane katika shughuli za biashara, siasa na dini. Anaendelea kusema kwamba vita vya miaka ya 70 vilichangia ujifunzaji wa Kiswahili kwa sababu wenyeji walitaka kujinasibisha na wazungumzaji wa lugha ya Kiswahili kutoka Tanzania ili kusaidiana katika vita vya wakati huo. Aidha, kuanzia

miaka themanini na tisa Kiswahili kilinawiri na kupata hadhi yake katika kutumika katika asasi tofauti tofauti mkiwemo biashara. Uwezo wa kuzungumza L.2 ni kiashiria kwamba mwanafunzi anaweza kustahamili pembejeo za L.2. Hivyo kulingana na mhimili wa nne wa Krashen, ni mwanafunzi ambaye i inaweza kuongezwa +1 yaani dhana mpya kwa msamati aliokuwa nao awali. Hivyo wasailiwa 060, 062 na 120 wameonyesha uwezo (Gardener 2000, 2010a) wa kuonyesha kwamba wana kipawa cha kuandika na kusoma Kiswahili na wanaweza kuendeleza mazungumzo kwa kukihusisha kibiashara.

### **M.S 056 alisema**

*“Babu muzaa mama alikuwa anaishi Kenya; alihamia huko wakati wa vita vya Amini; kila wakati alikuwa akitutembelea angetufundisha Kiswahili kidogo kidogo kwa mfano kutaja vitu na shughuli zingine; Pia kulikuwa na rafiki yangu ambaye alikipenda sana Kiswahili hivyo nami nikapata motisha wa kujifunza Kiswahili. Hivi sasa nimepata marafiki na wanunuzi wengi kupitia kuzungumza kwangu Kiswahili; hata wenzangu huniambia niwasaidie”.*

Kuingiliana kwa Msailiwa 056 babu yake pamoja na rafiki yake kulimfanya ajifunze baadhi ya misamati ya Kiswahili ambayo ilimwezesha kutumia Kiswahili kibiashara. Hii ina athari ya mwelekeo wakati wa kujifunza lugha. Mwingiliano unaweza kuathiri mjifunzaji lugha kwa namna hasi ama chanya. Kwa wale ambao wamekuwa na athari chanya; motisha chanya imewasaidia kujifunza Kiswahili kibiashara. Mabadiliko chanya pia yamesaidia ujifunzaji chanya wa Kiswahili kibiashara mionganoni mwa wafanyabiashara jijini Kampala.

### **M.S 133 alisema**

*Mimi sehemu nilikaa na Wachotara na Wanubi wengi sana. Hapa karibu tu Burkley. Hivyo katika mimi kama bado niko mdogo nilikuwa nacheza na watoto wenzangu. Tuliongea swahili na Kiganda. Wao apana jua Kiingereza. Nilifanya sirisiri maana wazazi wangu hawakutaka mimi kuongea Swahili. Walikuwa na biashara Kisenyi na walifunza sisi iyo biashara. Miaka ya themanini . Baadaye nimefungua hapa Mukwano na kuanza biashara yangu. Sasa mimi natumia ile Swahili yangu safi kuongea na wachuuzi.*

Alisema kwamba kando na kuendeleza biashara ana marafiki ambao walihamia Tanzania na Kenya. Huwa mara nyingi anawatembelea na kutuma watoto wake huko wakati wa likizo ili kujifunza Kiswahili. Wanafunzi ambao husomea Kiswahili Merikani hupata motisha kupitia mitandao ya kiteknolojia, kuna namna wanawasiliana na wazawa wa lugha ya Kiswahili ili kuboresha Kiswahili chao ama kufanya ziara ya kuenda Tanzania na Kenya.

Gardener na Tremblay (1994) na Gardener (2000) kwa kurejelea mhimili wa tatu yaani motisha changamani wanasema kwamba kwa kawaida huwa kuna Mtagusano chanya na

mtagusano hasi. Pale ambapo kunawakuwa na mtagusano chanya na kutangamana na wale wanajua lugha, huwa kuna mchango mkubwa katika mjifunzaji kujifunza L2; Hili limeshadidiwa na Muaka, (2020) kwamba licha ya kuwa wanafunzi wa Marikani hujifunza lugha ya Kiswahili kama lugha ya kigeni, huwa hawaridhiki na mafunzo hayo hadi wanapotangamana na wazungumzaji wa Lugha ya Kiswahili.. Mtindo huu ulielekea kuwa muhimu sana katika matumizi ya Kiswahili kibiashara. Krashen (1987) anasema mjifunza lugha huwa anapata pembejeo zenyе sifa za kisarufi zilizo zaidi ya kiwango chao kwa sababu huwa wanatangamana na umilisi wa lugha wanayojifunza. Katika biashara lazima kuwepo na msamiati mpya kila wakati. Hoffman (2000) na Troike (2012) wanasema kwamba watoto wanaweza kupata L2 kuitia mfumo sawia ama kutegemea wakati na mahali. Kulingana na yeze watoto wajifunzao lugha sawia ni wale watoto ambao hupata lugha yao mama na lugha ya kigeni bila tatizo lolote. Hao watoto wanaweza kuwa wanatoka kwenye mazingira ambayo nyumbani wanazungumza zaidi ya lugha moja. House (2002) na Mutenyo, Deborah na Okal, (2021) wameongezea kwa kusema kwamba licha ya kuwa na wingilugha nyumbani, watoto hao hujifunza lugha zote bila kuchagua mojawapo. Kwa kurejelea wakati na mahali anasema watoto hao husukumwa na motisha ndiyo maana wanaishia kujifunza ama kupata lugha zote ambazo ziko mazingirani mwao. Wasailiwa hawa wanasema kuwa mwingiliano uliwasaidia kujifunza msamiati katika Kiswahili wakiwa na umri mdogo na hata baadaye watu wazima waliweza kuwasiliana na wanunuzi waliomiminika jijini Kampala.

#### **4.3.2.2 Dukuduku**

Wafanyabiashara wawili (02/103) ambao waliwakilisha asilimia moja nukta (1.9 %), katika kujibu swalı la jinsi gani mtindo waliouchagua uliwasaidia kujifunza Kiswahili kibiashara. Walisema ni kutohama na dukuduku walihitaji kuhusu Kiswahili ndiyo walifanikiwa katika ujifunzaji wa Kiswahili kwa ajili ya biashara. Katika kujaza dodoso walisema kwamba dukuduku inakufanya uonekane kana kwamba una deni la kulipa. Msukumo huo ukiwa juu basi unajifunza Kiswahili pole pole bila kujiharakisha.

Matokeo yaliyotokana na mahojiano kati ya mtafiti na watafitiwa ambao walikuwa nane hasa waliofanyia kazi katika Ekedo ya Mukwano walisema kwamba Kampala ni mji ambao unahitaji mtu kuwa mjanja mjanja ndio aweze kufanya biashara. Wakati wa kukusanya data mfanyakibashara 146 alibaini kwamba yeze alikua na dukuduku ya juu dhidi ya kutumia Kiswahili.

### **M.S 146 alisema**

*Okukoola obusuubuzi Mkampala kyetaaga nga olimjagujagu.Nze bwendaba agguula ntandikirao, umeludi jooli mumanyi, bye yekaangamu nsimbayo kalala lafiki kalibu oba bosi leero unataka nini, maali weli iko safi kabisa .Mimi apana gopa kuongea swaili noonya seente*

Kufanya biashara Kampala kunataka mtu kuwa mjanja mjanja. Hivyo mimi nikiona mteja naanza tu rafiki umeludi kana kwamba namjua. Akishtuka tu naongeza neno lining rafiki karibu, ama boss leo wataka nini, mali safi kabisa. Mimi siogopi kuongea Kiswahili sababu natafuta pesa.(TY)

Garderner (2000) na Piggott (2008) wanasema kwamba mionganoni mwa vigeugeu ambavyo vinaweza kufanikisha ama kukwaza ujifunzaji na matumizi ya L2 ni dukuduku aliyonayo mjifunzaji wa lugha tumizi. Dukuduku ni dhana ya kisaikolojia mbayo inajishughulisha na hulka za mtu binafsi (Gardener, 2000) kwa muda mchache ama kulingana na hali ilivyo.

Dukuduku katika utafiti huu ilionyesha jazba na ragba ya mjifunzaji lugha katika kujifunza ili kuitumia katika mazingira ambapo lugha hiyo inastahili kutumika. Dukuduku huletwala na motisha changamani anbapo ni mhimili wa tatu wa Gardener (2000) pale ambapo mjifunzaji L.2 anatafakari juu ya lugha ambayo anaikuta mazingirani mwake. Ehrman na Oxford (1990) wanasema wanafunzi hawa hupenda kujumuika na wengine kwa shughuli za mazungumzo mahali wanaweza kuzungumza wakasikika bila kujali makosa ya kisarufi. Krashne (1987) na Gardener (2000) wanasema mwanafunzi huwa ashafikisha kiwango cha kuweza kutunga sentensi kwa kutumia lugha lengwa. Kwa wale ambao wana dukuduku ya juu huchukua muda kujifunza lugha ila kwa wale ambao wana dukuduku ya chini hufanikiwa kwa haraka katika kujifunza L2.

### **M.S 012 alisema ;**

*Ofcourse omusuubuzi olino kumuyiyya.Mwaniriza muluganda, nyabo/ssebo jangu wano, jangu nkuguzeeko; ssemberako wano; bwataadamu nenkuusako, nyabo /boss karibu.Rafiki angalia.....bwebityo luusi ne byoyogeera okimanyi byandiba bifu nayeomu obba babiri bakusemberera.*

Ndiyo lazima ubambanye kumvutia mnunuzi. Namkaribisha katika kiganda; bwana/bibi njoo hapa; njoo nikuuzie; jongea karibu, asiponijibu nabadilisha na kusema bibi/boss karibu. Rafiki angalia. Hivyo tu hata kama hujui unachozungumza huenda kisiwe na maana lakini mmoja amawawili watakusongelea .(TY).

Krashen (1987), Whyte (2006), Maclyntyre na Gregersen (2012a) kwa kuanganzia nadharia tete ya dhana mpya, huzua athari chanya kama vile dukuduku, motisha na kujiamini. Kwa

vile mchakato wa kuendeleza biashara ni wa kipindi kifupi, mfanyabiashara ambaye ana uwezo wa kutumia dukuduku ya chini anajipata amejifunza lugha tumizi na kuweza kuitumia mara kwa mara. Mjadala mwingine uliotokana na mahojiani kati ya mtafiti na mfanyabiashara, walinukuliwa wakisema,

### M.S 105

*Okufunna abaguzi otekwa kubba nga oyogeerayo ebigambo gambo bya luswahili ne lubaa nga lilomo mistake. Sisi bado soma Kiswahili kwa darasa; sasa onataja taja maneno ya Kiswahili kwa wakastoma ina kukaribish katika biashara; hapa kwa hoteli tumejifunza maneno kama iko biriani ya uhuru, pilau kuku, pilau masala mandazi tamu tamu, nyama choma na kachumbala bure. Hawa waswahili wanapenda kyakulyayao.*

Ili kupata wanunuzi unastahili kuongea ongea maneno ya Kiswahili hata kama kuna makosa. Sisi hatujasoma Kiswahili darasani; hivyo unataja taja maneno ya Kiswahili kwa mteja ili kumkaribisha katika biashara; hapa hotelini tumejifunza maneno kama; kuna biriani ya uhuru, pilau kuku, pilau masala, mandazi tamutamu, nyama choma na kachumbari ya bure. Hawa Waswahili wanapenda chakula chao (TY).

Hii ni njia moja ya kuwavutia wateja maana wanajua kwamba wanunuzi kutoka nje ya Uganda na hata wengine wa asili ya Wachotara na Sudan hutaka aina tofauti ya chakula ambacho siyo cha utamaduni wa Kiganda. Motisha changamani humfanya mjifunzaji L2 awe na dukuduku ya kujifunza L2 ili kufanikisha lengo analolihitaji. Lengo la wasailiwa ni kufanikisha biashara zao kwa kutumia Kiswahili.

Wakati wa uchunzaji mtafiti alishuhudia maongezi yaliyoibua mtindo wa dukuduku kati ya wanunuzi na wauzaji. Mmoja kati yao ataibuka na dukuduku hasa anapoonyesha jazba wakati wa kuongea.

### Mfano.16 Dukuduku ya juu

1. Mnz: 9      *Nguo ni pesa ngapi*
2. Muz: 7      *Engoye zona (nguo zote)*
3. Muz:10      *Lamula buli lugoye (mwambie bei ya kila nguo)*
4. Mnz:9      Yaani marinda ya watoto
5. Muz:7      Mbuno tulindeko abaana.(kwamba tusubiri watoto)
6. Muz:10      *Nedda agambye engoye za baana.Nandimugambye muluswaili naye ntya nandiyonena byenjogera.(Amesema nguo za watoto. Ningemwambia katika Kiswahili lakini naogopa nitaharibu ninachoongea)*

### **Asili: Data kutokana na uchunzaji (Machi, 2020)**

Muz.10 anataka kusema lakini anashikwa na uoga. Anafikiria kwamba akiongea atafanya makosa. Kwa wajifunzaji waliona dukuduku ya juu huwachukulia muda kujifunza lugha tumizi. Hawapendi kujikuta wanafanya makosa. Krashen (1987) na Maclyntrye (1995) wanasema kwamba mchakato wa ujifunzaji L2 huhitaji uingizaji na uhifadhi wa lugha ambayo mjifunzaji anajifunza. Wanaendelea kusema kwamba mjifunzaji lugha lengwa anapoathirika na dukuduku ya juu basi ujifunzaji huchukua muda mrefu.

Utafiti wetu unakubaliana na maelezo ya awali ya kina Mackey (2006) na Kia, Alipour na Ghaderi, (2009) kwamba dukuduku inaweza kutazamwa kwa hali mbili; yaani katika mazingira ya darasa na mazingira halisi ambapo mjifunzaji L2 anaweza kutumia katika mazingira ambayo yanamhitaji kutumia lugha hiyo kwa ajili ya mawasiliano ya kawaida kutegemea mahali na hali aliyomo.

#### **4.3.2.3 Kusikiliza**

Wafanyabiashara wengi jijini Kampala walitumia maneno ambayo walipata kupitia njia ya muziki hasa muziki wa kina Chameleon na wasanii wengine, Ilibainika kwamba wasailiwa ishirini (20/103) amba waliwakilisha asilimia kumi na tisa (19%) walitumia msamati amba walijifunza kutoka kwa wasanii amba waliimba nyimbo za Kiswahili. Mfanyabiashara (009) wakati wa kujaza hojaji aliandika kwamba kutumia mitandao ya kijamii kama **Youtube** na **Whatsapp** kuliwasaidia kujifunza siku za wiki, vokali pamoja na salamu ambazo zilikuwa na majibu.

Inasemekana kwamba kuanzia miaka ya sitini hali ya muziki Afrika Mashariki ilibadilika na miziki ikaanza kuimbwa katika kiluo, kikamba, kimijikenda, kidawida na lugha nyingi za Kenya kama moto nyikani, hata hivyo hizo nyimbo hazikupenyeza sana kama nyimbo za Kitanzania zilizoimbwa katika Kiswahili; Wanamziki kama kina Samba Mapangala, John Ngereza, na baba llunga wa Kongo na Sammy Kasule walianza miziki yao kwa kuchanganya lugha zao za asili na Kiswahili (Chimerah, 2010). Kutokana na hojaji kulipatikana data finyu mno ambazo zilielezea namna nyimbo zilifanikisha ujifunzaji wa Kiswahili kwa ajili ya biashara. Kutokana na mahojiano wasailiwa walipata muda wa kutosha kuelezea namna nyimbo mbalimbali ziliwafaa katika ujifunzaji wa Kiswahili kwa ajili ya biashara. Idadi ya waliohijiwa ilikuwa kubwa kiasi cha wasailiwa thelathini na moja (31) amba walifanikisha ujifunzaji wao kutumia nyimbo. Mfano;

## M.S 023 alisema,

*Chameleon yatuyamba nyoo ne nyimba zze za luswaili. Olabba kati nga Tubonge mulimo ebigambo nga; ningetaka nikuone nikupe. Kyangu nyoo okugamba omusuubuzi ali wala obba ali na kyeyelabiidde muduuka lyo ngolina kukyimuwa; nambari ya simu-awo ngoyaggala kumufuula kasitoma bwobba olesse new arrival nga omukubiira, ate kyangu okutegeera nti kitegeesa; namba ye simu, rafiki wa kweli, Mungu baba, nikukaribishe kwangu, nikupe chakula kitamu. Nalimpandika chakula/kyakulya. Kati naiga ate ngezaako okogera bulungi na abasuubuzi bwebajja wano.*

Chameleon alitusaidia sana na nyimbo za Kiswahili. Unaona kwa mfano kama katika nyimbo ya Tubonge kuna maneno kama *ningetaka nikuone nikupe*. Ni rahisi kumwambia mnunuzi ambaye yuko mbali ama kuna kitu alisahau katika duka lako na unastahili kumpa. *nambari ya simu* hapa kama unataka mununuzi awe mteja wako ndiyo maana ukileta mzigo mpya ni rahisi kumfikia tena maneno yenye namba ya simu ni rahisi kueleweka *Mungu baba, nikukaribishe kwangu, nikupe chakula kitamu*. Nilikuwa naandika chakula kama *kyakulya* lakini sasa nilijifunza tena najitahidi kuongea vizuri na wanunuzi wakija hapa (TY)

Krashen (1987) katika mhimili wa pili katika utaratibu wa ujifunzaji asilia anasema kwamba ujifunzaji wa miundo ya kisarufi huendelea kwa utaratibu unaoweza kutabirika. Kwa lugha fulani, baadhi ya miundo ya kisarufi hupatikana mapema, wengine huchelewa, bila kujali L1 ya mzungumzaji. Hata hivyo, haimaanishi kwamba sarufi inapaswa kufundishwa kwa utaratibu wa darasa ila katika mazingira halisi ujifunzaji waweza kujitokeza. Mazingira halisi ya ujifunzaji kwa wafanyabiashara ni mazingira yale ambayo wanafanya biashara jijini Kampala ambapo Kiswahili kinatumika. Kwa kupigia upatu mawazo ya Krashen (keshatajwa), Gardener (2000) anasema kwamba ujifunzaji wa L.2 hufanikishwa na kipawa cha mjifunzaji. Katika mhimili wake wa tatu wa motisha changamani na wa nne wa uwezo, ameeleza kwamba kupitia uwezo wa kujishughulisha katika mazingira halisi ya kutenda pamoja na kipawa cha kusikiliza, kucheza na kuimba nyimbo mjifunzaji hupata fursa ya kujifunza L.2. Kwa mujibu wa wafanyabiashara kipawa cha kusikiza muziki kilichangia pakubwa katika ujifunzaji wa Kiswahili kibiashara.

Wasanii tajika kama kina Joseph Mayanja (Chameleon) kuanzia miaka ya tisini alianza kuimba muziki kwa kutumia lugha ya Kiswahili. Matumizi ya nyimbo za Kiswahili pia katika maswala ya kidemokrasia hasa uchaguzi na utekelezaji wa majukumu ya kisiasa ulidhihirisha wakati wa kipindi cha utawala wa Yoweri Museveni kuanzia 1986 (Masereka, 2018). Demokrasia nzuri huimarisha uchumi. Uchumi hauwezi kuimarika kama hujagusia maswala ya biashara. Nyimbo zimekuwa asasi muhimu katika usambazaji wa Kiswahili

nchini Uganda hasa nyimbo za wasanii. Mumo humo ndimo wafanyabiashara wamekuwa wakichota msamiati kama, *chagua, bei ghali, rahisi, pesa, safari, lipa, mali* na kufarijiana wakatimambo hayaendi vizuri.

Wasailiwa walisema hakuna namna lugha na nyimbo inaweza kutenganishwa. Utafiti wetu uligundua Kwamba nyimbo za wasanii na siasa zilijengea sana umilisi wa matumizi ya Kiswahili kwa wafanyabiashara jijini Kampala.

#### **M.S 114 alisema,**

haaa mimi napenda sana Chamaeon sababu yeye naimba kwa luswahili tena nakijua sana; nakumbuka aliimba napenda bitu bya pei kali, Jamila na nyingi kabisa. Hivyo kama mtu anataka kukuseera (kukudhulumu) unasema bitu yako ni ya pei kali” halafu nah ii vunja mifupa kama meno bado iko. (Anaimba)

*Vunja mifupa kama bado meno iko x2  
Utakuja lia ukishapoteza muda wako x2*

Huu ulikuwa wimbo wa kina ‘Samba mapangala’ ambao ulivuma sana katika enzi za zamani. Ilikuwa rahisi mtu kutaja msamiati kama vunja na meno bila utata maana haikuonekana kuwani maneno mapya katika mazungumzo ya kawaida kati ya watu wa Uganda.

Hili ni dhihirisho kwamba mchango wa nyimbo uliwaisaidia sana wafanyabiashara Kampala kujifunza Kiswahili kibiashara. Walikiri kwamba kufanikiwa kwa ujifunzaji wa Kiswahili kulitokana na nyimbo, sauti na mafunzo kutoka kwa wasanii.

Faerch na Kasper (1980) walisema mojawapo ya mitindo bora ya ujifunzaji L2 ni kusikiza, kufuatilia michezo ya kuigiza (Gardener, 2000) ambayo imo katika lugha hiyo. Ilidhihirika kwamba kusikiliza muziki wa Kiswahili na kutafuta maana ya maneno hayo kwa pamoja kulichangia wafanyabiashara kukitumia Kiswahili kibiashara.

Wafanyabiashara walisema kwamba ni vigumu mtu kukaa darasani na kujifunza Kiswahili. Tena wakati wao Kiswahili hakikuwa somo ambalo lilipewa kipaumbele. Lugha za asili ndizo zilikubalika sana ama kujifunza au kufundishwa shulen. Hata vitabu ambavyo vinauzwa kwa ajili ya kusoma Kiswahili ni vigumu lakini ukisikiliza nyimbo za wasanii kama Chameleon, na Juliana inakuwa rahisi kujifunza misamiati mingine.

#### **M.S 051 alisema kwamba ,**

*Olabba ne bwe twasomanga mubibiina ebisooka bye enjili batuimbisanga ennyimba. Kati bwogobelera enyimba ezo offuna ebigambo oluvanyuma nobuza kyikyi je bitegeeza. Olabba kati nsobola no kuimba anthem*

*eyoluswahili kubba ebigambo buli wamu baluyimba ne omutab "ani wange bwaja okuva kusomero atuimbilamu. Mwatu enyimba nga, Jamila, Shida za dunia, vumilia, balilisa ne Usiende mbali name olwa Juliana zilimo ebigambo bingi; na luli mukampeni twaulila toka kwa bala bala olwa Besigye. Tolaba ntino enyimbe ezo ziigiriza bulungi Oluswaili. ate osobola kukozeesa ebyo bigambo bwooba ofunyeeyo omusuubuzi.*

Unaona wakati tukisoma masomo ya wali ya dini walikuwa wakituimbisha sana nyimbo za dini. Ukifuatilia hizo nyimbo unapata msamiati halafu baadaye unauliza maanya ya hayo maneno. Unaona sasa naweza kuimba wimbo wa Jumuiya ya Afrika Masharii katika Kiswahili kwa sababu kila mahali wanauimba n ahata kijana wangu huwa akitoka shulenii huwa anatuimbua. Yakhe nyimbo kama Jamila, Shida za dunia, Vumilia, Badilisha na Usiende mbali wa Juliana zina maneno mengi n ahata wakatu ule wa kugombea wa maraisi tulisikia Toka kwa barabara wa Byesigye. Huoni kama hizo nyimbo zinafundisha vizuri Kiswahili. Tena unaweza kutumia maneno hayo endapo umepata mnunuzi (TY).

Ujumbe unaweza kuwasilishwa kupitia njia tofauti ili mjifunzaji awe na urahisi wa kuupata na kuutumia kwa muda mrefu kutegemea tofauti za uelewa. Ujumbe unaweza kutolewa kimaandishi, kimasimulizi ama kwa kuona kutegemea na nadharia ya mpangilio. (Gardener, 2000). Ujumbe unaopatikana kupitia njia tofauti huelewaka vizuri ukiulinganisha na ujumbe wa mkondo mmoja (Anderson na Elloumi, 2004).

### **M.S 073 anaeleza kwamba ;**

*Iko maneno natumia namna nasikia muziki wa chameleon Kama ile ya valuvalu na Tubonge. Kama, wasikudanganye; nataka; rafiki; hera nyangi, fanya na nguvu, mwenye roho mbaya, watasema watachoka. kama mimi naona kasitoma wanafanyizia yeye pei mbaya mimi naambia yeye uyo nadanganya, ama naweza kusema ii kintu sii era nyangi. Tena kama kasitoma naambia mimi maneno mbaya mi nasema wewe iko roho mbaya. Most of those songs by chameleon can be used in simple Swahili to I help in doing business here. You can see I can gamble but communicate.*

Msailiwa 073 amekiri kwamba kuna maneno huwa anatumia kutokana na kusikiliza muziki wa muimbaji Chameleon. Maneno hayo yametokana na wimbo wa *Valu Valu* na *Tubonge*. Kuna maneno kama **wasikudanganye; nataka; rafiki; heranyangi, fanya na nguvu, mwenye roho mbaya, watasema watachoka**. Aliendelea kutoa mfano kwamba akiona wanamfanyia mteja bei ghali yeye anamwambia huyo **anadanganya** ama anaweza kusema *hiki kitu ni kizuri sii hela nyangi*. Tena mteja akimwambia maneno mabaya yeye humjibu *uko na roho mbaya*. Ametamatisha kwa kusema kwamba nyimbo nyangi za Chameleon zawenza kutumika katika ujifunzaji wa Kiswahili chepesi ambacho kinaweza kutumiaka katika mazingira ya kufanya biashara. Utafiti huu ulibaini kwamba matumizi ya nyimbo yalisaidia sana

wafanyabiashara kutumia Kiswahili kibiashara. Matumizi ya nyimbo yalikuwa kama motisha ambao ulijengeka kupertia mwelekeo chanya ambao uliwasaadidh kufanikisha biashara zao. Utafiti huu umekubaliana na Gardener (2000) ambaye katika modeli yake anasema kwamba mwelekeo kuhusu muktadhawa kujifunza lugha na mwelekeo kuhusu lugha lengwa husaidia mjifunzaji lugha ya pili kupata motisha wa kujifunza lugha lengwa na kufanikiwa kuitumia. Ameendelea kusema kwamba katika muhimili wa pili wa motisha changamano mjifunzaji hujikita sana katika kile ambacho anafikiri kitamfaa kukidhi mahitaji yake. Mahitaji ya mfanyabiashara ni kupata wateja na faida kutokana na mauzo yake.

Fleming (2001) pia amepigia upatu kwa kusema kwamba ufasaha ndiyo kipengele mwafaka ambacho kinasaidia kuongea na kuandika lugha yoyote ile hasa lugha ya pili. Alisema hili linawezekana mjifunzaji lugha ya pili anapo jishughulisha na fasihi ya nyimbo ama mashairi ya kusikiliza na kujifunza kimya kimya. Kwa kawaida hizi ni hulka za watu wenye sifa za unyamavu. Wanapokimya ni vigumu kuelewa kwamba unachokizungumza wanakielewa ila ukiwahuisha watakuonyesha kwamba wanajua. Hawa ni baadhi ya wafanyabiashara ambao walionyesha uoga wa kufanya makosa wakati wa kujifunza Kiswahili kibiashara.

Kupertia mjadala wa mahojiano wasailiwa thelathini na tano waliendelea kutoa mifano ya nyimbo za dini. Walisema kamba nyimbo za dini pamoja na nyimbo zingine za burudani ziliwasaidia kujifunza msamiati wa Kiswahili. Chimerah (2010) anasema kwamba fasihi ina ashiria utamaduni wa mtu na huwa na muathiriano chanya ama hasi kwa yule anayepokea ujumbe wa msanii. Anaendelea kusema kwamba muziki ulichangia sana maenezi ya Kiswahili Afrika Mashariki. Aidha, nyimbo humpa mjifunzaji lugha ya pili motisha na ari (Gardener, 2000) ya kufuutilia kile kinachoimbwa na kupata msamiati ambapo msamiati huo utamsaidia katika mawasiliano. Uganda ilichukua muda kuhalalisha ufundishaji wa Kiswahili darasani kwa sababu ya historia mbaya. Hivyo kwa wale walikutana na Kiswahili katika mazingira ambayo si rasmi mara nyingi walijifunza Kiswahili kupertia muziki wa wasanii mbalimbali. (Chimerah, 2010).

#### **4.3.2.4 Ujifunzaji halisia**

Matokeo yaliyonukuliwa kutokana na takwimu za hojaji yalionyesha kwamba, wafanyabiashara kumi (10 /103) idadi iliyowakilisha asilimia tisa (09%) walikiri kwamba kuwepo kwa kwa mazingira yaliyoshirikisha Kiswahili kuliwasaidia sana. Kutokana na majibu ya hojaji walisema kwamba ili kupata mafanikio yoyote katika lugha ya Kiswahili

ilikuwa bayana kujizoesha kuwa pale ambapo Kiswahili kilitumika. Waliendelea kusema kwamba huwa kuna maneno mapya mengi ya kujifunza, katika mfumo maalum wa matumizi ya Kiswahili. Kufanikisha hilo walisema kwamba inatakitana uwe na motisha chanya kuhusulugha ya Kiswahili ndiposa ujifunze.

Kupitia mahojiano mionganoni mwa wasailiya thelathini na mbili kuna wale waliosema kwamba mtu anaweza kuingiliana na wasemaji wa Kiswahili, kusikiliza na kusoma Kiswahili lakini pia inahitajika mtu awe na uwezo wa kusoma. Hivyo ni kufanya bidii kujifunza baadhi ya maneno katika Kiswahili ili yakusaidie katika kuzungumza na wanunuvi.

### **M.S 099 alisema**

*Embeera je tullimo tetulina kyakukola tulinokuiga luswaili ka kyibe kyibe kub" a katibakastoma abasinga kati bbava muni endalla ezitali za Buganda. Atte kati naffe walio ebyamaguzze bye tuja ekenya ne tubileeta. Olina kufubako nti okozessa luswaili ebiseera byoona kasita obeera mukyibuuga wano.*

Hali tuliyonayo kwa sasa hatuna la kufanya, lazima tujifunze Kiswahili kwa vyovyyote vile kwa sababu wanunuvi wengi sasa wanatoka nchi nyiningine ambazo si za Buganda. Nasi pia kuna bidhaa ambazo tunanunua kutoka Kenya na kuleta. Hivyo lazima ujitatidi kutumia Kiswahili wakati wote almradi uko hapa mjini (T.Y)

Krashen (1987) na Gardner (2000) wanasema kwamba mazingira halisi ni njia mwafaka ambayo humwezesha mjifunzaji lugha kwa sababu lugha hiyo itakuwa inatumika katika shughuli maalum za sehemu hizo. Mjifunzaji lugha anastahili tu kujihami na mwelekeo na motisha chanya kuhusu lugha anayojifunza. Krashen (1987) katika mhimili wake wa pili anasisitiza ujifunzaji ambao unatokana na mazingira halisi ambayo mjifunzaji L.2 anaweza kujifunzia. Kwamba inakua wepesi kwake kujizoesha na dhana mpya ambazo zinajitokeza akijifunza L.2. Dianne na Michael (1991) waliwahi kutaja kwamba ni vigumu kutenganisha motisha na mwelekeo kama nguzo muhimu ya kufanya mtumiaji wa L2 kujizatiti kutumia lugha tumizi. Mjifunza L2 anapokuwa na hamu ya kujifunza L2, hujifunza pia utamaduni na hulka za wazungumzaji wa lugha lengwa (Williams, 1994).

### **M.S 076 anafafanua**

*Nilijifunza Kiswahili kwa sababu wakati wa jeshi la Amini kama wange kusimamisha halafu ujibu kwa Kiswahili walifikiri kwamba wewe ulikuwa mmoja wao hivyo hungepata shida. Hiyo ndiyo ilinifanya nijifunze Kiswahili hata hivyo kwa sasa kimenisaidia katika kufanya biashara zangu. Wakati ule niliona kama tabu lakini nimejitatidi sana kujifunza na kukitumia na sasa kinanifaa.*

Gardener (2000) anasema ari aliyonayo mjifunzaji lugha na motisha anaoupata wakati wa kujifunza lugha hiyo huchangia pakubwa katika ujifunzaji wa L2. Ragba ya mtu kutaka kufanya kitu upata msukumo kutokana na mwelekeo alionao kufanikisha upataji wa umilisi wa lugha anayonuia kujifunza.

#### 4.3.2.5 Mwelekeo

Idadi ya wasailiwa ishirini (22/103) ambayo iliwakilisha asilimia sita (21%), walisema kwamba wao hawakupenda kujifunza Kiswahili ila walijitahidi kujifunza kwa ajili ya kufanya biashara. Wakati wa kujibu hojaji kauli ya kutopenda Kiswahili ilitolewa na msailiwa 041 kama alivyoeleza ;

*I didn't like Kiswahili even now am not really interested but I use few words to associate myself with my customers'.*

Sipendi Kiswahili hata sasa sina jazba nacho lakini natumia maneno machache kuwa sehemu moja na wanunuzi wangu (TY)

Gardener (2000) katika mhimili wake wa tatu anasema kwamba mwelekeo kuhusu lugha huchangia pakubwa katika ujifunzaji wa L2. Mwelekeo ukiwa hasi basi inamchukulia muda mrefu mjifunzaji kujifunza L2 ila mwelekeo na nia ikiwa chanya basi kiwango cha uwezo wa kuelewa kinakuwa juu. Ragba ya mtu kutaka kufanya kitu upata msukumo kutokana na mwelekeo alionao kufanikisha upataji wa umilisi wa lugha anayonuia kujifunza.

Wakati wa mjadala wa mahojiano kati ya mtafiti na wasailiwa ishirini na nane, nukuu ifuatayo ilijitokeza. Nukuu hii hapa chini ilitokana na msailiwa ambaye tayari ana mweleko chanya juu ya lugha ya Kiswahili lakini analazimika kujifunza kwa sababu anahitaji wateja.

#### M.S 081

*Nze banange singa kyisobokka luswairi sanduluyiize kuba silabba weng'enda kulukozesa. Kibi enekku zino banakenya ne batanzania be manji ate be batwala bintu bingi bwotalukozesa batambula ne bakuviira.*

Mimi jamani kama ingewezekana singejifunza Kiswahili kwa sababu sioni mahali popote naenda kukitumia, tatizo siku hizi Wakenya na watanzania ndio wengi na ndio wanachukua viti vingi hivyo usipotumia Kiswahili wanatoeka na kwenda zao (TY).

Mwelekeo hasi huleta changamoto katika ujifunzaji L2 pale ambapo mfanyabiashara ana mwelekeo hasi dhidi ya lugha tumizi inayokuwa vigumu kujifunza. Katika hali hii msailiwa anafanya hivyo tu wakati anapokuwa hana budi. Katika nafsi yake ni kana kwamba anasema, *haidhuru hebu tuu njaribu lakini si chaguo langu*. Dhana hii imekubaliana na Gardener

(2000) ambaye katika modeli yake anasema kwamba mwelekeo kuhusu muktadha wa kujifunza lugha na mwelekeo kuhusu lugha lengwa huathiri ujifunzaji lugha lakini wanaasaikolojia (Lalonde na Microft (1985) na Goold na Rimmer (2000) wanasesma kwamba licha ya hali hiyo kuwepo mjifunzaji anaibuka na msamiati katika lugha tumizi. Atakuonyesha hapendi lugha lakini endapo mazingira yatamlazimu basi atalazimika kuitumia.

**M.S 034 alisema kwamba ;**

*Banange nze singa si bya bizinesi sandiize luswahili kuba banamaje ba Amini batutulugunya. Nga mubisera ebyo buli woita walio lodibulooka, nga bakugamba toa kitambulisho, leta pesa nga tulooza ate amapesa ffe agekungoye bagaza kyi, wewe naenda wapi, wewe kaa chini, banage ao nga olutalo lukaaye. Naye kati ebintubyakuka olabba kati migambo bye twayiga kati bye tusinga kukozesa lwakuba twagala kusubuula.*

Jamani mimi kama si biashara singejifunza Kiswahili kwa sababu jeshi la Amini lilitunyanyasa mno sana. Wakati huo kila mahali ungepita ungepata kuna mzuio wa lodblock wangekusimamisha na kukwambia toa kitambuliso, leta pesa; tulikuwa twajiliza tena mapeesa ni ya nini bila kujua kwamba ni hela maana mapeesa katika lugha ya Kiganda ni vifungo vya nguo; wewe unaenda wapi; wewe kaa chini hapo kama vita vimechacha. Lakini kwa sasa vitu vimebadilika unaona sasa ule msamiati tulijifunza wakati huo ndiyo tunatumia sana kwa sababu twataka kufanyabiashara (TY).

Gardener (2000) anasema kwamba mjifunza lugha anapoathirika na mwelekeo hasi huwa inakuwa vigumu kujifunza L2 ama huchukuwa muda kujifunza lugha hiyo. Msailiwa 034 aliathirika na mwelekeo hasi wakati walipoingiliana na jeshi la kikoloni waliotumia Kiswahili vibaya. Hata hivyo baadaye motisha wa kufanya biashara ulifanya abadilishe mwelekeo kuwa chanya ili aendeleze biashara yake. Motisha mara nyingi husaidia mjifunza wa L2 kujitahidi kujifunza kwa sababu huwa ana msukumo chanya. Walisema kwamba kama si biashara hawangeona sababu ya kujifunza Kiswahili maana siyo lugha yao ya asili. Walidai kwamba ilikuwa kama kuwacha mila yao na kuendeleza utamaduni mwингine.

**M.S 145 alisema,**

*Kikulu kati Kampala yafuuka ya abagwila; olulimi lwaffe telikyakozesewa enyoo, osanga buli kabilia mweli ate nga betulinokukola nabo biznesi mungeriemo obba endalla tulinokuiga luswaili.*

Kwa kiasi kikubwa kwa sasa Kampala imekuwa ya watu ambao si wazawa; lugha yetu haitumiki vikamilifu, unapata kila kabilia liko na ndiyo tunaofanya biashara nao. Kwa njia yoyote ile inatulazimu kujifunza Kiswahili. (TY)

Maoni ya mfanyabiashara 076, 04, 145 yote yanaashiria kwamba bado kuna hiyo hali ya kuwa na mwelekeo hasi dhidi ya lugha ya Kiswahili. Japo wanakiri kwamba pole pole hali

hiyo inapungua, bado kuna mshiko ambao huwezi kufumbiwa macho. Lin (2007) anaamini kwamba kuna uwiano kati ya ujifunzaji, shughuli za ujifunzaji na malengo ya ujifunzaji wakati wa kushughulikia wanafunzi wenyе motisha changamani. Kwa hiyo mtindo wa kulazimika huwa na msukumo wa misaada mingine wakati wa kujifunza L2. Kwa hali hii mwanafunzi anaishia tu kujifunza kile kitakachomfaa kutegemea asasi tofauti. Utafiti uligundua kwamba wasailiwa hawa waliskumwa na motisha ya kufanya biashara, kuteka wanunuzi na kupata faida.

Hali kama hii imeangaziwa tena na Gardener (2007) na Nicholson (2013) juu ya mweleko. kwamba kuna aina mbili za mwelekeo wakati wa kujifunza L2, yaani mwelekeo wa kimaingiliano pale ambapo mjifunzaji wa lugha ya pili huwa na nia ya kujifunza na hufanya urafiki na wazungumzaji wa lugha lengwa. Mwelekeo wa pili ni mwelekeo kiutendaji ambao mjifunzaji lugha huwa nao. Hivyo katika utendaji mjifunzaji lugha hujishughulisha tu na mwelekeo w a k i m a i n g i l i a n o ambayo huchochea kuijendeleza kwa lugha hiyo. Hivyo anamatisha kwa kusema kwamba wajifunzaji lugha walio na mwelekeo wa kimaingiliano hupata motisha chanya juu ya ujifunzaji lugha ya pili lakini aliye na mwelekeo wa kiutendaji huenda ashindwe kujifunza haswa akiwa na motisha hasi. Ushuhudiaji wa mazungumzo kati ya wanunuzi yalibainisha kwamba miongoni mwa wafanyabiashara kuna wale ambao bado wako na mwelekeo hasi kuhusu lugha ya Kiswahili. Hata hivyo inabidi wajifunze kwa sababu wanataka hela.

Huu hapa ni mfano wa mazungumzo kati ya mfanyabiashara R. na mnunuzi T., wote ni wazungumzaji wa lugha ya Kiganda. Wako na wanunuzi ambao wanataka kuwashudumia lakini ile hoja ya kutumia Kiswahili inawakera. Kinachowapa motisha ni ile hali ya kupata pesa kutoka kwa wanunuzi.

### **Mfano wa Data 17 ya mwelekeo hasi kutokana na M. R &T**

- 1      Muz. R:    *Sweety omaliliza nsibbe (switi umemaliza nifunge)*
- 2      Mnz. T:    *Nkyelooza obba ngateeko kyi.Ye lwaki ongobagana.(bado nafikiria sijui niongeze nini.Lakini mbona wanifukuza?)*
- 3      Muz. R:    *Sikugobye naye bakongolee baimilride bagalla mbaguzze.(Sikufukuzi lakini naona wakongo wamesimama wantaka niwauzie)*

- 4 Muz. T: *Ka mbaviire mufutafute luswaili lwamwe nze lwantamantama dda (hebu niondoke muboronge Kiswahili chenu mimi kilinisinya tangu kitambo)*
- 5 Muz. R: *Olwooza nze alwaggala. Naye ndi nokukoola sente. Sweety geenda! (Wafikiri mimi ndio nakipenda-yaani Kiswahili. Hata hivyo lazima nitengeneze pesa. Switi nenda!.*

**Asili: Data kutokana na uchunzaji (Februari, 2022)**

Katika mfano wa 17, wauzaji T na R wote wameathirika na mwelekeo hasi dhidi ya lugha ya Kiswahili. Muz.T anaonyesha kuchukizwa na lugha ya Kiswahili. Tofauti na Muz. R ambaye hata kama hapendi Kiswahili motisha wa kupata pesa inamfanya astahamili matumizi ya Kiswahili. Utafiti huu unakubaliana na Gardener na Lambert (1972), Gardener (2000) na Gardener (2010a) kwamba mwelekeo dhidi ya lugha fulani unafanya mjifunzaji lugha ama kutojifunza lugha ama kuchukua muda mrefu kujifunza lugha hiyo. Mwelekeo unamfanya mjifunza lugha ya pili akose motisha ya kujifunza lugha hiyo.

**Mfano.18 Vizuio**

1. Muz. E: *(anapokea pesa kutoka kwa mnunuzi) Umesabua ngapi*
2. Mun. G: *Nini hiyo?*
3. Munz. Q: *Labda anauliza kama umehesabu pesa vizuri*
4. Muz. L: *(anaingilia ) Pangamavitu muzuri alafu piga esabu*
5. Muz. E: *(Akimaka) Kwani iko nini.pana elewa kusabua si ni swaili pia.*

**Asili: Data kutokana na uchunzaji (Februari, 2022)**

Muz. E anatamka vibaya neno kuhesabu. Ni kana kwamba hataki kusahihishwa. Anaona yuko sawa na anataka kila mtu akubaliane naye. Brown (2020) ametaja hali hiyo kama kasumba ya ujifunzaji wa L2. Mwanafunzi kama huyu hutafuta mbinu za kujitetea hata pale ambapo anajua kwamba amekosea. Anasema mchakato wa kufanya makosa na kusahihisha makosa ili mwanafunzi aboreshe ujifunzaji wake hupata kizuizi cha kasumba ya ujifunzaji lugha tumizi. Ila anasema kwamba mjifunzaji kama huyu hufanya masahihisho yake mwenyewe kwa wakati wake ambao anafikiri anaweza badala ya kulazimishwa kusahihisha makosa yake papo hapo. Mtindo huu unaibua mjadala mionganii mwa wanunuzi na wauuzaji lakini unasaidia wauzaji kujifunza Kiswahili kibiashara. Marekebisho ambayo yanafanywa kwa wakati wao unawajengea umilisi wa kutumia Kiswahili.

Gardener na Lambert (1972) pamoja na Lindsay (1999) wamefafanua namna, ufanisi wa

mjifunza lugha huanzia kwa L1 halafu mjifunzaji anapotangamana na watu wa jamii nyingine anaanza kujifunza lugha hiyo. Hivyo walipendekeza motisha tendaji inayompa motisha mjifunza L2 kutagusana na wazungumzaji wa L2 na kupenda kujifunza zaidi kwa ajili ya kukuza umilisi wa kuwasiliana. Wanaendelea kusema kwamba kinachosababisha ujifunzaji utokee ni motisha inayoambatana na mwelekeo. Hali ya kujifanya hupendi halafu wakati huo huo unakitumia, msingi wake ni motisha changamani ambaeo huzua mvutano akilini mwa mjifunzaji wa L2. Hii ndiyo hali inayotokea kwa wasailiwa ambaeo walidai kulazimika kujifunza Kiswahili kwa ajili ya biashara.

#### **4.3.2.6 Hamasa**

Matokeo ya utafiti yalionyesha kwamba wasailiwa kumi na sita (16/103 ) ambaeo waliwakilisha asilimia kumi na tano nukta tano (15.5 %) walikiri kwamba hamu ya kutaka kujifunza Kiswahili ndiyo iliwafanya wajifunze Kiswahili na kukitumia kibiashara. Dreyer na Oxford, (1996) wanasema mwanafunzi anapofanikiwa, husikia raha na kupata motisha kwa kujifunza L2 na kupenda hiyo lugha. Gardener (2000), Gong, Gao, Lyu (2020a) na Gardener (2010a) na wanasema motisha humfanya mjifunza lugha kupenda lugha anayojifunza na kukuza umilisi katika lugha iliyokusudiwa kujifunza. Waliendelea kwa kusema k u w a Kiswahili kina maneno yanayofanana na ya lugha za Kibantu. Hamu aliyonayo mjifunzaji wa lugha humfanya atumie hali yoyote ile kufanikisha ujifunzaji wa lugha hiyo. Hamasa ni hali ya kuelewa hali ya mtu, kiwango cha kujipongeza, kuzungumzia juu ya hisi na kujipongeza juu ya utendaji mzuri na kuridhia uelewa. MacIntyrena Gregersen (2012a, b) alifafanua umuhimu wa hisia chanya katika ujifunzaji wa L2. Alieleza kwamba hisia chanya ni muhimu sana kuliko hisia tu za kupenda kwa jumla kwa sababu zinachangia uingizi wa lugha kwa mwanafunzi, unakuza ushirikiano wake katika jamii na kutatua shida anazoweza kukumbana nazo wakati wa kujifunza L2.

Hamu ya kujipenda Kiswahili na utamaduni (Gardner, 2000) wake uliwafanya wajifunze Kiswahili na baadaye kukitumia katika biashara. Kwa wale walikuwa na asili ya nchi ama sehemu walikolelewa zilizokuwa zikitumia Kiswahili walisema kwamba, wao wanakipenda Kiswahili kwa sababu wanakitumia katika mazingira tofauti tofauti na baadhi yao walisema kupenda Kiswahili kuliwafanya wasisahau walikotoka. Awali katika utafiti huu tulitaja kwamba kando na khabila asilia za Uganda, kulikuwa na wafanyabiashara wengine ambaeo walitoka nchi zingine za Afrika Mashariki lakini walikuwa wanafanya biashara jijini Kampala. Wengi wao wameishi na kuwa wenyeji.

Kuelewa ni hali ya mtu kujiridhisha (Gardener,2010a) na kile anafikiria kwamba amefanikisha na kufanikiwa na kile alikitaka, kiwango cha wasiwasi, kuzungumzia juu ya hisi, kujipongeza juu ya utendaji mzuri na kuvuta pumzi ya kuridhia kile amepata ndiyo kukuza uelewa wa lugha lengwa. Dreyer na Oxford (1996) wameeleza kuwa mwanafunzi anapofanikiwa, kusikia raha na kupata motisha wa kujifunza L2 na kupenda hiyo lugha ndiyo mafanikio makubwa. Cohen na Olshtam (1993) wanasema hamasa hudhihirika pale ambapo mwanafunzi anafanikiwa kwa matumizi ya lugha aliyoisoma ama kuipata na kuielewa vizuri. Hivyo mfanyabiashara anapowasiliana na wenzake ama wanunuzi wake kwake huona kwamba ni ufanisi mkubwa na kila mtu anapofurahia mafanikio yake, basi atazidi kujifunza lugha lakini iwapo atakashifiwa na kufedheheshwa kila wakati basi atakuwa na mwelekeo hasi na kujifunza hautakuwepo. Matokeo ya mjadala wa mahojiano kati ya mtafiti yalionyesha kwamba wafanyabiashara kumi na watatu walikuwa wanakipenda Kiswahili. Kutokana na mahojiano hayo mfanyabiashara akieleza katika Kiingereza alisema;

### **M.S 118**

*I have been doing business for now ten years.I really love Kiswahili.During our time of bringing up Kiswahili was not a great deal. We knew it was for hooligans.But we are East Africans.We need to develop and we shall not develop if we don't use one language. I really missed learning Kiswahili. I love the language .I get young people here who help me but it would have been good if I had learnt it earlier.*

Nimekuwa nikifanya biashara kwa miaka kumi sasa. Nakipenda sana Kiswahili. Wakati wa tulikuwa tunakuwa Kiswahili hakikuwa na umuhimu. Tulijua nicha wahuni. Lakini sisi ni Wanaafrika Mashariki. Tunahitaji kuijendeleza na hatutaendelea kama hatutumii lugha moja. Nilikosa sana kujifunza Kiswahili. Ninapenda lugha. Ninapata vijana hapa ambao watanisaidia lakini ingekuwa vyema kama ningejifunza mapema (TY)

Hamasa ina nafasi ya kipekee katika kuhusisha shughuli na utambulisho wake. Yaani mtu anapo jishughulisha na kile akipendacho basi humsaidia kukitambulisha katika hali halisi na matokeo huwa chanya. Maandishi ya shirika la NIED (2009) yanasema kwamba lugha huchangia katika ukuzaji wa mtu na pia kukuza maarifa kwa jumla, hamu ya kutaka kusoma, uhakiki maadili na stadi changamani. Kupitia utafiti uliofanywa kwa wanafunzi waliokuwa wakijifunza Kiingereza kama L2 katika shule za sekondari za Namibia, ilibainika kwamba hamu ya kutaka kujifunza Kiingereza ilikuwa na mchango mkubwa kuwezesha wanafunzi hao kujifunza Kiingereza kama L2. Kiwango cha juu cha hamasa humsaidia mtu kuamua kufanya lile ambalo anaweza kufanya kwa hiari na kupenda au kutopenda.

Kukoleza kwamba wao walijifunza Kiswahili kwa sababu ya kukipenda ni ishara ya motisha chanya. Namna ambavyo walikipenda Kiswahili kiliwasaidia kuboresha umilisi wao wa kuwasiliana na wenzao na hata wanunuzi ambao walitoka nje mwa Uganda. Matokeo yetu yanakubaliana na wazo la Oxford (1996) kwamba kupenda hudhihirika pale ambapo mwanafunzi anafanikiwa (Guilbault, Harvey na Vallerand, 2020). Kwa matumizi ya lugha aliyoisoma na kuielewa vizuri. Nao kina Dreyer na Oxford (1996) walikiri kwamba usipoipenda lugha, inakuwa ngumu kujifunza na unaichukia. Kwao kupenda Kiswahili kulifanya wajifunze Kiswahili bila kuona ugumu wowote. Kwa njia ya kutilia mkazo namna baadhi ya wasailiwa walikipenda Kiswahili.

### **M.S 078**

*Nze luswaili nalwegomba daaa kuva miaka jjada. Lwe olulimi lwotateekamu amanyi maanji kulusoma. Nkwasagana mpola mpola . Ate kati bwendi omusuubuzi njijjakweyogela kuluiga nokulukozeesa.*

Nilitamani Kiswahili tangu miaka ya zamani. Ni lugha ambayo hutumii nguvu nyingi kusoma. Najitahidi polepole. Na hivi sasa kwa vile mimi ni mfanyakibashara nitaendelea kujifunza na kikitumia.(TY)

Katika ujifunzaji lazima mwanafunzi awe na hamu inayosukumwa na motisha wa kujifunza. Oxford (1996), anatumia mfano wa wanafunzi ambao walikuwa wanajifunza L2 darasani ila kwa muktadha wa wafanyakibashara wanajifunza kwa hali zisizo rasmi ili wawasiliane na wanunuzi katika lugha ya Kiswahili. Muaka (2020) akinukuu kazi ya Oxford na Shearin (1994) anasema kinachowapatia wanafunzi wengi motisha ya kusoma L2 ni kutokana na mafanikio wamepata ambayo inawafanya waendelee kupenda ujifunzaji wa L2. Katika kiunzi cha motisha cha Williams na na Burden (1997 ) anaelezea kwamba mwelekeo chanya juu ya lugha ya jamii lengwa na utamaduni humpatia motisha mjifunzaji L2 kujifunza lugha hiyo.

### **M.S 116 kutoka ekedi ya Mukwano ambaye anauza mabegi ya wanawake**

*Kuna namna tu tunawapenda wanunuzi wetu kutoka mataifa ya ujirani; Mkenya akifika hapa huwa anataka ahudumiwe mara moja aondoke; mtanzania licha ya kuwa na haraka atasema kwa sauti nyororo nay a unyeeyekevu, mKongo anarusha rusha na kuchanganya maneno ya Kiswahili na ya kilingala. Huwa tunapenda namna wanazungumza Kila anayekuja twajaribu kuzungumza kama wao ila Kiswahili chetu nacho huwa tumechanganya Kiganda ndani mwake.*

Mafanikio ya mfanyakibashara ni kuwa na wanunuzi wengi na biashara yake kuendelea.

Wanaokipenda Kiswahili walisema hawajilaumu kujifunza Kiswahili kwa sababu wanaweza kuwasiliana na wanunuzi kutoka pembe zote za Afrika Mashariki. Waliongezea kusema kwamba wanapotumia lugha asili na Kiingereza wanunuzi huwaona kama wana kiburi lakini wanapowasiliana katika Kiswahili wanunuzi huwaona kama wenzi wao na kuwaaminia kwa kile wanachouza. Hali ya kupenda hujenga uhusiano bora kati ya mfanyabiashara na mnunuzi na pia mfanyabiashara na mwenzake katika hali hiyo.

#### **4.3.2.7 Kuashiria**

Wasailiwa tisa (13/103) ambao ni asilimia kumi na mbili nukta sita (12.6%) wakati wa kujaza hojaji walikiri kutumia viashiria kama namna ya kupata msamiati wa vitu ambavyo vilikuwa vikitajwa na wasemaji wa lugha ya Kiswahili. Kutokana na matumizi mapana ya viashiria waliweza kuweka kumbukumbu ya baadhi ya msamiati wa Kiswahili waliokuwa wakitumia.

Ili kupata ufanuzi zaidi kuitia mahojiano mfanyabiashara 150 anaeleza;

#### **M.S 150**

*You can see in these shops we share. Everyone has a stole. So we arrange in the way that one has a stole for ladies skirts, another dresses, another tops, another children clothes. We call of them clothes (nguo) but we could not separate their names until customers from Kongo, Sudan, Kenya na Tanzania started to buy clothes in lampsome. We started learning types of clothes by customers pointing on what he/she wanted.*

Unaona katika hili duka tunashirikiana. Kila mmoja ana safu yake. Hivyo tunapanga kwa namna ambayo mmoja ana safu ya sketi za kike, nguo,s afu nyingine ni blauzi za kike, nyingine ni nguo za watoto. Tunaziita zote nguo ila tulikuwa hatuzitenganishi kwa majina hadi wateja kutoka Kongo, Sudan, Kenya na Tanzania walipoanza kununua nguo kwa wingi. Tulianza kujifunza aina za nguo kutokana wateja kuelekeza anachotaka. (TY)

Krashen (1987) anasema kwamba wakati w kukumbana na dhana mpya, kuna uwezekano mjifunzaji L.2 ashindwe kutaja kile ambacho anataka kuongea. Hivyo huishia tu kuashiria. Kwa kuongezea Gardener (2000) katika mhimili wa pili wa ari anasema kwamba katika juhudzi zote afanyazo mjifunzaji wa L.2 huwa kuna nia ambayo imemsukuma. Pili anaendelea kusema katika mhimili wake wa nne kwamba kila mjifunzaji wa L.2 ana uwezo wa kujifunza L.2. Uwezo huo unaweza kutokana na kipawa cha kuona na kutenda ama kusoma na kuandika. Hapa tunaona kipawa cha kuona na kutenda ambapo ni kuashiria. Kwingineko Ellis (2003) anasema kwamba ili mjifunza lugha ya pili kuelewa zaidi lugha lengwa, lazima

kuwepo na kiashiria anachokionaa ndiyo iwe rahisi kwake kujifunza L2. Wanunuzi mara nyingi hufuata kile wamekiona na kuwapendeza. Hili liliwafanya baadhi ya wafanyabiashara kutumia fursa hiyo ili kujifunza baadhi ya msamiati wa biashara katika Kiswahili. Mfanyabiashara mmoja ambaye alikuwa anauza mabegi na mikoba alikiri kwamba mara ya kwanza hakujuua nini maana ya mkoba. Kila wakati mnunuzi angemuuliza mikoba ni pesa ngapi yeze angewaambia kwamba hana. Hadi siku mmoja alifikiri anafanya usamaria alipomuelekeza mnunuzi mahali wanaiza mikanda kwa sababu alifikiri yule mgeni ameshindwa kutamka “enkoba” mkanda/mshipi katika Kiganda; Ilibidi mnunuzi aashirie mikoba/mabegi ndiyo akaelewa kilichokuwa kinaulizwa. Mahojiano kati ya mtafiti na msailiwa 140 namna alivyojifunza kutokana na kuashiria ni kama inavyodhahirishwa katika mjadala unaofuata hapa chini.

**Mtafiti:** *Ogambye mukuiga oluswaili kyavya muggwe bulikaseere okusongammu mubyotuunda (Umesema katika kujifunza Kiswahili kulitokana na wewe kila wakati kushiria kwa vitu unavyouza)*

**Msailiwa:140:**

*Ehh mwantu! Abasubuuzi bajanga wano mbu nkoba pei gani,nkoba pei gani. Nga mbagaamba nti hapana iko. Nendooza ntini ayaggala enkoba za kwesiba. Kyenakolla kwe kumsindika jebatundila enkooba.*

Ndiyo yakhe! Wateja huja hapa eti mkoba ni bei gani! Mkoba bei gani. Nawambia haiko. Nikafikiri kwamba anataka msidhipi ya kujifunga. Nilichofanya ni kumsukuma kwa aliyezwa anauza mishipi (TY).

**Mtafiti:** *Wakyuzuula otya nti ayaggala ensau:(Uligundua vipi kwamba alitaka mkoba)*

**Msailiwa 140:** *Anti yasongamu munsau zendina nagaamba, apana mshipi mimi taka hiyo mikoba. Aoneng’amba nti ooooh okay. Nentegeera nti ayagalla ensau. Ate kati naiga abbalala baziita begi.*

Aliashiria kwenye mikoba niliyonayo akasema, hapana mimi nataka hiyo mikoba. Hapo nikasema sawa. Nilielewa kwamba anataka mkoba. Tena sasa nilijifunza kwamba wengine huziita begi (TY).

Gardener (2000) katika mhimili wake wa nne yaani uwezo wa mjifunzaji, anafafanua kwamba kila mjifunzaji wa L.2 ana sifa za kuona na kutenda kile anachostahili kutenda. Katika hali ya kuashiria, anatambua jina ya kile kilichoashiriwa. Gardner (keshatajwa)

ameshadidiwa na Prah (2003) Oxford (2003) Palma na Madrigal (2021) katika tafiti zao kuhusu mitindo na mikakati ya ujifunzaji wa L2. Wameorodhesha vipengele vinne vya kintindo ambavyo humwezesha mjifunzaji wa L2 kujifunza lugha hiyo. Yaani kuona kile kinachofundishwa, kusikia anachosoma, kutembea na kuona kile kinachofundishwa na kugusa kile kinachofundishwa. Kwenye mazingira yasiyo rasmi ari ndiyo inayokuwa kipengele kikubwa kumsaidia mjifunzaji wa L2 bila kusahau matumizi ya viungo vya mwili. Kwa wafanyabiashara ambao walijifunza Kiswahili kupitia huu mtindo, walisema kungetokea mnunuzi ambaye alitaka marashi, Ilikuwa vigumu kutambua msamiati wa marashi bila mnunuzi kuashiria kwenye marashi aliyoyataka. Wengi wao wamejifunza Kiswahili kwa namna hiyo. Kwa kuongezea, data kutoka uchunzaji nayo iliwakilisha mtindo wa kuashiria. Wasailiwa katika mazungumzo yafuatayo wanadhihirisha walivyotafuta namna ambayo ingewawezesha kuwasiliana na wanunuzi katika soko la Kikubo;

### **Mfano. 12 Mazungumzo**

1. Mun. 11: (*Anaingia dukani huku amebeba mizigo mingine*) ehh! Nimechoka
2. Muz. 13: (*anamsongezea kiti cha plastiki. anamunyoshea mkono kumuashiria akae*)
3. Mun. 11: *Umeleta nini kipyta. Nataka new arrival*
4. Muz. 13: (*anashika kijiti na kuonyesha bidhaa alizo nazo*) hii, hii na iyo
5. Mun. 11: *Hivyo virauli na vikombe vyake ni bei gani? Halafu naona una oven nzuri na blenda tofauti tofauti. Kwani zatofautiana kwa bei?*
6. Muz. 13: *Anagusa vifaa anavyoulizwa na kuuliza hii! oba hii! Okay blenda hii ni mitwalo kumi, hii ni mitwalo nane.*

### **Data kutokana na uchunzaji; Macho 2022**

Kuna mazungumzo ambayo yanaendelea kati ya Mun:11 na Muz.13. Muuzaji anakuwa na maneno machache mno ya kujibu mnunuzi badala ya kutoa ufanuzi. Ilibainika kwamba kule kutumia sana kuashiria kulimsaidia kutambua baadhi ya majina ya bidhaa. Alikuwa hajui baadhi ya majina ya vyombo alivyokuwa akiiza katika Kiswahili. Ile hali ya kuashiria na kugusa akionyesha bidhaa ni namna alivyotambua na kupata kuelewa msamiati wavyo. Ufanuzi wa Reid (1987) ni kwamba watu wazima mara nyingi huhofia kujifunza huku wakifanya makosa. Wanapenda kuwa kwenye mazingira ambayo watatumia viungo vyao vya mwili kugusa ama kuashiria kile ambacho wanakiona. Kitu ambacho Oxford (2003) na

Benzehat (2021) wameeleza pia kwamba kujifunza kwa kugusa ni hali ya kufanya msamiati kung'ata akilini mwa mjifunzaji. Oxford na Benzehat (keshatajwa) anakubaliana na mawazo ya awali ya Brown na Douglas (2006) kwamba kisaikolojia mwanafunzi anayejifunza kuitia hali hii huwa ni yule mwanafunzi ambaye anachukua muda wake kujifunza bila kubabaikia ujifunzaji. Mtindo huu hutumiwa na wanafunzi ambao hawataki kuharakishwa katika ujifunzaji wao wa lugha tumizi katika mazingira ya kuendeleza mazungumzo.

#### **4.3.2.8 Hulkta za mjifunzaji**

Biashara yoyote ile huhusu kubadilishana bidhaa ama huduma. Ubadilishanaji huu hutokea kuitia mawasiliano kati ya muuzaji na mnunuzi. Tendo la ubadilishanaji bidhaa ambalo ndilo kiini cha biashara hutegemea mpangilio wa zamu kimatamshi kufanikisha biashara. Mpangilio huo hufanikishwa na tabia za ama muuzaji au mnunuzi. Kuna wale ambao wanapenda mzaha na kuna wanunuzi ambao huwa hawana muda wa mzaha. Matokeo ya hojaji yalieleza tu kwamba tabia za kushirikiana na wanunuzi ndizo zilizowasaidia wajifunze Kiswahili kwa ajili ya biashara .

Vile vile mjadala wa mahojiano kati ya mtafiti na wasailiya sita walisema kwamba tabia za mtu zinaweza kupelekea mjifunzaji Kiswahili ama akose kujifunza au kufanikiwa katika kujifunza lugha. Walieleza kuwa tabia hizi hutegemea hali alimo kisaikolojia wakati wa mawasiliano ya kubadilishana bidhaa. Endapo nafsi yake iko chanya basi atajumuika katika ujifunzaji lakini pale ambapo akili na hisia zake hazimruhusu kujifunza, basi hata ujifunzaji hautafanyika kama ilivyoelezwa na msailiwa 021;

*The truth is that I like jocking so much. Am not particular with place or person but when I get a chance where I can talk and jock with people who speak Kiswahili I do so. I often make jokes with buyers who come from different places where they speak Swahili and I enjoy it.*

Kwa kweli ninapenda mizaha sana. Sina uhakika na mahali ama mtu lakini nkipata fursa ninaweza kuongea na kufanya mzaha na watu wanaoongea Kiswahili basi nitafanya hivyo. Huwa ninafanya mizaha na wanunuzi ambao wanatoka maeneo tofauti tofauti ambapo wanaongea Kiswahili na huwa inanifurahisha.

Hali ya kubadilishana bidhaa na ujumbe hupelekea mfanyakiareshara awe na ari (Gardener, 2000). Krashen (1987) katika mhimili wake wa mfumo halisi anasema kwamba kwa wanafunzi ambao wana hulkta za kuongeaongea katika mazingira halisia ya ujifunzaji wa L.2 hujifunza kwa urahisi kuliko wale wanyamavu. Hoja ambayo imeshadidiwa na wataalamu mbalimbali kama Minti (2012); Nicholson (2013) Toboso na Mosol (2018) wanaeleza

kwamba watu huongeaongea wakati wa kujifunza L.2 kwa ajili ya kufanikisha mawasiliano. Wataalamu hawa wanatumia mfano wa Kiswahili wakifafanua kuwa wale wanoongeaongea wakati wa kujifunza Kiswahili hujifunza na kufanikisha mawasiliano. Kwa wajifunzaji ambao ni wanyamavu hali yao huwa ni tofauti. Hali hii inaelezwa na msailiwa 049 anayesema kuwa;

**M.S 049 alisema kwamba,**

*Kila mtu ana tabia yake. Kwa mimi siyo mtu wa kuongea ongea sana.  
Najuwa Kiswahili kidogo kidogo lakini iko Swahili ingine iko ngumu kabisa.  
Iko wakati nikuwa embarrassed kasitoma alifika kama mimi nimeenda fasi fulani. Niliambia yeye minakuja. Bado jua unasema ninakuja. Sasa siwezi ongea sana lakini kidogo kidogo mimi naelewa.*

Hulka hufanya mjifunzaji kuona haya anapojikuta amekosea alichotaka kuongea. Uoga wa kufanya makosa huwafanya wawe wanyamavu na waogope kuongea. Hivyo huwa wanachukua muda mrefu kujifunza. Hunges (2003) anasema kwamba wanafunzi kama hawa wakiwa wanazungumza hutokwa na jasho, wanasitasita na kuduwaan wanaposhindwa kuzungumza neno. Maelezo haya na utafiti wetu unaendana na wa mwanaasaikolojia Kameerer (1990) anayefafanua kwamba motisha na msukumo unaodokeza tabia za mtu, kiwango cha utendaji na nguvu ambazo mtu hutumia katika taasisi fulani humwezesha kufanikisha ama kutofanikisha ujifunzaji wa L2

Chomsky (1988) naye anasema kwamba mtoto hupata lugha bila mafundisho yoyote. Hii inamaanisha mtoto anapozaliwa huwa ana kipawa cha kupata lugha yoyote ile. Amerejelea kipawa hicho kama LAD na baadaye akakifafanua kama nadharia ya sifa bia. Anaendelea kusema kile kinachohitajika ni kipawa hicho kushtuliwa ndipo kianze kutumiwa na mtoto kupata na kujifunza lugha yoyote ile. Maelezo haya yanaongeza kukazia yale ya Krashen (1987) katika kiwango chake cha kwanza cha upataji lugha. Anasema ujifunzaji lugha ni mchakato usio fahima wa mtu ambao kuitia kwa mchakato huo kitivo cha kipawa cha ujifunzaji lugha hushtuliwa na kuanza kutumika na hatimaye kujenga umilisi wa lugha kwa ajili ya mawasiliano. Anaendelea kusema kwamba katika hatua ya unyamavu, huchukua muda wake kujifunza lugha. Lugha ya Kiswahili siyo ya kuparamia tu; unahitaji kumakinika, kujifunza kwa makini na polepole ndiyo uelewe kile ambacho kinazungumzwa; la sivyo utajikuta unafanya makosa na usielewane na mnunuzi wako. Ila kila wakati waliofanikiwa walijihifadhia misamiati hiyo akilini ili kuwawezesha kuendeleza mawasiliano kibiashara kila wakati wanakuwa na wanunuvi ambao wanatumia Kiswahili tu.

Kwa jumla kila mtu huwa ana yale ambayo anajua na huenda yeye mwenyewe asijue kwamba anajua dhana fulani. Kwa hiyo kipawa (Gardener, 2000) chake kinapokutana na msamiati fulani utakuta anafuutilia bila utata. Mara nyingi kiwango hiki huwa ni cha kisintaksia ambacho ni kiini cha sarufi kuwezesha kuwepo kwa mawasiliano sahihi. Licha ya kuwa kiwango cha kipawa cha wafanyabiashara si cha kiwango cha watoto, hata hivyo huwasaidia katika ujifunzaji wa Kiswahili kibiashara.

#### **4.3.2.9 Mpango binafsi**

Mahojiano kati ya mtafiti na wasailiya kumi na wawili walikiri kwamba kuna mpangilio walioufuata ili kutumia Kiswahili katika kuendeleza biashara. Hii ni kwa sababu hawakuwa na muda wa kutafuta madarasa ya kujifundisha Kiswahili hivyo kila mmoja angejipanga namna ya kujifunza na kutumia Kiswahili. Walisema kila kitu kinachoendelea katika maisha ya mtu ni kujipanga kisaikolojia, hali na shughuli. Miongoni mwao walisema mwanzo mpango binafsi unakufanya ufikirie ni nini kinahitajika ili kufanikisha kitu fulani. Mathalani utaanza vipi kutumia Kiswahili ambacho si lugha yako.

Kijikaratasi ambacho watafiti walikutana nacho kutoka kwa msailiya kinaonyesha namna walivyoagiza anunuliwe bidhaa fulani kutoka kwa mfanyabiashara mwenzake. Katika hicho kijikaratasi ametuma ujumbe kwa kutumia maneno ya Kiswahili kwa kuchanganya pia lugha asili *ni* kama ilivyo katika mfano ufuatao.

*"Mwami Njorogye nunuliya mimi hii bintu- ninunulie hivyo vitu". Diski, simu ya tekno. Ametumia maneno kama diskii ni sente ngapi (**ila akakumbuka kwamba angesema shilingi ngapi**) halafu akaandika siringi ngapi*

Alituelezea kwamba alianza kupanga fikra namna atakavyowasilisha ujumbe huo katika Kiswahili. Ujumbe ulipangika akilini kutumia L.1 halafu akauhawilisha ujumbe huo katika Kiswahili. Japo kuna maneno ambayo si sawa katika Kiswahili, utafiti wetu haukunuia kupima matumizi ya Kiswahili sanifu ila namna Kiswahili kinavyoweza kutumika katika biashara.

Maandishi haya yanaweza pia kutumika kwa wafanyabiashara tofauti na wanunuzi tofauti. La muhimu ni kujizoesha kutumia hayo maandishi halafu baada ya muda mrefu wa kuyatumia unaweza kuzungumza bila hata kutumia kijikaratasi ama kutafuta mahali ilipoandikwa. (Krashen, 1987), Purpura (1999) aligundua kwamba mpango binafsi ni mkakati bayana na mwafaka kwani humsaidia mwanafunzi kwa shughuli za kujipanga

namna anavyojifunza. Hata hivyo katika mawazo yanayofuata wataalamu wamesema kwamba mpango binafsi ni mtindo wa ujifunzaji L2. Wakati mwingine huenda mhusika akaandika maneno katika vijikaratasi ambavyo atarejelea wakati anapotaka kuvitumia au sivyo kuandika maneno machache mkononi mwake ili iwe rahisi kwake kuyatumia. Wanafunzi hawa huwa wanapenda kujisomea na kujifunza msamiati wao kwa wao. Hata pale Simlaw mfanyabiashara kwa jina Segujja alionyesha namna yeye huandika kwanza bidhaa anazoagiza kutoka Nairobi Kenya kisha anamtumia mfanyabiashara mwenzake ujumbe wa simu ambaye hununua na kutuma. Walisema wao hujipangia namna ya kujisomea, shughuli za kujifunza lugha lengwa, kukusanya zana na kujifunzia, kupanga muda na mahali pa kujisomea. Huu ni msukumo kutokana na ari aliyonayo mjifunzaji L2. Walisema mpango huu uliwasaidia kujifunza Kiswahili. Mpango binafsi humsaidia mjifunza L2 kumaliza shughuli zake za kujifunza kwa mfano kuna wale wanajiandikia vijikaratasi ambavyo walitarajia kuvitumia kila wakati wanataka kutumia lugha lengwa (Pupura, 1999). Mpango binafsi huenda sambamba na ujifunzaji binafsi. Mjifunza lugha anapopata motisha (Gardener, 2000) na ari ya kujifunza L2, hupanga yapi yatatangulia na yapi yatafuata. Ufanisi wa mtindo huu ni pale ambapo mjifunzaji amelekezwa na mhimili wa Gardner (2000) wa ari ya kujifunza yeye mwenyewe. Huenda kukatokea makosa yanayofanywa lakini haiwi kizuo cha kujifunza lugha ya Kiswahili kibiashara. Kipengele cha ujifunzaji binafsi ni kipengele cha stadi za kimaisha (Oxford, 1985) na anayejifunza anaenda kukitumia katika maisha yake.

Oxford (1985) na Purpura (1999) waliangalia mpango binafsi kama mikakati ya ujifunzaji wa L2 wakati Gardener (2000; 2010a; 2007) alipokuwa akielezea motisha changamani alisema, ni vigumu kutenganisha mikakati na mitindo kwa sababu mikakati ni tukio wakati mitindo ni msukumo mjifunzaji L2 alionao. Hivyo kama mjifunzaji L2 hana msukumo wowote hakuna jinsi ataanza kujipangia namna ya kujifunza. Cohen & Weaver (2011) anasema kwamba licha ya kuwa mikakati ni jinsi ya kupata ujumbe na ujuzi juu ya L2, ari na mwelekeo wa mjifunzaji l2 atatumia, itamsaidia kujijengea umilisi wakati wa kujifunza L2.

#### **M.S 074 alisema,**

*Mimi huwa wanunuzi kutoka nje ya Uganda kwa mfano Tanzania ama Kenya wakija kwa duka langu huwa ninarikodi mazungumzo baina yao na sisi wafanyabiashara halifu baadaye nasikiza namna walikuwa wakizungumza. Kwa kufanya hivi naigiza namna wanavyozungumza ili baadaye nikipata wanunuzi wengine najaribu kutamka namna wanatamka.*

Kitendo cha kurekodi mazungumzo huibua dhana ya upangaji. Msukumo na ari aliyonayo

juu ya matumizi ya Kiswahili kibashara ndiyo inayomfanya arekodi hayo mazungumzo ili yawe ya kufanya mazoezi kwa ajili ya kutumiwa kwenye biashara. Krashen (1987) katika mhimili wake wa nne anasema kwamba ingizo tambuzi ndilo muhimu katika umilisi wa lugha. Yaani mjifunzaji akionyesha umilisi wa L.2 basi huwa ameimarika katika kutunga sentensi sahili na changamani kama ilivyo katika msailiwa 074.

**Nukuu: M.S 093 alisema,**

*Katika You tube huwa kuna mwalimu anafundisha salamu na msamiati mbali mbali .Hili huwa nalifanya mapema sana nikifika hapa. Nimefanya hivyo kwa miaka mitatu. Hivyo huwa nahifadhi hayo mafunzo halafu narudia rudia nikishashika huo msamiati nafuta halafu naweka mwingine. Huwezi kuyashika yote kwa wakati mmoja hivyo huwa narudia wakati wangu wa kupumzika ama wakati sina wanunuizi.”*

Kuna mambo mengi ambayo yanaingiliana lakini katika muktadha huu tunamwangalia msailiwa namna anapanga mafunzo yake na ni vipi anakuja kutumia alichojifunza baadaye.

Katika utafiti wa Lindsay (1999) iligundulika kwamba upatanifu kati ya mitindo ya ujifunzaji na ufundishaji L2 hukuza ujifunzaji na wanafunzi kuridhika kwamba ujifunzaji ulikuwapo. Kwingineko Montgomery na Grout (1998); Goold na Rimmer; 2000 wanasisitiza kwamba, ni bora kuweka matini nyingi katika mitandao ya kielektroniki na shughuli nyingi zinazolenga viwango tofauti vya ujifunzaji ili mjifunzaji L2 ajichagulie kile ambacho anataka kujifunza kuititia mtindo anaoutaka. Watafiti hawa walisaidia kuwekea mkazo utafiti huu kuonyesha namna mjifunzaji lugha anavyoweza kutumia mtindo alioupenda ambao ulimwezesha kukuza umilisi wa kutumia Kiswahili kwa ajili ya biashara.

**M.S 098 alisema,**

*Watembeyi huwa wanaauza vitabu vidogo vidogo .kitabu kya kufundisha Luganda; iyo kyitabo wanaita ‘Swahili-Luganda Akatabo akayigiriza olulimi oluswayiri’. iko maneno mengi ya kusalamia, kununuwa, chakulya, manguo na bitu minge. Kyitabu iyo nasaidia mimi kupata maneno ya Kiswahili ya kutumia.*

Mtumiaji L2 huchagua nyenzo za lugha kwa mfano kuititia kuwaza, kuchanganua na kufanya mihtasari fupifupi, kuorodhesha na kupanga ujumbe ili kumrahisishia matumizi katika lugha tumizi. Krashen (1987) anafafanua ya kwamba wakati wa kujifunza L2 dhana mpya ya pembejeo zenyе sifa za kisarufi zilizo zaidi ya kiwango cha chini huwa na uwezo wa kupata sifa hizo. Hivyo ujifunzaji ni matokeo ya pembejeo zinazoleweka na sio zile zinazozalishwa. Pembejeo hufanywa kueleweka kwa msaada uliotegemea muktadha. Kwa mantiki hii mfanyakibashara hupanga ujumbe ambao amekutana nao katika mazingira ambayo

anayaelewa. Hali ya kujipangia ujumbe inatokana na nia, motisha na uwezo wa kujifanya mambo (Gardener, 2000; 2010).

Wataalamu hawa (Mowrers 1950, Gardener 1985, Cohen 1998, Long 1991, Gardener 2000, Moenika na Zhed-Babelon (2010); Nicholson, 2013) wanakubaliana kwamba mtindo ni njia mahsusini kisaikolojia ya kupata ujumbe na elementi za kusaidia ujifunzaji L2 wakati dhana hiyo inatendeke, mjifunzaji lugha kuitia tabia zake, nia, jitihada, mwelekeo kuhusu lugha na motisha changamani humsaidia mjifunzaji L2 kukuza umilisi wake na kutumia umilisi huo katika mazingira yanayostahiki. Ilikuwa bayana utafiti huu kushughulikia vipengele vyote sambamba ili kubaini jinsi wafanyabiashara hujikuta wanazungumza Kiswahili.

Kuna wale walisema kwamba mahali wangelisikia kwamba wamekwama, wangeashiria, ama kukodolea macho kile wanataka kukisema halafu mzungumzaji wa lugha lengwa angeliwasaidia kutamka kile mfanyabiashara alitaka kukitamka. Kwingineko walitumia fursa ya wanunuzi ambao hawakuwa na haraka kuuliza maneno ambayo yalikuwa magumu wakati wa mpokezano wa kimawasiliano kati yao na wanunuzi wao.

Tukumbuke kwa kiasi kikubwa ni vigumu kutenganisha mkakati na mtindo maana yana uhusiano wa karibu sana. Yana kamilishana hasa pale ambapo mjifunza wa L2 anataka kujijengea tajriba ya umilisi wa lugha lengwa (Cohen, 1998). Kwa mfano utafiti huu uligundua kwamba mtindo wa mpango binafsi unaweza kutokea kihali na kiutendaji. Hayo mawili yakiwezesha ujifunzaji wa L2, basi mkakati na mtindo kwa pamoja yamefanikisha ujifunzaji wa Kiswahili katika biashara mjini Kampala, Uganda. Kwingineko mwingiliano hutokea pale ambapo kuna mtagusano wa kawaida wa watu katika jamii na mtagusano na ukuruba kati ya wanunuzi na wauzaji. Hivyo, mkakati wa ukuruba wa mtagusano na ukuruba kati ya wanunuzi na wauzaji na mtindo wa mtagusano wa wafanyabiashara inaingiliana ili kufanikisha ujifunzaji wa Kiswahili mionganoni mwa wafanyabiashara. Kwa jumla mitindo ya ujifunzaji lugha hutegemea tabia, ujuzi na hali ya kisaikolojia ambayo inamsaidia mjifunzaji lugha kuwa na mwelekeo na mwngiliano katika mazingira alimo ya kujifunza lugha lengwa (Keefe, 1979).

#### **4.4 Changamoto zinazowakumba wafanyabiashara wakati wa kujifunza Kiswahili kibiashara**

Data zilizotokana na hojaji na usaili zilijibu swali la changamoto ambazo wafanyabiashara hukumbana nazo wakati wa kujifunza Kiswahili kibiashara. Aidha, data hizo zilipatikana

kwa kujaza maswali ya hojaji na mjadala wa ana kwa ana kati ya mtafiti na wasailiwa. Mhimili wa nne na tano wa krashen (1987) na mhimili wa Gardener (2000) wa tatu, nne na tano zilielekeza data kuhusu changamoto wajifunzaji L.2 hukumbana nazo wakati wa kujifunza L.2 kama katika mijadala itakayofuata.

**Jedwali 4.15: Changamoto ambazo wasailiwa walikumbana nazo kujifunza Kiswahili kama lugha ya biashara jijini Kampala**

No	Changamoto	Idadi	Asilimia
1	Changamoto za kisarufi	13	12
2	Changamoto za muda wa kujifunza	07	7
3	Kutumia lugha ya Kiswahili kimshtukizo	05	5
4	Lugha ya mseto	14	14
5	Mwelekeo hasi dhidi ya lugha ya Kiswahili	18	17
6	Ukosefu wa mafunzo rasmi ya Kiswahili	07	7
7	Athari za kisiasa	13	12
8	Mazingira ya kufanya biashara	04	4
09	Uoga	08	8
10	Tofauti za Kijinsia	05	5
11	Changamoto za kanuni na vipengele vya	09	9
Kisimu			
<b>Jumla</b>		<b>103</b>	<b>100%</b>

**Asili : Data ya Nyanjani kutokana na hojaji (Februari,2022)**

#### **4.4.1 Changamoto za kisarufi**

Wasailiwa kumi na tatu (13/103 ) waliojaza hojaji walisema kwamba lugha ya Kiswahili ni ngumu. Hoja nyingine ilikuwa kwamba mwingiliano wa lugha mama uliwaathiri sana wakati wa kujifunza Kiswahili kibashara. Mara nyingi walijikuta wakifanya makosa wakati wa kutumia Kiswahili. Miiongoni mwa makosa ambayo yalijitokeza yameorodheshwa katika jedwali 4.16 lifuatalo;

#### Jedwali 4.16: changamoto za kisarufi

Makosa	Kiswahili Sanifu
Pei kali	Bei ghali
Mucungwa	Mchungwa
Sowaani	Sahani
Saati	Shati
Mafuta (wakimaanisha ya taa)	Mafuta ya kujipaka ama ya taa
Saawa /chaa	Saa
Dulowa ya kkabada	Drowa ya kabati
Abari ya subui/Mchana/kyioni	Habari ya asubuhi/mchana/jioni
Natunda manguo pei msuli	Nauza nguo kwa bei nzuri
ii bintu pei kani?	Hivi vitu ni bei gani
Mi nausa muzuri apana ipia wewe	Ninauza vizuri sikuibii
Kitambulisho yako iko wapi	Kitambulisho chako kiko wapi
Twende kwa poolisi	Hebu twende kituo cha polisi
Alitumanga mali na basi ya Buscar	Alitura mali/mizigo kwa basi la Buscar
Bosi njoo kesho tapata bintu muzuri	Bosi njoo kesho utapata vitu vizuri
Lafiki Chacha/kati wee napita kupita?	Rafiki sasa wewe unapita kupita?

*Asili ya data:Nyanjani kutokana na mahojiano,Februari 2022*

Kutokana na hizo data utaona kwamba kuna utata wa kutamka sauti /p/ badala yake wanatamka /ph/ ya mpumuo ama /b/ ambapo wakati wa kutamka sauti hewa haiachiliwi kama ile ya Kiswahili ya kipasuo. Kwao sauti ya kipasuo ni /bb/ ambapo ni konsonanti ambatani. Makosa mengi yaliyotajwa wakati wa kukusanya data yalitokana na udondoshaji baadhi ya sauti, uchopekaji wa sauti na uhamishaji wa L.1 katika matumizi ya Kiswahili. Kwa mfano wazungumzaji wa lugha ya Kiganda huwa wana utata wa kutamka sauti /r/ hivyo mara nyingi palipo na neno lenye sauti /r/ wao hutumia /l/ halafu pia mahali kuna /sh/ wanatumia/s/. Katika konsonanti 18, Matovu (1978) anasema hakuna saiti /sh/ hivyo mara nyingi wanatumia sauti /s/ mahali pana sauti /sh/ ya Kiswahili. Japo baadaye Nakibuuka (1995) aligawa sauti hizi kifonolojia na kuweka sauti /sh/ sehemu ya ufizi kaaka gumu ila mifano anayotoa ya kutamka sauti hizo ni katika Kiingereza kama (Sheep, sheet nk.) Mifano ya maneno yanayotokana na sauti hizo ni michache kutoka lugha ya Kiganda. Katika Kiswahili sauti /sh/ ni ya sehemu bapa la ulimi na kaaka gumu (Hymes,1975; Mgullu,1999; Habwe na Karanja, 2004; Massamba, 2012) na mifano yake ni mingi katika lugha ya Kiswahili.

Vile vile kwa mahali pa kutamkia sauti ya /h/ ya glota katika Kiswahili (Mgullu,1999; Habwe na Karanja, 2004) huleta utata katika matamshi ya maneno kama *habari*, *ujambo*, *huendi*, nk. walikuwa wakiyatamka kama *abari*, *ujambo*, *uendi* nk. Hii ni kwa sababu sauti hii haiko katika fonolojia ya kiganda. Krashen (1987) katika mhimili wake wa nne na tano wanasesma

kwamba wakati wa kujifunza mjifunzaji L.2 dondosha baadhi ya sauti ama kuchopeka ili kufaniksha ujifunzaji wa L.2. Anapokuwa na mwelekeo chanya na uwezo wa kusoma na kuandika humsaidia kufanikisha ujifunzaji katika L.2.

Wakati wa mahojiano kati ya mtafiti na wasailiwa, msailiwa alieleza namna alikumbwa na changamoto wakati walikuwa wanapewa mafunzo na mwalimu aliyefaa kuwafunza Kiswahili chini ya KACITA.

### **M.S 090**

*Walio akaseera omusuubuzi ommu yangamba nti nataka mafuta paka, nze namugamba nti mafuta iko petrol station ate nga ga taala si gakwesiiga. Yambuza nali nkoola kyi nga tosobola kutuunda ebizigo. Nanyiiga naye nembuza lwakyi agambye nti nveeo ate nga ntuunda bizigo. Kyambeerera ekizibu okutegeera nti yali ayagala bizigo*

Kuna wakati mteja mmoja aliniambia kwamba anataka mafuta ya kupaka, mimi nilimwambia mafuta yako kwa petrol station tena ni ya taa hakuna ya paka. Aliniuliza nilikuwa nafanya nini kama siwezi kuza mafuta; nilikasirika lakini nikauliza kwa nini anasema niondoke na ninauza *bizigo*; ilikuwa vigumu kugundua kwamba alitaka mafuta ya kujipaka (TY).

Alieleza changamoto aliyokumbana nayo wakati akimuhudumia mnunuzi ambaye alimfikia akihitaji mafuta ya kujipaka. Kuna baadhi ya utamaduni pale ambapo jina linaweza kuibuka na maana tofauti kumuktadha. Katika lugha ya Luganda mafuta huwa ni ya taa lakini ya kujipaka yana jina lake tofauti na mafuta katika Kiswahili pale utapata mafuta ya taa, mafuta ya kujipaka n.k

### **M.S 154 alisema,**

*Learning a foreign language is one of the hardest things one can do in an old age. What makes a foreign language so difficult is the effort we have to make to transfer between linguistically complex structures. It's also challenging when you start to think how and when you will learn another language .It needs a lot of effort and dedication.In a situation where getting profits is a priority you forget to put language in the fore front.*

Kujifunza lugha ya kigeni ni mojawapo ya mambo magumu zaidi ambayo mtu anaweza kufanya katika uzee. Kinachofanya lugha ya kigeni kuwa ngumu sana ni juhudzi tunazopaswa kufanya ili kuhamisha kati ya miundo changamano ya lugha. Pia ni changamoto unapokaa kufikiria jinsi na lini utajifunza lugha nyingine. Inahitaji juhudzi nyingi na kujitolea. Katika hali ambayo kupata faida ni jambo la kwanza unasahau kupatia lugha kipaumbele (TY).

Krashen (1987) katika hatua ya tatu ya ujifunzaji lugha anasema kwamba katika hatua hii mwanafunzi huwa anajaribu kutunga sentensi katika L.2 na mara nyingi sentensi hizi

hubuka na makosa kwa sababu mjifunzaji anawazia na kuhamisha sheria za L.1. Hoja ambayo imekolezwa na Gardener (2000), Gass na Selinker (2008) kwamba mjifunzaji wa L.2 hukumbana na changamoto nyingi wakati wa kujifunza L.2. Hali hii inaweza kuibua motisha hasi ambayo inaweza kuchelewesha ujifunzaji wake.

#### **4.4.2 Muda wa kujifunza**

Data kutokana na hojaji zilionyesha kwamba wasailiwa saba (07/103) walikuwa na upeo na muda mchache wa kujifunza Kiswahili. Walisema kila wakati walikutana na wanunuzi tofauti ambao walikua na msamiati tofauti na walitarajia wazungumze namna wanazungumza. Wengine waliona ni kana kwamba hawajali ila msamiati ndiyo huwa umepotea. Muda pia ulikuwa kipengele kingine ambacho ni changamoto wakati wa kujifunza Kiswahili kibiashara. Biashara ni sekta yenyewe shughuli mno hivyo ilikuwa vigumu kwao kutenga muda wa kutosha wa kujifunza Kiswahili kwa ajili ya biashara namna anavyoeleza mfanyabiashara M.S 017

#### **M . S 017:**

*You come here early and leave at night when you are tired theres no way you can get time to learn Kiswahili. Our chairman for traders in Kampala City brought for us a teacher to teach us Kiswahili but he would not teach for one hour; This time was not enough and we were equally many who wanted to learn Kiswahili.*

Hapa unaingia mapema na kutoka usiku kama umechoka hakuna namna utaanza tena kupata muda wa kujifunza Kiswahili. Kiongozi wa wafanyabiashara alituletea mwalimu kutufundisha Kiswahili lakini alikuwa anafundisha kwa saa moja tu; huu muda ulikuwa hautoshi na wengi tulitaka kujifunza Kiswahili (TY).

Mfanyabiashara 029 alitoa sababu zilizowafanya washindwe kujifunza Kiswahili kibiashara.

*Sisi kama wafanyabiashara tunahitaji kujifunza mambo ambayo ni ya biashara; Lakini yule mwalimu alitufundisha Kiswahili kupitia KACITA alikuwa anatufundisha mambo mengi kwa lisaa limoja (saa moja). Alitufundisha ngeli kwa lisaa limoja hata sasa sikumbuki kitu.*

Krashen (1987) katika mhimili wake wa nne wa dhana mpya, anasema kwamba mwanafunzi anapoanza kuwasiliana na wazungumzaji wa L.2 basi huwa umilisi wake katika hiyo lugha umeanza kuimarika kutegemea motisha na dukuduku aliyonayo. Hata hivyo katika mhimili wa tano anasema kwamba ili mjifunzaji apate umilisi vizuri, lazima mtu aangalie umilisi alio nao mjifunzaji na muda ambao mjifunzaji L.2 anatangamana na lugha yenye .

Ehrman na Oxford (1989) na Gardner (2000, 2010) wanasema kwamba athari ya motisha juu

ya ujifunzaji wa L2 huathiri ujifunzaji wa lugha. Waliendelea kusema kwamba uchaguzi wa taaluma na muda wa ujifunzaji huathiri ujifunzaji wa L2 ambao huambata na motisha ya ujifunzaji. Waliokipenda Kiswahili walidai kwamba wangkuwa na muda wa kutosha wangkuwa wamejifunza Kiswahili vya kutosha. Malalamishi ya muda yametolewa katika nukuu ifuatayo;

#### **M.S 145:**

*Nayagalla bansoomese ebigambo tugezze omusuubuzi bwaja mbuze onataka nini, ekyintu kino ssente bweziti, bwentambula mbuuze nyiinza nyta kufuna emaali nae ekyiffo ekyokubogula. Obba bangaambe bwooba oyagalla kwogera nomusubuuzi ouuwo nya kuandika nyta ksiimu obba njogera nya. Ekyeembi batusomesa manya ngeli, abantu bawaka ate kati sibijukira bukungi. Ezo ngeli nzibu enyo ate ffe kati obwongo bwaguba. Nalabba nga bimalila budde.*

Nilitaka nifundishwe mambo kama vile mnunuzi akija nimuulize unataka nini, bidhaa hii ni pesa fulani, nikisafiri niulize viperi nitapata mali na mahali pa kununulia bidhaa. Ama niambiwe ukitaka kufanya mawasiliano na mnunuzi wako nitaandika namna gani ujumbe kwa simu ama nitazungumza viperi. Kwa bahati mbaya walitufundisha sijui mambo ya ngeli watu wa nyumbani, hata sasa sikumbuki nilichosoma. Hizo ngeli ni ngumu za kuelewa na akili yetu ishakomaa. Niliona tu wananimalizia muda (TY).

Hata hivyo kuna wale walidai kwamba muda ambao walikuwa wakipewa mafunzo ulikuwa ni mdogo sana na walikuwa na mwalimu mmoja ambaye angefundisha darasa la wafanyabiashara wasiopungua chini ya mia sita. Msailiwa huyo aliendelea kusema kwamba ukumbi wa KCCA (Kampala Capital City Authority) ambao walikuwa wakifundishwa Kiswahili kwa kupitia mpango ulioanzishwa na mwenyekiti KACITA (Kampala City Traders“ Association) ulikuwa mdogo. Kila wakati walihudhuria ukumbi huo ungefurika na wafanyabiashara zaidi ya mia tano na tulikuwa na mwalimu mmoja ambaye angelichukua tu saa moja kutupa mafunzo. Wengi wao waliambulia patupu. KACITA ni chama ambacho kina kusanya baadhi ya wafanyabiashara jijini Kampala. Kando na mpango wa mafundisho mbalimbali huwasaidia katika mambo mbalimbali kama ya mikopo ya benki, haki za wafanyabiashara katika Ekedo na soko, kuunganisha wafanyabiashara na wamiliki wa Ekedo na maduka ya soko zilizo patikana jijini Kampla, kusimamia ushuru endapo kuna mfanyabiashara yejote ambaye alikumbwa na matatizo nk.

#### **4.4.3 Kutumia lugha ya Kiswahili kimshutikizo**

Kutofanya mazoezi ilikuwa mojawapo ya changamoto za kujifunza Kiswahili kibiashara. Wasailiwa watano (05/103 ) ambao waliwakilisha asilimia nne nukta nane (4.8%) walikiri

kwamba licha ya mazingira wanamofanya biashara, ilikuwa vigumu kutumia Kiswahili mahali pengine popote. Kuanzia mwaka wa 1971-1979 wakati wa utawala wa Rais Idi Amini inakumbukwa kwamba alipendekeza matumizi ya Kiswahili kwa asasi zote licha ya wabaganda kukipinga. Licha ya katiba ya 1995 kutaja kwamba Kiswahili kitatumika kama lugha ya pili rasmi nchini Uganda, matumizi hayo yamepuuzwa kwa watu wengi, Chimerah (2010) hivyo ni nadra kutumia kwa mazingira ya kawaida. Hii imezidi kuwa changamoto ya kukuza umilisi wa mawasiliano katika Kiswahili mionganoni mwa wafanyabiashara jijini Kampala. Wakati wa mahojiano kati ya mtafiti na wasailiwa, malalamishi yalitolewa kama inavyoonyeshwa katika nukuu hii hapa chini,

### **M.S 102**

*You know you have to gamble with the Kiswahili language .Its try and era.If Kiswahili was taught like any other language in schools during our days we would have grasped a little to use in our daily life and business.Other than Kiswahili as a business person i have learnt many languages without using books or grammar of that language.I gamble with vocabulary of say Arabic, chineese feew!i find myself interacting with Chineese business people.*

Unajua inabidi ubabanye maneno katika lugha ya Kiswahili. Ni mambo bahati na sibu. Kama Kiswahili kingefundishwa kama lugha nyingine shulenii enzi zetu tungekuwa tumeshika kiasi cha kutumia katika maisha na biashara zetu za kila siku. Zaidi ya Kiswahili mimi kama mfanyakibashara. Nimejifunza lugha nyingi bila kutumia vitabu au sarufi ya lugha hiyo. Najaribisha msamati na kusema Kiarabu, Kichina! Feew! Najikuta nikitangamana na wafanyakibashara wa China. (T.Y).

Wasailiwa wengi walilaumu uongozi wa awali ambao haukufanya mikakati ya ufundishaji Kiswahili katika viwango vya awali. Waliokosa mafunzo kama hayo wanalaumu vibaya hali yoyote ile ambayo ilipinga matumizi ya Kiswahili nchini Uganda.

#### **4.4.4 Lugha mseto**

Wafanyakibashara kumi na nne (14/103) ambao waliwakilisha asilimia kumi na tatu (13%) walisema kwamba kuwepo kwa lugha nyingi jijini Kampala kulikuwa kizungumkuti katika ujifunzaji wa Kiswahili kibiashara. Uganda ina zaidi ya lugha 56. Kwa zile ambazo zilifanyiwa maandishi ni kama kumi. Hata hivyo kutokuwepo lugha ya taifa ya matumizi, raia wana uhuru wa kutumia lugha ambayo wanataka kulingana na muktadha. Hivyo inakuwa vigumu kumthibiti mtu kwa kutotumia lugha ya taifa ambayo haipo. Utafiti uligundua kwamba mji mkuu wa Kampala ni mji wa lugha nyingi. Licha ya kuwepo na zaidi ya lugha 56 lugha za kigeni nazo hutumika kutegemea na matakwa ya mtumiaji.

Miongoni mwa lugha ambazo zilififikirika kuwa ni za kigeni ni pamoja na Kiswahili, Kifaransa, Kichina, Kiarabu na lugha nyingine ambazo ziko karibu na mipaka ya Uganda. Walibaini kwamba Kiswahili chenyewe pia kilikuwa na viswahili viswahili vingi. Kwao hawakujua Kiswahili sanifu kilikuwa kipi, hivyo waliishia kujizoesha na kile wanunuzi wao walitumia. Kupitia mjadala wa mahojiano na wasailiwa, mtafiti alifanikiwa kupata nukuu ifuatayo;

**M.S 098;**

*Sisi hatujui tujifunze Kiswahili cha wapi; Kiswahili cha Kenya ni rahisi kidogo lakini Kiswahili cha Tanzania, Kongo na Burundi ni kigumu, maneno mengine ni magumu. Tena tushakuwa watu wazima kujifunza lugha zaidi ya moja inakuwa ni vigumu.*

Utafiti pia uligundua kwamba si kila mtu aliweza kuwasiliana vizuri katika Kiswahili kwa sababu ya kuchanganyika kwa ndimi nyingi ilihali wafanyabiashara wanatangamana na kila wanunuzi na lazima wawahudumie. Inakuwa ni vigumu kujikita katika lugha moja kwani itaonesha ubaguzi na hata hupoteza wanunuzi. Krashen (1987) katika mhimili wake wa tano anasema kwamba ni muhimu mjifunzaji L.2 kuelekezwa katika ujifunzaji wa lugha moja mahsus. Gardener (2000) anasema katika hali ambapo lugha inaelekea kuwa ngumu kuna uwezekano kwamba mjifunzaji ataibuka na mwelekeo hasi kuhusu lugha hiyo.

Wataalamu hawa wameshadidiwa na Herman (2009) ambaye anasema kwamba wanafunzi ambao lugha zao za kwanza hazitumiki shulenii hushuhudia viwango vya chini vya ujifunzaji wa L2, hivyo kuwa na uwezekano mdogo wa kuchangia uchumi wa nchi na maendeleo ya kitaaluma. Utafiti huu uliusika moja kwa moja katika kubaini changamoto wafanyabiashara hukumbana nazo wakati wa kujifunza Kiswahili kibiashara. Biashara ni sekta ambayo nayo huchangia uchumi wa nchi. Wengi wao walikiri kwamba Kiswahili siyo lugha ambayo wanatumia nyumbani kwa mawasiliano. Hali hii iliwaapelekea kuchukua muda mrefu kujifunza Kiswahili kwa sababu walikuwa wanajifunzia tu katika mazingira walimokuwa wakifanya biashara zao. Kiswahili kilihitaji uelewa mwingi wa msamiati na namna ya kuitumia. Kila mnunuzi alikuja na msamiati wake. Mingine ilikuwa migumu na mingine ilikuwa ikieleweka hivyo walijifunza kidogo tu. Wakati mwingine ilibidi watumie Luganda-Kiswahili ili kuwasiliana na wanunuzi. Hili kwa wakati mwingine lingezua utata wa kimaana. Licha ya matumizi ya Kiswahili; Kiganda kilitumika sana hivyo kwa wakati mwingine walijikuta wanazungumza kwa Kiganda kwa wanunuzi ambao hawakujua Kiganda ama kubadilisha msimbo kulingana na namna wangetathmini mwonekano wa mtu.

Mfano walioutoa ni kufikiria kwamba kila mwanamke aliyekuwa mweupe na hajui Kiganda angechukuliwa kuwa ni Mkongomani wakati hata hajui kusalimia kwa KiKongo ama Kiswahili. Athari za kutazama na kumtathmini mtu kutumia fikira makosa kwamba alielewa kile ulichokuwa ukizungumza. Hii ilikuwa changamoto kubwa angeanza kuzungumza Kiswahili ila tu mnunuzi ndiye aliyeanzisha kuongea.

(Cook, 1993; Burt na Dulay, 1973; Schmidt, 1980) wanasema kwamba mwanafunzi wa L2 anapojifunza kwa mazingira ya wingiluga, hujikuta anachanganya mifumo ya lugha kutoka lugha tofauti kwa lugha anayojifunza. Ufafanuzi wa wataalamu hawa unashadidia utafiti wetu pale ambapo makosa kama hayo yaliibuka miengoni mwa wasailiwa. Kulitokea kuathiriana kwa maneno kama *sabua/kuhesabu, unafanyizia/unatumia, ndito/msichana, wayo/wao, kubahatisha/kuhangai*ka nk. Hali ya kutaka watumie Kiswahili sanifu kwa baadhi ya wanunuzi ilikuwa ni vigumu kwao. Kiluganda-Kiswahili kimechukua nafasi kubwa katika matamshi ya wazungumzaji wengi nchini Uganda hasa sehemu za biashara.

#### **4.4.5 Mwelekeo hasi dhidi ya lugha ya Kiswahili**

Tofauti za uongozi wa kifalme ulifanya Kiswahili kipingwe vikali. Data kutoka kwa hojaji ilionyesha kwamba wasailiwa kumi na nane (18/10 ) ambao waliwakilisha asilimia kumi na saba (17%) walikiri kwamba mwelekeo hasi dhidi ya matumizi ya Kiswahili umechangia pakubwa matumizi ya Kiswahili jijini Kampala. Mmoja wa wasailiwa alisema ni vigumu kuzungumza na kila mnunuzi katika Kiswahili haswa kwa wazawa ambao ni wanganda. Unapoanza kuzungumza Kiswahili ni kana kwamba unataka kujikita katika nasaba ambayo siyo yako ama wengine wanakuachia bidhaa yako na kuondoka. Kando na Mazingira ya biashara ni vigumu kuendeleza matumizi ya Kiswahili kwa wanajamii wa nyumbani.

Upinzani dhidi ya lugha ya Kiswahili ulianza tangu enzi za zamani. Ujiwa wa dini ya Kikristu ulifanya matumizi ya Kiswahili kuonekana kama lugha ya kigeni ya kuendeleza Kiislamu. Chimera (2000) akimrejelea Whiteley (1969) anasema kando na tishio la dini ya Kiislamu, kulikuwa pia na kabali la Waganda ambao walidai Kiswahili ni lugha ya kigeni hivyo haina mashiko yoyote na lugha wa Kiganda. Pia Buganda ilikuwa na mfalme wake na lugha ya Kiganda. Matumizi ya Kiswahili yanepotosha kaida na tamaduni ya Buganda na kufikiria kila mtu yuko sawa nao. Wakati wa mahojiano mfanyakia 029 akisema kwa mhemko kwamba;

*Kiriza nti luswaili telwaali olulimi lwaffe naye kyitukakatako kulukozesa lwa kubba twetabika naAbagwiira kuva bweli bwa Ugandana abasubuuzi abe*

*njaulo. Olusawaili lwatufuula bakimbizi munsoonga etitategeerekeka. Bapoolisi baali bazibu enyoo nga bakozeesa luswaili nga batufosinga kogeera luswaili. Singa si busuubuzi sandiize luswaili ate silabba lwakyi omwana wange asome luswaili.*

Tukubali kwamba lugha ya Kiswahili haikuwa lugha yetu ila tunalazimika kutumia kwa sababu ya Mtagusano na wageni kutoka nje mwa Uganda na wafanyabiashara tofauti. Kiswahili kilifanya wengi wetu tukawa wakilbizi kwa sababu zisizoeleweka. Askari walikuwa wakali wakitumia Kiswahili na kutulazimisha kuzungumza Kiswahili: Kama si biashara singejifunza Kiswahili na hata sioni kwa nini mtoto wangu afunzwe Kiswahili(TY).

Aliwasilisha changamoto kwa huzuni na namna zilimuathiri katika ujifunzaji wa Kiswahili. Mwelekeo hasi dhidi ya lugha ya Kiswahili. Kulingana na maelezo ya huyu msailiwa, athari hasi ilitokana na mitazamo ya awali kuhusu matumizi ya Kiswahili. Ni vigumu kumbadilisha na kumwambia kwamba haikuwa lugha ya Kiswahili ila waliokitumia ndio walipanda mbegu mbovu za matumizi ya Kiswahili (Mukama, 1995). Hoja ambayo imeshadidiwa na Gardener (2000) ambaye katika modeli yake anasema kwamba mwelekeo kuhusu muktadha wa kujifunza lugha na mwelekeo kuhusu lugha hukwaza ujifunzaji wa lugha. Wasailiwa walikiri kwamba hakuna namna biashara inaweza kuendelezwa bila matumizi ya Kiswahili. Hivyo walijaribu kushawishi wenao ambao bado wana mwelekeo hasi kubadilisha mwelekeo na kuanza kujifunza Kiswahili polepole ili kuendeleza vizuri biashara.

#### **4.4.6 Ukosefu wa mafunzo rasmi ya Kiswahili**

Kuanzia jadi mfumo wa ujifunzaji haukuwa rasmi. Mafunzo yalitolewa kwa wakati fulani na sehemu maalum kama chini ya mti ama kwa mduara watu wakiota moto majira ya jioni. Hata hivyo ujio wa wakoloni ulirasmisha asasi ya elimu na inakiskiwa kwamba kila mtu lazima apitie mfumo huo. Kwa hali ya Kiswahili ilivyo nchini Uganda, historia yake ni tofauti. Kutokana na majibu ya hojaji wasailiwa saba (07/103) waliowakilisha asilimia sita nukta saba (6.7%) walibaini kwamba kutopata mfumo rasmi wa masomo ya Kiswahili kibiashara uliathiri umilisi wao wa kujifunza Kiswahili kibiashara. Walidai kwamba mafunzo ambayo yalikuwa yameandalika na KACITA yaliwapa mafunzo ya jumla. Hata hivyo wakati wenyewe wa kujifunza Kiswahili ulikuwa ni mfupi sana na Kiswahili walichokuwa wanafunzwa kwao kilikuwa kigumu mno kulingana na namna walivyokitumia wakifanya biashara. Pia ilikuwa vigumu wao kutambua hasa ni Kiswahili gani wangeweza kujifunza na kukitumia. Hali hii ilitokana na wanunuzi tofauti tofauti kutoka maeneo tofauti kutumia Kiswahili kinachotaofautianana. Ikumbukwe kwamba kihistoria ujifunzaji wa Kiswahili nchini Uganda umesukwa na hali ya kuridhiana na kutoridhiana kuhusu mitaala na ufunzaji

wa lugha, lini na wakati gani Kiswahili kifunzwe na kiwango cha kufundisha Kiswahili. Mfanyabiashara mmoja alisema kwamba waliwaweka katika ukumbi wa City Hall wawe wakisoma Kiswahili. Alisema kwamba namna Kiswahili kilivyofundishwa, ilikuwa tofauti na namna walivyokitumia katika mazingira walimokuwa wakifanya biashara. Walisema kwamba Kiswahili ambacho walijifunza kilikuwa kigumu kuliko kile walichotumia wakati wa kufanya biashara.

#### **M.S 122 alisema**

*Ffe abekoleera bwananyini tebatufaako. Kubba kati tulinekiibina bandikyikoze nga teka nti buli omusuubuzi eyewandisa mukibiina kya banabizinesi nte ffena tulunokusoma lulimi luswairi. Bino bituyamba kukoleera wamu nne banabizinesi banaffe kukulakulana*

#### **4.4.7 Athari za kisiasa**

Wanasiasa huwa na mchango mkubwa katika ujenzi wa taifa. Maamuzi ambayo wanafanya huathiri nchi kwa namna moja ama nydingine. Wasailiya kumi na tatu (13/103) waliowakilisha asilimia kumi na mbili (10%) na wasiiliwa wengine ishirini na mbili ambao waliwasilisha hoja zao kupitia mjadala wa mahojiano walikiri kwamba siasa zilikuwa kikwazo kikubwa katika ujifunzaji na matumizi ya Kiswahili kibiashara; Tangu Kiswahili kipendekezwe kutumika ni kipindi cha Rais Idi Amini ndiyo Kiswahili kilipamba moto. Rais Idi Amini alikuwa na nia nzuri ya matumizi ya Kiswahili kwa wakati huo ila jeshi la wakati wake ulifanya watu kukichukia Kiswahili na mtu ye yote ambaye anazungumza Kiswahili.

Kuna wale ambao walisema kwamba kama si biashara hawangejifunza Kiswahili kwa sababu jeshi la Amini lili wanyanyasa sana. Msailiya 094 alisema kwamba wakati huo kila mahali ungepita ungepata kuna mzuio wanakusimamisha wakikwambia;

*“Toa kitambuliso, leta pesa,” Mfanyabiashara mmoja alisema. Tulikuwa tunajiuliza tena “mapesa” ni ya nini bila kujua kwamba ni pesa kwani “mapesa” katika lugha ya kiganda ni vifungo vya nguo; wewe unaenda wapi; wewe kaa chini hapo kama vita vimechacha. Lakini kwa sasa vitu vimebadilika unaona sasa tunakitumia kwa ajili ya matumizi ya biashara”.*

Waliopitia hali kama hii walisema wanatumia Kiswahili tu kwa ajili ya kupata wanunuvi na wala si kwa ajili walikipenda Kiswahili. Baada ya utawala wa Idi Amini Rais Museveni alikipenda Kiswahili na kukitumia pia katika mazingira rasmi.”

Napenda kuwatajia umuhimu wa lugha moja ambayo inaweza kuzungumzwa na watu wote Afrika Mashariki hata katika utangamano. Kiingereza, Kifaransa, na lugha nyinginezo zinazotumika sio nzuri sana katika mawasiliano kwa sababu si kila mtu anaweza kuzungumza lugha hizo. Mimi mwenyewe nilifundishwa Kiingereza kwa miaka 17 na hata sasa siwezi kuzungumza vizuri. Lugha ambayo itafaa ni Kiswahili hasa kwa ajili ya utangamano (Museveni, 1990).

Hii imebaki tu kama tamko na maandishi ila bado msisitizo unatakikana. Kiswahili kimekuwa kikitumika kwa wingi na wanasiasa na wala si kwa ajili ya biashara. Hiki kinabaki kitendawili kwa wafanyabiashara kama kweli Kiswahili kitawasaidia wafanyabiashara pia ama wanasiasa pekee.

#### **4.4.8 Mazingira ya kufanya biashara**

Wasailiwa ishirini na wanne (04/103) waliowakilisha asilimia nne (4%) wakati wa kujaza hojaji walisema kwamba mazingira ambayo walikuwa wakifanya biashara yalikuwa magumu. Kuna wakati walipata changamoto kuitia wafanyabiashara wenzao ambao waliwaonea wivu ama kutotaka kushirikiana nao. Kwa wale ambao hawakujuu Kiswahili walifikiri kwamba waliokuwa wakitumia Kiswahili walipata wanunuzi wengi kuwaliko ama kujionyesha kwamba ni weledi wa lugha nyingi. Katika mjadala wa majadiliano walisema kwamba Kiswahili kiliishia tu pale ambapo walikuwa wanawasiliana na wanunuzi ama wafanyabiashara wenzao lakini walipokuwa wakifika nyumbani ilikuwa vigumu kuendeleza mazoezi ya Kiswahili wakati jamii ilikuwa nyumbani kwao walikuwa hawakitumii.

Kwingineko matumizi mabaya ya awali ya lugha ya Kiswahili yalifanya Kiswahili kichukuliwe kama lugha ya wahuni. Maneno kama *fungua mlango! Toa pesa! Onatoka wapi !!!* Yalitumika kwa makali kutoka kwa ama wanaojua lugha ama kutokana na wazawa wa lugha hiyo, hivyo kufanya watu wengi kuchukia Kiswahili. Iteleweke kwamba mikakati na mitindo ya ujifunzaji L2 husukumwa na ari, mwelekeo na motisha (Gardener, 2010) na mazingira mazuri ya ujifunzaji (Chomsky 1968; Selinker 2008 na Krashen 1987). Mwanafunzi hujaribu kujifunza lugha kutokana na kupenda utamaduni, kuzungumza na kuiga kaida na tamaduni za lugha lengwa, mazingira ya kikoloni yalipelekea wajifunzaji kuchukizwa na matumizi mabaya ya Kiswahili ya wakati huo. Walipendekeza kushirikisha waziri wa maswala ya biashara na viwanda namna wafanyabiashara wanaweza kunufaika kibashara kwa kutumia Kiswahili ambacho kitawaunganisha wafanyabiashara wenzao katika nchi nyingine.

#### **4.4.9 Uoga**

Matokeo ya hojaji na mjadala uliotokana na mahojiano ulionyesha kwamba uoga wa kujifunza Kiswahili uliwafanya wachelee kujifunza Kiswahili. Walisema kwamba wakati mwingine ilikuwa vigumu kuzungumza Kiswahili wakihofia kwamba wangelifanya makosa. Wakati wa mahojiano mfanyabiashara 130 alisema

*Nze silwakubba sisobola kwogeera luswaili naye ntya buti kuloogera. Nze sizalibwa mubaswaili ntya okogeera naabantu abamanyi luswaili. Ekyizibbu kyili mukoogera naabo abamanyi enyoo luswaili. Baanji tutya kogera kubba tujjakuswala oba lusi noyoogeera mafukule. Wandibba owemula nga toomanyi obba okolla mistakes omunntu nakusekeleela.*

Mimi si eti siwezi kuongea Kiswahili lakini naogopa Kukiongea. Mimi sizaliwi uswahilini naogopa kuongea na wajuao Kiswahili. Shida ipo katika kuongea nao wajuao sana Kiswahili. Wengi tuaogopa kuongea kwa sababu tutaaibika ama sivyo tuongee vitu ambavyo havipo. Unaweza kuwa unaongea matusi kama hujui ama unafanya makosa halafu mtu akakuchekelea (TY).

Uoga kama ilivyoelezwa na Chomsky (1965) na Krashen (1987) hutokea pale ambapo mjifunzaji lugha huathirika na umilisi na utendaji wa lugha. Wanaendelea kusema kwamba umilisi wao huathirika pale ambapo anaogopa kutuma umilisi wa lugha katika kutafakari na kutoa neno lililo sahihi kutegemea ujuzi, utambuzi na kumakinika katika sheria za lugha lengwa; wanaoathirika na hii hali huwa ni wanafunzi wanyamavu maana wanataka kujichukulia kama shujaa wanaofahamu lugha bila makosa. Wasailiwa walisema kuwa kila kitu huwa na utata kikianza, lakini kadri unapoendelea kuwa na mazoea nacho unazidi kuelewa. Walichohitaji ni kujiamini.

#### **4.4.10 Tofauti za kijinsia**

Jinsia kama kipengele cha jamii huathiri ujifunzaji wa lugha ya pili: Wasailiwa tano (05/103) waliwakilisha asilimia tano (5%) wakati wa kujibu hojaji walithibitisha kwamba wanawake huwa na motisha wa juu katika ujifunzaji wa L2 tofauti na jinsia ya kiume. Kulingana na mwelekeo wao waliona wanawake huwa ni wenye kujifunza L2 kwa haraka; sababu walizotoa ni kwamba wanawake huwa na kustahamili wakati wa kujifunza L2 na huwa na upole chanya wakati wa kuwasiliana na wazungumzaji wa lugha lengwa. Ni wepesi wa kufanya marafiki, wepesi wa kujaribisha na hata wanaweza kutumia Kiswahili katika mazingira nje ya biashara. Ila Ilisemekana kwamba kilichokuwa kinawazuia Wakati mwingine ilikuwa tu dukuduku ya juu ambayo huwafanya waogope kujifunza L2; na huchukua muda kujifunza L2. Kupitia mjadala na mmoja wa wafanyabiashara alisema

kwamba,

*Kujifunza lugha huwa ni rahisi kwa wanawake na watoto wadogo. Wanawake wanazungumza zungumza sana kuliko sisi wanaume. Sisi huwa si watu wa kujifunza funza lugha nyingi ila kama umelazimika kufanya hivyo.*

Kwa kutilia mkazo (Gardener na Lambert,1972, Liu,1973, Oxford na Nyikos,1990) wanasema jinsia ya kike huwa na motisha na mwelekeo chanya na hutumia mikakati na mitindo ya ujifunzaji wa L2 tofauti na jinsia ya kiume ambao wanapenda kufanya mambo yao ya kimyakimya. Wao hawatangamani sana kama jinsia ya kike (Oxford,1989; Nyikos,1990; Ehrman na Oxford; Prokop,1989). Hii ndiyo sababu hupelekea jinsia ya kiume kuchukua muda mrefu kujifunza L2. Kwa kufafanua zaidi, wanasaikolojia Larsen na Long (2000), Zhuanglin (1989) na Boyle (1987) katika kazi ya Savile-Troike (2012) wanasema kwamba katika ujifunzaji wa lugha iwe L1 ama L2, jinsia ya kike hufaulu sana kuliko wanaume. Wanaamini kwamba wanaume na wanawake huzaliwa na tofauti za kiisimu kwa sababu wanawake huzungumza na kujifunza lugha ngeni haraka kuliko wanaume.

Kiswahili kimeenda kikikubalika. Wanasiasa wengi wamekuwa wakihamasisha na kupigia debe matumizi ya Kiswahili. Kwa hiyo ni wakati wafanyabiashara washirikiane na wanasiasa kama hao kuendeleza biashara kwa kutumia Kiswahili.

#### **4.4.11 Kanuni na vipengele vya kiisimu**

Ujifunzaji wa L2 kwa kiasi kikubwa kumefungamana katika vipingele vya isimu kuliko tu mawasiliano. Wasailiwa tisa (09/103) ambao waliwakilisha asilimia tisa (9%) walitanabahi kwamba Kiswahili walichohitaji kilikuwa tu cha mawasiliano licha ya kusisitiziwa sheria za lugha namna walivyokuwa wakifundishwa ngeli na mwalimu ambaye walipangiwa kujifunza. Wameungwa mkono na wafanyabiashara ambao walihusika katika mahojiano ya ana kwa ana wakati wa kukusanya data. Walisema kwamba mkondo huo wa ujifunzaji ulifanya masomo ya ujifunzaji Kiswahili kibiashara yakawa magumu sana kuliko matakwa na malengo yao ya Kufanikisha biashara. Wasailiwa walisema kwamba maneno mengine yalikuwa na zaidi ya maana moja ambayo iliwakanganya. Maneno yaliyowapatia changamoto ni kama nyanya/bibi, mwanamke/mke, mshipi/mkanda nk. walisema kwamba wao walijua kwamba nyanya ndiyo (tomatoes) halafu bibi (wife), mwanamke (any woman) mke pia (any woman) walishangazwa kusikia kwamba ‘bibi’ ni ***mama wa mzazi wa kike au kiume***. Wasailiwa waliendelea kusema kwamba mfumo wa ujifunzaji Kiswahili ulikuwa mpana sana. Kwao waliona kwamba Kiswahili kimejifunga sana katika (ngeli) kuliko

kuzungumza tu lile mtu alifikiria ni sawa. Kujifunza sauti za Kiswahili pia ilikuwa ni chananoto kwao. Kwa mfano (**ky-ch**), (**s-c**), (**ng'-ng**)

Long (1990) na Gardener (2000) wanasema mtagusano na motisha wa kufunza lugha ndiyo hufanikisha ujifunzaji wa L2. Anatahadharisha wajifunzaji wa L2 kwamba siyo lazima wawe weledi wa fonolojia, mofolojia na sintaksia ya lugha hiyo ila washughulike na maana ya kisemantiki kulingana na mazingira ambayo anatumia lugha hiyo. Anaendelea kusema kuwa ujifungaji katika kanuni na vipengele vya lugha hukwamisha ujifunzaji wa lugha hiyo. Jjinga na Bakize (2021) wanasema kwamba wakati Kiswahili kinatumiwa zaidi kama L.1 au L.2 katika muktadha wa Kenya na Tanzania, nchini Uganda kwa kiasi kikubwa Kiswahili kinachukuliwa kama L.3 sio tu kwa ajili ya asili yake lakini pia kutokana na kukosekana kwa matumizi mengi nchini. Hii inaashiria kuwa hata vitabu vinavyoagizwa kutoka nje vimekusudiwa kutumiwa na Wanafunzi wa Kiswahili wa L.1 na L.2 wala si lazima kwa wanafunzi wa L.3 wa Uganda kutokana na mazingira ambayo Kiswahili kinawekwa katika muktadha wa nchi nzima.

#### **4.5 Kuchanganua mikakati ya namna ya kutatua changamoto zinazowakabidhi wafanyabiashara kufanikisha ujifunzaji Kiswahili kibiashara**

Katika kujibu swali la nne, walitoa mapendekezo ambayo waliamini yangetatua changamoto za ujifunzaji wa Kiswahili kibiashara, msailiwa 090 katika kujibu namna ya kutatua changamoto za kisarufi alipendekeza bora kuwepo na machapisho katika Kiswahili ama tafsiri kutoka lugha asili katika Kiswahili. Tafsiri hizo na maandishi zilenge msamiati wa biashara;

*Nze mbadde nteesa nti wabeleo obutabbo nga bulimu obugambo bwa Luganda bwe bavumula munimi za njaulwo nga mulimuo luswaili noluzungu. Ebiggambo ebyo bibelee nga ebikwatagana ne'engeri eyobusuubuzi. Bino ebbitabo ebisiinga byebaisa wanno mbu luganda – Luswaili tebutuyamba nyoo kubba ebigambo ebilimu bwogera kubintu bya bulijo naye sinyo nti bya busuubuzi. Obba tufunne CD nga zavunulibwa muluswaili nga za bizinesi nga bwolabba efilimu enjogerere.*

Mimi nilikua napendekeza kwamba pawepo na vitabu ambavyo vina msamiati wa luganda ambao umetafsiriwa katika lugha tofauti kwa mfano Kiswahili na Kiingereza. Huo msamiati uwe unalandana na shughuli za biashara. Hivi vitabu ambavyo huwa vinapitishwa hapa kwetu vya Luganda-Kiswahili havitusaidii sana kwa sababu mambo yaliyomo ni ya kawaida na wala si ya biashara. La sivyo, tupate CD ambazo zilisha tafsiriwa katika Kiswahili na za Kiswahili namna unavyoona filamu ambazo zilitafsiriwa.

Kwa upande wa vitabu ambavyo vilikuwa na msamiati mgumu waliomba kuwepo CD, ambazo zina dialojia na namna ya kuwasiliana na wanunuzi; hivyo watajijengea umaarufu wa kuzungumza Kiswahili na kutambua msamiati mwafaka wa kutumia katika kibiashara. Katika hoja hii Fesi-Dagil (2022) pamoja na Jjinga na Bakize (2021) wamependekeza mafunzo na matumizi ya walimu wa ndani mwa nchi kama wakuzaji nyenzo zilizorahisi kutumiwa, kubuni, na kuzalisha nyenzo za kujifunzia lugha zinazohusiana na uzoefu na mahitaji ya wanafunzi wa ndani. Ina maana kwamba kuna uwezekano wa kuzalisha nyenzo za ujifunzaji kwa ajili ya biashara.

Msailiya 145 Badala ya kuwa na madarasa makubwa kama ya KACITA, walipendekeza kupata makundi madogo madogo ya kujifunza Kiswahili, kuhudhuria warsha ndogo ndogo juu ya mafunzo ya Kiswahili ama kujitafutia walimu ambao wangewapatia hela kidogo na kuwafundishia sehemu ambazo waliandaa kwa kila mtu binafsi. Warsha za Kiswahili zingewasaidia kutumia Kiswahili mara kwa mara. Nor-Farhma na Hamida (2003) wamependekeza kwamba wakati wa kujifunza L.2 ni bora mwanafunzi ajifunze lugha katika makundi madogo madogo ili waweze kufanikisha ujifzaji wao.

Msailiya 102 baada ya kulalamikia athari ya matumizi mabaya ya uongozi awali wa serikali alisema kuwa sasa hivi kuna mipango mizuri ya nchi na utangamano wake katika Afrika Mashariki. Hivyo alipendekeza kuwepo sera mwafaka ambayo itaweka wazi matumizi ya Kiswahili katika sekta ya biashara na sekta nyingine. Alisema kwamba Kiswahili hakistahili. Krashen(1987) anasema kwamba katika uamiliaji lugha mazingira asilia huchangia katika motisha ambao unamuwezesha mjifunzaji lugha kupendekeza njia mwafaka ambazo zitafanikisha ujifunzaji wake. Hoja hizi zimepigiwa upatu na Comstock na Kamara (2003) pamoja na Swartz (2003) kwamba mjifunzaji akishatambua changamoto anazopitia, inakuwa rahisi kwake kuona namna ambavyo angeweza kuzishughulikia.

Walipendekeza kushirikisha waziri wa maswala ya biashara na viwanda namna wafanyabiashara wanaweza kunufaika kibiashara kwa kutumia Kiswahili ambacho kitawaunganisha na wafanyabiashara wenzao katika nchi nyingine. Sera ya matumizi ya lugha ya biashara iwekwe ili kwa wale ambao wamejizatiti kutumia Kiswahili wasionekana kama ni wanafiki kwa wafanyabiashara wenzao.

Hivi karibuni kumeandikwa vitabu vya lugha nyepesi vya kiwango cha watoto wa shule za msingi. Waliobahatika kupeleka watoto wao kwenye shule za msingi zinazofundisha

Kiswahili, walitumia fursa hiyo kutumia vitabu vya watoto wao nyumbani kujifunza Kiswahili ama wakati mwingine kufundishana na watoto wao nyumbani. Wengine walionekana na vitabu vya tafsiri katika maduka walimokuwa wakiendeleza biashara zao. Walitumia pia kufundisha wenzao. Hali hii ya kujifunza na kutumia Kiswahili baina ya mwanafunzi kwa mwanafunzi itawasaidia kujijengea umilisi wa matumizi ya Kiswahili kibiashara. Krashen (1987) katika mhimili wake wa tatu anasema kwamba katika kiwango hiki sarufi ya lugha huamiliwa kwa utaratibu katika muktadha asilia, pale ambapo katika mhimili wa tano anasema kwamba ili mjifunzaji aelewé kile anajifunza basi hali hisivu huwa ipo. Kwa kushadidiwa na Gardener (2000) na Gass na Selinker (2008) anasema kwamba endapo ujifunzaji umeanza kuwa mgumu, ili mwanafunzi apate motisha ya ujifunzaji, anaweza kuhamisha mofimu za L.1 zilizokaribiana na zile za L.2 ili kujua kutamka neno katika L.2. Kupitia mijadala iliyotokana na mahojiano kati ya mtatifi na wasailiya kuna mapendekezo yaliyotolewa kuhusu namna wafanyabiashara wanaweza kubadilisha mwelekeo kwa mfano M.S 029 anasema;

*Mbadde nteesa nti tuyinza okujao obutayagaala nga tuwa ekyiyiibwa ennimi za abalaa nga oluswaili nkukubyia ebiloozo na kuuliliza abalala bakyigambako kyi nga bwe tutaddeko aboogera oluswaili. Okwekubira wammu nga tuwayamu na bali abayitamubuzibu obbo naye atte makyusa batya tufunne okuyambiwa ouktegeerekeka.*

Napendekezaka kwamba tunawaze kutataua mtazamo hasi kwa kuheshimu lugha za wengine kama Kiswahili pia kushauriana na kusikiliza maoni, mapendekezo na wenzako wanaozungumza lugha ya Kiswahili. Kuhimizana katika kushiki katika kujadili wale wamepitia changamoto hizo walifanikiwa vipi hadi kubadilisha mtazamo ili kupata msaada unaostahiki (TY).

Gardener (2000) kwa kuhusisha mhimili wake wa tano anasema kwamba uhusiano kati ya mwelekeo wa lugha na L2 hufikiwa kwa kuhusisha vipengele vya motisha vya mwelekeo wa lugha au mielekeo kwa wazungumzaji asilia wa lugha lengwa. Hivyo tunaweza kujiuliza ni kwa kiwango gani wafanyabishara wazawa wa Uganda wanapenda Kiswahili? Je, wanakithamini? Je, tathmini wanayotoa kuhusu Kiswahili ni chanya ama hasi? Ni bora kutambua mwelekeo hasi umetokea katika kiwango kipi ili utatuliwe.

Garderner (2000) katika mhimili wake wa tatu anasema kwamba kando na tofauti inayorejelea motisha ya kujifunza lugha , umuhimu na kushiriki kwake, inahitajika pia kubainisha tofauti kuhusu mahitaji ya lugha na matumizi ya lugha. Kwa kutumia mhimili wa nne anasema kwamba licha ya kuwa wanafunzi wanaweza kuwa na ala (za nje) na uwezo wa kuunganisha ala (za ndani) za kujifunza lugha, wanaweza pia kuwa na sababu tofauti za

kutumia lugha. House (2002) amefafanua zaidi katika hoja ya Gardener (2000) kwa kutofautisha kati ya lugha ya mawasiliano na lugha ya utambulisho. Anasema kwamba watu wa lugha nyingi wanaweza kuchagua lugha moja na kuitumia kwa mahitaji yao. House (keshatajwa) ametoa mfano kwamba wajifunzaji wanaweza kutumia L.1 kueleza utambulisho wao wa kitamaduni na kutumia L.2 kama chombo cha kuwasiliana na kuelewana (Dégi, 2012). Lugha moja isichukuliwe kama ndiyo fahari kwa nyingine ila inapaswa kuzingatiwa kama lugha ya maendeleo (Hoffman, 2000).

#### **4.6 Hitimisho**

Sura hii ambayo ilikuwa kitovu cha utafiti, imejadili kwa kina madhumuni manne ya utafiti huu sambamba na kujibu maswali ya utafiti. Madhumuni yamegusia, uchanganuzi na uwasilishaji wa mikakati, mitindo na changamoto za ujifunzaji Kiswahili kama lugha ya biashara mionganoni mwa wafanyabiashara jijini Kampala na mikakati ya namna ya kutatua changamoto hizo. Katika madhumuni ya kwanza ni wazi kwamba wafanyabiashara hawakutambua kwamba kulikuwa na mikakati na mitindo ya ujifunzaji L2 ambayo walitumia kujifunza Kiswahili kama lugha ya biashara. Ingawa mikakati na mitindo tofauti ilitajwa, waliishia kuchagua ile ambayo walidhani walikua wakitumia.

Hivyo majibu ya madhumuni ya kwanza yaligawanyika katika sehemu mbili. Sehemu ya kwanza ilitaja mikakati ambayo walitumia ikiwa ni; nyimbo, mwanafunzi kwa mwanafunizi, matumizi ya lugha chanzi, kuongea mawasiliano, mtagusano na ukuruba kati ya wanunuvi na wauzaji, matumizi ya teknolojia, mpango binafsi, utambuzi na upatikanaji tena. Katika sehemu ya pili walitaja mitindo ambayo waliafiki walikuwa wakitumia kujifunza Kiswahili ambayo ni; mwingiliano, dukuduku, kusikilza, mwelekeo, hamasa, kuashiria, na mpango binafsi. Katika madhununi ya pili vile vile jinsi wafanyabiashara walitumia mikakati na mitindo ya kujifunza Kiswahili kibiashara iligawanyika katika sehemu mbili. Kufuatia mgawanyo ili kuonyesha namna mikakati iliwezesha ujifunzaji wa Kiswahili kibiashara, ni pamoja na; mpangilio wa fonimu, kuhamisha sauti kutoka lugha chanzi, matumizi ya tafsiri, kujifunza kuititia mitandao ya kijamii, redio na televisheni, kutagusana na waliokijua Kiswahili, kujipanga namna ya kujifunza, kusoma maandishi mbalimbali ya Kiswahili na kurudisha kumbukumbu kwa yale waliyosikia ndio iliwezesha ujifunzaji. Katika sehemu ya pili ya kuonyesha namna mitindo iliwezesha ujifunzaji wa Kiswahili kama L2, kulikuwepo na maingiliano kati ya jamii ya wafanyabiashaa, wanunuvi na jamii nyinginezo, msukuo wa dukuduku uliwafaa sana, usikizaji wa nyimbo za wasanii nchini Uganda, bongo flavor,

nyimbo za dini na siasa, mazingira halisi yalichangia pakubwa katika ujifunzaji, mwelekeo, kuhamasika, kuashiria vitu mbalimbali na kujipanga kisaikolojia kulisaidia kujifunza Kiswahili kama lugha ya biashara. Katika madhumini ya tatu ilibainika kwamba kulikuwa na changamoto walizokumbana nazo mionganini mwazo zikiwa; changamoto za kisarufi, muda wa kujifunza, kutumia lugha kimshtukizo, lugha mseto, mwelekeo hasi dhidi ya lugha ya Kiswahili, ukosefu wa mafunzo rasmi, athari za kisiasa, umri na mazingira ya kufanya biashara. Mikakati ya namna ya kutatua changamoto hizo ilishughulikiwa katika madhumuni ya nne kwamba kunaweza kuwepo madarasa madogo ya kujifunzaji, kuwepo sera mwafaka kuhusu ujifunzaji wa Kiswahili kwa wafanyabiashara, wafanyabiashara ambao wameanza kuongea Kiswahili wanaweza kutumia fonimu zinazokaribiana na fonimu za Kiswahili wakati ambapo watakuwa wanataka kuwasiliana katika Kiswahili.

## **SURA YA TANO**

### **MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO**

#### **5.1 Utangulizi**

Sura hii imewasilisha muhtasari wa utafiti. Lengo kuu la utafiti limeelezwa pamoja na upeo wa utafiti na yaliyomo katika kila sura. Vile vile muhtasari wa matokeo umejadiliwa kwa kueleza jinsi utafiti huu ulivyofanikiwa katika kuyafikia malengo matatu ya utafiti huu. Mapendekezo nayo yalifanywa kwa ajili ya utafiti wa baadaye.

#### **5.2 Muhtasari wa Utafiti**

Utafiti ulihusu mikakati, mitindo, changamoto na mikakati ya utatuzi wa changamoto za kujifunza na kutumia Kiswahili kama lugha ya biashara miongoni mwa wafanyabiashara jijini Kampala, Uganda. Sura ya kwanza ilishughulikia usuli wa utafiti, historia ya Kiswahili nchini Uganda, kwa nini matumizi ya Kiswahili katika biashara, mikakati na mitindo ya kujifunza Kiswahili kama lugha ya biashara na swala la utafiti. Vile vile sura hii ilishughulikia maswali ya utafiti na madhumuni ya utafiti. Madhumuni ya kwanza yalikuwa; kufafanua mikakati na mitindo ya kujifunza Kiswahili kama lugha ya biashara kwa wafanyabiashara jijini Kampala, Uganda, ya pili ni kutathmini jinsi mikakati na mitindo mbalimbali huwezesha kujifunza Kiswahili kama lugha ya biashara jijini Kampala, Uganda na ya tatu ni kupambanua jinsi wafanyabiashara hukumbana na changamoto zilizowakabili wakati wa kujifunza Kiswahili kibiashara na madhumuni ya nne yalikuwa kupendekeza mikakati ya utatuzi wa changamoto walizokabiliana nazo wakati wa kujifunza Kiswahili kama lugha ya biashara jijini Kampala, Uganda. Upeo wa utafiti ulihusisha, sehemu tatu ambazo ni Ekedi ya Mukwano, Simlaw International Limited na soko la Kikuubo. Ni katika Ekedi hizo ndimo mlipatikana maduka ya; kuuza vitabu, vipodozi na manukato, vyombo vya nyumbani, nguo mpya, vifaa vya ujenzi, mikahawa, mikoba, rununu, kupokea na kubadilisha hela, na sehemu za msalani. Hapo ndipo utafiti ulipata wasailiwa mia mbili sitini (260) walioteuliwa kidhamirifu. Wahusika wafanyabiashara wanoafanyia katika Ekedi mbili za Simlaw International Limited na Mukwano Arcade, na soko moja la Nakikubo, wafanyabiashara wanaotangamana na wanunuzi wanaotumia Kiswahili kutoka nje na ndani ya Kampala, wafanyabiashara wanaojifunza na kutumia Kiswahili Kibiashara na wanaofanyia biashara mjini Kampala ndio walioteuliwa.

Kiunzi cha nadharia ya Krashen (1987) na Gardener (2000) kilihusishwa katika

kuchanganua mikakati, mitindo na changamoto za ujifunzaji Kiswahili kama lugha ya biashara.

Nadharia ya Krashen ina mihimili mitano ambayo ni; nadharia tete ya upataji/ujifunzaji wa lugha ya pili, nadharia tete ya mfumo asili, nadharia tete ya ufuatilizi, nadharia tete ya dhana mpya, na nadharia tete ya kuchujio athari. Nadharia ya pili ambayo ilitumiwa ilikuwa ya Gardener ambayo mihimili yake ni; jitihada, nia, motisha changamani, uwezo wa kufanikiwa, na mwelekeo. mhimili wa kwanza wa Krashen wa upataji na ujifunzaji lugha na ule wa kwanza jitihada na wa pili nia wa Gardener iliongoza madhumuni ya kwanza ya kuchanganua mikakati na mitindo ya kujifunza Kiswahili kama lugha ya biashara. Mhimili wa nne wa nadharia tete ya dhana mpya na mhimili wa nne wa nedharia tete ingizi pamoja na mhimili wa tatu yaani motisha changamni, mhimili wa nne wa uwezo wa kufanikisha ujifunzaji pamoja na mhimili wa tano wa mielekeo yote ikiwa ni ya Gardener ilisaidiana kuchanganua madhumuni ya pili, ya kutathmini jinsi mikakati na mitindo huwezesha kujifunza Kiswahili kama lugha ya biashara jijini Kampala. Mhimili wa nne wa nadharia tete ya dhana mpya pamoja na mhimili wa tano wa nadharia tete ingizi wa Krashen pamoja na mhimili wa tatu yaani motisha changamani, wa nne amba ni uwezo wa kufanikiwa pamoja na wa tano ya Gardener ilisaidia kuchanganua madhumuni ya tatu. Madhumuni ambayo ni kubainisha changamoto za ujifunzaji Kiswahili kama lugha ya kibiashara na jinsi ya kukabiliana nazo.

Sura ya pili ilishughulikia tahakiki ya maandishi yaliyohusiana na mikakati na mitindo ya jumla ya ujifunzaji wa lugha ya pili, namna mikakati na mitindo huwezesha ujifunzaji wa lugha ya pili huku tukidhamiria Kiswahili kama lugha ya biashara na changamoto zinazotokana na ujifunzaji wa lugha na namna ya kuzitatua.

Sura ya tatu ilishughulikia mbinu ambazo zilitumika katika utafiti. Muundo mseto ulitumika katika kuchanganua data kiwingiidadi na kithamano. Utafiti ulizingatia maeneo mawili, yaani eneo la kijiografia ambapo ni jiji la Kampala katika Ekedi ya Mkwano, Simlaw International Limited na soko la Kikuubo. Eneo la kiakademia ilihuisha dhana iliyohusu mikakati na mitindo ya kujifunza Kiswahili kama L2. Sura hii vile vile iliangazia idadi lengwa ya wafanyabiashara na idadi lengwa ya maduka yaliyohusishwa katika utafiti. Mchakato wa usampulishaji na sampuli uliteuliwa kwa minajili ya kukusanya data. Mbinu zilizotumika katika kukusanya data zilikuwa hojaji, usaili na Uchunzaji. Vifaa vyta kukusanya data

vilikuwa hojaji, mwongozo wa mahojiano, simu mahiri na tarakilishi. Hojaji na dodoso vilitumiwa katika usaili halafu simu mahiri ikasaidia katika uchunzaji, vile vile tarakilishi ilihifadhi na kuchanganua data. Maswala mengine yaliyoshughulikiwa katika hii sura yalikuwa ni utegemezi na udhabit, namna data iliwasilishwa na kuchanganuliwa na maadili ya utafiti. Sura ya nne iliwasilisha matokeo na uchanganuzi wa madhumuni ya kwanzu kuhusu mikakatina mitindo iliyotumiwa na wafanyabiashara kujifunza Kiswahili kama lugha ya biashara jijini Kampala, namna mikakati na mitindo iliviyotumiwa na wafanyabiashara kujifunza Kiswahili kama lugha ya biashara na changamoto za ujifunzaji Kiswahili kama lugha ya biashara na namna ya kukabiliana na changamoto hizo.

### **5.3 Hitimisho**

Utafiti ulijkita katika malengo matatu makuu. Hitimisho imepambanuliwa kwa muhtasari kulingana na malengo hayo namna inavyoonyeshwa hapa chini.

#### **5.3.1 Mikakati na mitindo ya kujifunza Kiswahili kama lugha ya biashara jijini Kampala, Uganda**

Matokeo ya utafiti ya mikakati na mitindo ujifunzaji Kiswahili kama L2 kwa wafanyabiashara yilibainisha kuwa takriban asilimia 100% ya wasailiwa walikiri kutojua kwamba kulikuwa na mikakati na mitindo ya ujifunzaji L2. Utafiti ulipambanua baadhi ya mikakati na mitindo ili kuwapa mwanga watafitiwa kuhusu mikakati na mitindo waliyokuwa wakitumia kwa kutofahamu. Kwa kutumia usaili na kuhusisha hojaji na dodoso, matokeo yalionyesha mikakati ambayo ilikuwa ikitumiwa kujifunza Kiswahili kama lugha ya biashara ambapo ni: kuuliza maswali, ukariri, kuongea, kumbukizi, mawasiliano, mwanafunzi kwa mwanafunzi, mazoezi, utambuzi na mtagusano na ukuruba kati ya wanunuzi na wauzaji.

Vile vile utafiti ulibainisha mitindo ya ujifunzaji L2 kwa sababu asilimia 100% ya wasailiwa walikiri kutofahamu kwamba kulikuwa na mitindo ya ujifunzaji wa L2 ambayo walitumia kujifunza Kiswahili kwa ajili ya biashara. Mitindo iliyopatikana kwa kutumia usaili ilikuwa; kupenda, mwengiliano, dukuduku, sikizi, mwelekeo, mtagusano na ukuruba kati ya wanunuzi na wauzaji, tofauti za kimaumbile, tabia za mjifunzaji, uzungumzaji na unyamavu. Walikiri kutumia; kupenda, mwengiliano, dukuduku, usikizi, mwelekeo, mitagusano ya ukuruba kati ya wauzaji na wanunuzi, tabia za mjifunzaji katika kujifunza Kiswahili kama lugha ya biashara.

### **5.3.2 Namna mikakati na mitindo mbalimbali iliwezesha ujifunzaji wa Kiswahili kama lugha ya biashara jijini Kampala, Uganda**

Matokeo kuhusu namna mikakati na mitindo mbalimbali namna iliwezesha kujifunza Kiswahili kama lugha ya biashara kwa data zilizopatikana kwa kutumia usaili na vifaa veya kukusanya data ambavyo vilikuwa hojaji na dodoso. Ilionyesha kwamba ili kupata kuhifadhi msamiati wa maneno ya kutumia katika Kiswahili kibiashara, walisikiliza nyimbo kutohuna na muziki wa wasanii tofauti tofauti wa Uganda na wasiokuwa wa Uganda almradi walikuwa wanatumia Kiswahili, walijumuika katika mawasiliano baina yao na wanajamii ambao walikijua Kiswahili, wanunuzi ambao walitumia Kiswahili na wafanyabiashara wenzao ambao walijua Kiswahili. Walijifunza kupertia mitando ya teknolojia kama simu mahiri, *Youtube* na kufuata walimu wa mitandaoni, radio na televisheni. Kwa kupertia njia hiyo walikuza stadi za kusikiliza na kuongea, walijitahidi kuomba msaada kwa wanunuzi wao na mionganini mwa wafanyabiashara wenyewe, kukumbukia waliyowahi kusikia na wakati mwengine kubahatisha maneno kadhaa katika Kiswahili. Kwa kuongezea walihuisha matumizi ya lugha chanzi (kutumia mpangilio wa fomula, matumizi ya fomula katika sentensi, kuhamisha sauti kutoka lugha chanzi hadi Kiswahili, matumizi ya tafsiri, na kutumia msamiati mbalimbali katika kuunda sentensi ambazo nyingi zingefikirika ama kutungwa kwa lugha chanzi halafu zikahaushwa katika Kiswahili). Kwingineko usikilizaji wa nyimbo uliwafanya wapate ari na motisha ya ujifunzaji wa Kiswahili kibiashara. Walipenda kuona wengine wakizungumza Kiswahili hivyo kuiga msamati bora na lafudhi kutoka kwa wanunuzi ambao walitoka sehemu mbalimbali.

Fauka ya hayo, hali ya kufanya mazoezi, kutumia utambuzi na mitagusano ya ukuruba ya kati ya wanunuzi na wauzaji kati yao na wanunuzi kuliwapatia msingi bora wa kujifunza na kutumia Kiswahili kibiashara. Mitindo kama mwengiliano uliwasaidia kubadilisha mwelekeo kuhusu lugha ya Kiswahili, kuweka jitihada na nia ya kujifunza Kiswahili kufanikisha biashara. Walijiweka katika hali ya dukuduku ya chini ili kujitahidi kujifunza baadhi ya msamiati wa Kiswahili na kuitumia katika kuunda sentensi. Kusikiliza nyimbo tofautitofauti za Kiswahili, vitimbi na michezo ya Kiswahili iliawezesha kuhifadhi maneno ya Kiswahili ambayo iliwafaa katika kufanikisha mazungumzo katika biashara. Kujiwangia namna na muda wa kujifunza kulifanya wakusanye misamiati ambayo walirejelea mara kwa mara na hivyo kujiimarisha katika matumizi yake kwenye biashara. Kupenda ni motisha ambao huwa ndani ya mtu anapopenda kitu fulani. Sababu ya kupenda huhuishwa na nini atafaidika

nacho. Hivyo walikipenda Kiswahili ambapo ilikuwa msukumo chanya wa kutumia Kiswahili katika kufanikisha biashara.

Kwa kutumia mbinu ya uchunzaji na simu mahiri data zilizopatikana katika hali halisi ya mazingira ya kuendeleza biashara zilionyesha kwamba kulikuwa na mikakati na mitindo ambayo wafanyabiashara walikuwa wakitumia bila kufahamu kwamba walikuwa wakiitumia kujifunza Kiswahili kwa ajili ya biashara. Miongoni mwayo ni mikakati kama; mwanafunzi kwa mwanafunzi, ukariri, mazoezi, kuomba msaada, mawasiliano, kuuliza maswali, upatikanaji tena, utambuzi na mitindo kama dukuduku, mwelekeo, kuashiria, kujistahi na vizuio.

### **5.3.3 Changamoto ambazo wafanyabiashara walikumbana nazo wakati wa kujifunza Kiswahili kama lugha ya biashara jijini Kampala, Uganda**

Katika hali ya kujifunza Kiswahili kama lugha ya biashara, wafanyabiashara walikumbana na changamoto kama; changamoto za kisarufi, muda wa kujifunza, kutumia lugha ya Kiswahili kimshtukizo, lugha nyingi ambazo zilikuwa zikitumika katika maeneo ya kufanyia biashara, mwelekeo hasi dhidi ya lugha ya Kiswahili ambao ultokana na historia mbaya ya awali ya matumizi ya Kiswahili. Mazingira ya ujifunzaji lugha ya Kiswahili hayakuwa mazuri kwani kuna wale ambao bado walikuwa na mwelekeo hasi dhidi ya matumizi ya Kiswahili, matumizi ya Kiswahili yalikuwa tu sehemu za kufanyia biashara na wala si ya jamii walimokuwa wakiishi, hivyo ilikuwa vigumu kuthibiti matumizi ya Kiswahili nje ya biashara. Kusita na kugugumia wakati wa kuzungumza maneno ya Kiswahili, kuchanganya lugha mama hasa kwa Wabantu wakati wa kuwasiliana na wanunuvi katika Kiswahili. Wanailoti walikumbana na baadhi ya sauti kwa sababu lugha zao mama hazikuwa na baadhi za sauti kama za Kiswahili;. Umri nao ulikuwa ni changamoto kwani walisema kwamba ujifunzaji lugha ukiwa mtu mzima huwa ni vigumu maana mwanzo unafikiri kwa lugha chanzi ndiyo utafsiri maana katika lugha lengwa na tena walikuwa na mambo mengine ya kufikiria kuliko kujifunza lugha nyingine. Kwa kuongezea , matokeo ya utafiti yalionyesha kwamba baadhi yao walikuwa na uoga wa kujifunza Kiswahili kwa sababu ya kufanya makosa, vile vile waliona jinsia ya kike ndiyo walikuwa na nafasi kubwa ya kujifunza Kiswahili kibiashara kuliko jinsia ya kiume. Kampala kuwa mji mkuu kuna lugha nyingi zinazotumika, ilikuwa changamoto kwa wafanyabiashara kuamua ni lugha gani watachagua dhidi ya nyingine ili kufanikisha biashara zao. Pia walisema kwamba hata Kiswahili ambacho kilikuwa kikitumiwa na wanunuvi kiliwakanganya kwa sababu Kiswahili cha

wanunuzi kutoka Kenya, Tanzania na Kongo kilitofautiana. Kanuni na vipengele vya kiisimu vya Kiswahili viliwatatiza katika utunzi wa sentensi. Pia walikiri kwamba uvivu waliokuwa nao ndio uliwafanya wachelee kujifunza Kiswahili kibiashara.

#### **5.3.4 Mikakati ya namna ya kutatua changamoto zinazowakabili wafanyabiashara ili kufanikisha ujifunzaji Kiswahili kibishara jijini Kampala, Uganda**

Majibu kutokana na wasailiwa kwa kutumia hojaji na mahojiano walipendekeza kuwepo na machapisho katika Kiswahili ama tafsiri kutoka lugha asili katika Kiswahili. Walipendekeza tafsiri zisiwe za kawaida tu ila ziwe na msamiati wa kibiashara. Kwamba endapo patakuwa na machapisho basi viwepo na msamiati wa kiwango chao ambao hawana tajriba ya kutosha katika usomaji wa Kiswahili ama wapate rekodi zilizo na dialojia kuhusu shughuli za biashara.

Baada ya kuona kwamba ukubwa wa madarasa waliyokuwa nayo yalikuwa kikwazo, walipendekeza kugawa katika makundi madogo madogo ambayo yangefanikisha ujifunzaji bora. Kando na madarasa ya kusoma, walipendekeza pia kuwa na warsha za biashara na nchi zingine ambazo zinatumia Kiswahili kama lugha ya mawasiliano kufanikisha biashara.

Waliona kwamba njia nyingine ya kutatua changamoto za ujifunzaji wa Kiswahili kibiashara ni kuhusisha waundaji sera ambazo zitafanikisha matumizi ya Kiswahili katika biashara na kuwawezesha wafanyabiashara wa Uganda kuweza kutangamana na wafanyabiashara wengine katika Afrika Mashariki. Walisema kwamba ili kutatua changamoto ya mweleko hasi ni kuona umuhimu wa lugha nyingine na kuziheshimu haswa kwa madhumuni ya maendeleo. Walipendekeza kushirikiana na wengine walio na mweleko hasi ili kupata namna walitatuwa hali hiyo.

#### **5.4 Mapendekezo kwa mujibu wa madhumuni ya utafiti**

Mapendekezo mbalimbali yametolewa kwa kuzingatia madhumuni ya utafiti namna yanavyowasilishwa katika sehemu inayofuata.

#### **5.4.1 Mapendekezo kuhusu mikakati na mitindo ya ujifunzaji wa Kiswahili kama lugha ya biashara jijini Kampala, Uganda**

Wanazuohas a kutoka eneo la Afrika Mashariki wanastahili kupanua uwanja wa ufundishaji Kiswahili kama lugha ya pili kwa mazingira yasiyo rasmi na yaliyo rasmi. Kuandika matini ndogo ndogo, kuhusisha mijadala ya kuzungumza, tamasha na makongamano yanayoleta

taaluma mbalimbali kwa pamoja inatukuza ujifunzaji wa Kiswahili katika sekte tofauti tofauti.

Kwa kiasi kikubwa mikakati na mitindo imependekezwa na kutumika katika mazingira ya wanafunzi walio ughaibuni. Ni wakati sasa wanataluma ya Kiswahili kufanya utafiti juu ya namna mikakati na mitindo ya ujifunzaji Kiswahili katika mzingira ya Kiafrika yanaweza kufanikisha ujifunzaji Kiswahili kwa biashara na hata asasi nyingine zisizo asasi ya elimu. Msamati uliotumiwa kufafanua mikakati ni mgumu kwa mtu wa kawaida kuelewa kwa urahisi. Aidha, mitindo ilielekea kuwa ya kisayansi kuliko hali ya kawaida ambayo ilihitaji utaalamu wa kisaikolojia wa juu kufafanua.

Kuna haja ya kutoa masomo ya kimsingi kwa asasi zote ambazo zinaendeleza uchumi wa nchi hasa biashara. Katika nchi ambazo Kiswahili hakikuwa L1 kwa mfano Uganda, ni vyema kushirikisha mikakati na mitindo ya ujifunzaji ya L2 katika kujifunza Kiswahili. Hii ni kwa sababu hata kwa wale walikiri kuelewa Kiswahili kidogo, hawakutambua kwamba kulikuwa na mikakati na mitindo ya kujifunza Kiswahili kama L2.

Mchakato wa ujifunzaji lugha ya pili huwa unataofautiana mionganini mwa wajifunzaji. Hivyo mikakati na mitindo yaweza kutofautiana mionganini mwa wajifunzaji kutegemea motisha wa ndani na wa nje. Kuna wale ambao wanahifadhi kwa haraka maneno na kuunda sentensi kwa haraka,kuna wale ambao wanaanza na kuelewa sauti,maneno halafu sentensi, kuna wale ambao wanajifunza kwa kutafakari juu ya maana ya kile ambacho anajifunza huku akihusisha na lugha ya kwanza. Hizi dhana zote zinachukua nafasi tofauti katika kila mjifunzaji lugha ya pili. Hivyo utafiti ynaweza kufanywa kubainisha tofauti hizo.

#### **5.4.2 Mapendekezo kuhusu Jinsi mikakati na mitindo inavyowezesha ujifunzaji Kiswahili kama lugha ya biashara jijini Kampala, Uganda**

Mikakati na mitindo ya kujifunza Kiswahili inastahili ifafanuliwe katika Kiswahili ili wanayoitumia wawe na ufahamu kwa kile wanachowasilisha. Ufafanuzi katika Kiswahili utawezesha kuzua aina tofauti tofauti za mikakati na mitindo kwa wazawa wa Afrika na mazingira ya Kiafrika. Shughuli mbalimbali zinaweza kuandaliwa ili kuwawezesha wafanyabiashara kupata njia bora ambayo wanaweza kutumia kujifunza Kiswahili kwa biashara.

Pamoja na hayo, ni muhimu kuweka miundombinu ambayo inaweza kusaidia wafanyabiashara kujifunza na kutumia Kiswahili bila vikwazo vyovoyote.

#### **5.4.3 Mapendekezo kuhusu changamoto zinazowakabili wafanyabiashara wakati wa ujifunzaji wa Kiswahili kama lugha ya biashara jijini Kampala, Uganda**

Kuna haja ya kufanya uhamasishaji juu ya lugha ya Kiswahili na ufanisi wake katika maendeleo ya uchumi wa nchi. Uhamasishaji unaweza kufanya kupitia vyombo vyahabari, mitandao ya mtagusano na ukuruba kati ya wanunuzi na wauzaji, wasanii na wanasiasa. Hii itaonesha umoja wa kushikamana kwa pamoja kwa mahitaji mamoa na malengo sawa.

Katika ujifunzaji lugha yoyote ile kutafsiri ni sehemu mwafaka ya kujifunza lugha. Kuna hajaya kutafsiri matini ndogondogo/vipeperushi ambavyo vitakuwa na msamiati mwepesi wa kufanikisha ujifunzaji Kiswahili kwa ajili ya biashara.

Mwelekeo juu ya lugha mwanafunzi anajifunza, makundi anayotangamana nayo, majirani na jamii huwa na mchango mkubwa katika ujifunzaji wa L2. Inaweza kuwa mchango chanya ama hasi. Kwa hiyo mazingira kwa jumla yanayomzunguka mjifunzaji lugha ya Kiswahili yanastahili yaye ambayo yatafanikisha ujifunzaji wa Kiswahili.

Dhana ya uvivu wa kusoma imejitokeza katika watu wengi hata wale ambao si wafanyabiashara. Inastahili kuwekwa semina na warsha ambazo zinaweza kukuza kipawa cha kusoma na kufanya mazoezi kile kinachosomwa. Wafanyabiashara wakipata fursa ya kusoma hivyo vitabu watahimizwa kutumia msamiati unaotokana na matini hizo katika kufanikisha matumizi ya Kiswahili kibiashara.

Wafanyabiashara wanastahili kutumia mikakati tofauti tofauti na mitindo ya ujifunzaji wa L2. Kuna haja ya kuhamasisha watu wa asasi tofauti tofauti mkiwemo wafanyabiashara umuhimu wa matumizi ya Kiswahili hasa kwa utangamano wa jumuiya ya Afrika Mashariki na kwagineko.

Ni bora kutambua kwamba mikakati na mitindo ya ujifunzaji L2 ina mchango mkubwa sana katika ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili. Asilimia kubwa ya makundi ya ujifunzaji lugha huwa hawapitii katika mfumo rasmi wa mafunzo pale ambapo kuna mwalimu na mbinu mwafaka za ufundishaji L2. Hivyo mjifunzaji ana wajibu wa kufaragua namna anaweza kujifunza. Wanaojifunza Kiswahili kama L2 wanastahili kujijengea stadi za uvumilivu ili

kukumbana na jamii ndogo ambayo bado ina mwelekeo hasi dhidi ya matumizi ya Kiswahili. Wahimize wengine kujifunza na kutambua umuhimu wa Kiswahili katika kuendeleza biashara.

Ni bora kuwasiliana mara kwa mara katika Kiswahili hata kama mtu hayuko katika maeneo ya biashara. Hili litawajengea umilisi mpana wa kutumia Kiswahili kila wakati. Kuwasiliana katika lugha ya Kiswahili kutawatoa uoga wa kijifunza Kiswahili kama lugha ya pili wakifikiri kwamba kila wakati unapozungumza Kiswahili lazima kutakuwa na makosa.

Uhamasishaji ni muhimu sana kwa wafanyabiashara wote na watu wa kawaida mashinani juu ya matumizi ya Kiswahili. Katiba ya Uganda inaruhusu matumizi ya Kiswahili. Vile vile Kiswahili sasa ni lugha rasmi ya Afrika Mashariki na Afrika nzima kwa jumla. Ni kwa ajili hiyo jamii inastahili kutambua kwamba hakuna hatia kutumia Kiswahili. Watu wawe huru Kiswahili siyo kukiona kwamba ni cha kundi fulani tu. Hili litasaidia kutatua baadhi ya changamoto ambazo zinajitokeza wakati wa kujifunza Kiswahili.

Inastahili kuwepo na machapisho katika Kiswahili ama tafsiri kutoka lugha asili katika Kiswahili. Tafsiri hizo na maandishi zilenge msamiati wa biashara. Kunaweza kuandaliwa CD, ambazo zina dialojia na namna ya kuwasiliana na wanunuzi; hivyo watajijengea umaarufu wa kuzungumza Kiswahili na kutambua msamiati mwafaka ya kutumia wakati wa kujifunza Kiswahili kibiasara

Badala ya kuwa na madarasa makubwa kama ya KACITA, wanaweza kuunda makundi madogo madogo ya kujifunza Kiswahili, kuhudhuria warsha ndogo ndogo juu ya mafunzo ya Kiswahili ama kujitafutia walimu ambao wangewapatia hela kidogo na kuwafundishia sehemu ambazo waliandaa kwa kila mtu binafsi. Warsha za Kiswahili ziliwasaidia kutumia Kiswahili mara kwa mara.

Pia mafunzo yanaweza kutolewa kwa njia zisizo rasmi kama kudhuru sehemu za maeneo ambayo biashara zinaendelezwa katika mazingira ambayo Kiswahili peke yake ndiyo lugha ambayo inatumiwa katika shughuli za biashara. Maeneo ya kuzuru yanaweza kuambatana na tamasha za muziki ama maonyesho ya vitu ambavyo vinauzwa katika soko mbalimbali ili wafanyabiashara jijini Kampala wapate fursa za kutangamana na wenzao katika sekta hiyo.

#### **5.4.4 Mapendekezo kuhusu mikakati ya kutatua changamoto zinazowakabili wafanyabiashara ili kufanikisha ujifunzaji Kiswahili kibishara jijini Kampala, Uganda**

Kuandaliwe makongamano ambayo yanaelezea umuhimu wa kutumia Kiswahili na

maendeleo yake katika sekta ya biashara nchini Uganda, Afrika Mashariki na kwingineko. Hili litasaidia katika kubadilisha mwelekeo kuhusu lugha ya Kiswahili.

Ni muhimu kwa serikali ya Uganda kufikiria kuhusu suala la lugha ya taifa. Kuna uwezekano wa kuwa na lugha za taifa zaidi ya mbili ama tatu kulingana na mipango ya nchi na mikakati ya kuendelea kiuchumi kupitia biashara.

### **5.5 Mapendekezo ya tafiti za baadaye**

Utafiti huu uliongozwa na kiunzi cha nadharia ya ufuatilizi na nadharia ya motisha. Ipo haja ya kuchunguza nadharia nyinginezo za hivi karibuni ambazo zinaweza kuwekea misingi thabiti juu ya mikakati na mitindo ya ujifunzaji lugha ya Kiswahili katika biashara na nyanja nyingine za maisha. Utafiti linganishi waweza kufanywa kwa kuhusisha wafanyabiashara wa jijini Kampala na labda nchi nyingine ambayo Kiswahili si lugha yake ya kwanza lakini wafanyabiashara wanatumia Kiswahili kuendeleza biashara zao. Aidha, Utafiti kama huu vile vile unawezwa kufanywa kwa kuhusisha kundi dogo au kubwa kuliko kundi lilitoleuliwa na utafiti huu. Vile vile unaweza kuteua mazingira tofauti na mbinu tofauti za kukusanya data. Vilevile yatakikana pawepo uhamasishaji mpana juu ya matumizi ya Kiswahili kama lugha ya biashara na lugha ya mawasliano ya mawanda mapana ili kutatua dhana ya mwelekeo hasi na motisha hasi.

Watekelezaji sera khusu lugha wanamchang'o mkubwa sana katika kupelekeea Lugha kukutana na changamoto nyingi zikiwemo hasi ama chanya. Mweleko kuhusu lugha hutegemea mtazamo wao kwa lugha inayopendelewa na sera. Hivyo Kwa hali yoyote, mafanikio kama sera ya lugha katika utekelezaji na hata uundaji wake, inategemea sana mitazamo kuelekeza lugha inayopendelewa, hasa mionganoni mwa wale walio katika sehemu ya uongozi. Hivyo watekelezaji na waundaji sera waweke mikakati mwafaka ambayo itawezesha matumizi ya Kiswahili kibiashara mionganoni mwa wafanya biashara.

### **5.6 Hitimisho ya sura hii**

Sura hii ilitoa muhtasari wa kila sura kwa kueleza muhtasari wa utafiti, hitimisho ambayo ilizingatia madhumuni ya utafiti na vilevile mapendekezo. Mapendekezo yalitolewa kwa kuegemea madhumuni ya utafiti na hatimaye mapendekezo ya tafiti za baadaye.

## MAREJELEO

- Adam, F & Podmenik,D. (2005). *Qualitative Research in a Changing Epistemic Context.* The Case of a Small Social Science Community [41 paragraphs]. *Forum Qualitative Sozialforschung / Forum: Qualitative Social Research*, 6(3), Art. 40,
- Adam, J. Kamuzora, F. (2008). *Research Methodology for Business and Social Studies*. Morogoro; Mzumbe Book Project.
- Aidah, M. (2020). *The role of Language in National Development. Case of Kiswahili in Uganda*. (Makala yaliyowasilishwa Rongo-Bado hayajachapishwa)
- Anderson, N. (2002). *The role of metacognition in second language teaching and learning*. Washington, D.C., ERIC. ED 463 659.
- Anderson, T, na Elioumi, F. (2004). *Theory and practice of online learning*. Athabasca, C.A: Athabasca University
- Arcand, J. L. (1996). Development Economics na Language. The Earnest Search for Mirage. *International Journal of the Sociology of Language*, 12(1); 119-158 Association of Secondary School Principles.
- Archibald, J. (1998). Second language phonology, phonetics, and typology. *Studies in SecondLanguage Acquisition*, 20(2), 189–211.
- Armfast, J. S na Holmen, A. (2010). *Second Language Learning in International* encyclopedia of education (3<sup>rd</sup> ed).
- Bachman, L. F. (1990). *Fundamental Considerations in Language Testing*. Oxford: OxfordUniversity Press.
- Baker, M. (2001). *Foundation of Bilingual Education and Bilingualism*. Clevedone. Multilingual Matters Limited.
- Baker, M. (2001). *Translation and Interpretation*. London: Routledge Publishers.
- BAKITA (2019). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*. Toleo la Pili. Longhorn Publishers Dar-es Salaam Tanzania
- Barbie. E (1992). *The Practice of Social Research*. Toleo la sita.Belmont, CA: Wordsworth Publishing Company
- Benzehaf, B. (2021). Language Learning Strategies reported by Successful English Language Learners. *Journal of Applied Language and Culture Studies*, 4, 143-160.
- Benziers, D. (1961). *Learning our Language*. London .Longmans Dreen na Co,
- Bialystok, E. (1990). *Comunication strategies*. Oxford :Blackwell
- Bialystok, E. (1978). *A theoretical model of second language Learning*. Language Learning, Wileyonline Library. <https://onlinelibrary.wiley.com/doi/10.1111/j.1467-1770.1978.tb00305.x>
- Bialystok, E. (2001). *Bilingualism in development: Language, literacy, and cognition*. Cambridge, UK: Cambridge University Press
- Bosire, E. O. (2002). *Educational publishing in African languages with a focus on Swahili in Kenya*. Moi University Press

- Brett, A.G. (2000). A study of teaching communication strategies to beginners in German.Unpublished M.A dissertation .University of Southampton
- Brewton, E. na Millword, L.(2001). *Organizational Research Methods*: Sage
- Brocelow, E. na Park, H. (1995). Moral conservation in second language prosody. In J. Archibald (ed), *Phonological acquisition & phonological theory* (pp.151-168).Hillsdale, NJ: Erlbaum.
- Brown, H. D. (1994). *Principles and Practices of Language Learning and Teaching*. Eaglewood Cliffs, NJ: Prentice Hall.
- Brown, H. D. (2007). *Principles of Language Learning and Teaching*.5th Edition (M) London. Longman. Press.
- Brown, H. D. na Douglas, H. (2006). *Language learning and teaching*. Pearson EducationLtd
- Brown, H.D. (2020). Literature Review of theories of Second Language Acquisition: Katika *Journal of Applied Linguistics & Language Research*: Vol.7pp 80-86
- Bryman, A. (2015). *Social Research Methods*. (5th ed) Oxford University.
- Buliba, A. Mayaka, G. na Riro, M. (2014). *Misingi za Nadharia na Mbini za Utafiti*. Mwanza. Serengeti Educational Publishers.Tanzania
- Bwege, C. (2012). English in Tanzania: *A Linguistic Cultural Perspective* JLTIC, 167-182.
- Canale, M. na Swain.M (1980). Theoretical bases of communicative approaches to second language teaching and testing. *Applied Linguistics*, Vol.1:1-47.
- Chamot, A. U. (2005). *Language learning strategy instruction: Current issues and research [J]*.*AnnualReviewofAppliedLinguistics*,25,112-130.
- Chamot, A.U. (1987). The Learning Strategies of ESL students. Katika A.Wenden na Rubin (Eds), *Learner Strategy in Language Learning*. Eaglewood Cliffs. NJ: Prentice Hall.
- Chamot, A.U na O'Malley, J.M (1987). The Cognitive Academic Language Learning Approach: Abridge to the Mainstream. *TESOL Quarterly*, 21,227 249.
- Cherry, K. (2019). *American Psychology and Association. Ethical Principles of Psychological and Code of Conduct*. Amended 2017.
- Chien, K. L. (2010). *An Over View of Language Learning Strategies*. Articles Vol 7.
- Chimerah, R. (2010). Kiswahili: *Past present and Future*. Nairobi University Press
- Chiraghdin, S. na Munyapala, M. E (1977). *Historia ya Kiswahili*. Oxford University Press.Nairobi
- Chomsky, N. (1965). *Aspect of Theory of Syntax*. Cambridge. Massachusetts: M.I.T Press
- Chomsky, N. (1968). *The Sound Pattern of English*. New York. Harper na Raw Publishers
- Chomsky, N. (1988). *Language Problem of Knowledge*. Cambridge: The MIT Press
- Clarke,H na Clarke,E.(1977) . *Psychology and Language* .Harcourt Brace Jovanovich.
- Cohen, A. D. (1998). *Strategies in learning and Using a Second Language* (M) . Longman.

- Cohen, A. D. na Olshtain, E. (1993). *The production of speech acts by EFL learners..*<https://onlinelibrary.wiley.com/doi/abs/10.2307/3586950>
- Cohen, A. D. na Weaver, S. J. (2011). Strategies-based instruction for second languagelearners. Katika W.A. Renandya na G. M Jacobs. *Learners and LanguageStrategies.*
- Cohen, A.D. (1996). *Second Language and Use Strategies: Clarifying the issues.* Centre for Advanced Research and Language Acquisition. Minnepals:U.S.A.
- Cohen, A.D. na Weavers, S. J (2005). *Styles and Strategies Based Instruction: A Teachers Guide.*Center for Advanced Research on Language Acquisition Working paper series.
- Cohen, A.D, Weaver, S.J, na Li, Tao-yuan. (1995).The impact of strategies-based instruction on speaking a foreign language. *Research Report.* Minneapolis: Center for Advanced Research on Language Acquisition, University of Minnesota.
- Comstock, R., na Kamara, C. (2003). Adult language/learning disability: Issues and resources. Ilipakuliwa kutoka ERIC database. ERIC Document Number: ED 482 311.
- Cook, V. (1993). *Linguistic and Second Language Acquisition.* St. Martin's Press.
- Cook, V. (2001). *Second Language Learning and Teaching.*3<sup>rd</sup> Edition .Oxford University Press.Inc
- Cooper, D. R na Schindler, P.S. (2001). *Business Research Methods.* 7<sup>th</sup> Edition. McGraw-HillPublication.
- Cooper, L. R. (1989). *Language planning and social change.* Cambridge University Press
- Coopersmith.S (1967). *The Antecedents of self-esteem.* W.H Freeman and Company.
- Corder, S. P. (1983). *Error Analysis and Interlanguage.* London: U.O.P.
- Corder, S. P. (1967). The Significance of Learner's Errors IRAL, 5.161-169.
- Creswell, J. W (2008). *Educational Research,* 3rd ed. Pearson Creswell, J.W (2009). *Research Design.* Sage
- Creswell, J. W na Miller, D. L (2000). *Determining validity of qualitative inquiry. Theory intoPractice.*39(3),124-131.  
[https://www.tandfonline.com/doi/abs/10.1207/s15430421tip3903\\_2](https://www.tandfonline.com/doi/abs/10.1207/s15430421tip3903_2)
- Crook, C. (1994). *Computers and the collaborative experience of learning.* London Routledge
- Crotty, M. (1998).*The foundation of social research.* Sage.
- Cummins, J. (1979). Cognitive Academic Language Proficiency, Linguistics Inerdependence, the optimum age question and some other matters. *Working papers on Bilingualism,* no 19,121-129.
- David, C. (1997). *A Dictionary of Linguistics and Phonetics.* Blackwell.
- David, C. (2010). *The Cambridge Encyclopaedia of Language.* Cambridge University Press
- De vaus, D.A (2001). *Research Design in Social Research.* Sage
- Degi. Z, (2012). *Types of multilingualism expored in the Transylvanian school*

*context.Jezikoslovije* 13(2):645-666

- Denzin, N.K. na Lincoln, Y.S (2008). The Discipline and Practice of Qualitative Research. Katika Denzin, N. K na Lincoln, Y. S (eds), *Strategy of Qualitative Inquiry*: California: Sage.
- DeWalt, K. M., & DeWalt, B. R. (2011). *Participant observation : A guide for fieldworkers*. Lanham, Md: Rowman & Littlefield.
- Dianne,L.F. an Michael,H.L. (1991). *An Introduction to Second Language Acquisition Research*. Longman inc.
- Dörnyei, Z. (1994b). Understanding second language motivation: On with the challenge. *Modern Language Journal*. 78, 515-523.
- Dreyer. C na Oxford. R. (1996). *Learning Strategies in Second Language Learning*. Cambridge University Press
- Dulay, H. and Burt, M. (1973). Should we teach children syntax *Language Learning* 23. 245–258.
- Dulay.H na Burt, M (1973). *Error and Strategies on Child's Second Language Learning*, Katika Tesol Quarterly Vol. 8pp129-136.
- Durojaye, M. S. (1976). *An Introduction to Education Psychology*. Evans Brothers Publishers
- Eckert, P. (2003). *Languages and Gender*.Cambridge University Press(Ed). Business Education Publishers Limited.
- Eckert, P. (2007). *Languages and Gender*: Cambridge university press (Ed). Business Education Publishers Limited.
- Ehrman, M. (1990). The role of personality type in adult language learning: An on-going investigation. Katika T. Parry, S. na C. W. Stansfield (Eds.), *Language aptitude reconsidered* (pp. 126-178). Englewood Cliffs, NJ: Prentice Hall Regents.
- Ehrman, M. (1996). *Second Language Learning Difficulties*: Looking Beneath the Surface.
- Ehrman, M. E. na Oxford, R. L. (1990). Adult Language Learning Style and Strategies in an Intensive Training Setting (J) *Modern Language Journal*, 74(3)
- Ehrman, M. na Rebecca, O. (1989). Effects of sex differences, career choice and psychological type on adult language learning strategies. *The Modern Language Journal*73/1,13.
- Ehrman, M. na Oxford, R. (1995). Cognition plus: correlates of language learning success.*Modern Language Journal*,79,67.
- Eisner, E. W. (1991). *The enlightened eye. Qualitative Inquiry and enhancement of educational practice*. Macmillan Publishing Company.
- Ellis, R. (1986). *Understanding Second Language Acquisition*. Oxford University Press
- Ellis, R. (1994). *The Study of Second Language Acquisition*. Oxford University Press
- Ellis,R. (1997). *Second Language Research and Language Teaching*. Oxford University Press
- Ellis, R. (2003). *Language Style and Strategies*. Oxford Gala learner in multisector

- courses.* Heinle na Heinle.
- Ellis, R. (2005). Instructed language learning and task-based instruction. Katika E. Hinkle (Ed.), *Handbook of Research in Second Language Teaching and Learning* (pp. 713-728). Mahwah Lawrence Erlbaum.
- Emma, W. (2020). *The Mission of Apolo Kivebulaya.* Religious Encounter & Social Change in The Great Lakes. Twaweza Communications. Nairobi Kenya
- Esther, M. L na Leonard, M. (2000). *African languages and literature in the 21st century.* Palgrave Macmillan.
- Eysenck, M.W. (1979). Anxiety. Learning and Memory: A Reconceptualization Journal of Research in Personality, 13, 363-385.
- Ezat, A. K. (2015). Learning Strategies in Second Language Acquisition; Lorestan University, Khorramabad, Iran (Tasnifu ya Uzamili) Bado haijachapishwa.
- Faerch, C., na Kasper, G. (1980). Procedural knowledge as a component of foreign language Learners Communicative competence. Katika H. Boete na W. Herrlitz (Eds), *Kommunicationim (Sprach)* Unterrich. Utrecht:
- Fasold, R. na Linton, J.C (2006). "Universal Properties of Language „katika Fasold R na Linton J.C (wah) An Introduction to Language and Linguistics. New York: Cambridge University Press.
- Fathman, A. (1975). *The Relationship between Age and Second Language ProductiveAbility, Language Learning.* 21, 245-253.
- Felder, R.M. na Henriques, E. R. (1995). Learning and Teaching Styles in Foreign SecondLanguage Education. *ForeignLanguage Annals.* 28. Vol. 121-31.
- Field, A. (2005). Reliability analysis. Katika : Field, A. Ed, *Discovering statics' using spss.* 2<sup>nd</sup>. Edition, Sage London
- Fleming, N. (2001). *Teaching and Learning Styles.* VARK Strategies Christchurch.
- Franken, R. E. (1982). *Human Motivation.* Monterey, C.A Brooks and Cole Publishing Co.
- Fromkin, V, na Rodman (1993). *An Introduction to Language.* Harcourt. Brace
- Galloway, V. na Labarca, A. (1991). From Student to learner. Style, process and Strategy Katika D.W. Birckbichler (Ed), *New Perspective and New Directions in Foreign Language Education.* Lincolnwood, IL: National Textbook Company, 111-158.
- Gardener, R. C. (2007). *Motivation and second language acquisition.* Pata Linguarum, 8, 9-20.
- Gardener, R.C. (2010). *Motivation and Second Language Acquisition. The Socio-Educational model.* Peter Language Publishing
- Gardener, R.C. (2010a). Motivation and Second Language Acquisition. *The Socio-educational model.* Peter Langage Publishing.
- Gardener, R.C. (2010b). Second Language Acquisition. A Social psychological perspective katika R.B Kaplam (Ed), *The Oxford handbook of applied linguistics.* Oxford University Press.
- Gardner, R. C. (1960). Motivational variables in second-language acquisition. Tasnifu ya

- Uzamifu bado haijachapishwa, McGill University, Montreal, Canada.
- Gardner, R. C. (1979). Social psychological aspects of second language acquisition. Katika Giles and R. St Clair (Bds), *Muage and Social Psychology*, pp. 193-220. Oxford: Blackwell
- Gardner, R. C. (1985). Social Psychology and Second Language Learning: *The Role of Attitudes and Motivation*. Edward Arnold Publishers.
- Gardner, R. C. (1985a). *The Attitude/Motivation Test Battery: Technical Report*. Ontario, Canada: University of Western Ontario, Department of Psychology.
- Gardner, R. C. (1988). The socio-educational model of second language learning: Assumptions, findings and issues. *Language Learning*, 38, 101-126. doi/abs/10.1111/j.1467-1770.1988.tb00403.x
- Gardner, R. C. (2000). Correlation, causation, motivation and second language acquisition. *Canadian Psychology*, 41, 1-24.
- Gardner, R. C. (2010). *Motivation and second language acquisition: The Socio-educational Model*. New York: Peter Lang.
- Gardner, R. C., na Lambert, W. E. (1959). Motivational variables in second language acquisition. *Katika Jarida la Saikolojia*, 13, 266-272.
- Gardner, R. C., na Lambert, W. E. (1972). *Attitudes and Motivation in Second Language Learning*. Newbury House.
- Gardner, R. C., Lalonde, R.N., and Moorcroft, R. (1985). *The Role of Attitudes and Motivation in Second Language Learning: Correlational and Experimental Considerations*. *Language Learning*, 35, 207-227.
- Gardner, R. C., na MacIntyre, P. D. (1993). *A student's contributions to second language learning. Part II: Affective variables*. *LanguageTeaching*, 26, 1-11.
- Gardner, R. C. na Tremblay, P. F. (1994). On motivation, research agendas, and theoretical frameworks. *Modern Language Journal*, 78, 359-368.
- Gardner, R. C, Smyth, P. C., Clément, R., na Gliksman, L. (1976). Second language learning: A social psychological perspective. *Canadian Modern Language Review*, 32, 198-213.
- Gardner, R.C. (2007). *Motivation and second language acquisition*. Porta Linguarum,
- Garfinkel, A. (1972). Teaching Languge Via Radio. A review of resources. *MLJ*, 56 158-162.
- Garibaldi, E. S. (2013). *Second Language Acquisition. The Effects of Language and Motivation*. HaskolIslands Hugvisindasvio.
- Gass, S na Selinker, L (1994). Second Language Acquisition. An Introductory Course in. N. Absamra (2003). *An Analysis of Errors in Arabic Speakers'*. English Writtings.
- Gass, S.M. na Mackey, A. (2012). The Routledge Handbook of Second Language Acquisition, London, Routledge; Lightbown, P.M. and Spada, N. (2013) How Languages are Learned, Oxford, Oxford University Press;

- Gass, S. (2022). *Studies in Second Language Acquisition*. Cambridge Press
- Gay, L.R., Mills, G.E. na Airasian, P. (2006). *Educational Research: Competences for Analysis and Applications*. Merrill Greenwood.
- Ghalebi, R., Sadighi, F. na Bagheri, M. S (2020). Vocabulary Learning Strategies: A Comparative Study of EFL Learners. *Cogent Psychology*, 7(1) 1825306 doi:10:23311908.
- Gomm, R. (2000). *Case Study Method. Key Issues, Key texts*. London: Sage Publishers.
- Gong, Y., Gao, X. na Lyu, B. (2020a). *Teaching Chinese a Second Language or Foreign Language to non-chinese learners in mainland* (2014-2018). *Lang Teach*.53,44-62.doi:10.1017/S0261444819000387.
- Goold, A. na Rimmer, R. (2000). Factors affecting performance in first year computing. *SIGSE Bulletin*, 32(2)39-43.
- Green, J., na Oxford, R. (1995). A Closer Look at Learning Strategies, L2 Proficiency and Gender. *TESOLQuarterly*,29(2),261-292.
- Griffiths, C. (2003). Patterns of Language Strategy Use, System 31,367-383. New Zealand.
- Griffiths, C. (2004). Language learning strategies: Theory and research school of foundationstudies. New Zealand.
- Grix, J. (2010). *The Foundation of Research*. Toelo la Pili. Palgrave Macmillan
- Guba, E. G. na Lincoln, Y.S. (2000). *Fourth Generation Evaluation*. Sage Publications.
- Guilbault, V., Harvey, S. P., & Vallerand, R. J. (2020). Dancing with passion: A look at interpersonal relationships. *Psychology of Sport and Exercise*. <https://doi.org/10.1016/j.psychsport.2020.101667>.
- Giles, H. na Clair, R (Eds.), *Language and Social Psychology*. Basil Blackwell.
- Habermans, J (1981). The theory of Communicative Action. VOL.1 in Reason and Realisation of Society. T. Mc Carthy. Trans Boston: Beacon Press
- Habwe, J. (2018). Hali na maendeleo ya lugha ya Kiswahili Nchini Sudan Kusini. *Ismu nafasihi ya lugha Za Kiafrika*. Moi University Press.
- Habwe, J., na Karanja.P.(2004). *Misingi ya Sarifi ya Kiswahili*. Phoenix Publishers.
- Hajimia, H., Sigh, M. K. S, na Chethiyar, S. D. M. (2020). Second Language Acquisition: Krashen Monitor Natural Approach. *PEOPLE: International Journal of Social Sciences*, 6(3),87-99.<https://oadoi.org/10.20319/pijss.2020.63.8799>.
- Hans, J.E. (1990). *Biological Dimensions of Personality*: The Guildford Press
- Hardach, S. (2018). Speaking more than one language can boost economic growth.
- Hartman, F. R. (1963). A Behaviouristic Approach to Communication: A Selective Review of Learning Theory and a Derivation of Postulates. *Audio Visual CommunicationReview*, 11(5), 155–190.
- Hassan, A. (2000). Communication in intercultural discourse, Tasnifu ya Uzamili ambayo haijachapishwa. Chuo Kikuu Kenyatta.
- Herman, H. (2009). The Start and Progress of a Language Instruction research Project in

- Africa. *The Spirit of Bagamoyo. The Implication of Language for Peace and Development.* Mkuki na Nyota Publishers.
- Herman, M. P. D. (2015). A Direct Translation Analysis of Mobile Phone User Guide. An Applied Linguistics Study, IOSR. Katika *Journal of Humanities and Social Sciences* (IOSR-JHSS), 20. PP01-09.
- Hoffman, C. (2000).*The spread of English and the growth of multilingualism with English in Europe.* katika: Cenoz, Jasone, Ulrike Jessner (eds), *English in Troupe. The acquisition of a third language*, 1-21. Clevedon: Multilingual Matters
- Holland, M., Kaplan, J. na Sams, M. (1995). *Intelligent Language Tutors: Theory Shaping Technology.* Mahwah, NJ: Lawrence Erlbaum.
- House, J. (2002).Developing pragmatic competence in English as a lingua franca katika Karlfried Knapp, Christiane Melerkord (eds),*Lingua franca communication*,245-267 Franfurt am Main.Peter Lang
- Hughes, A. (2003). *Testing for Language Teachers.*Cambridge .
- Hymes, D. (1975). On communicative competence. KatikaPride na Holmes (Eds).
- Jenkins, R. (2000). *The Phonology of English as an International Language.* Oxford University Press.
- Jiingo, C. & Bakize (2021). Modelling Contemporary Perspectives on Materials Development for Kiswahili Pedagogies in Ugandas Lowers Secondary School. Katika *African Journals Online* Issn: 0023-1886
- Jilala, H. (2016).*Nadharia za Tafsiri,ukalimani na uundaji wa istilahi.* Daud Publishing Company Limited.
- Jonathan, W. (2013).*Essentials of Business Research.* Guide to doing your research project. Sage
- Joppe, M. (2000). The Research Process.*The Quantitative report journal.*8(4) pp.597-607.
- Kajubi, W. (1989). Education for national integration and development: Report of the Education Policy Review Commission. Kampala, Uganda: Ministry of Education.
- KAKAMA (2019). A Report on Capacity Assessment of Development na Use of Kiswahili in East African Kiswahili Commission.
- Kameerer, C.V.(1990). *Motivation as a prerequisite.* Oxford University Presss.
- Katrina. R, (2004). *Testing Krashen Input Hypothesis:*A Study in a male Czech Adult Acquiring English.Masryk University in Brno.Tasnifu ya uzamili.
- Keefe, J. (1979). *Student Learning Style. Diagnosing na Prescribing Programs* (M) Peston.Y. A National Association of Secondary School Principals.
- Kembo –Sure na Ogechi.N.O (2006). Language Planning for and Reform. An Alternative Language Policy for Kenya. In Kembo-Sure, S. Mwangi and N.O. Ogechi. (Eds.) *Language Planning for Development in Africa.* (pp.37-54). Moi University Press.
- Kia, M., Alipour A, na Ghaderi, E. (2009). Study of learning styles and their roles in the academic achievement of the students of Payanne Noor University. *Turkish Online Journal of Distanc Education.*TOJDE,10(2),17-28.

- Kiango, J. G. (2002). Nafasi ya Kiswahili Katika Ujenzi wa Jamii Mpya ya Afrika Mashariki. Katika, *Nordic Journal of African Studies*.11(2):185-197.
- Kimaro, H. (2015). *Changamoto Zinazokumba Ufundishaji wa Kiswahili*. National Media,Com
- King, K. A. (2006)."Child Language Acquisition" katika Fasold R na Linton J.C (wah) *An Introduction to Language and Linguistics*. Cambridge University Press.uk (205-234).
- Kishe, A. M. (2018). Kiswahili na utangamano wa jumuya ya Africa mashariki: *Kiswahili Utangamano na Maendeleo ya Africa Mashariki*. KAKAMA.
- Kitetu, W.C. (2003). *Ethical Issues in Data Collection, in Social Sciences. Getting into the field*. Catherine Wawasi Kitetu (ed) AICD/Department of Languages na Linguistics, Egerton University.
- Kombo, D. K., na Tromp, D.L.A. (2016). *Proposal and thesis writing*. An introduction, Nairobi Paulines Publications Africa –Kenya.
- Kothari, C. R (2003). *Research Methodology: Methods and Techniques*. New Delhi Wishwa Prakashan
- Krashen, S. (1976). Formal and informal linguistic environments in language acquisitionandlanguagelearning.*TESOLQuantity*,10,157-68.
- Krashen, S. (1977). *Some issues relating to the monitor model*. katika H. Brown et al (eds), 144-158.
- Krashen, S. (1994). The input hypothesis and its rivals. In N. Ellis (Ed.) *Implicit and explicit learning of languages*. (p. 45-77). London: Academic Pre
- Krashen, S. D. (1982). *Principles and practice in 2nd language acquisition*. Pergamon Press.
- Krashen, S. D (1985). *The input hypothesis*. Longman.
- Krashen, S. D. na Terrel.D .T. (1983). *The Natural Approach*. Hayward Press.
- Krashen, S. D. (1977). *Some issues relating to the monitor model*. Katika H. Brown nawenzake (eds), 144-158.
- Krashen, S. D. (1987). *Principles and Practice in Second Language Acquisition*. New YorkPrentice Hall International.
- Krashen, S. D. & Fahad, A. (2020). Krashen Theories on Second Language learning. University of Kentucky
- Krashen, S. D. (1981). *Second Language Acquisition and Second Language*.Oxford Pergamon Press.
- Krashen, S. D. (2011). Free voluntary reading. Santa Barbara, CA: ABC-CLIO.
- Krashen,S. D na Terrell, T. D (1983). The Natural Approach: Language acquisition in the Classroom. doi:[10.5785/1-2-506](https://doi.org/10.5785/1-2-506)
- Krejcie, R. V. na Morgan, D.W., (1970). Determining Sample Size for Research Activities. *Educational and Psychological Measurement*. <https://journals.sagepub.com/doi/abs/10.1177/001316447003000308>
- Kvale, S (1996).*Interviews views. An Introduction to Qualitative Research Interviewing*.

- Thousand Oaks, CA: Sage Publications
- Ladefoged, P. (1971). *A Course in Phonetics*. Harcourt Brace Jovanovich, Inc.
- Lalonde, R. N. na Gardner, R. C. (1985). On the predictive validity of the Attitude/Motivation Test Battery. *Journal of Multilingual and Multicultural Development*, 6, 403-412.
- Lalonde, R. N., na Microsoft, R. (1985). *The Role of Attitudes and Motivation in Second Language Learning: Correlational and Experimental Considerations*. *Language Learning*, 35, 207-227.
- Lam, W.Y. K. (2010). Implementing communication strategy instruction in the ESL oral classroom: What do low proficiency learners tell us? *TESOL Canada Journal*, 27 (2). 11-30.
- Lambert, W.E. (1974). Culture and language as factors in learning and education. Katika Aboud, F. E. na Meade, R. D. (eds.) *Cultural factors in learning and education*, Bellingham, Washington, Fifth Western Washington Symposium on Learning.
- Lambert, W.E. (1967). Social Psychology of Bilingualism. *Journal of Social Issues*, 23, 91109. *Language strategies in language learning* Englewood Cliffs, N. J. Prentice Hall.
- Larsen-Freeman, D. na Long, M. (1991). *Introduction to Second Language Acquisition Research*. Longman
- Lawrence, G. (1984). A synthesis of learning style research involving the MBTI. "Journal of Psychological Type," 8, pp2-15.
- Leaver, B. L. (1986). *Hemispherity of the brain and foreign language teaching*. "Folia Slavica," 8, pp76-90.
- Lenneberg, E. (1976). *Biological Foundations of Language*. John Wiley and Sons.
- Levy, M. (1997). Theory-driven CALL and the development process. *Computer Language Learning*. 10, 41-56
- Li, C. L (2021). Understanding EAP Learners Beliefs about Language Learning from a social-cultural perspective: A Longitudinal Study at an EMI Context in mainland China. <https://onlinelibrary.wiley.com/doi/10.1111/ijal.12402>
- Lin, G. H (2007). A Case study of seven Taiwanese English as a Foreign language freshman non-English majors parpectives about learning fire communication strategies .Tasnifu ya Uzamili,bado haijachapishwa.Texas A&M University, College Station
- Lina. A (2017). Changamoto zinazowakabili walimu katika ufundishaji wa Kiswahili katika shuleza upili nchini Kenya. Makala ya Kioo cha Lugha <https://www.ajol.info/index.php/kcl/article/view/159249>
- Lindsay, E. K. (1999). An analysis of matches of the teaching style and the uses of education technology. *The American journal of distance education*, 13(2), 113-119.
- Long, M. H. (1983). Does second language instruction make a difference? A review of the research [J]. *TESOL Quarterly*, 17, 359-382.
- Long, M.H. (1991). Focus on form: A design feature in language teaching methodology[C].katika K. de Bot, R. Ginsberg, na C. Kramsch (Eds.), *Foreign*

- language research in cross-culture perspective* (pp.39-52).
- Long, M. H. (1990). Linguistic conversational Adjustments to non-native speaker, studies in 2nd Language Acquisition Research. Gorde, West Germany.
- Lucy, J. (2014). Why language skills are great for business. *The guardian* (Guardian smallbusinessnetwork).
- Macaro. E (2001). *Learning Strategies in Foreign na Second Language Classroom*. London: CPD, Ebbw, Vale.
- MacIntyre, P. D. na Gardner, R. C. (1991). *An Instrumental Motivation in Language Study: Who says it isn't effective?* Studies in Second Language Acquisition, 13, 57-72.
- MacIntyre, P. D., na Charos, C. (1996). Personality, attitudes, and affect as predictors of second language communication. *Journal of Language and Social Psychology*, 15, 3-26. <http://dx.doi.org/10.1177/0261927X960151001>.
- MacIntyre, P., & Gregersen, T. (2012a). Emotions that facilitate language learning: The positive-broadening power of the imagination. *Studies in Second Langauge Learning and Teaching*, 2, 193–213.
- Mackey, A. (2006)."Second Language Acquisition" katika Fasold, R na Linton, J.C (Wah) *An Introduction to Language and Linguistics*. Cambridge University Press. 433-462
- Maclyntyre, P. D (1995). How Does Anxiety Affect Second Language Learning? A Reply to Sparks and Ganschow. *The Modern Language Journal*,79,90-99. <https://doi.org/10.1111/j.1540-4781.tb.05418.x>
- Masereka, L. (2018). Kiswahili, Siasa na Demokrasia nchini Uganda. *Kiswahili Utangamano na Maendeleo Endelevu ya Afrika Mashariki*. KAKAMA.Zanzibar Tanzania.
- Massamba, D. P. B. (2012). Sarufi Maumbo ya Kiswahili Sanifu (SAMAKISA); Sekondari na Vyuo. Dar es Salaam: TUKI
- Mathooko , P.M (2007).*Isimu Jamii.Misingi ya Nadharia,Nairobi*:Njiko Books.
- Maxwell, J. A. (1992). *Understanding and validity in qualitative research*. Harvard Educational Review, 62, 279-299
- Mayaka, G, Aswan, B, Matinde,R.(2014).*Misingi ya Nadharia na Mbinu zaUtafiti*. Serengeti Educational Publishers.LTD
- Mazrui, A.,M.&Njogu,K.(2018). Language Policy in African Higher Education: Between Dependency and Decolonisation. Rajend Meshrie and David Bradley (Eds). *The Dynamics of Language*.Cape Town:UCT Presss,kur.264-279
- McCawley, J. D. (1974). Review of Chomsky and Halle; *The Sound Pattern of English*.Katika IJAL 40; 50-88.
- McDonough, S. H (1986). *Psychology in Foreign Language Teaching*. George Allen and Unwin.
- Mertens, D. M. (2008). *Mixed Methods and the Politics of Human Research*. In Clark,V.P naCreswell, J. W(eds). Sage
- Mfitumukiza, S. (2018).The Beginnings of the Aglican Church in Bufumbira and the East

- African Revival Experiences in the area. *The East African Revival Through 80 Years. Testimonies, Stories and Reflecion*s.
- Mwesigwa Mugabi Publications.
- Mgullu, R. S. (1999). *Mtaala wa Isimu*.: Longhorn Publishers
- Miles, M. B. na Huberman, A.M (1994). *Qualitative Data Analysis*. California Sage.
- Miller, D. C., & Byrnes, J.P. (2001). *To achieve or not to achieve: A self-regulation perspective*. <https://psycnet.apa.org/record/2001-05329-002>.
- Minti, G. (2012). *Politeness and speech accommodation in intercultural business negotiations*: a case study of Igembe and Somali mira traders Nairobi unpublished thesis
- Mkude, D. (2005). The Passive Construction in Kiswahili. *Research Institution of Language and Cultures of Asia and Africa (ILCAA)* Tokyo University of Foreign Series Vol.4.
- Mkwinda-Nyasulu. B. (2013). Role of Language in Socio-Economic development: *The Semiotics are right*.
- Moenikia, M. na Zahed-Babelon, A. (2010). *The Role of Learning Style in 2nd Language Learning among Distance education structures procedure social na behavior sciences* 2 (2010) 1169-1173.
- Mogore, G. (2018). Changamoto za Kufundisha Shule za Chekechea katika Mazingira ya Wingi-Lugha Mjini Garissa. *Isimu na Fasihi ya Lugha za Kitaifa*. Moi University Press
- Mohochi, S. (2018). Kiswahili na ushikishwaji wa Umma wa Africa Mashariki. *Kiswahili Utangamano na Maendeleo Endelevu Afrika Mashariki* .KAKAMA, Zanzibar Tanzania
- Momanyi, C. (2018). Kiswahili: Rasilimali ya Kiuchumiya Afrika Mashariki. *Kiswahili Utangamano na Maendeleo Endelevu Afrika Mashariki* .KAKAMA, Zanzibar Tanzania
- Monica, H. (2003). *Globalization, the new economy and the modification of language and identity*. Maktaba ya mtandaoni. <https://doi.org/10.1111/j.1467-9841.2003.00238.x>
- Monica, H. (2003). *Language, Skills and authenticity in the global new economy*. Xinjie, C. Robert, J.V Amado, M.P (2021). the Role of Passion in Second Language Learning and Flourishing. *Journal of Happiness Studies*. <https://doi.org/10.1007/s10902>
- Montano, J.X. (2017). Learning Strategies in Second Language Acquisition [https://www.researchgate.net/publication/321214935\\_Learning\\_Strategies\\_in\\_Second\\_Language\\_Acquisition](https://www.researchgate.net/publication/321214935_Learning_Strategies_in_Second_Language_Acquisition). DOI: [10.17265/1539-8080/2017.08.001](https://doi.org/10.17265/1539-8080/2017.08.001).
- Montgomery, S., na Grout, L. (1998). Student learning styles and their implications for teaching. Michigan: *Centre for Research on Learning and Teaching* (CRLT), University of Michigan.
- Moody, R. (1988). "Personality Preferences" na Foreign Language Learning". *The Modern Language Journal*. 72: 389-401. <http://doi.org/csf634>.
- Moshman, D. (1993). Adolescent reasoning and adolescent rights. *Human Development*.

- Moss, D. & Ross-Feldman, L. (2003). Second language acquisition in adults: From research to practice. Imepakuliwa Agosti 8, 2021, kutoka Center for Applied Linguistics: [http://www.cal.org/CAELA/esl\\_resources/digests/SLA.html](http://www.cal.org/CAELA/esl_resources/digests/SLA.html)
- Muaka; L. (2020). *Linguistic Commodification and Africa's Linguistic Identities: Creating Nexus. African Languages and Literatures in the 21st Century.* Palgrave Macmillan
- Mugenda, O. M. na Mugenda, A. G (2003). *Research methods: Quantitative and qualitative approaches:* Nairobi Acts Press
- Mugenda, O. M., na Mugenda, A. G. (2012). *Research Methods: Quantitative and Qualitative Approaches.* Acts Press.
- Mukama, R.(1995).Uendelezaji ,Ukuzaji na Usambazaji wa Kiswahili Uganda Katika ,A. S. K. Mlacha (Mh) *Kiswahili Katika Kanda ya Afrika Mashariki.uk* 38-48.TUKI ChuoKikuu Dar es Salaam.
- Mukuthuria, M. (2006). Kiswahili na its expanding roles of development in east African Cooperation: *A Case of Uganda. Nordic Journal of African Studies* 15(2):154-165.
- Muranga, M. J. K. (2018).East African Revival and Its Impact on Church and Society in Uganda.In.*The East African Revival through 80 Years.Testimonies, Stories and Reflecions.* Mwesigwa Mugabi Publications.
- Museveni, Y. K. (1990). Address by the President of the Republic of Uganda to the Third Congress of the Organization for Social Sciences Research in Eastern African (OSSREA) Kampala Uganda (May).
- Mutembei, A. (2016). Utandawazi wa Lugha za Kiafrika: Nafasi ya Kiswahili Sanifu Katika Afrika inayobadilika. Jilala, H (Mh). *Nadaharia za Tafsiri, Ukalimani na Uundaji wa Istilahi.*Daud Publishing Company Limited
- Mwansoko, H. J. M. (2016). Ukuzaji wa Kiswahili Kupitia Tafsiri. *Nadaharia za Tafsiri, Ukalimani na Uuundaji wa Istilahi.* DAUD Publishing Company Limited
- Myers, J.L, Well, A.D na Larch Jr.R.F (2013). *Research design and stastical Analysis.*
- Myles, F. na Mitchel (2004). *From Data to Theory; Representation of Linguistic Knowledge in SLA. Transactions of the Philological Society,*102, 139-168.
- Naiman, N., Frohlich, M., na Todesco, A. (1975). *The good language learner;* "TESOLTalk,"6,pp58-75.
- Nakatani, Y .(2010). Identifying strategies that facilitate EFL Learners oral communication: A classroom study using multiple data collection procedures.*The modern language journal.* 94 (1).116-136.
- Nakibuka, K. M. (1995). *Okwanjula phonologia w'oluganda akatabo akasoka.* MakerereUniversity Press
- Nelly, Z. (2009). *A Drama in Language Teaching; A Challenge for Creative Development*
- NIED. (2009). National Institute for Development, NSSCH, English Secondary Language Syllabus Grade 11 na 12 Okahandja.
- Nicholson, S. J. (2013).Influencing Motivation in the Foreign Language Classroom.*Journal of International Education Research,* 9(3), 277-286.

- Nick, C. E (2008). The dynamics of second language emergence: Cycles of language use, language change, and language acquisition Katika, *The modern language journal*, 92(2), 232-249.
- Northwood, B. (2014). *Passion, persistence & learning Japanese*. Makala iliyowasilishwa katika kongamano 18 katika masomo ya Kijapani. A paper presented at the Proceedings of the 18th Conference of the Japanese Studies. Chama cha Australasia katika Chuo Kikuu cha Kitaifa cha Australia.
- Nor-Farhana. M. F na Hamida.Y. (2003). Language learning challenges and solution at Melaka Foundation College. *Jarida la Journal of Education and Social Sciences*, Vol. 9, Issue 2,
- Nyiikos, M. (1990).Sex-Related Differences in Adult Language Learning: Socialization and Memory Factors. *The Modern Journal*, 74,273-286.<https://doi.org/10.1111/j.1540-478.1990.tb01063.x>
- O'Malley, J. M (1995). *Classification of Language Learning Strategies*. Cambridge University Press
- O'Malley, J. M. na Chamot, A. U (1990). *Learning Strategies in Second Language Acquisition*. Cambridge University Press.
- O'Malley, J. M., na Chamot, A. (1990). *Learning Strategies in Second Language Acquisition*. Cambridge: Cambridge University Press.
- O'Malley, M., na Oxford R (1990). *Learning Strategies in Second Language Acquisition*. Cambridge University Press.
- Oxford, R. (1989). The use of language learning strategies: A synthesis of studies with implications for strategy training. "System," 12(2), pp235-47.
- Oxford, R. (1990). "Language learning strategies: What every teacher should know." New York: Newbury House/ Harper na Row.
- Oxford, R. (1992/1993). Language Learning Strategies in a Nutshell: *Update and ESL Suggestions TESOL Journal*, 2(2)18-22.
- Oxford, R. (1994). Language Learning Strategies: *An Update*. University of Alabama.
- Oxford, R. (2003). *Language Learning Style and Strategies*. Cambridge University Press.
- Oxford, R. na Nyikos (1989). Variables affecting choice of language learning strategies by university students. *The modern language journal*, 73/3,291-
- Oxford, R. na Shearin, J. (1994). Language Learning Motivation: Expanding the Theoretical Framework. *The Modern Language Journal* 78:12- 28.
- Oxford, R., na Nyikos. (1989). Variables affecting choice of language learning strategies by university students. *The Modern Language Journal*, 73/3, 291-300.
- Oxford, R.L. na Cohen,A.D (1992). Language Learning Strategies: *Crucial Issues of Concepts and Classification*. *Applied Language Learning*, 3,1-35.
- Pahari, A. P., na Kaira, G. (2013). Use of mobile phones as research instruments for data collection. *Indian Journal of Community Health*: Vol 25 No 2

- Pakhare, A. P., Kaira G. (2013). Use of Mobile Phones as Research Instrument for DataCollection.*Indian Journal of Community Health*.VOL25.
- Palma,A.J.C na Madrigal,D.V (2021).An explanatory inquiry into second language acquisition of junior high school.Non members.*Technium Social Sciences Journal*,20 (1) 163-171.
- Paribakht, T. (1985).Strategie Competence and language proficiency.Applied Linguistics.6,132- 146.
- Parry, T. S. (1984). "The relationship of selected dimensions of learner cognitive style, aptitude, and general intelligence factors to selected foreign language proficiency tasks of second-year students of Spanish at the secondary level." Tasnifu, Ohio StateUniversity,Columbus,
- Peter, G. (2012).*Attitudes to Language*.Cambridge University.Kitabu cha mtandaoni.<https://doi.org/10.1017/CBO9780511844713>.
- Phillips, A. (2007). *Multiculturalism with culture*. Princeton NJ Princeton University Press
- Piggott, J. (2008). Toward classroom-friendly models of motivation: A data-led investigationinto student perceptions of motivating and demotivating classroom factors, and the relationship between student orientations and preferred classroom activities. Tasnifu ya Uzamili.
- Politzer, R. na McGroarty, M. (1985). An Exploratory Study of Learning Behaviours and TheirRelationship to Gains in Linguistic and Communicative Competence. *TESOLQuarterly*,19,103-123.
- Poulisse, N. (1990). Variation in learners use of communication strategies. Katika R. Dudana. P, Riley (eds.), *Learning Styles*, First European Seminars (pp.77-87). Nancy. Univasitaries de Nancy.
- Prah, K. K. (2003)."Going Native: Language of Instruction for Education, development and African Emancipation". Language of Instruction in Tanzania and South Africa (LOITASA):14-34.
- Pring, R.(2000). *Philosophy of Educational Research*.:Continuum.International Publishing Group.
- Prokop, M. (1989).Learning Strategies for Second Language Users:*An Analytical Approachwith Case Studies*. The Edwin Mellen Press.
- Punch, K. F. (2009). *Introduction to Research Methods in Education*.:Sage
- Purpura, J. (1999). Learner Characteristics and L2 Text Performance. Katika R.L Oxford (ed). *Language Learning Strategies in the Context of Autonomy, Synthesis of Findings from the International Invitational Conference on Learning Strategy Research* (pp. 61-63), Teachers College, Columbia University, New York, NY
- Rae, B. S. (1973). *Moral Choices: An Introduction to Ethics*.USA: International Bible Permission of Zondervan.
- Rahim, M., Riaz, A. na Saif, S. (2008). An Investigation into the factors affecting the use of language learning strategies by Persia ELF Learners. *Canadian Journal of Applied Linguistics*,11(2),31-60.
- Reece, I na Walker, S. (1997). *Teaching, training and learning*. A practical Guide (3rd

edition)

- Reid, J. M. (1987). The learning style preferences of ESL students. "TESOL Quarterly," 21, pp87-111. <https://onlinelibrary.wiley.com/doi/abs/10.2307/3586356>
- Reid, J. M. (1998). *Understanding learning style in the second language classroom* [M]. Prentice Hall Regents.
- Richard, M.F na Eunice,R.H (1995). *Learning and Teaching Styles I Foreign and Second Language Education. ForeignLanguage Arnals*.Vol.1.pp.21-31.
- Richards, J. C. (1985). *The context of language teaching*. Cambridge University Press.
- Ritgero, E., na Garibaidi S. (2013). Second languages acquisition. The effects of language and motivation. HASKOLI ISLANDS. HugvisindasvioRobert, Karika *Research in African Literatures*, Vol 39 Issue 3 pp 99-120.
- Rock, J. (2012).Teaching and researching motivation (2nd ) edn. [Review of the book *Teaching and researching motivation*, by Dornyeina E.Ushioda] The Electronic Journal for English as a Second Language.16(2)1-4.
- Rosenberg, A. (2008). *Making The Case for Popular Songs in East Africa*: Samba Mapangalana Shaban
- Rubin, J. (1975). What the 'good language learner' can teach us [J]. TESOL Quarterly, 9(1),41-51.
- Rubin, J. (1987). Learner Strategies. *Theoretical Assumptions, Research History, Anthropology*. Eagle wood Cliffs Heinle na Heinle
- Rubin, J. na Thompson, I. (1994). *How to be a more successful Laerner*, 2nd ed. Heinle na Heinle
- Ryanga, S. A. (2018). Utangamano na Mshikamano wa Jamii za Mipakani Afrika. *Kiswahili Utangamano na Maendeleo Endelevu ya Afrika Mashariki*. KAKAMA.Zanzibar
- Sapir, E. (1949). The Psychological Reality of Phonemes". Katika Mandelbaum, D.G(mh) *selected writings of Sapir* uk. 46-60 Berkeley. University of California Press.
- Sapir, E. (1985). *Culture, Language and Personality: Selected Essays* (Vol.342). Oakland: University of California Press
- Sarah, N. M. N., na Leonard. M. (2019). *Dhima na Changamoto ya Tafsiri katika ufundishaji wa Kiswahili Nchini Uganda*: Makala ya CHAUKUDU. Haijachapishwa)
- Saranray, L., na Meenakshi, K. (2016). The influence of Anxiety in Second Language Learning: A Case with Reference to Engineering Students in Tamil Mada, India. *Indian Journal of Science and Technology*, Vol 19.
- Saunders, M. (2009). *Research methods*. Harlow Essex. Prentice
- Saville-Troike, M. (2012) Introducing Second Language Acquisition, Cambridge, Cambridge University Press
- Schmidt, R. (1994). *Deconstructing consciousness in search of useful definitions for appliedLinguistics*. AILAReview, Vol:11-16.
- Schwarz, R., & Terrill, L. (2000). Adult English language learners and learning disabilities. Center for Adult Language Acquisition.

- Scollon, R. na Scollon S. W. (2001). *Intercultural communication, a discourse approach*, 2eds. Oxford: Blackwell publishers
- Seale, C. (2000). *The Quality of Qualitative Research*. Sage
- Seliger, H. (1984). Processing Universals in Second Language Acquisition. In F.
- Selinker, K. (1972). Second Language Acquisition Speaking a Foreign Language. ResearchReport. Minneapolis, Minnesota, USA.
- Selinker, L., na Gas (2008). Second Language Acquisition. *The Role of the Native Language: An Historical View*. New York na London Routledge.
- Senkoro, F. E. M. K (2018). Kiswahili Africa: Jana, leo na kesho 2018:46 (KAKAMA)
- Sewangi,S.S (2007).Uundaji wa Istilahi za Kiswahili Kileksografia na athari zake Katika .*NordicJournal of African Studies*.16(3):333-344.
- Shamoo, E.A. na Resink, B.R. (2003). *Responsible Conduct of Research*. Oxford University Press.
- Shelly, S. (2017). *Importance of Language in Development*, Makala iliyowasilishwa Washington State University.
- Shipman, S., na Shipman, V. (1985). Cognitive styles: Some conceptual, methodological, and applied issues. In E. Gordon (Ed.), "Review of research in education," v12, pp229-91.Washington, DC: American Educational Research Association.
- Shulman, L. (1986). Paradigms and Research Programmes in the Study of Teaching". Katika M. Wittrock (ed.). *Handbook of Research on Teaching*, London: McMillan. 6 (2), 95-105.
- Shulz, R. (1991). Second Language Acquisition themes and teaching practice. How do they fit: *The Modern Language Journal*. 75,17-26. <https://doi.org/10.2307/32983/>
- Simiyu, F. W. na Kavoi, J. M. (2013). *Stadi za Mawasiliano na Mbinu za Kufundishia Kiswahili*. Serengeti Educational Publishers (T) Limited Mwanza Tanzania.
- Skehan, P. (1991). Individual differences in second language learning. *Studies in Second Language Acquisition*, 13 275-298 doi/10.1017/S0272263100009979
- Skinner, B.F (1957). *Verbal behavior theory*: Cambridge University. UK
- Ssekamwa .J.C (2000). *History na Development of Education in Uganda*, Kampala Fountain Publishers.
- Stern, H. H. (1983). *Fundamental Concepts of Language Teaching*. Oxford, England: Oxford University Press
- Stern, H. H. (1992). Issues and Options in Language Teaching. 262-266 Oxford. OUP
- Suleiman, A. M. (2010). *Kiswahili kwa Vyuo vyia Walimu wa Kiswahili*. Nairobi .East African Publishers. Kenya
- Suri, H. (2011). Purposeful sampling in qualitative research synthesis. *Qualitative research journal*. [/doi/10.3316/QRJ1102063/full/html](https://doi.org/10.3316/QRJ1102063/full/html)
- Susan, M., Jennifer. B. & Luke, P. (2013).Second Language Acquisition: An introduction Course. 4<sup>th</sup> edn. Routledge. New York

- Swain, M. (1985). Communicative Competence. Some Roles of Comprehensible Input na Comprehensible Out-put in its Development. IN S.M na C.G Madden (eds). *Input Second Language Acquisition*: Cambridge, M.A Newbury House 235-253.
- Taksiran, A .(2010). Exploring EFL Students casual Attributes of perceived success and Failure in Language Learning Process. (Tasnifu ya uzamili) hajachapishwa. Anadolu University.
- Tarone, E. (1989). *Focus on Language Learner*. Oxford University Press
- Tarone,E. na Yule, G. (1989). *Focus on The Language Leaner*. Oxford: Oxford University Press.
- The (1995) .*Constitution of Uganda*.Government of Uganda.
- Timoth, J. na Forns, J. R. (2003). *Social Disability in Cross-Cultural Research* .Hoobken. Edited by Jane Hawkins
- Tobias. S. (1983). *Anxiety and Cognitive Processing of Instruction*. <https://www.researchgate.net/publication/235059775>
- Toboso, M.B, na Mosol, K. (2018). *Lugha za kiafrika katika teknolojia na biashara. Majukumu ya kama ya ishirini na moja*.
- Towell, R na Hawkins, R. (1994).*Approaches to second language acquisition*.Clevedon: Multilingual Matters
- Troike, M. S. (2012). *Introducing Second Language Acquisition*. (Toleo la 2), Cambridge: Cambridge University Press.
- TUKI (2007). *Kamusi ya Kiingereza-Kiswahili*. Toleo la Tatu. Dar-es-Salaam.
- Uganda Government 1992. *Government White Paper on Implementation of the Recommendation of the Report of the Education Policy Review Commission*.
- Vigotysky, L .S. (1978). Mind in Society: *The development of hings psychological Process*: Cambridge University, M.A Harvard University Press.
- Walshe. C, Ewing. G, Griffths, J (2011). *Using observation as a data collection method to help understand patient and professional roles and actions in palliative care settings*.Palliative Medicine 26(8). DOI:[10.1177/0269216311432897](https://doi.org/10.1177/0269216311432897)
- Wanyanya, W. (2020). Umuhimu wa Kufundisha Lugha ya Kiswahili katika shule za Sekondari nchini Uganda. *East African Journal of Swahili Studies*, Vol. 2 Issue 1, 2020.
- Weaver, S.J. na Cohen, A, D. (1994). Making Learning Strategy instruction a reality in the foreign language curriculum. In. C. Klee (Ed), *Faces in a Crowd*: The individual learner in multisection courses. Boston: Henle na Heinle.285-323
- Weiner, B. (1992). *Human Motivation. Metaphor Theories and Research*. Newbury Park, CA: Sage
- Wellington, J. (2000). *Educational Research: Contemporary Issues and Practical Approach*. London:Continuum
- Wenden. A na Rubin.J (1987). *Learner Strategies in Language Learning*. New Jersey, Prentice Hall

- Wenden, A. (1985). *Learner strategies* [J]. TESOL Newsletter, 19, 1-7.
- Whitely, W. H. (1969). *Swahili. The Rise of a National Language*. Methuen na Co. London.
- Whyte, D. (2006). *Four reasons why languages as a skill are good for business brain*. EMEAEnterprise na Education at Rosseta Stone
- Williams, A. (1999). Communication Accommodation Theory and Miscommunication: Issues of Awareness and Communication Dilemmas. *International Journal of Applied Linguistics*, Vol.9, No.2,151-163.
- Williams, L. (1979). *The Modification of Speech Perception and Production in Second Language Learning. Perception and Psychophysics*, 26 (2), 95-104.
- Williams, M. (1994). Motivation in Foreign na Second Language Learning. *An Interactive Perspective , Educational na Child Psychology*; 11(2), 77-84
- Williams, M. na Burden (1997). *Psychology for Language Teachers' Social constructivists approach*. Cambridge: Cambridge University Press.
- Winter, C. (2000). *A Comparative Discussion of the Notion of Validity in qualitative and quantitative Research*. The Qualitative Report, 4(3-4),
- Wipf ,J. (1984). Shortwave radio and the second language class. MLJ, 68,7-12
- Wittrock, M. (1977).*Learning and Instruction*.Berkley,C.A :McCutchan
- Wong-fillmore, L. (1979). *Individual differences in second language acquisition*. In C. Fillmore D. Kempler (Eds *Individual in language ability and language behavior*: New York Academic Press.
- Xian, C. (2010). *Using Imitation and Recitation to Improve Oral English as a Second Language*.College Standards,China.
- Zehler, A. M. (2005). *Working with English language learners: strategies for elementary and middle school teachers* Imepakuliwa Julai 18 kutoka. <https://www.semanticscholar.org/paper>.

## VIAMBATISHO

### Kiambatisho A: Kiunzi cha Motisha cha Dornyei's (1994)

<b>KIWANGO CHA LUGHA</b>					
Mfumo wa motisha mwingiliano					
Mfumo wa motisha tumishi					
<b>KIWANGO CHA MWANAFUNZI</b>					
Mahitaji ya mafanikio					
Kujiamini					
Ari ya matumizi ya lugha					
Hali ya kawaida					
Ufanisi					
<b>HALI YA UJIFUNZAJI</b>					
Vipengele vya motisha katika kozi Mahsus					
Shauku	Ufaafu	Matarajio	Ridhaa		
<b>Vipengele mahsus vya motisha ya mwalimu</b>					
Msukumo wa Ushurikishaji	Mamlaka	Kujumuika kwa moja kwa moja	Uwasilishaji	Mawasilisho	Mrejesho
Makundi mahsus	Vipengele vya motisha		Mwisho ulioeleweka		
Kaida na mfumo wa kuzawadia					
Mshikamano wa makundi					
Mpangilio wa mwisho					

**Kiambatisho B: Kiunzi cha Motisha cha Williams na Burnens (1997)**

<b>ATHARI ZA NDANI</b>		
Ari ya shughuli ya ndani		
Kiwango cha kutaka kujuua	Kiwango cha maamuzi juu ya changamoto	
Kufahamu umuhimu wa shughuli		
Uhusiano wa mtu binafsi na shughuli	Thamana ya matokeo	
Ari ya ndani kulingana na shughuli		
<b>Hali ya Uasili</b>		
Sehemu ya kawaida		
Sehemu ya kumiliki uasili na matokeo		
Uwezo wa kupanda mielekeo thabiti		
<b>Ustadi</b>		
Kujihisi kwa umilisi		
Kuelewa maendeleo ya umilisi wa uwanja uliochaguliwa		
Ufanisi		
Dhana binafsi		
Kutambua uwezo na changamoto juu ya umilisi ulio nao		
Utathmini juu ya uamuzi wa mafanikio na upungufu		
Kujitathmini		
Kujifukiria		
<b>Mwelekeo</b>		
Mwelekeo juu ya lugha kwa jumla		
Mtazano juu ya lugha lengwa		
Mwelekeo juu ya jamii na tamaduni ya lugha lengwa		
<b>Athari zingine</b>		
Kujiamini		
Ragba ,kuogopa		
<b>Maendeleo ya umri na Viwango</b>		
Uana		
<b>Athari za nje</b>		
<b>Wau wengine wenye thamana</b>		
Wazazi	Walimu	Walio na umri au mazingira

		sawa
<b>Hali ya mwingiliano na athari zingine</b>		
Mapatano na maafikiano ya ujifunzaji		
Hali na kiwango cha mrejesho		
Hali na Kiwango cha sifa		
Kuadhibu na maonyo		
<b>Mazingira ya ujifunzaji</b>		
Utulivu	Vifaa	
Muda kwa siku, wiki na mwaka		
Ukubwa wa darasa na shule		
Maadili ya darsa na shule		
<b>Mazingira mapana</b>		
Familia pana		
Mfumo wa elimu		
Kiwango cha kipaumbele		
Kaida za utamaduni		
Matarajio ya jamii na mwelekeo		

**Kiambatisho C: Mchakato wa Kupata Watoa Taarifa kutoka katika Sampuli**

Ikiwa Wango ni:	Sampuli Itakuwa:	Ikiwa Wango ni:	Sampuli Itakuwa:	Ikiwa Wango ni:	Sampuli Itakuwa:	Ikiwa Wango ni:	Sampuli Itakuwa:
10	10	90	73	240	148	500	217
15	14	95	76	250	152	550	226
20	19	100	80	260	155	600	234
25	24	110	86	270	159	650	242
30	28	120	92	280	162	700	248
35	32	130	97	290	165	750	254
40	36	140	103	300	169	800	260
45	40	150	108	320	175	850	265
50	44	160	113	340	181	900	269
5	48	170	118	360	186	950	274
60	52	180	123	380	191	1000	278
65	56	190	127	400	196	1100	285
70	59	200	132	420	201	1200	291
75	63	210	136	440	205	1300	297
80	66	220	140	460	210	1400	302
85	70	230	144	480	214	1500	306

*Chanzo: Krejcie na Morgan (1970: 608)*

## Kiambatisho D: Mfano wa mpango binafsi

Day Mande Date 15/12/2019

Ebintu b70 nglenda kutum79 tkenyq

AMASIMU

1	TECHNO CAMON 12AHV	/ TECNO POUVOIR 3 AH
2	HUAWEI P40 PRO NE	P40
3	VIVO Y11 (32GB)	
4	SAMSUNG GALAXY A41	
5	NOKIA 5 310	NA INFIX NOTE 6

FLASHI DISIKI

2	4GB	} MWAMI NJOROGYE AJJAKUNHAMBA SSENTE MMELICA
4	4GB	
24	4GB	

SIMU KAYE

1	TECHYO
2	TAB - OS
3	NOKIA
4	INFIX

MWAMI NJOROGYE NGULILATA EBINTU BINO  
IWAMANGA

MWAMI NJOROGYE NUNULITA MIMI HII BINTU

- SIMU -TECNO CAMON 12A (12) NA TECNO POUVOIR (20)  
NOKIA 5 310 (20)  
INFIX NOTE 6 (22)

FLASHI DISIKI NI SENTE NGAPI - SORI SIRINGI NGAPI  
SIMU KAVA : NUNUWA TECNO(50) NOKIA (40) INFIX (40)  
AMBIA MIMI SIRINGAI NGAPI HALAF TATUMA NA M-PESA  
ASANTI SEGUTIX.  
HAPA SIMLAW LTD



## **Kiambatisho E: Hojaji kwa wafanya biashara**

Jina langu ni Mutenyo Aidah mwanafunzi anayesomea kozi ya uzamifu katika Chuo Kikuu cha Maseno-Kenya. Mimi ni mzaliwa wa hapa Uganda maeneo ya Mashariki mwa Uganda. Hojaji hili linakusudia kuchunguza juu ya mikakati na mitindo ya inayotumiwa wakati wa kujifunza Kiswahili kibashara na kuangazia changamoto wafanyabiashara hukumbana nazo wakati wa kujifunza Kiswahili kibashara. Majibu yatakayopatikana yatahifadhiwa na kutumiwa kwa lengo la uchunguzi pekee kwa ajili ya kiakademis.

1. Jina lako/siyo lazima.....
2. Jinsia
  - a. Mwamamke
  - b. Mwanaume
3. Unafanya biashara gani hapa?.....
4. Umemaliza miaka mingapi katika biashara yako?. Kati ya
  - a. 1-2
  - b. 3-5
  - c. 6-10
  - d. 11-15
  - e. 16-zaidi
5. Elimu yako ni ya kiwango kipi?
  - a. Chuo Kikuu
  - b. Elimu ya sekondari
  - c. Shule ya msingi
  - d. Sikusoma
6. Je,umewahi kupata mafunzo ya Kiswahili kama lugha ya biashara?
  - a. Ndiyo
  - b. La
7. Kama jibu lako ni (ndiyo) umetumia mikakati na mitindo ipi katika kujifunza Kiswahili kama lugha ya biashara
  - a.Mikakati.....
  - b.Mitindo.....
8. Kama jibu lako ni (la) je ungependa kutambulishiwa mikakati na mitindo ya ujifunzaji wa lugha ya pili?

a.Ndiyo

b. La

9. Mikakati ya jumla ya ujifunzaji lugha ya pili

- Mawasiliano
- Kuomba msaada
- Nyimbo
- Kijamii
- Kitekinolojia
- Kufidia
- Kumbukizi
- Mpango binafsi
- Mwanafunzi kwa mwanafunzi
- Kuongea
- Mtagusano na ukuruba kati ya wanunuzi na waizaji
- Utmbuzi
- Utatikanaji tena
- SKuchangana na kubalisha msimbo

10. Mitindo ya jumla ya ujifunzaji wa Lugha ya pili

- a. Mwingiliano
- b. Kusikiliza
- c. Kupenda
- d. Dukuduku
- e. Jitihada
- f. Mazingira halisia

11. Katika mikakati na mitindo ambayo umetajiwa je kuna ile ambayo umekuwa ukitumia kujifunza Kiswahili kibiashara bila kufahamu? Itaje

- a. Mikakati.....
- b. Mitindo.....

12. Kando na hiyo ambayo umetajiwa kuna mingine ambayo umekuwa ukitumia kujifunzaKiswahili kama lugha ya biashara?.Itaje

.....  
.....  
.....  
.....

13. Ni jinsi gani mikakati na mitindo uliyotaja hapo juu imekusaidia kujifunza Kiswahili lugha ya biashara?

- a. Mikakati.....

14. Kuna changamoto zozote umekumbana nazo wakati wa kujifunza Kiswahili kama lugha ya biashara?

a. Ndiyo

b. La

15. Kama ndiyo eleza changamoto hizo ulzokumbana nazo wakati wa kujifunza Kiswahili kama lugha ya biashara.

.....

.....

.....

.....

.....

16. Ni mikakati ipi ulifanya kutatua changamoto ambazo ulikumbana nazo wakati wa kujifunza Kiswahili kibiashara kama lugha ya biashara?

---

---

---

---

---

17. Unapendekeza nini kuhusu mikakati na mitindo ya ujifunzaji wa Kiswahili kama lugha ya biashara?

ASANTE

### **Kiambatisho F: Mwongozo wa mahojiano**

1. Hapa unapofanya akazi panaitwaje?
2. Je unafanya biashara ipi?
3. Biashara uliyoitaja umeifanyia kwa miaka mingapi?
4. Je unafahamu kwamba kuna mikakati na mitindo ya kujifunza Kiswahili kibiashara? Kama haujui je ukitaliwa utatambua ni mikakati na mitindo ipi umekuwa ukitumia kujifunza Kiswahili kibiashara?
  - a. Mikakati
  - b. Mitindo
5. Ni jinsi gani mikakati (4a) uliyotaja hapo juu imekusaidia kujifunza Kiswahilikibiashara.
6. Ni jinsi gani mitindo (4b) uliyotaja hapo juu imekusaidia kujifunza Kiswahilikibiashara.
7. Kiswahili kimekisaidiaje kuendeleza biashara yako?
8. Je, Kuna changamoto zozote umekumbana nazo wakati wa kujifunza Kiswahili kamalugha ya biashara?
9. Changamoto hizo ulizitatua vipi
10. Je una mapendekezo yoyote juu ya mikakati na mitindo ya ujifunzaji Kiswahili kama lugha ya biashara?

## **Kiambatisho: G Mwongozo wa uchunzaji**

**Mwongozo wa uchunzaji kuhusu mikakati na mitindo katika mazingira asili ya uendelezaji biashara**

<b>SN</b>	<b>Mkakati</b>	<b>Seheme ya matumizi</b>			<b>Mtindo</b>	<b>Sehemu ya matumizi</b>		
		<b>S.I.L</b>	<b>MUK</b>	<b>KIK</b>		<b>SIL</b>	<b>MUK</b>	<b>KIK</b>
1.	Mawasiliano				Mwingiliano			
2.	Kuomba msaada				Kusikiza			
3.	Nyimbo/ukariri				Kupenda			
4,	Kijamii				Dukuduku			
5.	Kiteknolojia				Jitihada			
6.	Kufidia				Mazingira Halisia			
7.	Kumbukizi				Mtazamo			
8.	Mpango binafsi				Viashiria			
9.	Mwanafunzi kwa mwanafunzi							
10.	Mtagusano na ukuruba kati ya wanunuvi na wauzaji							
11.	Utambuzi							
12.	Upatikanaji tena							
13.	Kuchanganya na kubadilisha msimbo							


**TAZ:**

**SIL-** Simlaw International Limited

**MUK-**Mukwano

**KIK-**Kikuubo

## Kiambatisho:H Mfano wa mahojiano kati ya mtafiti na wasailiwa




## Kiambatisho: Mfano wa majibu ya dodoso

13.	Kando na mikakati na mitindo hiyo hapo juu kuna mingine ambayo umekuwa ukitumia kujifunza Kiswahili kama lugha ya biashara? ..... <i>Katika biashara yangu</i>	
14.	Ni kwa jinsi gani umetumia Mikakati na mitindo katika biashara yako? ..... <i>Kupitia kuyatiba kusimbi na kusikiliza. Dzimka za Kiswahili</i>	
15.	Ni jinsi gani mikakati na mitindo uliyotaja hapo juu imekusaidia kujifunza Kiswahili kama lugha ya biashara? ..... <i>Jalansaidia kukuza biashara yangu na Kwendelea mbele kitedha</i>	
16.	Kuna changamoto zozote umekumbana nazo wakati wa kujifunza Kiswahili kama lugha ya biashara?	
a.	Ndiyo	<input checked="" type="checkbox"/>
b.	La	<input type="checkbox"/>

	Kama jibu lako ni ndiyo basi taja changamoto hizo. ..... <i>ki...lalu...uzengi...mwanamgalizi...kutumihili...kame...lugha...ya... wefizi...na...ni...kujifunza...kathawati...watu...kiswahili...uzingizi...hiyo</i>	
18.	Ni kwa jinsi gani ultatua changamoto ulizotaja hapo juu? ..... <i>Mungarukio...kufunduhia...walu...kuthuli...funda...ya... Kiswahili...Katika...Kwendeleza...literatura</i>	

Asante kwa wakati wako.

**Kiambatisho H:Barua ya kuenda uwanjani kukusanya data**



## Kiambatisho I:Barua ya kuomba ruhusa ya kukusanya data

Kabale University  
Institute of Language Studies  
P.O.Box 317  
Kabale  
20<sup>th</sup>/03/2020

Office of Directorate of Education and Social Services  
Kampala City Council Authority, Uganda  
P.O. Box 7010  
Kampala, Uganda

Dear sir/Madam

**REF: Request to carry out research in Kampala Business Centre**

Refer to the above subject matter. My name is Mutenyo Aidah, (registration number, PhD/FA/00088/2016). A Ugandan tracking my PhD from Maseno University in Kenya. The study is in the field of Kiswahili language. The topic of my study is *Strategies and Styles of learning Kiswahili as a business language among Kiswahili Traders in Uganda-Kampala District*. Areas of study are Mukwano Acharde, Simlaw International Limited and Kikuubo Market. The period of data collection will be between April- June 2020.

The data collection is for academic purpose and not any other purpose. Your permission will be of great use and shall be cherished in the contribution and successful completion of this study. Looking forward for your consideration.

Yours faithfully

N/A,

Mutenyo Aidah

## Kiambatishi J:Kibali cha REC



(+256) 0312 307400  
rec@ciu.ac.ug  
www.rec.ciu.ac.ug

To: Aidah Mutenyo  
Clarke International University  
  
Type: Initial Review

10/01/2022



Re: CLARKE-2022-334: Strategies, Styles And Challenges Of Learning Kiswahili As A Business Language Amongst Traders In Kampala, Uganda

I am pleased to inform you that at the 26th convened meeting on 10/01/2022, the Clarke International University REC, committee meeting, etc voted to approve the above referenced application.  
Approval of the research is for the period of 10/01/2022 to 10/01/2023.

As Principal Investigator of the research, you are responsible for fulfilling the following requirements of approval:

1. All co-investigators must be kept informed of the status of the research.
2. Changes, amendments, and addenda to the protocol or the consent form must be submitted to the REC for review and approval **prior** to the activation of the changes.
3. Reports of unanticipated problems involving risks to participants or any new information which could change the risk benefit: ratio must be submitted to the REC.
4. Only approved consent forms are to be used in the enrollment of participants. All consent forms signed by participants and/or witnesses should be retained on file. The REC may conduct audits of all study records, and consent documentation may be part of such audits.
5. Continuing review application must be submitted to the REC **eight weeks** prior to the expiration date of 10/01/2023 in order to continue the study beyond the approved period. Failure to submit a continuing review application in a timely fashion may result in suspension or termination of the study.
6. The REC application number assigned to the research should be cited in any correspondence with the REC of record.
7. You are required to register the research protocol with the Uganda National Council for Science and Technology (UNCST) for final clearance to undertake the study in Uganda.

The following is the list of all documents approved in this application by Clarke International University REC: